# FASIRI YA BIBLIA ISIYOGHARIMIWA

## *UNAWEZA KUIELEWA BIBLIA!*

## *PITIO LA AGANO LA KALE*

## *MWANZO - MALAKI*

NA BOB UTLEY,
PROFESA MSTAAFU WA KANUNI ZA UFASIRI
(UTAFASILI WA BIBLIA)

BIBLE LESSONS INTERNATIONAL, MARSHAL, TEXAS
2002 (Imehaririwa 2010)

# PITIO LA AGANO LA KALE
# MWANZO – MALAKI

**Dkt. BOB UTLEY**
**Bible Lessons International**

## ORODHA YA YALIYOMO

I. MWONGOZO WA USOMAJI MZURI WA BIBLIA ..... i

II. UFUNGUZI WA MASOMO ..... 01
- A. MANENO YALIYOTUMIKA ..... 01
- B. KWANINI KUJIFUNZA AGANO LA KALE ..... 01
- C. NAMNA YA KUJIFUNZA AGANO LA KALE ..... 02
- D. RAMANI YA MSINGI ..... 02
- E. MATUKIO YA MSINGI ..... 04

III. TORATI
- A. MWANZO ..... 11
- B. KUTOKA ..... 25
- C. MAMBO YA WALAWI ..... 34
- D. HESABU ..... 51
- E. KUMBU KUMBU LA TORATI ..... 57

IV. MANABII WA KWANZA
- A. YOSHUA ..... 65
- B. WAAMUZI ..... 65
- C. RUTHU (MAANDIKO) ..... 80
- D. SAMWELI ..... 85
- E. WAFALME ..... 94

V. JEDWALI – WAFALME WA UFALME ULIOGAWANYIKA

VI. MAANDIKO

A. MAMBO YA NYAKATI ..... 115

B. EZRA ..... 123

C. NEHEMIA ..... 130

D. ESTA ..... 137

VII. FASIHI YA HEKIMA ..... 144

A. USHAIRI WA KIEBRANIA ..... 148

B. VITABU

AYUBU ..... 151

ZABURI ..... 159

MITHALI ..... 169

MUHUBIRI ..... 175

WIMBO ULIOBORA ..... 183

VIII. MANABII WAKUBWA

A. UTANGULIZI WA UNABII WA AGANO LA KALE ..... 189

B. VITABU

ISAYA ..... 193

YEREMIA ..... 213

MAOMBOLEZO ..... 220

EZEKIELI ..... 225

DANIELI ..... 232

IX. MANABII WADOGO

HOSEA ..... 238

YOELI ..... 245

AMOSI ..... 251

OBADIA ..... 260

YONA ..... 266

MIKA ..... 271

NAHUMU ..... 277

HABAKKUKI ..... 282

ZEFANIA ..... 287

HAGAI ........ 292
ZEKARIA ........ 297
MALAKI ........ 303

# MWONGOZO KWA USOMAJI MZURI WA BIBLIA:

# UTAFITI BINAFSI KWA UKWELI ULIOTHIBITIKA

Tunaweza kuufahamu ukweli? Unapatikana wapi? Tunaweza kuuthibitisha kimantiki? Kweli, kuna mamlaka ya kimsingi? Kuna imani kamili inayoweza kulinda maisha yetu, na ulimwengu wetu tuliomo? Kuna maana yeyote katika maisha? Kwa nini tuko hapa? Tunakwenda wapi? Maswali haya yanauliza kwa watu wote wenye tafakuri zenye uwiano—wameyatawala maarifa ya binadamu tangu mwanzoni mwa nyakati (Mhu. 1:13-18; 3:9-11).

Naweza kukumbuka utafiti wangu binafsi kwa ajili ya ungamanisho la maisha yangu. Nimekuwa mwamini katika Kristo kwenye umri mdogo, awali kabisa nikizingatia juu ya ushahidi wa watu wengine muhimu kwenye familia yangu. Nilivyokuwa kufikia utu uzima, maswali juu yangu na ulimwengu ninamoishi ulivyokuwa.Tamaduni za kawaida na dini hazikuleta maana yeyote kwenye uzoefu niliousoma au kukutana nao. Ulikuwa ni muda wa kuchanganyikiwa, kutafuta, kutamani, na mara nyingi fikra zisizokuwa na tumaini katika uso wa ulimwengu mgumu, usiojali nilimoishi.

Wengi walidai kuwa na majibu kwa maswali haya ya msingi, lakini baada ya utafiti na kufikiri nikapata majibu yao yamelenga juu ya (1) falsafa binafsi, (2) hadithi za kubuniwa za kale, (3) uzoefu binafsi, au (4) Saikolojia zilizojichomoza. Nilihitaji digrii fulani ya uthibitisho, baadhi ya vielelezo, kiasi cha busara ambamo ningelenga mtazamo wangu wa kidunia, kiini cha uzima wangu, sababu yangu ya kuishi.

Niliyapata haya katika usomaji wangu wa biblia. Nilianza kutafuta ushahidi wa udhamini nilioupata katika (1) utegemezi wa historia ya biblia kama ulivyothibitishwa na elimu kale, (2) usahihi wa Nabii za Agano la Kale, (3) umoja wa jumbe za Biblia zaidi ya miaka 1600 ya kutolewa kwake na (4) shuhuda binafsi za watu ambao maisha yao yalibadilika moja kwa moja baada ya kusoma biblia. Ukristo, kama mfumo wa imani na kuamini uliounganishwa, una uweo wa kukabiliana na maswali magumu ya maisha ya mwanadamu. Siyo haya tu yanaweza kutoa muundo kazi, lakini mwelekeo unaotokana na uzoefu wa imani za kibiblia uliniletea furaha zenye hisia na ustahimili.

Nilijiridhisha ya kuwa nimepata kiini cha uzima wa maisha yangu—Kristo, kama ninavyoelewa kupitia maandiko.Ulikuwa ni uzoefu mgumu, msukumo wenye kuweka huru. Ingawa, naweza kukumbuka mshituko na maumivu yalipoanza kunifahamisha juu ya tafasiri ngapi tofauti ya kitabu hiki zimetetewa, wakati mwingine hata ndani ya makanisa hayo ya aina moja. Nikithibitisha mwongozo wa Ki-Mungu na uaminifu wa biblia haukuwa mwisho, lakini ni mwanzo pekee. Ni kwa vipi naweza kuthibitisha au kukataa tafsiri zinazotofautiana na kugongana za kurasa nyingi ngumu ndani ya maandiko kwa wale waliokuwa wakidai mamlaka yake na uaminifu?

Kazi hii imekuwa lengo la maisha yangu na hija ya imani. Nilifahamu ya kuwa imani katika Kristo imeniletea furaha na amani kubwa. Mawazo yangu yametamani baadhi ya imani kamili katikati ya nadharia ya utamaduni wangu na mfumo wa imani gonganishi wa dini na majivuno ya kimadhehebu. Katika utafiti wangu wa mitazamo halali kwenye utafsiri wa fasihi ya kale, nilishangaa kuvumbua historia yangu, ya kitamaduni, ya kimadhehebu na uzoefu wa kipendeleo. Kwa kawaida kabisa, mara nyingi, nimesoma Biblia ili kuimarisha mtizamo wangu. Nimeutumia kama chanzo cha mfumo wa imani kuvamia imani nyingine wakati nikijihakikishia usalama wangu na utoshelevu. Ni kwa namna gani utambuzi wa maumivu haya yalikuwa kwangu!

Ingawa siwezi kuwa kipingamizi moja kwa moja, naweza kuwa msomaji mzuri wa biblia. Naweza kuweka ukomo wa upendeleo kwa kutambua na kukubali uwepo wao. Sijawaweka huru,lakini nimeukabiri udhaifu wangu. Mtafsiri mara nyingi ndio adui mbaya wa usomaji mzuri wa biblia!

Hivyo ngoja nitaje baadhi ya dhanio nilizoleta kwenye usomaji wa biblia ili, msomaji, aweze kuzichunguza pamoja nami:

(1) Ninaamini biblia ni uvuvio wa ki-pekee wa ufunuo binafsi wa Mungu mmoja na aliye wa kweli. Kwa hiyo, ni lazima itafsiriwe katika mwanga wa kusudi la Ki-Ungu la mwandishi wa mwanzo (yaani Roho) kupitia mwandishi wa kibinadamu katika muundo wa historia uliokusudiwa.

(2) Ninaamini Biblia inakusudi na ujumbe uliowekwa pamoja. Haina mkanganyiko ndani yake, ingawa inajumuisha (njia ngumu na zinazokinzana). Hivyo basi, mtafsiri mzuri wa biblia ni biblia yenyewe.


(3) Ninaamini kwa kila kurasa (pasipo kujumuisha unabii) ina maana moja iliyosimama kwenye kusudi la mwanzo la mwaandishi aliyevuviwa. Ingawa hatuwezi kutia shaka kutambua kusudi la mwandishi wa mwanzo, viashirio vingi daima vimeelekeza katika uelekeo wake;

    a. Aina ya uwasilishaji (aia ya fasihi) inachaguliwa kuelezea ujumbe
    b. Mtindo wa kihistoria na/au muda maalumu ulioshawishi maandiko kuandikwa
    c. Muundo wa fasihi wa kitabu husika pamoja na kila fasihi moja
    d. Muundo wa maandishi (elezewa kwa fasaha) wa fasihi moja kama zinavyo husiana na ujumbe
    e. Umbo la kisarufi husika lililowekwa kuwasilisha ujumbe
    f. Maneno yaliyochaguliwa kuwakilisha ujumbe


    Jifunze ya kila eneo hili liwe chanzo cha mafunzo yetu katika aya. Kabla sijaelezea njia zangu za usomaji mzuri wa biblia, hebu nielezee angalau njia zisizosahihi zinazotumiwa siku hizi zilizopelekea kuwepo kwa tafsiri tofauti nyingi na hivyo basi zinatakiwa kuepukika.

1. Kutojali mazingira ya fasihi ya vitabu vya Biblia na kutumia kila sentesi, ibara, au maneno binafsi kama maelezo ya kweli yasiyohusiana na kusudi la mwandishi wa mwanzo au mtindo mpana. Hii mara nyingi huitwa “uhakiki wa andiko”
2. Kutoujali muundo wa ki-hisoria wa vitabu kwa kubadilisha muundo wa ki-historia unaodhaniwa kuwa ni mdogo au usiosaidika kutoka kwenye andiko lenyewe.
3. Kutojali muundo wa kihistoria wa vitabu na kusoma kama gazeti la mtaani lililoandikwa asili kwa wakristo binafsi wa kisasa.
4. Kuupa muundo wa kihistoria wa vitabu kwa kuliistiari andiko ndani ya ujumbe wa falsafa/theolojia isioendana na wasikiaji wa kwanza na kusudi la mwandishi wa mwanzo.
5. Kutojali muundo wa mwanzo kwa kubadilisha mtindo wa theolojia ya mtu, mafundisho yanayopendeka, au mambo ya kisasa yasiyoendana na kusudi la mwandishi wa mwanzo na ujumbe uliotolewa. Tabia hii mara nyingi hufuata usomaji wa mwanzo wa biblia kama kigezo cha kuanzisha mamlaka ya mnenaji. Hii mara nyingi hurejewa kama “mwitikio wa msomaji” (utafsiri wa-andiko-lililomaanisha-kwangu).

Kwa wastani, vitu vitatu vinavyoendana vinaweza kupatikana katika mawasiliano ya binadamu yalioandikwa.




Siku za nyuma, mbinu tofauti za usomaji zimenitazamisha juu ya moja kati ya vitu vitatu. Lakini kweli tunatamka kwa dhati uhuisho wa Biblia wa kipekee na mchora uliofanyiwa mabadiliko unaofaa zaidi:




Kwa kweli vitu hivi nyote vitatu lazima vijumulishwe katika mchakato wa ufasiri. Kwa kusudi la uthibitisho, ufasiri wangu unalenga juu ya moja kati ya vitu viwili: mwandishi wa mwanzo na maandiko. Ninayamkinika kujibu matusi mabaya niliyoyachunguza (1) shutumu au kutakasa maandiko na (2) tafasili ya "mwitikio wa msomaji" (unamaanishwa nini kwangu).Matusi yanaweza kutokea katika kila hatua. Ni lazima kila mara tuchunguze mienendo yetu, upendeleo wetu, mbinu na matumizi. Lakini ni kwa jinsi gani tunaweza kuyachunguza kama hapatakuwepo na mipaka ya ufasihi, ukomo au kigezo? Hapa ni pale kusudi la mwandishi na muundo wa maandiko yaliponipa baadhi ya vigezo kuzuia maeneo ya fasiri zilizo halali.

Katika kuangazia hizi mbinu za usomaji zisizofaa, zipi ni baadhi ya mitazamo mizuri ya usomaji mzuri wa biblia ambao unatoa digri ya uthibitisho na misimamo?

Katika hatua hii sijadili mbinu pekee za ufasiri wa namna mahususi lakini kwa pamoja kanuni halali kwa aina yote ya maandiko ya kibiblia. Kitabu kizuri kwa namna ya mitazamo mahususi ni *How To Read The Bible For All Its Worth*, ya Gordon Fee na Douglas Stuart, kilichochapishwa na Zondervan.

Utaratibu wangu mwanzoni ulinitizamisha juu ya msomaji aliyemruhusu Roho Mtakatifu kuangaza biblia kupitia kwa miduara minne ya usomaji binafsi. Hii inamfanya Roho, andiko na msomaji wawe kiwango cha mwanzo, na siyo cha juu. Vile vile hii inamlinda msomaji kutokuwa na mwanya wa kushawishiwa na mtoa maoni. Nimesikia ikisemwa: "Biblia inaangazia zaidi katika fasihi". Hii haimaanishi kukashifu maoni juu ya msaada wa usomaji lakini ni ombi kwa muda unaofaa kwa matumizi yao.

Tunalazimika kuusaidia ufasiri wetu kutoka katika andiko lenyewe. Maeneo matatu yanatoa angalau ukomo wa uthibitisho:

(1) muundo wa kihistoria
(2) mazingira ya fasihi
(3) muundo wa kisarufi (vipashio)
(4) matumizi ya maneno ya kisasa
(5) vifungu sambamba vyenye kuhusiana

Tunahitajika kuweza kutoa sababu na mantiki zilizo nyuma ya ufasii wetu. Biblia ndiyo chanzo pekee cha imani yetu na mazoezi. Kwa huzuni, mara nyingi wakristo hawakubali juu ya kile kinachofundishwa au kukiri.

Mizunguko mine ya usomaji imeundwa kutupatia utambuzi wa ufasili ufuatao:

(1) Mzunguko wa kwanza wa usomaji
  (a) Soma kitabu katika mkao mmoja. Soma tena katika fasili tofauti , kwa matumaini kutoka katika fasili tofauti za nadharia
    (i) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
    (ii) Mlinganyo wenye nguvu (TEV, JB)
    (iii) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
  (b) Angalia kiini cha kusudi la uandishi mzima. Tambua dhamira yake.
  (c) Tenga (ikiwezekana) fasihi moja, sura, ibara au sentesi inayoelezea waziwazi Kiini cha kusudi au dhamira
  (d) Tambua fasihi tanzu yenye nguvu
    i. Agano la kale

1) Simulizi za waebrania
2) Mashairi ya waebrania (fasihi za hekima, zaburi)
3) Unabii wa ki-Ebrania (lugha ya mjazo, shairi)
4) Alama za siri za ki-sheria

ii. Agano jipya
1) Simulizi (Injili, matendo)
2) Hadithi za mafumbo (Injili)
3) Barua/nyaraka

(2) Mzunguko pili wa usomaji
(a) Soma kitabu kizima tena, ukitafuta kufahamu mada muhimu au masomo.
(b) Elezea kwa muhtasari wa mada muhimu na elezea kwa kifupi yaliomo kwa maelezo rahisi
(c) Angalia kusudi la maelezo yako na eleza kwa mapana kwa msaada wa usomaji.

(3) Mzunguko wa tatu wa usomaji.
(a) Soma tena kitabu kizima, ukitafuta kutambua muundo wa ki-historia na Matukio lengwa kwa ajili ya uandishi kutoka katika kitabu cha Biblia yenyewe.
(b) Taja vipengele vya ki-historia ambavyo vinatajwa katika kitabu cha Biblia.
(i) Mwandishi
(ii) Tarehe
(iii) Wapokeaji
(iv) Kusudu mahsusi la uandishi
(v) Mwelekeo muundo wa kitamaduni unaorandana na kusudi la mwandishi
(c) Panua maelezo yako kwa kiwango cha aya kutoka katika sehemu ya kitabu cha biblia unayotafasiri. Mara nyingi tambua na kuelezea fasihi. Inaweza kuwa na vifungu na aya nyingi. Hii inakuwezesha wewe kufuata wazo na muundo wa maandiko ya mwandishi wa mwanzo.
(d) Angalia muundo wako wa kihistoria kwa kutumia msaada wa usomaji

(4) Mzunguko wa nne wa usomaji
(a) Soma tena bayana fasihi moja katika tafasiri nyinginezo nyingi
(b) angalia fasihi au muundo wa kisarufi
(i) Misemo ya kujirudia Waefeso.1:6, 12, 14
(ii) Muundo wa kisarufi unaojirudia Warumi 8:31
(iii) Mbinyo wa mawazo (dhana zinazoafikiana)
(c) Taja vipengele vifuatavyo:-
(i) Istilahi muhimu
(ii) Istahili zisizo za kawaida
(iii) Muundo muhimu wa kisarufi
(iv) Maneno magumu, ibara, na sentesi
(d) Angalia njia muhimu zilizosambamba
(i) Angalia njia za wazi za ufundishaji kwenye somo lako kwa kutumia
a) Vitabu vya thiolojia
b) Biblia za marejeo
c) Itifaki
(ii) Angalia maneno mawili yanayokinzana katika somo lako. Kweli nyingi za ki-Biblia zinatolewa katika rahaja mbili zinazofanana. Migongano mingi ya ki-madhehebu hutokea kutokana nauthibitisho nusu wa maandiko ya Biblia. Biblia zote

zimevuviwa. Ni lazima tutafute ujumbe mzima ili kutoa mlinganyo wa ki-maandiko katika tafasiri zetu.

(iii) Angalia milinganisho ndani ya kitabu, kilekile, mwandishi Yule Yule, au namna ileile, Biblia ina mfasiri wake mzuri kwa sababu ina mwandishi mmoja ambaye ni Roho Mtakatifu.

(e) Tumia misaada ya kusoma kuangalia uchunguzi wako wa muundo wa kihistoria na tukio.
   (i) Soma biblia
   (ii) Ensaikolopidia za biblia, vitabu vya mkononi na kamusi
   (iii) Tangulizi za biblia
   (iv) Fasihi za biblia (katika hatua hii kwenye usomaji wako ruhusu jamii ya waamini, waliopita na waliopo, kusaidia na kusahihisha usomaji wako binafsi)

Katika hatua hii tunageukia matumizi, umechukua muda kuelewa andiko katika muundo wake, sasa lazima utumie katika maisha yako, utamaduni wako, na elezea mamlaka ya Ki-biblia kama "uelewa ule mwandishi wa ki-biblia wa mwanzo alivyosema katika zama zake na kutumia ukweli huo katika zama hizi".

Matumizi lazima yafuate utafasiri wa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika muda na mantiki. Mtu hawezi kutumia njia ya Biblia katika zama zetu mpaka pale tutakapo fahamu kile alichokuwa akikisema katika zama hizo. Njia ya Biblia isimaanishe kile asicho kimaanisha!

Maelezo yako kwa kirefu, kwa kiwango cha aya (mzunguko wa usomaji #3) yatakuwa mwongozo wako. Matumizi lazima yafanyike katika kiwango cha aya, na sio kiwango cha neno, maneno yana maana pekee katika mazingira, ibara zina maana pekee katika mazingira na sentensi zina maana pekee katika mazingira. Mtu pekee aliyevuviwa ambaye amejumuishwa katika mchakato wa utafsiri ni mwandishi wa mwanzo. Kipekee unafuata utangulizi wake kwa mwanga wa Roho Mtakatifu. Lakini nuru sio uvuvio. Kusema "asema Bwana"lazima, tufungamane na kusudi la mwandishi wa mwanzo. Matumizi lazima yaendane bayana na kusudi lote la uandishi mzima, maandishi bayana, na muendelezo wa kiwango cha aya.

Usiruhusu mambo ya zama hizi yatafasiri Biblia, iruhusu Biblia ijiongee yenyewe. Hii itatuhitaji kuvuta kanuni kutoka kwenye andiko. Hii itakubalika kama andiko litaiwezesha kanuni. Bahati mbaya wakati mwingi kanuni zetu ni "zetu" na si kanuni za ki-maandiko.

Katika kutumia Bibilia, ni muhimu kukumbuka kuwa (isipokuwa katika unabii) maana moja na moja pekee itakubalika kwa andiko la Kibiblia pekee. Maana hiyo iendane na kusudi la mwandishi wa mwanzo kama alivyo eleza tatizo au hitaji katika zama zake. Mengi ya matumizi yanayowezekana yanaweza kutolewa kutoka katika maana hii moja. Matumizi yatategemea mahitaji ya wapokeaji lakini ni lazima yaendane na maana ya mwandishi wa mwanzo.

Zaidi ya hapo nimejadili mantiki na mchakato wa ki-maandiko uliojumuishwa kwenye utafasiri na matumizi. Sasa ngoja nijadili kwa kinaga ubaga mwelekeo wa kiroho wa utafasiri. Mfuatano ufuatao umekuwa wa msaada sana kwangu.

(1) Omba kwa ajili ya msaada wa Roho (kama vile 1Kor. 1:26-2:16)
(2) Omba kwa ajili ya msaada binafsi na kusafishwa kutoka katika dhambi inayojulikana (kama vile 1 Yohana 1:9)
(3) Omba kwa ajili ya hamu kubwa ya kumjua Mungu (kama vile Zab. 19:7-14, 42:1, 119:1)
(4) Tumia utambuzi wowote mpya mara moja katika maisha yako.
(5) Baki mnyenyekevu na anayefundishika.

Ni vigumu kuweka mlinganyo kati ya mchakato wa kimantiki na uongozi wa kiroho wa Roho Mtakatifu. Dondoo zifuatazo zimesaidia kulinganisha hizi mbili:

(1) Kutoka kwa mwandishi James W.Sire, *Scripture Twisting*, IVP, kr. 17-18
"Nuru huja kwenye mawazo ya watu wa Mungu na sio tabaka la watu wa kiroho. Hakuna daraja la ualimu katika ukristo wa kibiblia. Hakuna kuongoza, hapana mtu awaye yote ambaye tafsiri zote nzuri zitoke kwake. Na hivyo, wakati roho mtakatifu anatoa karama maalumu ya hekima,

maarifa na utambuzi wa kiroho huwa pamoja. Hakutoa hizi kwa wakristo waliokirimiwa kuwa wao ndo pekee watafsiri wenye mamlaka ya Neno lake. Ni juu ya kila watu wake kujifunza, kuamua na kutambua kwa kufanya marejeo kwenye Biblia ambayo inasimama kama yenye mamlaka hata kwa wale ambao Mungu amewapa uwezo pekee. Kwa kufupisha, wazo mnalofanya kupitia kitabu kizima ni kuwa Biblia ni ufunuo wa kweli wa Mungu kwa watu wote, ya kuwa ni mamlaka yetu ya mwisho katika mambo yote ambayo inayaongelea, kuwa sio fumbo lote lakini inaweza kueleweka vya kutosha na watu wa kawaida kwa kila tamaduni."

(2) Juu ya Kierkegaard, inayopatikana toka kwa Benard Ramm,*Protestant Biblical Interpretation (tafsiri ya biblia ya ki-protestanti*) Uk.75:

Kutokana na Kierkegaard, kisarufi, misamiati na usomaji wa kihistoria wa Biblia ulikuwa ni muhimu lakini utangulizi wa usomaji wa kweli wa Biblia na kusoma Biblia kama neno la Mungu mmoja lazima alisome kwa moyo wake wote mdomoni mwake, kutoka ncha ya kidole, na shauku ya matarajio katika mazungumzo na Mungu. Usomaji wa Biblia pasipo tafakari, kutojali au kielimu, au weledi sio usomaji wa Biblia kama neno la Mungu, kama mmojawapo asomavyo barua ya mapenzi isemavyo, tena mmoja asoma kama neno la Mungu."

(3) H.H Rawley katika *The Relevance of the Bible*, Uk.19:

"Hakuna uelewa mdogo wa kisomi wa Biblia, ingawa yote, inaweza kumiliki hazina yote. Haidharau uelewa huo, kwa kuwa ni muhimu kwa uelewa wote. Lakini ni lazima iongeze uelewa wa kiroho wa hazina ya kiroho ya kitabu hiki kwa ujumla. Kwa huo uelewa wa kiroho kitu fulani ambacho ni zaidi ya hadhari ya kiroho ni muhimu. Mambo ya kiroho ni utambuzi wa kiroho, na wanafunzi wa Biblia wanahitaji fikra za upokeaji wa kiroho. Ile hamu ya kumtafuta Mungu ambayo inaweza kumsababisha ajitoe kwake. Ni kama kupita zaidi ya usomaji wa kisayansi kuingia kwenye urithi wa utajiri wa hiki kitabu kikubwa kuliko vyote."

*Study Guide Commentary (Mwongozo wa usomaji) wa* fasihi umeundwa kusaidia njia zako za utafsiri katika njia zifuatazo:

1. Maelezo fasaha ya kihistoria yanayotambulisha kila kitabu baada ya kufanya "Mzunguko wa usomaji #3" angalia taarifa hizi.
2. Utambuzi wa ki-mazingira unapatikana katika kila kurasa. Hii itakusaidia kuona jinsi gani maandishi/fasihi imeundwa.
3. Katika kila mwanzo wa kifungu au fasihi kubwa inaunganisha mgawawanyo wa aya na maelezo ya kichwa cha makala yanatolewa kutoka katika tafsiri za kisasa.
    a. United Bible Society Greek Text.Toleo la nne lililobadilishwa (UBC)
    b. The New American Standard Bible 1995 ya kisasa (NASB)
    c. The New King James Version (NKJV)
    d. The New Revised Standard Version (NRSV)
    e. Today's English Version (TEV)
    f. The Jerusalem Bible (JB)

Aya zilizogawanywa hazikuvuviwa. Lazima ziyakinishwe kutoka katika mazingira fulani. Kwa kulinganisha tafsiri nyingi za kisasa kutoka tafsiri nyingi za ki-nadharia na mitizamo ya kitheolojia, tunaweza kuchanganua muundo unaokusudiwa wa mawazo ya mwandishi wa mwanzo.

Kila aya ina ukweli mmoja mkubwa. Huu uliitwa "mada ya sentensi" au wazo la kati la andiko, hilo wazo lililounganishwa ni ufunguo kwa tafsiri nzuri ya kihistoria na kisarufi. Mmojawapo asitafsiri, kuhubiri au kufundisha chini ya aya, vilevile ukumbuke ya kuwa kila aya inahusiana na aya zingine. Hii ndo maana kiwango cha aya kinachoelezea kitabu kizima ni muhimu. Ni lazima tuweze kufuata mtiririko wa kimantiki wa somo lililotolewa na mwandishi wa mwanzo aliyevuviwa.

4. Muhtasari wa Bob unafuata mtazamo wa kifungu kwa kifungu kwa utafsiri wake. Hii inatulazimisha kufuata mawazo ya mwandishi wa mwanzo. Muhtasari unatoa habari kutoka sehemu nyingi.
    a. Mazingira ya fasihi

    b. Utambuzi wa kihistoria na tamaduni
    c. Habari za kisarufi
    d. Usomaji wa neno
    e. Njia muhimu zilizo sambamba
5. Mahali fulani katika fasihi, andiko lililochapishwa toka toleo jipya la Marekani (1995 mpaka sasa hivi) litaongezewa na tafsiri za matoleo mbalimbali ya kisasa.
    a. New King James Version (NKJV) ambayo unafuata mswaada wa “Upokeaji wa Maandiko halisi”.
    b. The New Revised Standard Version (NRSV) ambayo ni rudio la neno-kwa-neno Kutoka katika Umoja makanisa asili ya Revised Standard Version
    c. The Today’s English Version (TEV) ambayo ni tafsiri ya mlinganyo wa nguvu Kutoka American Bible Society.
    d. The Jerusalem Bible (JB) ambayo ni tafsiri ya Kiingereza inayotegemea kutoka tafsiri ya Mlinganyo wa nguvu wa Katoriki ya Ufaransa.
6. Kwa wale wote ambao hawasomi Kiyunani, ukilinganisha na tafsiri za kiingereza inaweza kusaidia kutambua matatizo katika andiko:
    a. Tofauti za mswada
    b. Maana ya maneno mbadala
    c. Muundo na maandiko magumu ya kisarufi
    d. Maandiko tata yenye mana zaidi ya mbili

    Ingawa tafsiri za kiingereza haziwezi kuleta suluhu kwenye matatizo hayo yanayalenga kama sehemu ya ndani na usomaji kamili.
7. Karibia kila kifungu, maswali muhimu ya majadiliano yanatolewa ambayo yanajaribu kulenga maswala muhimu ya utafsiri wa sura hiyo.

Juzuu za Mwongozo wa Masomo (*Study Guide Comme ntary Volumes*) sasa zinapatikana:

Vol. 0 Semina juu ya “Waweza Kuielewa Biblia”
Vol. 1 Mtangulizi wa Kwanza wa Kikristo; Mathayo
Vol. 2 Injili Kama Ilivyoandikwa na Marko: Marko na 1 & 2 Petro
Vol. 3A Mwana Historia Aitwaye Luka:Injili Kama ilivyoandikwa na Luka (inapatikana mnamo 2003)
Vol. 3B Mwana Historia Aitwaye Luka: Kitabu cha Matendo ya Mitume (inapatikana 2003)
Vol. 4 Nyaraka na Barua za Wanafunzi Wapendwa: Injili ya Yohana, 1, 2 na 3 Yohana
Vol. 5 Injili Kama Ilivyoandikwa na Paulo:Warumi
Vol. 6 Nyaraka za Paulo kwa Kanisa lenye Misukosuko: 1 &2 Wakorintho (inapatikana 2002)
Vol. 7 Barua za kwanza za Paulo: Wagalatia na 1 & 2 Wathesalonike
Vol. 8 Nyaraka za Paulo akiwa Gerezani: Wakolosai, Waefeso, Filemoni na Wafilipi
Vol. 9 Safari ya Nne ya Paulo ya Umisionari: 1 Timotheo, Tito na 2 Timotheo
Vol. 10 Ukuu wa Agano Jipya: Waebrania
Vol. 11 Ndugu wa Kiukoo wa Yesu Wazungumza: Yakobo na Yuda
Vol. 12 Tumaini katika Nyakati Ngumu—Pazia la Mwisho: Ufunuo
Vol. 1AOT Namna Yote Yalivyoanza: Mwanzo 1-11

# UFUNGUZI WA SOMO

I. MAANA ZA MANENO YANAYOTUMIKA MARA KWA MARA

A. MAJINA YA MUNGU

1. El
2. Elohim
3. YHWH
4. Adoni
5. El Shaddai

B. MAJINA YA MAANDIKO NA FASIRI:

1. Andiko la Kimasoreti (MT)
2. Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale kutoka Kiebrania (LXX)
3. Vulgate
4. Midrash
    a. Halakah - fasiri juu ya Torati
    b. Haggada - hadithi na mifano juu ya Agano lote la Kale
5. Lijitabu la sheria za Kiyahudi
    a. Mishnah - desturi za mazungumzo juu ya Torati kutoka katika waalimu wa Kiyahudi maarufu
    b. Gemara - na waalimu wa Kiyahudi wa baadaye
6. Targums
7. Magombo ya Bahari ya Chumvi

II. KWANINI KUJIFUNZA AGANO LA KALE

A. Lilikuwa maandiko pekee ambayo Yesu na Mitume walikuwa nayo. Walinukuu kutoka huko mara kwa mara.

B. Ni ufunuo wa Mungu mwenyewe. Limevuviwa.

1. Mathayo 5:17ff
2. 2 Timotheo 3:15-17
3. 1 Wakorintho 2:9-13
4. 1 Wathesalonike 2:13
5. I Petro 1:23-25
6. 2 Petro 1:20-21
7. 1 Petro 3:15-16

C. Liliandikwa kwa ajili yetu.

1. Warumi 4:23-24; 15:4
2. 1 Wakorintho 9:9-10; 10:6, 11

D. Namna gani Wakristo wanatakiwa kuliitikia?

1. Mijongeo kadhaa ya kihistoria
2. kwa kulitunza kikamilifu
3. kwa kutolipuuzia kikamilifu
4. kwa kuliheshimu kama ufunuo lakini si linalofunga
5. Sio njia ya wokovu
    a. Warumi 4
    b. Mdo. 15; Wagalatia 3

6. Waebrania
7. Ni ufunuo wa Mungu kwa mwanadamu. Lina kusudi katika maisha yetu. Linatengeneza msingi kwa ajili ya Agano Jipya (ahadi ya utimilizwaji.)

III. NAMNA GANI TUNAJIFUNZA AGANO LA KALE (BIBLIA) Baadhi ya kanuni za msingi za ufasiri:

A. Biblia imeandikwa kwa lugha ya kawaida ya kibinadamu:
1. Mungu hafichi ukweli.
2. Mungu amejidhihirisha mwenyewe katika uwezo wetu wa kuelewa.

B. Msingi wa ufasiri sahihi ni kusudio la asili lililovuviwa na mwandishi. Hii inapatikana katika maana iliyowazi ya maneno yaliyotumika na mwandishi na kueleweka kwa wasikiaji wa asili. Hivyo, kwa ufasiri sahihi wa kifungu, mtu sharti azingatie taarifa zifuatazo:
1. mazingira ya kihistoria;
2. muktadha wa kifasihi;
3. aina ya uwasilishaji (aina ya fasihi);
4. sarufi (muundo wa maneno);
5. maana ya maneno ya kisasa;
6. aina ya kimuktadha ya mwandishi.

C. Biblia yote imevuviwa (2 Tim. 3:16), hivyo, fasiri bora ya Biblia ni Biblia.
Tunaita hii "ulinganifu wa imani" au vifungu vinavyofanana:
1. tunaangalia kifungu kinachoeleweka zaidi;
2. tunatazama kusudio lipitalo yote la Mungu;
3. tunatazama ukweli unaowasilishwa kwa jozi zinazokinzana.

D. Mtu anawezaje kutofautisha kweli za kidesturi na zile za muda zipitazo kutoka katika desturi zilizo katika mpito na kweli za milele?:
1. Je kweli ya Agano la Kale inathibitishwa na mwandishi wa Agano Jipya?
2. je Biblia ina mfanano wa aina moja katika uwasilishaji wake wa kweli hii?
3. je kweli imevalishwa katika namna ya maneno yaliyowazi ya kidesturi?

IV. RAMANI YA MSINGI YA MASHARIKI YA KARIBU YA KALE KAMA INAVYOHUSIANISHWA NA AGANO LA KALE

A. Vyanzo vya maji (kutoka magharibi kwenda mashariki)
1. Bahari ya Mediterania (Kuu au bahari ya Juu)
2. Mto Nile
3. Bahari ya Shamu (Mto Chinnereth)
4. Ghuba ya Aqaba
5. Mto (au brook) ya Misri
6. Bahari ya Chumvi (Bahari ya Chumvi)
7. Mto Yordani
8. Mto Yabbok
9. Mto Arnoni
10. Bahari ya Galilaya
11. Mto Frati
12. Mto Hedekeli

13. Ghuba ya Uajemi (Bahari ya Chini)

B. Nchi ambazo zimeleta matokeo kwa watu wa Mungu katika Agano la Kale (magharibi kwenda mashariki)

1. Rumi
2. Uyunani
3. Caphtor (Krete)
4. Kittimu (Kipro)
5. Misri
6. Filistia
7. Yuda
8. Israeli
9. Edomu
10. Moabu
11. Ammoni
12. Foenike (Lebanoni)
13. Shamu
14. Wahiti (Anatolia)
15. Arabuni
16. Ashuru
17. Babeli
18. Uajemi
19. Media
20. Elamu

C. Miji Mikuu ya nchi kubwa [jaribio la Pili]

1. Memphis (Misri)
2. Yerusalemu (Yuda)
3. Samaria (Israeli)
4. Tiro (Foenike)
5. Dameski (Shamu)
6. Ninawi (Ashuru)
7. Babeli (Babeli)
8. Susa (Uajemi)

D. Miji mingine muhimu [jaribio la tatu]

1. Uru
2. Harani
3. Megiddo
4. Shekemu
5. Yeriko
6. Betlehemu
7. Hebroni
8. Beersheba
9. Avarisi/Zoani/Tanisi

10. Thebesi

E. Milima [jaribu la tatu]
   1. Ararati
   2. Hermoni
   3. Tabori
   4. Ebali au Gerizimu (Shekemu)
   5. Karmeli
   6. Nebo/Pisgah
   7. Sayuni/Moriah (Yerusalemu)
   8. Sinai/Horebu

V. MATUKIO YA MUHIMU YA AGANO LA KALE


A. Matukio yasiyokuwa na tarehe (Mwa. 1-11)
   1. uumbaji
   2. anguko
   3. gharika
   4. mnara wa Babeli

B. Tarehe kumi na matukio:
   1. Kipindi cha Mababa wa Imani (Mwa. 12-50 & Ayubu) — 2000 K.K
   2. kutoka (safari ya Kutoka Misri) — 1 445/1290 K.K
   3. kumiliki (Yoshua ) — 1400/1250 K.K.
   4. ufalme ulioungana (Sauli, Daudi, Suleimani) — 1000 K.K.
   5. ufalme uliogawanyika (Rehoboamu-Yeroboamu I) — 922 K.K.
   6. Anguko la Samaria (Israeli) — 722 K.K
   7. anguko la Yerusalemu (Yuda) — 586 K.K.
   8. tamko la Kipro (Uajemi) — 538 K.K.
   9. hekalu la pili — 516 K.K
   10. ufungaji wa Agano la Kale (Malaki) — 430 K.K.


C. Maadui wakubwa wa Watu wa Mungu:
   1. Misri
   2. Kanaani
   3. Filistia
   4. Shamu
   5. Ashuru
   6. Babeli
   7. Uajemi
   8. Uyunani
   9. Rumi

D. Wafalme katika kalenda ya matukio:
   1. Ufalme ulioungana
      a. Sauli


   b. Daudi
   c. Suleimani
2. Israeli
   a. Yeroboamu I
   b. Ahabu
   c. Yeroboamu II
   d. Hoshea
3. Yuda
   a. Rehoboamu
   b. Uzia
   c. Hezekia
   d. Manase
   e. Yosia
   f. Yehoakimu
   g. Yehoakini (miezi 3 )
   h. Zedekia
   i. Gedilia (Mtawala wa Uajemi)
   j. Yehoahazi (miezi 3)
4. Uajemi
   a. Koreshi II (550-530 K.K)
   b. Cambyses (530-522 K.K.)
   c. Dario I (522-486 K.K.)
   d. Ahausuero I (486-465 K.K)
   e. Artashtaza I (465-424 K.K.)
5. Angalia orodha kamili ya wafalme wa Yuda na Israeli pamoja na wafalme wa Ashuru, Babeli na Uyunani mwishoni mwa 1 & 2 Wafalme.



MALAKI
ARTAXERXES I (P)
XERXES I – AHASUERO (P)
EZRA 7-10
NEH.
ESTA
10
UKUTA WA YERUSALEMU – NEHEMIA
KURUDI MARA YA TATU – EZRA
9
UAJEMI
DARIO I (P)
CAMBECE II (P)
KORESHI II (P)
BELSHAZA (B)
NABONIDA (B)
OBADIA
YOELI
HAGAI
ZAKARIA
EZRA 1-6
8
KURUDI MARA YA PILI – ZERUBABELI
KURUDI MARA YA KWANZA – SHESHBAZA
KURIMBILIA
UHAMISHONI
BABELI
NEBUKADREZA (B)
NABOPOLASA (B)
YEREMIA
EZEKIELI
DANIELI
NAHUMU
HABAKUKI
SEFANIA
h i j k l m n o
1 & 2 WAFALME
2 MAMBO YA NYAKATI
P – GEDALIA (P)
O – ZEDEKIA (J)
n – YEHOAKINI (J)
m – YEHOAKIMU (J)
L – YEHOAHAZI (J)
k – YOSIA (P)
j – MANASE (J)
i – HEZEKIA (J)
h – UZIA (J)
g – YEROBOAMU II (I)
ASHURU
ASUR-BANI-PALI (A)
ESAR-HADONI (A)
SENAKERIBU (A)
SAGONI II (A)
YONA
SHALMANESA V (A)
TIGRATH-PILESERI III (A)
AMOSI
HOSEA
6
g
ISAYA
MIKA
ELIYA
ELISHA
e
f
ISRAELI
YUDA
5
4
f – AHABU (I)
e – YEROBOAMU I (I)
d – REHOBOAMU (J)
c – SULEIMANI (UM)
b – DAUDI (UM)
a – SAULI (UM)
SHAMU
FILISTIA
KANAANI
MISRI
Law. Kumb. Kut. Hes.
Yoshua
Waamuzi
1 & 2 SAMWELI
3
1 MAMBO YA NYAKATI
2
Mwa. 12-50
1
AYUBU
MWANZO 1-11
MNARA WA BABELI (4)
GHARIKA YA NUHU (3)
ANGUKO LA MWANADAMU (2)
UUMBAJI (1)
DR. BOB UTLEY
BIBLE LESSONS INT'L 96

# NJIA ZA MAJI





**MASHARIKI YA KARIBU YA KALE**


MATAIFA
WAHITI
UMEDI-UAJEMI
ASHURU
KITIMU
FOENIKE
SHAMU
ELAMU
BABELI
ISRAELI
FILISTIA
AMMONI
MOABU
YUDA
ARABUNI
EDOMU
MISRI
MIDIANI
KAS
MAGH
MASH
KUS
MASHARIKI YA
KARIBU
YA KALE



MIJI MIKUU
MILIMA
KAS
MAGH
MASH
KUS
MASHARIKI YA KARIBU YA KALE


MIJI MINGINE
2.
3.
4.
5.
6.
7.
8.
9.
10.
1.
KAS
MAGH
MASH
KUS
MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE

# UTANGULIZI WA KITABU CHA MWANZO

I. JINA LA KITABU
   A. Katika Kiebrania (MT) hili ni neno la kwanza la kitabu, *Bereshith*, "hapo mwanzo" au "kwa njia ya mwanzo."

   B. Kutokana Tafsiri ya Maandiko ya Kale ya Kiyunani hili ni "Mwanzo" ambalo humaanisha "mwanzo" au "asili" ambalo limechukuliwa kutoka 2:4a. Yumkini huu ni ufunguo wa mwandishi "tungo-muhtasari" au kwa ulinganifu wa kuhusianisha na wasifu tofauti wa pamoja kama waandishi wa Babeli walivyofanya. Msingi wa muhtasari wa kifungu unaonekana nyuma zaidi kuliko mbele.

II. URASIMISHAJI
   A. Hii ni sehemu ya kwanza ya sheria ya Kiebrania inayoitwa "Torati" au "mafundisho" au "sheria."

   B. Hii ni sehemu ya tafsiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani yanayofahamika kama vitabu vitano vya Musa (magombo matano).

   C. Wakati mwingine huitwa "Vitabu Vitano vya Musa" kwa kiingereza.

   D. Mwanzo-Kumbukumbu la Torati inahusiana moja kwa moja na uumbaji kupitia maisha ya Musa.

III. AINA YA UWASILISHAJI – Kitabu cha Mwanzo kimsingi ni Ki-theolojia, simulizi ya Kihistoria lakini pia inahusisha aina nyingine za aina za kifasihi.
   A. Ushairi, mfano, 2:23; 4:23 (huenda 1-2)

   B. Unabii, mfano, 3:15; 49:1 na kuendelea (pia wa ki-ushairi)

IV. UANDISHI
   A. Biblia yenyewe haimtaji mwandishi. Kitabu cha Mwanzo hakina vipengele vya "mimi" kama ilivyo Ezra, Nehemia au sehemu ya "sisi" kama ilivyo Matendo ya Mitume.

   B. Utamaduni wa Kiyahudi:
      1. Waandishi wa Kale wa Kiyahudi wanasema Musa aliandika kitabu hiki:
         a. Ben Sirah "Ecclesiasticus" 24:23, aliandika yapata mwaka wa 185 K.K.
         b. Baba Bathra 14b, Sehemu ya Kitabu cha Maadili na Sheria za Kiyahudi
         c. Philo wa Iskandria, Misri, mwanafalsafa wa Kiyahudi, aliandika mara tu kabla ya huduma ya Yesu
         d. Flavius Josephus, mwana historia wa Kiyahudi, aliandika mara tu baada ya huduma ya Yesu.
      2. Torati ni moja ya muunganiko wa mambo ya kihistoria. Baada ya kitabu cha Mwanzo kila kitabu kinaanza na shukurani "na" (isipokuwa kitabu cha Hesabu).
      3. Huu ulikuwa ni ufunuo kwa Musa
         a. Musa anasemekanaa kukiandika:
            (1) Kutoka 17:14
            (2) Kutoka 24:4, 7

(3) Kutoka 34:27, 28
(4) Hesabu 33:2
(5) Kumbukumbu la Torati 31:9, 22, 24-26

b. Mungu inasemekana aliongea kupitia kwa Musa:
(1) Kumb. 5:4-5, 22
(2) Kumb. 6:1
(3) Kumb. 10:1

c. Musa inasemekana aliongea maneno ya Torati kwa watu:
(1) Kumbukumbu la Torati 1:1, 3
(2) Kumbukumbu la Torati 5:1
(3) Kumbukumbu la Torati 27:1
(4) Kumbukumbu la Torati 29:2
(5) Kumbukumbu la Torati 31:1, 30
(6) Kumbukumbu la Torati 32:44
(7) Kumbukumbu la Torati 33:1

4. Waandishi wa Agano la kale wanamsifia Musa:
   a. Yoshua 8:31
   b. II Wafalme 14:6
   c. Ezra 6:18
   d. Nehemia 8:1; 13:1-2
   e. II Mambo ya Nyakati 25:4; 34:12; 35:12
   f. Danieli 9:11
   g. Malaki 4:4

C. Utamaduni wa Mkristo
1. Yesu anasimulia dondoo kutoka katika Torati ya Musa:
   a. Mathayo 8:4; 19:8
   b. Marko 1:44; 7:10; 10:5; 12:26
   c. Luka 5:14; 16:31; 20:37; 24:27, 44
   d. Yohana 5:46-47; 7:19, 23
2. Baadhi ya waandishi wa Agano Jipya wanasimulia dondoo kutoka katika Torati ya Musa:
   a. Luka 2:22
   b. Matendo ya Mitume 3:22; 13:39; 15:1, 15-21; 26:22; 28:23
   c. Warumi 10:5, 19
   d. I Wakorintho 9:9
   e. II Wakorintho 3:15
   f. Waebrania 10:28
   g. Ufunuo 15:3
3. Makasisi wa kanisa la kale wanaukubali uandishi wa Musa. Ireneaus, Clement wa Iskandria, Origen na Tertullian wote walikuwa na maswali juu uhusiano wa Musa na kanuni za sasa za muundo wa kitabu cha Mwanzo.

D. Uanazuoni wa kisasa
1. Kuna uwazi wa baadhi ya wahariri wa Torati yawezekana kufanya kazi za kale zifahamike zaidi kwa wasomaji wa sasa):

a. Mwanzo 12:6; 13:7; 14:14; 21:34; 32:32; 36:31; 47:11
b. Kutoka 11:3; 16:36
c. Hesabu 12:3; 13:22; 15:22-23; 21:14-15; 32:33 na kuendelea
d. Kumbukumbu la Torati 3:14; 34:6
e. Waandishi wa kale walifundishwa elimu ya juu. Mbinu zao zilitofautiana nchi na nchi:
   (1) Katika Mesopotamia hawa walikuwa makini sana hawakubadili cho chote, na hata kuangalia kazi zao kwa usahihi. Hapa ni tanbihi ya kale ya kiuandishi ya Sumeria, ("kazi imekamilika toka mwanzo hata mwisho, imekwisha nakiriwa, kufanywa bora zaidi, linganisha, na kuthibitishwa kwa ishara na ishara" tangu 1400 K.K.)
   (2) katika Misri nakala huru ya andiko la kale iliyosahihishwa kwa kufanywa upya kwao kwa ajili viongozi wa kisasa. Waandishi katika Qumran wanafuata mtizamo huu.

2. Wanazuoni wa karne ya 19 wanatoa nadharia kwamba Torati ni mchanganyiko wa maelezo yanayotokana na vyanzo vingi kuhusiana na kipindi cha wakati kilicho kipana (Graft-Wellhausen). Hili lilijikita juu ya:
   a. majina tofauti ya Mungu,
   b. jozi dhahili ya ufanano katika andiko,
   c. muundo wa mambo,
   d. theolojia ya maelezo.
3. Vyanzo vya kudhaniwa na tarehe:
   a. Chanzo J (kimetumia YHWH) - 950 K.K.
   b. Chanzo E (kimetumia Elohim) - 850 K.K.
   c. JE imeunganishwa pamoja - 750 K.K.
   d. Chanzo D ("kitabu cha sheria," 2 Fal. 22:8, kilivumbuliwa wakati wa matengenezo ya Yosia ambapo kufanywa upya kwa Hekalu kulikuwa kisio la kitabu cha Kumbukumbu la Torati, kiliandikwa na kuhani asiyefahamika wakati Yosia akimsaidia matengenezo.) - 621 K.K.
   e. Chanzo P (vifaa vya kikuhani hasa desturi na taratibu) - 400 K.K.
   f. Kuna uwazi dhahiri wa mhariri mwingine katika Torati. Wayahudi wanatetea kwamba ilikuwa:
      (1) Kuhani Mkuu wakati za kuandika,
      (2) Yeremia Nabii,
      (3) Ezra Mwandishi - IV Esdras anasema aliandika tena kwa sababu yale ya awali yaliharibiwa wakati wa kuangamizwa kwa Yerusalemu mwaka wa 586 K.K.
   g. Hata hivyo, nadharia ya J. E. D. P. inasema zaidi juu ya nadharia zetu za kisasa na jamii zaidi kuliko ushahidi kutoka katika Torati (R.K. Harrison, *Introduction to the Old Testament,* kr. 495-541 na *Tyndale's Commentaries* "Leviticus", kr. 15-25).
   h. Sifa ya fasihi ya Kiebrania
      (1) Jozi za kufanana, kama Mwa. 1 na 2, zimezoeleka katika Kiebrania. Mara nyingi maelezo ujumla hutolewa na kufuatiwa na jambo maalumu. Yumkini hii ikawa ni njia ya kuusisitiza ukweli au kusaidia ukumbusho wa Unenaji.
      (2) Waalimu wa sheria wa kale wanasema majina makuu ya Mungu yaliyozoeleka yana maana Kithiolojia:
         a) YHWH – jina la Uungu kwa ajili ya maagano kama anavyohusiana katika Israeli kama Mwokozi na Mkombozi (kama vile Zab. 103).
         b) Elohim – Uungu kama Muumbaji, Mtoaji, na Mhimili wa maisha yote duniani (kama vile Zab. 104).

(3) Imezoeleka kwenye fasihi isiyo ya kibiblia ya Mashariki ya Karibu kwa muundo mbalimbali na msamiati unaojitokeza kwenye kazi ya fasihi iliyoungana (Harrison, kr. 522-526).

E. Ushahidi kutokana na maelezo ya fasihi ya Mashariki ya Karibu ya Kale maelezo unadokeza kwamba Musa alitumia maelezo ya kikabari au mtindo wa fasihi simulizi ya Mesopotamia kuandika kitabu cha Mwanzo. Hii sio njia ya kumaanisha dokezo la kupunguza uvuvio lakini ni kujaribu kuelezea tukio la kifasihi la kitabu cha Mwanzo. Kwa kuanza katika Mwa. 37 alama ya ushawishi wa mtindo wa Kimisri, muundo na msamiati unaonyesha ishara kwa Musa kutumia labda utoaji wa fasihi au mapokeo ya fasihi simulizi kutoka kwa Waisraeli wakiwa Misri. Muundo mzima wa elimu ya Musa ulikuwa ni wa Kimisri! Sura ya kweli ya fasihi ya vitabu vitano vya Musa sio dhahili. Ninaamini kwamba Musa ni mtungaji na mwandishi mkubwa wa Vitabu Vitano vya Musa, ingawa alitumia waandishi na/au kuandika na mapokeo ya fasihi simulizi. Kihistoria na kwa uaminifu wa vitabu hivi vichache vya awali vya Agano la Kale ni dhahili.

V. TAREHE

A. Kitabu cha Mwanzo kinafunika nyakati kutoka uumbaji wa ulimwengu kwa familia ya Ibrahimu. Inawezekana kuweka tarehe ya maisha ya Ibrahimu kutoka fasihi ya kiulimwengu ya nyakati. Tarehe inaweza kuleta karibu 2000 K.K., millennia ya pili K.K. Msingi wa hii ni:
   1. baba kutenda kama kuhani katika familia (kama Ayubu),
   2. maisha yalikuwa ya kuhama hama kufuata malisho na makundi ya mifugo,
   3. uhamaji wa watu wakati wa kipindi hiki.

B. Matukio ya awali ya Mwa. 1-11 ni kweli matukio ya “kihistoria” (inawezekana “matukio ya kihistoria”) lakini Isiyobadilika kwa maarifa yanayopatikana sasa.

C. Ni lazima ikumbukwe pale tunapojifunza kitabu cha Mwanzo kwamba matukio ya kihistoria yameandikwa na Musa ambaye aliwaongoza watu wa Mungu kutoka Misri: (1) 1445 K.K., iliyosisitizwa kwenye I Wafalme 6:1; au (2) 1290 K.K., iliyosisitizwa kwenye akiolojia. Hivyo basi, kama kwa mapokeo ya fasihi simulizi, hakifahamiki chanzo cha uandishi au kulenga ufunuo wa ki-Uungu, Musa anaandika , " jinsi gani yote yalivyoanza" na "kwa nini."

VI. VYANZO VYA KUTHIBITISHA MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. Vitabu vingine vya Kibiblia
   1. Uumbaji - Zaburi 8, 19, 50 & 104
   2. Wakati wa Ibrahimu – Ayubu

B. Vyanzo vya akiolojia ya ulimwengu
   1. Ya awali kabisa yenye kufanana inayofahamika ya mpangilio wa desturi wa kitabu cha Mwanzo 1-11 ni Ebla vibao vya kikabari kutoka Kusini Mwa Shamu yapata mwaka 2500 K.K., viliandikwa kwa ki-Akkadia.
   2. Uumbaji
      a. Jambo la Ukaribu wa maelezo ya ki-Mesopotamia yenye kuhusika na uumbaji, *Enuma Elish*, tangu yapata mwaka 1900-1700 K.K., yalipatikana katika maktaba ya Ashurbanipal huko

Ninawi na sehemu zingine kadhaa. Kuna vibao saba vya kikabari vilivyoandikwa kwa ki-Akkadia vyenye kuelezea juu ya uumbaji wa Marduk.

(1) Hawa miungu, *Apsu* (maji baridi-mwanaume) na *Tiamat* (maji bahari-mwanamke) hawakuwa na utiifu, watoto wenye makelele. Miungu hawa wawili wanajaribu kuinyamazisha miungu midogo.

(2) Mojawapo wa miungu ya mtoto, *Marduk*, alisaidiwa kumshinda *Tiamat*. Huyu aliumba dunia kutokana na mwili wake.

(3) *Marduk* aliumba mwanadamu kutokana na kumshinda mungu mwingine, *Kingu*, ambae alikuwa ni mume wa *Tiamat* baada ya kifo cha *Apsu*. Mwanadamu anatokana na damu ya *Kingu*.

(4) *Marduk* alikuwa mkuu wa hekalu la miungu yote ya Babeli.

b. "Mhuri wa uumbaji" ni kibao cha kikabari ambacho kina picha ya mwanaume na mwanamke wakiwa uchi pembeni mwa mti wa matunda na nyoka aliyejizonga kwenye shina la mti na akiwa juu ya bega la mwanamke kama vile anaongea naye.

3. Uumbaji na Gharika - "*The Atrahasis Epic*" ina kumbukumbu za uasi wa miungu wadogo kwa sababu ya kazi zaidi na uumbaji wa wanadamu wawili wawili saba ili kutekeleza wajibu wa hii miungu midogo. Kwa sababu ya: (1) wingi wa watu zaidi, na (2) makelele. Mahitaji ya mwanadamu yalipungua kwa tauni, ukame mara mbili na hatimaye gharika, iliyopangwa na *Enlil*. Matukio haya makuu yanaonekana kwa amri ile ile kwenye Mwa. 1-8. Kikabari hiki kinapatana tangu wakati ule ule kama *Enuma Elish* na *Gilgamesh Epic*, tangu mwaka 1900-1700 K.K. Yote ni kwenye Akkadia.

4. Gharika ya Nuhu

a. Kibao cha Sumeria kutoka Nippur, kiitwacho *Eridu Genesis*, tangu yapata mwaka 1600 K.K., kinaeleza juu ya *Zivsudra* na gharika inayokuja.

(1) *Enka*, mungu wa maji, alionya gharika inayokuja.

(2) *Zivsudra*, kuhani-mfalme, aliokolewa katika merikebu kubwa.

(3) Gharika ilidumu kwa siku saba.

(4) *Zivsudra* alifungua dirisha la merikebu na kuwaachilia ndege kadhaa ili kuona kama nchi kavu imejitokeza.

(5) Pia alitoa sadaka ya kuteketezwa ya ng'ombe dume na kondoo alipotoka ndani ya merikebu.

b. Mchanganyo wa gharika ya Babeli kutoka katika hadithi nne za Sumeria, unaofahamika kama *Gilgamesh Epic* kiasili tangu yapata miaka 2500-2400 K.K., ingawa muundo wa mchanganyo ulikuwa wa kikabari -Akkadia, ni baadae zaidi. Huu unazungumza juu ya mkombozi dhidi ya gharika, *Utnapishtim*, aliyemwambia *Gilgamesh*, mfalme wa *Uruk* jinsi atakavyoepuka gharika kuu na alipewa uzima wa milele.

(1) *Ea*, mungu maji, alionya juu ya kuja kwa gharika na kumwambia *Utnapishtim* (muundo wa Babeli wa *Zivsudra*) kutengeneza merikebu.

(2) *Utnapishtim* na familia yake, pamoja na miti ya dawa iliyochaguliwa, waliokoka na gharika.

(3) gharika ilidumu kwa siku saba.

(4) merikebu ikaja ikatua kwenye Mlima Nisir, kaskazinimashariki mwa Uajemi.

(5) alituma nje ndege aina tatu tofauti kuona kama nchi kavu bado imejitokeza.

5. Fasihi ya Mesopotamia ambayo inaelezea gharika ya kale kwamba imechorwa kutoka katika chanzo kile kile. Majina mara nyingi yamebadilika lakini dhamira ni ile ile. Na mfano ni kwamba *Zivsudra, Atrahasis* na *Utnapishtim* wote ni wafalme wanadamu wale wale.
6. Mfanano wa kihistoria wa matukio ya awali ya kitabu cha Mwanzo yanaweza kuelezewa katika nuru ya kabla ya kutawanyika mwanadamu (Mwa. 10-11) maarifa na uzoefu wa Mungu. Kiini hiki cha kweli cha kumbukumbu ya kihistoria kilichofafanuliwa kwa undani na kubuniwa katika mambo ya gharika ya leo iliyozoeleka ulimwenguni pote. Vile vile pia inaweza kusema juu ya: uumbaji (Mwa.1-2) na mwanadamu na muunganiko wa kimalaika (Mwanzo 6).
7. Siku ya mababa wa imani (shaba ya kati)
    a. Vibao vya Mari-kikabari halali (desturi ya Waamoni) na maandiko binafsi yaliyoandikwa kwa Akkadia tangu yapata mwaka 1700 K.K.
    b. Vibao vya Nuzi – kikabari vina maelezo ya familia Fulani (desturi ya Horite au Hurrian) yameandikwa kwa Akkadia kutoka maili 100 kusini mashariki mwa Ninawi yapata miaka 1500-1300 K.K. ina kumbukumbu ya familia na utaratibu za kibiashara. Kwa mifano maalumu zaidi, tazama Walton, kr. 52-58.
    c. Vibao vya Alalak - maandiko ya kikabari kutoka kaskazini mwa Shamu yapata mwaka wa 2000 K.K.
    d. baadhi ya majina yamepatika kwenye kitabu cha Mwanzo yametajwa kama majina ya sehemu kwenye Vibao vya Mari: Serug, Peleg, Tera, Nahor. Majina mengine ya kibiblia pia yamezoeleka: Ibrahamu, Isaka, Yacobo, Labani na Yusufu.
8. "Uhusiano wa kujifunza uandishi wa historia unaonyesha kwamba, pamoja na Wahiti, Wayahudi wa kale walikuwa waangalifu zaidi, wenye malengo na kuwajibika kuweka kumbukumbu za historia ya mashariki ya karibu," R. K Harrison katika *Biblical Criticism*, uk 5.
9. Elimu ya kale inathibitisha kuwa na msaada katika kuimarisha historia ya Biblia. Hata hivyo, neno la onyo ni muhimu. Elimu ya kale sio mwongozo kabisa wa kuaminika kwa sababu ya:
    a. mbinu dhaifu kwenye uchimbuaji wa awali,
    b. upendeleo mbalimbali wa tafsiri zilizobuniwa kwamba zimepatikana,
    c. haikubaliani na utaratibu wa kupanga miaka ya Mashariki ya Karibu Kale ya (ingawa mmoja anaweza kufanikiwa kutoka kwenye mzingo wa mti).

C. Maelezo ya uumbaji wa Misri yanaweza kupatikana kwenye John H. Walton, *Ancient Israelite Literature in Its Cultural Context*. Iendayo kwa kasi kubwa, MI: Zondervan, 1990. kr. 23-34, 32-34.
1. Katika fasihi ya ki-Misri uumbaji huanza na isiyo na umbo, machafuko, maji ya kale. Uumbaji ulikuwa unaonekana kama umbo linalojitokeza nje ya maji yenye machafuko.
2. Katika fasihi ya ki-Misri kutoka Memphis, uumbaji ulitokea kwa kutamkwa neno na Ptah.

D. Anwani za makundi ya kiinjili juu ya kosmolojia:
1. Taasisi ya Utafiti wa Uumbaji (Dunia Changa)
   S. L. P 2667
   El Cajon, CA 92021-0667
2. Sababu za Kuamini (Dunia Nzee)
   S. L. P 5978
   Pasadena, CA 91117

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI (MUKTADHA)

A. Muhtasari wa msingi wa Musa kutumia tungo "kizazi cha" (*toledoth*):
   1. asili ya mbinguni & ulimwenguni, 1:1-2:3
   2. asili ya ubinadamu, 2:4-4:26
   3. kizazi cha Adamu, 5:1-6:8
   4. kizazi cha Nuhu, 6:9-9:17
   5. vizazi vya wana wa Nuhu, 10:1-11:9
   6. vizazi vya Shemu, 11:10-26
   7. vizazi vya Tera (Ibrahimu), 11:27-25:11
   8. vizazi vya Ishmaeli, 25:12-18
   9. vizazi vya Isaka, 25:19-35:29
   10. vizazi vya Esau, 36:1-8
   11. vizazi vya wana wa Esau, 36:9-43
   12. vizazi vya Yakobo, 37:1-50:26 (#1-11 ina historia ya nyuma ya fasihi ya Mesopotamia lakini #12 ina asili ya fasihi ya Misri.)

B. Ainisho la kimakusudi:
   1. uumbaji kwa ajili ya mwanadamu na wa mwanadamu, 1-2
   2. ubinadamu na anguko la uumbaji, 3:1-11:26
   3. mwanadamu kwa ajili ya watu wote (3:15), 12-50
      a. Ibrahimu (12:1-3), 11:27-23:20
      b. Isaka, 24:1-26:35
      c. Yakobo, 27:1-36:4
         (1) Yuda (uzao wa Masihi)
         (2) Yusufu (urithi wa nchi mara mbili), 37:1-50:26

VIII. KWELI KUU

A. Ni kwa namna gani yote yalianza?
   1. Mungu (1-2). Mtazamo wa Biblia ulimwenguni sio imani ya kuabudu miungu wengi lakini ni katika kuamini Mungu mmoja. Hailengi "kwa namna gani" uumbaji lakini katika "nani." Ilikuwa ya pekee zaidi kwenye nyakati zake.
   2. Mungu anataka ushirika. Uumbaji ni hatua pekee kwa ajili ya Mungu kuwa na ushirika na mwanadamu.
   3. Hakuna uwezekano wa kuifahamu Biblia iliyobakia pasipo kitabu cha Mwanzo 1-3 na 12.
   4. Mwanadamu ni lazima apokee kwa imani ili kuyafahamu ni nini mapenzi ya Mungu (Mwa 15:6 na Rum.4)

B. Ni kwa nini dunia ni ovu na isiyo na haki? Ilikuwa “njema sana" (1:31), lakini mwanadamu alitenda dhambi (3). Matokeo ya kutisha ni dhahili:
   1. Kaini alimuua Abeli, (4)
   2. kisasi cha Lameki (4:23)
   3. uovu wa mwanadamu, (6:5,11-12; 8:21)
   4. ulevi wa Nuhu (9)
   5. mnara wa Babeli, (11)
   6. kuamini miungu mingine ya Uri

C. Ni kwa namna gani Mungu anaenda kuimarisha?
   1. Masihi atakuja (3:15)
   2. Mungu anamuita mmoja ili kuita wote (Mwa. 12:1-3 & Kut. 19:5-6)
   3. Mungu yuko tayari kutenda kazi na mwanadamu aliyeanguka (Adamu, Hawa, Kaini, Nuhu, Ibrahimu, Wayahudi na wa Mataifa) kwa neema yake njema:
      a. Ahadi
      b. maagano (yasiyo amrishi na yaliyo amrishi)
      c. sadaka
      d. kuabudu

IX. MANENO NA/AU TUNGO NA WATU WA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

A. Misamiati na Tungo
   1. "Mungu akasema..." 1:3,6,9,14,20,24 (toleo la NASB na NIV)
   2. "Na tumfanye..." 1:26; 3:22; 11:7 (NASB na NIV)
   3. "Kwa sura yetu" 1:26,27; 5:1,3; 9:6 (NASB na NIV)
   4. "Bwana Mungu akitembea" (elimu ya binadamu) 3:8 (NASB na NIV)
   5. Nefili 6:4 (NASB na NIV)
   6. Agano 6:18; 9:9-17 (NASB na NIV)
   7. "Ibrahimu alimwamini BWANA; naye akamhesabia jambo hili kuwa haki 15:6 (NIV “Abramu alimwamini Bwana naye akamhesabia haki”)
   8. Wema (*hesed*) 24:12,27; 32:10 (NIV, “fadhila”)
   9. Nyumba ya waabudu sanamu (*teraphim*) 31:19,30,34 (NIV, “miungu ya ndani ya nyumba”)
   10. Utabiri 44:5 (NASB na NIV)

B. Watu wa kuwatambua kwa muhtasari
   1. Sethi 4:25
   2. Henoko, 5:21-24
   3. Methusela, 5:22, 25-27
   4. Shemu, 9:18; 10:27-31
   5. Kanaani, 9:20-27
   6. Nimrodi, 10:8-10
   7. Tera, 11:24-32
   8. Lutu, 11:31
   9. Ibrahimu, 12:18
   10. Melkizedeki, 14:18
   11. Hagari, 16:1
   12. Ishmaeli, 15:15; 25:12-19
   13. Isaka, 21:3
   14. Labani, 24:29
   15. Ketura, 25:1
   16. Yakobo (Israeli), 25:26; 32:28
   17. Dina, 30:21
   18. Potifa, 37:36
   19. Tamari, 38
   20. Manase & Efraimu, 41:51,52

X. MAENEO YA KI-RAMANI

A. Ramani ya awali - Mwanzo 1-11 (kwa tarakimu)
   1. Bustani ya Edeni, 2:8
   2. Mto Hidekeli, 2:14
   3. Mto Frati, 2:14
   4. Milima ya Ararati, 8:4
   5. Shinari, 10:10; 11:2
   6. Babeli, 10:10; 11:9
   7. Ninawi, 10:12
   8. Myebusi, 10:16
   9. Sodoma, 10:19; 13:10
   10. Uri ya Wakaldayo, 11:28
   11. Harani, 11:31-32

B. Ramani ya pili ya Mwanzo 12-50 (kwa tarakimu)

1. Shekemu, 12:6; 33:18
2. Betheli, 12:8; 13:3; 35:6
3. Negevu, 12:9; 13:1
4. Mto Yordani, 13:10-11
5. Hebroni, 13:18; 23:2
6. Bahari ya chumvi, 14:3
7. Kadesh Barnea,14:7; 16:14
8. Dameski, 14:15
9. Salemu, 14:18
10. Mto wa Misri, 15:18
11. Jangwa la Shuri, 16:7
12. Moabu, 19:37
13. Waamoni, 19:38
14. Beer-sheba, 21:14; 26:33
15. Nchi ya Wafilisti, 21:32
16. Jangwa la Parani, 21:21
17. Nchi ya Moria, 22:2
18. Aramu, 24:10
19. Edomu, 25:30; 36:1;8-9,19
20. Mto Yaboki, 32:22
21. Betlehemu, 35:19
22. Nchi ya Gosheni, 45:10; 46:34

## XI. MASWALI YA KIMAUDHUI YA MWANAFUNZI

MASWALI KATIKA KITABU CHA MWANZO 1-11


1. Je, Biblia imejadili asili ya Mungu?
2. Je, Biblia inapingana na sayansi juu ya uumbaji?
3. Ni kwa namna gani Mwanzo 1 inasimulia maelezo ya uumbaji mwingine wa mashariki ya karibu?
4. Elezea maneno *fiat* na *ex nihilo*.
5. Kwa nini kuna tofauti mbili za majina ya uungu kwenye sura ya. 1 na 2?
6. Je, kuna maelezo tofauti mawili ya uumbaji wa mwanadamu?
7. Je, inamaanisha nini kwamba mwanaume na mwanamke wameumbwa kwa sura ya Mungu?
8. Kwa nini wingi umetumika katika uhusiano wa Mungu mmoja? 1:26, 27; 3:22; 11:7
9. Kwa nini sura ya 3 ni ya muhimu sana kwenye ufahamu wa Biblia iliyobakia?
10. Je, wanyama waliongea (3:1) kuthibitisha maelezo haya ni hadithi ya kubuniwa?
11. Kwa nini 3:15 ni ya muhimu sana?
12. Ni kwa namna gani 3:16 inatumika katika maisha ya kisasa?
13. Je, kulikuwa na miti maalumu miwili au mmoja kwenye bustani ya Edeni?
14. Taja mafanikio kwenye jamii ambayo ilitokana na uzao wa Kaini, 4:16-24.
15. Ni nini lilikuwa kusudi la Gharika?
16. Ni nini lilikuwa kusudi la mwanadamu kujenga mnara wa Babeli?

MASWALI KATIKA KITABU CHA MWANZO 12-50


1. Kuna utofauti gani kati ya maagano ya Nuhu na Ibrahimu?
2. Ni kwa namna gani Agano la Ibrahimu linasimulia kwa wasio Wayahudi?
3. Ni ishara zipi mbili za udhaifu na ukosefu wa imani zinazoonekana kwa Abramu katika sura ya 12?
4. Melkizedeki ni nani na kwa nini Abramu alimpa yeye sehemu ya kumi?
5. Kwa nini 15:12-21 ni ya muhimu sana?
6. Watu hawa watatu ni wakina nani kwenye sura ya 18? (kwa nini na wapi)?
7. Kwa nini Ibrahimu alidanganya kuwa Sara sio mke wake? Je alimdanganya nani?
8. Kwa nini Rebeka na Yakobo walimfanyia hila Isaka? (27)
9. Fafanua ni kwa nini Reubeni, Lawi na Simeoni walikataliwa kuwa uzao wa Masihi? (34 na 49)

10. Elezea ndoto ya Yusufu kwa maneno yako mwenyewe. (37)
11. Kwa nini Yusufu alijifanya kuwa hawatambui ndugu zake?
12. Kwa nini kila mwana wa Yusufu alipata urithi sawa na watoto wengine wa Yakobo?


*Mwanzo 1-11*




Mwanzo 12-50




MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE


MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE
KAS
MAGH
MASH
KUS

# PALESTINA




VIPIMO KATIKA MAILI

# UTANGULIZI WA KITABU CHA KUTOKA

I. JINA LA KITABU

A. Katika kitabu cha Waebrania (MT) hili ni neno la kwanza la kitabu, "na haya ndiyo maneno (majina)."

B. Katika tafsiri ya LXX hili ni neno *ek 'odos* ambalo linamaanisha "pishana" au "kingana."

C. Katika Toleo la Kilatini la Jerome hili ni "kutoka."

II. URASIMISHAJI

A. Hii ni sehemu ya kipengele cha kwanza cha Sheria ya Kiebrania iitwayo "Torati" au "mafundisho" au "Amri."

B. Kipengele hiki kinajulikana kama Vitabu Vitano vya Kwanza vya Biblia (magombo matano) katika LXX.

C. Wakati mwingine hili linaitwa "Vitabu Vitano vya Musa" katika lugha ya Kiingereza.

D. Hili linahusisha maelezo endelevu ya kihistoria yaliyotolewa na Musa kutoka uumbaji kupitia maisha ya Musa, Mwanzo- Kumbukumbu la Torati.

III. AINA YA UWASILISHAJI – Kitabu cha Kutoka kinahusisha aina tatu za namna za uandishi.

A. Masimulizi ya kihistoria, Kut. 1-19; 32-34

B. Ushairi, Kut. 15

C. Viainishi vya Hema la kukutania, Kut. 25-31, na matengenezo yake, 35-40

IV. UANDISHI

A. Torati hii ni moja ya maelezo yaliyounganishwa. Kitabu cha Kutoka kinaanza na kiunganishi "na." Tazama mjadala kwa urefu katika kitabu cha Mwanzo mtandaoni.

B. Kuna maeneo kadhaa katika kitabu cha Kutoka ambayo inasemekana kwamba Musa aliyaandika: 1.17:14; 2. 24:4, 12; 3. 34:27, 28

C. Yoshua 8:31 inainukuu Kutoka 20:25 na kudhani kuwa hiki ni cha Musa. Yesu anainukuu Kut. 20:12,17 na kudhani kuwa ni ya Musa, Mk. 7:10.

V. TAREHE YA KITABU CHA KUTOKA

A. Kumekuwa na maoni ya wasomi ya aina mbili kuhusiana na tarehe ya Kitabu cha Kutoka:

1. Kutokana na I Fal. 6:1, ambayo inasema, miaka "480 kutoka kipindi cha Uhamisho hadi ujenzi wa Hekalu la Suleimani"

   a. Suleimani alianza kutawala mnamo 970 K. K. Hiki kinaelezwa kwa kurejelea mapigano ya *Qarqar* (853 K.K.) kama tarehe fulani ya kuanza.

   b. Hekalu lilijengwa katika mwaka wake wa nne (965 K.K.), na Uhamisho ulijiri yapata miaka 1445/6 K.K.

2. Historia hii ingekifanya kipindi hiki kujiri katika karne ya 18 ya Utawala wa Jamii ya Kimisri.

   a. Utawala wa Farao unaweza kuwa *Thutmose III* (1490-1436 K.K.).

   b. Farao wa kitabu cha Kutoka anaweza kuwa *Amenhotep II* (1436-1407 K.K.).

      (1) Baadhi wanaamini ushahidi unatokana na Yeriko uliojikita katika ukweli kwamba hakuna makubaliano ya kisuluhishi kati ya Yeriko na Misri wakati wa kipindi cha utawala wa *Amenhotep III* (1413-1377 K.K.).

      (2) Maandiko ya *Amarna* yanayaandika makubaliano ya kiusuluhishi yaliyoandikwa katika ondoleo kumhusu *Habiru* kuhusiana na kuitawala nchi ya Kanaani katika utawala wa *Amenhotep III*. Hivyo, kipindi cha uhamisho kilijiri kipindi cha utawala wa *Amenhotep II*.

(3) Kipindi cha Waamuzi si cha muda mrefu ikiwa karne ya 13 ndiyo kipindi cha Uhamisho.

3. Uyamkini wa matatizo haya yanayohusiana na vipindi hivi ni:
    a. Tafsiri ya Maandiko ya Kale ya Kiebrania kwenda Kiyunani (LXX) ina miaka 440 si 480.
    b. Inawezekana kwamba miaka 480 ni uwakilishi wa vizazi 12 vya miaka 40 kila mmoja, hivyo, namba ya uwakilishi.
    c. Kuna vizazi 12 vya makuhani kuanzia kwa Aruni hadi kwa Suleimani (kama vile I Nya. 6), kisha 12 kuanzia kwa Suleimani hadi kufikia Hekalu la Pili. Wayahudi, kama walivyo Wayunani, walikihesabu kizazi hiki kama miaka arobaini. Hivyo, kuna kipindi cha miaka 480 nyuma na mbele (matumizi ya namba za kiishara) (kama vile Bimson's *Redating the Exodus and Conquest*).
4. Kuna maandiko mengine matatu ambayo yanataja tarehe maalumu:
    a. Mwanzo 15:13,16 (kama vile Matendo ya Mitume 7:6), miaka 400 ya utumwa;
    b. Kutoka 12:40-41 (kama vile Gal. 3:17);
        (1) MT – miaka 430 ya ugenini ndani ya Misri
        (2) LXX – miaka 215 ya ugenini ndani ya Misri
    c. Waamuzi 11:26 – miaka 300 kati ya siku za Yefta na mavamizi (inakiunga mkono kipindi cha 1445)
    d. Matendo 13:19, kuhamishwa, kutangatanga na kutawanyishwa – miaka 450
5. Mwandishi wa kitabu cha Wafalme aliyatumia marejeleo maalumu ya kihistoria na hakuzirudia idadi (Edwin Thiele, *A Chronology of the Hebrew Kings*, kr. 83-85.

B. Ushahidi wa kimajaribio kutokana na utafiti wa mambo ya kale unaonekana kulenga tarehe maalum ya maalum ya mwaka 1290 K.K., au karne ya 19 ya Utawala wa Ufalme wa Kimisri.
1. Josefu alikuwa na uwezo wa kumtembelea babaye Farao siku ile ile. Farao wa kwanza mwenyeji ndiye aliyeanza kuyaondoa makao makuu ya Misri kutoka Tebesi na kuyarudisha Bonde la Mto Nile, mahali paitwapo *Avaris/Zoan/Tanis* mahali ambapo palikuwa makao makuu ya zamani ya Hyksos, ambapo palikuwa *Seti I* (1309-1290). Huyu anaweza kuwa Farao yule mtesaji.
    a. Huu unaonyesha kwendana na sehemu mbili za uleweshaji kuhusu Hyksos mtawala wa Misri.
        (1) Astele amekuwepo wakati huu wa Rameses II ampapo hii ni kumbukumbu iliyoasisiwa na Avaris miaka mia nne kabla (1700's K.K. na Wa-Hyksos)
        (2) Unabii wa kitabu cha Mwanzo 15:13 unazungumzia miaka 400 ya mateso.
    b. Hili linamaanisha kwamba kuhimarika kwa nguvu ya Joseph kulikuwa chini ya *Hyksos* (wa Kisemiti) Farao. Utawala mpya wa Kimisri unarejelewa katika Kut. 1:8.
2. Hili *Hykso*, neno la Kimisri lenye maana ya "watawala wa nchi za kigeni," ambao hawakuwa kundi la watawala wa Wasemiti wa Kimisri, waliokuwa chini ya Misri mnamo karne ya 15 na 16 na Himaya zake (1720- 1570 K.K.). Baadhi hutaka kuwahusianisha hawa na kushamiri kwa utawala wa Joseph. Tukiipunguza miaka 430 ya Kut. 12:40 kutoka miaka 1720 K.K., tunakipata kipindi cha miaka 1290 K.K.
3. Mwana wa Seti I alikuwa Ramesesi II (1290-1224). Hili ni jina linalotajwa kama moja ya ghala za miji zilizojengwa na watumwa wa Kiebrania, Kut. 1:11. Pia eneo hili hili lililo ndani ya Misri karibu na Gosheni linaitwa Ramesesi, Mwa. 47:11. *Avaris/Zoan/Tanis* lilijulikana kama "Nyumba ya Ramesesi" kuanzia mwaka 1300- mwaka 1100 K.K.
4. Thutmoses III alijulikana kama mjenzi mkuu, kama alivyokuwa Ramesesi II.
5. Ramesesi II alikuwa na mabinti 47 waliokuwa wakiishi maeneo mbalimbali.
6. Utafiti wa mambo ya kale umeonyesha kwamba miji mingi mikuu ya ki-Kanaani iliyokuwa imezungushiwa kuta (Hazor, Debir, Lachish) iliharibiwa na kujengwa upya kwa haraka mnamo

1250 K.K. Katika kuikubali miaka 38 ya kipindi cha kutangatanga hili linaendana na kipindi cha miaka 1290 K.K.

7. Utafiti wa mambo ya Kale umebaini rejea ya Waisraeli kuishi Kusini mwa Kanaani rejea iliyo katika kumbukumbu ya Stele mrithi wa Ramesesi *Merneptah* (1224-1214 K.K. [kama vile Stele ya Merneptah, aliyopewa mwaka 1220 K.K.]).
8. Miji ya Edomu na Moabu inaonekana kufanywa utambulisho wa taifa lenye nguvu la miaka 1300 K.K. Nchi hizi hazikuwekwa pamoja mnano karne ya 15 (Glueck).
9. Kitabu kilichopewa jina la *Redating the Exodus and Conquest* kilichoandikwa na John J. Bimson, kilichochapishwa na Chuo Kikuu cha Sheffield, 1978, kinaupinga ushahidi wote wa utafiti wa mambo ya kale kuhusiana na uwekaji wa awali wa tarehe halisi ya matukio haya.

VI. UTATANISHI MWINGINE WENYE KUHUSIANA NA KITABU CHA KUTOKA

A. Idadi ya watu walioishi katika kipindi hiki cha Uhamisho iko mashakani
1. Hesabu 1:46; 26:51 inawasilisha kuwa kulikuwa na watu wapatao 600,000 wenye umri ufaao kupigana (umri wa miaka 20-50, kama vile Kut. 38:26). Hivyo, mtu akiwakadiria wanawake, watoto na wazee, idadi ya milioni 1.5 hadi 2.5 inawezekana.
2. Hata hivyo, neno la Kiebrania la elfu, *Eleph*, linaweza kumaanisha:
   a. umoja wa familia au ukoo, Yoshua 22:14; Waamuzi 6:15; I Samueli 23:23, Zek. 9:7
   b. umoja wa kijeshi, Kut. 18:21,25; Kumb. 1:15
   c. elfu halisi, Mwa. 20:16; Kut. 32:28
   d. hili lilitumika kiishara, Mwa. 24:60; Kut. 20:6 (Kumb. 7:9); 34:7; Yer. 32:18
   e. kutokana na Ugaritiki (asili ya lugha ya Kisemiti), konsananti zenye kufanana ni *alluph* ambazo zimamaanisha "mtemi" (kama vile Mwa. 36:15). Neno hili lingemaanisha kwamba kwa Hes. 1:39 kulikuwa na watemi 60 na watu 2700 Kutoka kabila la Dani. Tataizo linakuja pale panapokuwepo idadi dhahiri ya watemi wengi kwa watemi idadi ya watu katika baadhi ya makabila.
   f. Kuna mjadala mzuri katika toleo la NIV Study Bible, uk. 186.
3. Utafiti wa mambo ya kale unabaini kuwa ukubwa wa majeshi ya Misri na Ashuru katika kipindi hiki ulikuwa katika makumi ya maelfu. Baadhi ya vifungu vilivyo katika Yoshua vinaonekana kumaanisha kwamba Israeli alikuwa na jeshi lipatalo 40,000, (kama vile Yos. 4:13; 7:3; 8:3,11,12).

B. Njia zilizo katika Kitabu cha Kutoka zinatatanisha
1. Mahali pa: (1) miji ya Kimisri; (2) vyanzo mbalimbali vya maji; na (3) makambi ya miji ya kale ya miji ya Kiebrania yote haya yanatatanisha.
2. Hili neno "Bahari ya Shamu" kiuhalisia ni *Yam Suph*, ambapo :
   a. inamaanisha, "bahari ya magugumaji" au "bahari ya mafunjo." Hii inaweza kuyarejelea maji ya chumvi, Yona 2:5; I Fal. 9:26 au maji yasiyo ya chumvi, Kut.. 2:3; Isa. 19:26. Kwa mara ya kwanza toleo la LXX lilitafsiri neno hili kama “Bahari ya Shamu,” likifuatiwa na toleo la Kilatini na kisha toleo la King James.
   b. hili liliirejelea “bahari ya kusini” au “bahari iliyo ukingoni (mwa dunia).” Hii ingeweza kuwa imeirejelea Bahari ya Shamu ya sasa, Bahari ya India au Ghuba ya Uajemi.
   c. hili lilikuwa na matumizi kadhaa katika Agano la Kale (kama vile Hes. 33:8,10).
3. Yamkini kuna njia tatu zinazohusisha vyanzo tofauti tofauti vya maji:
   a. Njia ya kaskazini – hii ilikuwa kandokando ya pwani ya Mediterranea, ikifuatisha njia kuu ya wafanya biashara inayojulikana kama "njia ya Wafilisti." Hii ingekuwa njia fupi sana kuifikia

Nchi ya Ahadi. Chanzo cha maji ambacho wangekumbana nacho kingekuwa moja ya vile vyenye kina kifupi, maeneo ya mabwawa yaitwayo: Sirbonis au Ziwa Menzalch. Hata hivyo, yampasa mtu kuielewa Kut. 13:17 ambayo inaonekana kuukanusha uwezekano huu. Pia kuwepo kwa ngome za Kimisri kandokando ya njia hii kuliweka zuio dhidi ya uwezekano huu.

b. Njia ya kati – hii ingeyahusisha maziwa ya kati yaitwayo: (1) "Maziwa Machungu"; (2) "Ziwa Bala"; (3) "Ziwa Timsa." Hii pia ilikuwa ikiufuatisha njia ya msafara huu kupitia jangwa la Shur.

c. Njia ya kusini – hii ingehusisha chanzo kikuu cha maji ya chumvi ambapo kwa sasa tunakiita Bahari ya Shamu. Pia kuna njia ya msafara kutoka eneo hili ambayo iliunganishwa na "Njia Kuu ya Wafalme" (Barabara ya ng'ambo ya Yordani kuelekea Dameski) huko Ezion-Geber.
   (1) Kuzuia huku ni kutokuwepo kwa mafunjo katika chanzo hiki cha maji.
   (2) Kwa kwenda moja kwa moja hii ni kwamba I Fal. 9:26 inasema Ezion-Geber iko juu ya Yam-Suph.
   Hii ingeweza kuwa Ghuba ya Aqaba au sehemu fulani ya Bahari ya Chumvi (kama vile Hes. 21:4; Kumb. 27; Amu. 11:16; Yer. 49:12).

d. Kitabu cha Hesabu 33 kinaonyesha tatizo kwa uwazi. Katika mst. 8a "wakapita katikati ya bahari," kisha mst. 10 wakapanga karibu na "Bahari ya Shamu," chanzo tofauti cha maji.

e. Chanzo maji cho chote kilifungwa, huu ulikuwa muujiza wa Mungu. Israeli ilipewa silaha kutoka kwa askari wa Kimisri waliokufa ambao sehemu zao za miili zilizamishwa majini, muujiza mwingine, Kut. 14:30; 15:4-5.

f. Inawezekana kutokana na maandiko mengine kwamba "hii *yom suph*" haikuonyeshwa katika mchoro, chanzo cha cha maji kilichojificha kilicho huko kusini. Katika maandiko mengine Bahari ya Indi au ghuba ya Bengeli inaitwa "*yom suph*."

4. Eneno mahususi la Mlima Sinai pia linatatanisha
   a. Ikiwa Musa alizungumza kimaandishi na si kwa vielelezo vya siku ya tatu ya safari aliyomuomba Farao (3:18; 5:3; 8:27), huu haukuwa wakati wa kutosha kupata miji ya makumbusho kusini mwa rasi ya Sinai. Hivyo, baadhi ya wasomi wanaukadiria mlima huu kuwa karibu na oasisi ya Kadesh-Barnea.
   b. Mji wa makumbusho huitwao "Yebeli Musa," katika Jangwa la Dhambi, unao mambo kadhaa katika kupendelewa kwake:
      (1) eneo kubwa tambarare kabla ya kuufikia mlima,
      (2) Kumb. 1:2 inasema kuwa ilikuwa safari ya siku kumi na moja kutoka Ml. Sinai hadi Kadesh-Barnea,
      (3) Hili neno "Sinai" si neno la Kiebrania. Hili linaweza kuunganishwa na Jangwa la Dhambi, ambalo lilirejelea kichaka kidogo kilicho jangwani. Jina la Kiebrania la mlima huu ni Horebu (jangwa).
      (4) Ml. Sinai umekuwa mlima wa makumbusho tangu karne ya 4 B.K. Huu uko katika "nchi ya Midiani" ambayo ilichukua eneo kubwa la rasi ya Sinai na Arabia.
      (5) Inaonekana kwamba utafiti wa mambo ya kale umelihakikisha eneo la baadhi ya miji iliyotajwa katika maelezo ya kitabu cha Kutoka (*Elim, Dophkah, Rephidim*) kama wenye kuanzia upande wa magharibi mwa Rasi ya Sinai.

VII. VYANZO VYA UTHIBITISHO WA MAZINGIRA YA KIHISTORIA:

A. Hakuna ushahidi hata kidogo ulioandikwa toka Misri kuhusu kitabu cha Kutoka. Huu si adimu kwa upande wa *YHWH* kuiondoa miungu ya Kimisri moja kwa moja.

B. Kuna baadhi ya mifano ya kumbukumbu ya sheria zinazofanana na *Amri Kumi za Mungu*
   1. Zile *Sheria* za *Lipit-Ishtar* (za Kisumeria), kutoka kwa mfalme wa Isini (1934-1924 K.K.)
   2. Zile *Sheria* za *Eshnunna* (Babeli ya kale), iliyopewa mwaka 1800 K.K. kutoka katika utawala wa Dadusha, mfalme wa Ashnunna
   3. Mkusanyiko wa Sheria za Hammurabi (Babeli ya kale) kutoka kwa mfalme wa Babeli, Hammurabi (1728-1686 K.K.)
   4. Mkusanyiko wa sheria za wafalme wa ki-Hiti Mupsilis I au Hattusilis I, kuanzia mnamo mwaka 1650 K.K.
   5. Mkusanyiko wa sheria za ki-Mesopotamia ambazo kimsingi zinajikita katika sheria za kiraia ambapo sheria za kibiblia kimsingi zinajikita katika dini/sheria za kimadhehebu."...tungeweza kupendekeza upendeleo wa kiraia katika mfumo wa kimadiliko na upendeleo wa kimadhehebu katika sheria ya Kiisraeli..., katika Mesopotamia, makosa ya jinai mwishowe yanatazamiwa katika uhusiano na jamii; ambapo katika Israeli, makosa yote ya jinai mwishowe yanakuwa dhidi ya Mungu." Walton, uk. 80.
   6. Albrect Alt katika *Essays on Old Testament History and Religion*, Oxford, 1966, kr. 81-132, ametambulisha aina mbili za sheria:
      a. za kilaghai, ambapo ni vishazi tegemezi. Hizi zinabainishwa na muundo wa "ikiwa...kisha". Huu haujitokezi katika desturi za kidini au kijamii bali unaeleza zuio la umuhimu.
      b. zilizoimarishwa vema, ambazo hazitumii vishazi tegemezi.
         (1) Kut. 21 na Kumb. 27:15-26 zinatumia nafsi ya tatu na kuihusianisha na mtu, vizuizi maalumu.
         (2) Law. 18:7-17 na Kut. 20/Kumb. 5 zinatumia nafsi ya pili na ni za jumla katika mawanda yake.
      c. sheria za ki-Mesopotamia kimsingi ni za kilaghai ambapo za ki-Israeli kimsingi ni za uimarifu.

C. Kama ulivyo mjadala wa mawazo huru ya kale kwamba Musa hakujua kuandika, utafiti wa mambo ya kale umethibitisha kuwepo kwa alfabeti za kale za ki-Kanaani ambazo zilikuwa zikitumika Misri siku za Musa.
   1. Ulinganifu toka mwaka 1400 K.K umebainiwa kulingana na watumwa wa ki-Semiti katika migodi ya Kimisri iliyoko Sinai (kama vile Albright, BASOR, #110 [1948], uk. 12-13).
   2. Utengefu (ushairi uliotenganishwa ulitumika kuyapokea maandishi) kutoka Bonde la Malkia umebainiwa huko Thebes, Albright, BASOR, #110 (1948), uk. 12.

VIII. VIPENGELE VYA KIFASIHI (MUKTADHA)
A. Maelezo ya Kimuhtasari
   1. Israeli katika Misri, 1-11
   2. Israeli anaiacha Misri, 12-18
   3. Israeli huko Ml. Sinai, 19-40
      a. Sheria za maisha huko Ml. Sinai, 19-24
      b. Sheria za kumiliki huko Ml. Sinai, 25-40
         (1) Usanifu wa Hekalu, 25-31
         (2) Kurudiwa kwa uasi na agano, 32-34
         (3) Kujengwa upya kwa Hekalu, 35-40

B. Mapigo
   1. Haya yalionyesha hukumu ya Mungu juu ya miungu ya Misri. Haya yanaonekana kutokea kwa kipindi cha miezi 18. Haya yanahusisha matukio ya asili, yangali pamoja na:
      a. hukumu ya nguvu
      b. hukumu ya uweza
      c. eneo la nguvu
   2. Maelezo mafupi ya mapigo 10
      a. Nile iligeuka kuwa damu, 7:14-25
      b. vyura, 8:1-15
      c. chawa, vigugunaji, 8:16-19
      d. nzi, 8:20-32
      e. magonjwa juu ya wanyama, 9:1-7
      f. majipu, 9:8-12
      g. mvua ya mawe, 9:13-35
      h. nzige, 10:1-20
      i. giza, 10:21-29
      j. malaika wa kifo, kifo cha mzaliwa wa kwanza, 11:1-8

C. Orodha ya sikukuu/siku ya kufunga ya sura ya 23:
   1. Sabato ya juma 23:3
   2. Pasaka (siku ya 14 Nisan), 23:5; Kutoka 12
   3. Mkate Usiotiwa Chachu (siku ya 15-21 ya Nisan), 23:6-8; Kumb. 16:1-8
   4. Matunda ya Kwanza (siku ya ya 22ya Nisan), 23:9-14
   5. Pentekoste ya Sikukuu ya Majuma (siku 50 baada ya siku ya 21 ya Nisan, siku ya 6 sivan), 23:15-21; Kumb. 16:9-12
   6. Kupiga Baragumu (siku ya Tishri), 23:23-25; Hes. 29:1-6
   7. Siku ya Upatanisho (siku ya 10 Tishri), 23:26-32; Hes. 29:7-11
   8. Sikukuu ya Vibanda (siku ya 15 Tishri), 23:33-44; Hes. 29:12-40; Kumb. 16:13-17

D. Undani wa Muhtasari
   1. tazama R. K. Harrison, *Introduction to the OT*, uk. 560-562
   2. tazama E. J. Young, *An Introduction to the OT*, uk. 63-72
   3. tazama NIV Study Bible, uk. 85-87

IX. KWELI KUU

A. Kipengele hiki kinaendeleza historia inayoanzia katika kaitabu cha Mwanzo. Hiki kinaeleza maendeleo ya nyumba iliyochaguliwa katika taifa lililochaguliwa. Ijapokuwa wanawekwa utumwani humo Misri, hatimaye wataimiliki Nchi ya Ahadi (Mwa. 12:1-3; 15:16).

B. Hiki kinaandika kuhusu sheria ya agano Ml. Sinai (Horebu)
   1. Namna tunavyotakiwa kuishi! (Amri Kumi za Mungu na maongezeko)
   2. Namna tunavyotakiwa kuabudu (Hekalu, makuhani, matukio, wakati, na jadi)
   3. Hii ni “namna ya” kuliongoza Hekalu (Mambo ya Walawi)

C. Hiki kinaeleza matendo makuu ya upendo na huruma ya Mungu kwa Israeli yaliyotabiriwa kwa Ibrahimu, Mwa. 15:16.

D. Tendo la Mungu kumshughulikia linaonyesha ulinganifu kati ya ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu:
   1. Mungu aliufanya moyo wa Farao kuwa mgumu
      a. 7:3, 13
      b. 9:12
      c. 10:1, 20, 27
      d. 11:10
      e. 14:4, 8
   2. Farao aliufanya moyo wake kuwa mgumu
      a. 8:15, 32
      b. 9:34

X. MANENO NA/AU VIFUNGU NA WATU WA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

A. Maneno na Vifungu
   1. Kiti cha kuzalia, 1:16 (NIV, kimeza cha kuzalia)
   2. vua viatu vyako, 3:5 (NASB na NIV)
   3. "tusafiri siku tatu," 3:18; 5:3; 8:27 (NASB na NIV)
   4. "Nitaufanya moyo wako kuwa mgumu," 4:21; 7:3, 13; 9:12, 35; 10:1, 20, 27 (NASB na NIV)
   5. wachawi, 7:11, 22 (NASB na NIV)
   6. asiye na hila, 12:5 (NIV, asiye na dosari)
   7. nguzo ya wingu, 13:21-22 (NASB na NIV)
   8. manabii, 15:20 (NASB na NIV)
   9. mkate (manna), 16:4, 8, 14-15, 31 (NASB na NIV)
   10. ufalme wa makuhani, 19:4-6 (NASB na NIV)
   11. kuangamizwa kabisa (*herem*), 22:20 (NIV, kuharibiwa)
   12. nguzo zilizotengwa, 23:24 (NIV, jiwe lililotengwa)
   13. naivera, 25:7 (NASB na NIV)
   14. kiti cha rehema, 25:17 (NIV, kifuniko cha upatanisho)
   15. *Urimu* na *Thumimu*, 28:30 (NASB na NIV)
   16. Kile kitabu, 32:32-33 (NASB na NIV)
   17. mikate ya Wonysho, 35:13 (NASB na NIV)

B. Watu wa kuwatambua kwa Muhtasari
   1. Wa-Hyksosi, 1:8
   2. malaika wa Bwana, 3:1,4
   3. Mimi Niko (YHWH), 3:14; 6:3 (NIV, Mimi Niko Ambaye Niko)
   4. Reueli, 2:18; Yethro, 3:1;
   5. Finehasi, 6:25
   6. mwangamizaji, 12:23
   7. Nadabu & Abihu, 24:1
   8. Amaleki, 17:8-16
   9. Kerubi, 25:19 18:11-12


XI. MAENEO KWA RAMANI (kwa hesabu)

1. Pithom, 1:11
2. RamesesI, 1:11
3. MidianI, 2:15
4. Ml. Horebu, 3:1
5. Gosheni, 8:22
6. Yam Sufu, 10:19 (NIV, Bahari ya Shamu)
7. Jangwa la Shur
8. Jangwa la Sin
9. Jangwa la Parani
10. Njia ya Bahari (Wafilisti), 13:17
11. Guba ya Agaba


XII. MASWALI YA KI-MAUDHUI KWA MWANAFUNZI

1. Kwa ninmi Farao aliwaogopa Waebrania? 1:7-10
2. Kwa nini watoto wanaume kutupwa mtoni? Kwa nini nyumba ya Farao ilikuwa ikioga mtoni? Kwa nini kubadilika kwa maji ya kulikuwa kwa muhimu sana?
3. Kwa nini Musa alikimbilia Midiani?
4. Kwa nini tendo la Mungu kulifuunua jina lake kwa Musa lilikuwa la muhimu? (3:13-16)
5. Je! 3:22 inasema nini kuhusu mgogoro kati ya *YHWH* na miungu ya Misri?
6. Ni kwa namna gani Kut. 6:3 katika mwangaza wa mwonekano wa *YHWH* katika Mwanzo 4:26?
7. Ni kwa namna gani mapigo yalileta madhara katika eneo la Misri?
8. Je! Mungu ameufanya moyo wa Farao kuwa mgumu ili kuuondoa utashi wake?
9. Nini umuhimu wa kifo cha mzaliwa wa kwanza?
10. Waebrania walizipata wapi silaha zao za kivita?
11. Ni katika njia zipi tendo la Musa lilimfikisha mji wa Yethro. Sura ya 18 inamaanisha kuwa yeye anaamini katika *YHWH*?
12. Nini maana ya Israeli kuwa ufalme wa makuhani?
13. Orodhesha Maneno Kumi.
14. Orodhesha siku za sikukuu za sura ya 23.
15. Chora picha ya Hekalu na samani zake.
16. Je! Ndama wa Dhahabu wa sura ya 32 anaashiria nini?

# KUTOKA



# PALESTINA



# UTANGULIZI WA MAMBO YA WALAWI

I. JINA LA KITABU

A. Katika Andiko la Kiebrania (MT) ni neno la kwanza la kitabu, "Naye (YHWH) akaita."

B. Kitabu cha desturi za Kiyahudi (Mishnah) kilikiita "sheria ya makuhani."

C. Kutoka fasiri ya LXX ni "Kitabu cha Kiyunani."

D. Tafsiri ya Agano la Kale ya Kilatini ya Jerome iliipa jina la"Mambo ya Walawi."

II. URASIMISHAJI

A. Ni sehemu ya kwanza ya Kanoni ya Kiebrania iitwayo "Torati" au "mafundisho" au "Sheria."

B. Sehemu inajulikana kama Vitabu vitano vya Musa (vitabu vitano) katika LXX.

C. Mara nyingine inaitwa "Vitabu Vitano vya Musa" kwa lugha ya kiingereza kilichotafsiriwa.

D. Inajumuisha hadithi inayoendelea ya Musa tokea uumbaji na maisha ya Musa, Mwanzo-Kumbukumbu la Torati.

III. AINA YA UWASILISHAJI - Kitabu zaidi sana ni kuhusu utengenezaji wa sheria, isipokuwa kwa masimulizi ya kihistoria ya sura za 8-10.

IV. UANDISHI -Sura 1:1 inaandaa mara kwa mara utaratibu unaojirudia rudia (mara 35) "YHWH alimwambia Musa." Angalia mjadala wa kina katika uainisho wa Mwanzo.

V. TAREHE - Linganisha Kut. 40:2, 17 pamoja na Hes. 1:1. Hii inaonesha kwamba alipewa Musa na Mungu katika mwezi wa kwanza wa mwaka wa pili baada ya Kutoka. Angalia mjadala wa kina katika uainisho wa Kutoka.

VI. VYANZO VYA UTHIBITISHAJI WA MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. Taratibu za kisheria huko Mesopotamia

1. Sadaka kimsingi ilikuwa ni chakula kinachotolewa kwa mungu. Madhabahu ilikuwa ni meza ya mungu ambapo chakula kilikuwa kikiwekwa. Licha ya madhabahu ilikuwepo chetezo cha uvumba ambayo ilivutia usikivu wa mungu. Kulikuwa hakuna maana ya kiibada katika damu. Mbeba upanga alikata koromeo la mnyama. Chakula kilishirikishwa kati ya miungu, mfalme-kuhani na wahudumu. Mtoa sadaka hakupokea chochote.
2. Hakukuwa na sadaka ya upatanishi.
3. Ugonjwa au maumivu vilikuwa ni adhabu kutoka kwa miungu. Mnyama alileta na kuharibiwa; hii ilifanyika kama mbadala kwa ajili ya mtoaji.
4. Taratibu za Isareli zilikuwa tofauti. Ilionekana kuwa na asili kutokea kwa mtu aliyemrudishia Mungu sehemu ya kazi yake kwa chakula cha lazima (kama vile Mwa. 4:1-4; 8:20-22).

B. Taratibu za sheria huko Kanaani (zinazofanana sana na za Israeli)

1. Vyanzo
   a. simulizi za kibiblia
   b. fasihi za kifoenike
   c. Mbao za Ras Shamra kutoka Ugariti juu ya miungu ya Wakanaani na hadithi za kimiujiza kutokea mnamo mwaka 1400 K.K.
2. Sadaka za Israeli na Kanaani zilikuwa na ufanano sana. Hatahivyo, hakuna msisitizo uliowekwa katika damu za waathirika katika sadaka za Kanaani.

C. Taratibu za Sheria huko Misri
   1. Sadaka zilitolewa lakini hazikusisitizwa
   2. Sadaka hazikuwa muhimu bali mtazamo wa mtoaji ulihesabiwa muhimu
   3. Sadaka zilikusudiwa kusitisha ghadhabu ya miungu
   4. Mtoa sadaka alitumaini ukombozi au msamaha

D. Mfumo wa Utoaji wa Sadaka wa Israeli - Sadaka za Israeli zilikuwa karibu kwa wakanaani ingawa sio muhimu kuhusiana nazo kabisa.
   1. Tungo zenye maelezo
      a. Sadaka ilikuwa ni maelezo ya dhahiri ya hitaji la mwanadamu kwa Mungu
      b. Sheria ya Agano la Kale ambayo inarekebisha sadaka haiwezekani kusemwa kuanzisha sadaka (kama vile Mwa. 7:8; 8:20)
      c. Sadaka ilikuwa ni dhabihu (mnyama au majani)
      d. Sharti iwe sadaka ambayo iatakuwa kamiliau sehemu ikiteketezwa juu ya madhabahu kwa ajili ya shukrani kwa Mungu.
      e. Madhabahu ilikuwa ni sehemu ya kutoa sadaka na iliashiria uwepo wa Mungu
      f. Sadaka kilikuwa ni kitendo cha nje cha ibada (maombi ambayo yalifanywa nje)
      g. Maana ya sadaka ni "maombi yaliyofanyiwa kazi" au "maombi ya kiibada." Umuhimu wa ibada na ubaguzi wetu wa ki-desturi kinyume chake unafunuliwa katika Gordon J. Wenham (Tyndale, Numbers, ukurasa wa 25-39). Mambo ya Walawi na Hesabu vyote vinajumuisha kiwango kikubwa cha aina hiui ya vitu jambo linaloonyesha umuhimu wake kwa Musa na Israeli.
   2. Sadaka iliyojumuishwa
      a. Zawadi kwa Mungu
         (1) inajumuisha shukrani kwamba vitu vyote ni vya Bwana
         (2) Vitu vyote ambavyo Bwana anavyo, ni Mungu amempatia
         (3) hivyo, ni haki kwamba mwanadamu anatakiwa amshukuru Mungu
         (4) Ilikuwa ni aina yake ya zawadi kwa Mungu. Ilikuwa ni kitu ambacho mwanadamu alikihitaji kwa ajili ya ustawi wake mwenyewe. Ilikuwa ni zaidi ya utoaji wa kitu tu, ilikuwa ni kitu alichokihitaji. Ilikuwa ni kumpatia sehemu yake kwa Mungu.
         (5) kwa kuteketeza zawadi ambayo haiwezi kurejeshwa
         (6) sadaka ya kuteketezwa inakuwa haionekani na inakwenda juu kwenye ulimwengu wa Mungu
         (7) mwanzoni madhabahu za kale zilijengwa katika sehemu ambapo Mungu alitokea. Madhabahu ilikuja kutazamwa kama sehemu takatifu, hivyo sadaka ililetwa pale.
      b. Kufanya utakazo wa maisha yote ya mtu kwa Mungu
         (1) sadaka ya kuteketezwa ilikuwa ni moja ya sadaka tatu za hiari.
         (2) Mnyama mzima aliteketezwa kuelezea kwa Mungu shukrani zetu kuu.
         (3) Hii ilikuwa n zawadi inayoeleweka zaidi kwa Mungu.
      c. Ushirika na Mungu
         (1) kipengele cha komunyo ya sadaka
         (2) mfano ungekuwa sadaka ya amani ambao ulimuwakilisha Mungu na mwanadamu katika ushirika
         (3) sadaka ilitolewa kupata au kupokea ushirika huu

d. Upatanisho wa dhambi
   (1) pale mwanadamu alipotenda dhambi alimuomba Mungu kurejesha mahusiano (agano) ambayo mwanadamu alikuwa ameyavunja
   (2) Hakukuwa na karamu ya pamoja pamoja na sadaka ya dhambi kwasababu ya mahusiano yaliyovunjika
   (3) umuhimu wa damu
      (a) iliwekwa juu ya madhabahu kwa ajili ya mwanadamu
      (b) iliwekwa katika vazi kwa ajili ya kuhani
      (c) iliwekwa juu ya kiti cha rejhema kwa ajili ya Kuhani Mkuu na taifa (Law. 16)
   (4) kulikuwa na aina mbili za sadaka za dhambi. Ya pili inaitwa sadaka ya hukumu au sadaka ya makosa. Ndani yake mkosaji alitakiwa kurejesha Mwisraeli mwenzake kile ambacho kilikuwa kimechukuliwa au kuharibiwa pamoja na sadaka ya mnyama.
   (5) hakukuwa na sadaka kwa ajili ya kosa la mbeleni ambalo halijatokea au dhambi ya kukusudia, 4:1, 22, 27; 5:15-18;22:14

E. TARATIBU KWA AJILI YA SADAKA MBALI MBALI
1. SURA YA 1
   a. Kanuni ya Utangulizi, "Bwana alimwambia Musa ," 1:1-2; 4:1; 5:14; 6:1,19; 7:22, 28
      (1) Kutoka katika kundi la mifugo
      (2) "Wakati," mstari wa 2, unaonesha kwamba hii haikuwa lazima bali ya kujitolea
   b. Sadaka ya Kuteketezwa, mistari ya 3-17 (6:8-13)
      (1) Madhabahu
         (a) Madhabahu ya shaba, ambayo pia ilikuwa ikiitwa madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa, madhabahu ya mlango wa Hema, au madhabahu ya mbao za shittim, ikifunikwa na shaba (kama vile Kut. 27)
         (b) hii iliitofautisha na madhabahu ya uvumba (madhababu ya dhahabu) katika Mahali Patakatifu (kama vile Kut. 30)
         (c) mkaa utokao katika madhabahu ya shaba ulichukuliwa kwenda katika madhabahu ya uvumba
         (d) madhabahu ya shaba ilikuwa katikati ya lango la Hema
         (e) madhabahu ilikuwa na pembe ambazo zilikuwa mahali pake patakatifu zaidi. Damu ilitumika kwenye pembe (kama vile Kut. 30:10).
         (f) Pembe zilikuwa hasa kwa ajili ya:
            i. ishara ya mikono kushikilia sadaka juu
            ii. uwakilishi wa nguvu na uweza udumuo (Kumb. 33:17; II Sam. 22:3.)
            iii. baadaye, yeyote aliyeshikilia mapembe ya madhabahu alikuwa salama mpaka jambo lake liamuliwe na mahakama (1 Wafalme 1:50-51; 2:28)
      (2) Sadaka
         (a) kondoo asiyekuwa na waa anayetajwa kwanza kwasababu ya umuhimu wake na gharama, mstari wa 3
         (b) mbuzi dume au kondoo, mstari wa 10
         (c) njiwa au kinda la hua, mstari wa 14 (utoaji kwa ajili ya masikini)
      (3) Sehemu ya Sadaka ya kuteketezwa ilikuwa mlangoni mwa Hema la Kukutania

(4) Kuwekea mikono - hii ilikuwa ni kwa ajili ya ng'ombe madume, sio kwa mbuzi, kondoo au ndege, mstari wa 4
   (a) mtoaji wa sadaka alifanya hivi mwenyewe (sio kuhani)
   (b) Wengi wanafikiri kwamba kilikuwa ni kitendo cha uwakilishi wa kuhamisha hukumu
   (c) baadhi wanaamini kwamba kwamba:
      i. mnyama huyu anatoka kwa mtu huyu fulani
      ii. sadaka ilitakiwa kuwasilishwa kwa jina la mtoaji
      iii. tunda la sadaka hii linaenda kwa Yule aliyeweka mikono yake kwa mnyama
(5) Uchinjaji
   (a) ng'ombe dume -"mbele za Bwana" inayofanywa na mtu atoaye sadaka. Mtoa sadaka alitakiwa kuuwa, kuchuna ngozi na kumkatakata mnyama. Jukumu la kuhani (isipokuwa katika sadaka za umma) lilianza pale mtu alipoleta mnyama kwenye madhabahu.
   (b) kondoo au mbuzi, mstari wa 11 -"upande wa kaskazini mwa madhabahu mbele za Bwana" Palipangwa hasa sehemu maalumu kwa ajili ya wanyama hawa wadogo wadogo.
   (c) ndege - Kuhani alimuua mnyama na kutoa sadaka. Mtoaji aliya kutoa matumbo ya ndege.
(6) Namna ya kushughulikia damu
   (a) Wanyama
      i. Kuhani alirusha damu kwenye madhabahu na kuinyunyiza pembezoni mwa madhabahu.
      ii. Uhai wa mnyama ulikuwa katika damu (kama vile Mwa. 9:4; Law. 17:11). Uhai ulikuwa tayari ni wa Mungu, hivyo damu haikuwakilisha sehemu yoyote ya zawadi ya mtu.
      iii. Damu ya ndege ilitengenezewa mahali itiririke pembezoni mwa madhabahu na haikuteketezwa katika moto.
(7) Namna ya kushughulikia Nyama
   (a) ng'ombe dume, mstari wa 6
      i. Mtoaji alichuna ngozi ya sadaka. Kuhani angeweza kutunza ngozi (kama vile 7:8)
      ii. Mtoaji alikatakata vipande vipande
      iii. Kuhani aliweka sadaka yake katika madhabahu kwa mpangilio kama ilivyokuwa wakati ikiwa hai
      iv. Miguu na vilivyomo ndani vilioshwa na maji kutoka katika sehemu ya kuoshea.
      v. Kuhani aliteketeza vitu vyote katika madhabahu

c. mazingira ya Sadaka ya Kuteketezwa
   (1) Karamu ya Mahema, Mahema
   (2) Siku ya Upatanisho
   (3) Wiki za Karamu, Matunda ya Kwanza au Pentekoste
   (4) Karamu za Mbiu
   (5) Mganda wa Sadaka ya Kutikiswa (Law. 23)

(6) Karamu ya Mikate isiyotiwa Chachu, Pasaka
(7) Mwanzo wa miezi, Mwezi Mpya
(8) Sabato

d. Umuhimu wa Sadaka ya Kuteketezwa
(1) Zawadi kwa Mungu
(2) Kuonekana kama sadaka zenye thamani zaidi.
(3) Inaonekana kushughulikia dhana ya dhambi kwa ujumla au shukrani.
(4) Wazo kamilifu zaidi la uwakilisho wa kidhabihu.
(5) Uwakilishi wa Dhabihu wa maisha ya mtu
(6) Inawakilisha utakaso kamili wa maisha ya mtu katika huduma kwa Mungu
(7) Thamani ya viwango vya sadaka
(a) Ng'ombe dume
(b) kondoo– mbuzi
(c) ndege
(8) Hii inaonesha kwamba yeyote mwenye utambuzi wa hitaji la kiroho angemkaribia Mungu. Mungu alikidhi mahitaji kwa watu wote.

e. Maelekezo maalum kwa Makuhani, 6:8-12
(1) Sadaka ya kuteketezwa ilibakia usiku mzima upande wa moto uwakao wa madhabahu
(2) Moto ulitunzwa kwa uendelevu chini ya sadaka ya kuteketezwa
(3) maelekezo yanayojumuisha mavazi ya Kuhani
(4) Maelekezo yanayojumuisha kuondolewa kwa majivu

2. SURA YA 2:1-16 (6:14-23)

a. Utangulizi
(1) Sura hii inajikita katika sadaka za mbegu
(2) Sadaka za mbegu (Sadaka ya Mbegu) inatoka katika mzizi unaomaanisha "(zawadi) ." Ilifanyika neno la kiufundi kwa zawadi zisizo za wanyama au za mimea.
(3) Baada ya Uhamisho, sadaka za mbegu zinaonekana kama mbadala wa sadaka ya kuteketezwa na sadaka ya amani na walimu wa kiyahudi wanasema ingeweza kutolewa pekeyake na maskini sana.
(4) Agano la Chumvi pia lilitajwa katika Hes. 18:19 na 2 Nyakati 13:5. Chumvi ilikuwa kinyume cha chachu. Ilitumika kama uwakilishi wa agano la Mungu kwasababu lilikuwa haliharibiki na la milele.

b. Sadaka ya Mbegu ilijumuisha mazao ya kazi ya mtu yakitolewa kwa ajili ya Mungu.
(1) Ilikua ni zawadi kwa Mungu kutoka kwenye chakula cha kila siku cha watu.
(2) Ilikuwa ni mbadala wa jumla (hasa siku za baada ya uhamisho) kwenda kwenye sadaka ya kuteketezwa au sadaka ya amani.
(3) Sadaka ilikuwa kukidhiwa kwa mahitaji ya Mungu kwa kuhani. Ni sehemu ndogo tu iliteketezwa kama ukumbusho wa kitu kizima.
(4) Neno "kumbukumbu" inaelezea sehemu iliyotolewa, au sehemu ile ambayo inaleta ukamilifu mbele za BWANA.
(5) Dhana ya Agano Jipya juu ya dhana ya Karamu ya Bwana kama"kumbukumbu inaelezea dhana hii ya Agano la Kale.
(6) Tofauti kati ya maneno "(patakatifu) holy" na "(Patakatifu zaidi) most holy" ni:
(a) "patakatifu" - kuhani na familia ingeila mahali popote pasafi

(b) "patakatifu pa patakatifu" - inaweza kuliwa na makuhani tu na katika makutano ya Hema ya Kukutanikia

c. Aina
   (1) Unga usiokandwa (kwa ajili ya matajiri), 2:1-3
   (2) mikate iliyookwa au keki, 2:4-11
   (3) Masuke ya kijani ya mahindi au ngano (kwa ajili ya masikini), 2:12-16
      (a) Unga usiokandwa ilikuwa ni sadaka ya juu zaidi. Ilikuwa ni bora zaidi juu ya unga wa nagano.
      (b) Mkate uliookwa
         i. mafuta kilikuwa ni kiungo
         ii. Uliandaliwa katika kikaango, mstari wa 4.
         iii. juu ya kikaango cha chumvi, mstari wa 5.
         iv. katika chungu cha udongo cha kukaangia, mstari wa 7.
      (c) Masuke ya kijani au ngano
         i. lazima yawe makavu
         ii. yavunjwe katika vipande vidogo vya kati
         iii. yapangwe kama jozi yam lo mbele ya wageni.

d. Viungo
   (1) Unga mlaini ulichanganywa na mnyama asiyekuwa na mawaa
   (2) Mafuta ilikuwa ni ishara ya utajiri na hivyo uwakilishi wa uwepo wa Mungu
      (a) Ilitumika kwa ajili ya chakula, kutolea sadaka, dawa na upako
      (b) Yawezekana matumizi ya mafuta yalitakiwa kuwa mbadala wa sadaka ya mafuta
   (3) Uvumba ulitokea India au Uarabuni
      (a) Ulionekana kama kitu kisafi zaidi yenye manukato ya kuvutia
      (b) Yalikuwa na uwakilishi wa maombi na sifa
   (4) Chumvi
      (a) Utunzaji wa uhai na pamoja na yenye sifa ya kutunza
      (b) Yawezekana zaidi kwa ajili ya ushirika wa mezani kuliko utunzaji
   (5) Vipengele vilivyowekwa kando
      (a) Chachu iliwekwa kando, mstari wa 11
         i. yawezekana kwasababu ya utengenezaji wa kilevi
         ii. Chachu ilihusianishwa na uharibifu
         iii. ingeweza kutolewa pamoja na malimbuko kwenda kwa kuhani
      (b) Asali iliwekwa kando
         i. maji yake yalitokana na matunda na sio nyuki
         ii. yawezekana kwasababu ya matumizi yake katika Ibada za Wakanaani

e. Taratibu za utoaji wa Sadaka
   (1) Ililetwa kwa kuhani. Alishughulikia swala zima (2:2, 9, 16)
   (2) Sehemu ya sadaka ilitakiwa kuliwa na kuhani katika madhabahu. Ilikuwa takatifu zaidi.

f. Umuhimu
   (1) Zawadi kutoka kwa wasio na cheo kwenda kwa wenye vyeo
   (2) Kuteketeza sehemu yake kuliwakilisha utakaso wa sehemu ya maisha ya mtu ya kazi yake kwa Mungu
   (3) Maana ya dhahiri

(a) Sadaka ya kuteketeza - utakaso wa maisha ya mtu
(b) Sadaka ya Chakula - uwekaji wakfu wa kazi ya mtu ya kila siku

g. Maelekezo maalumu ya Sadaka ya mbegu, 6:14-23
(1) Sadaka ilitolewa mbele ya madhabahu
(2) Kazi ilitolewa kama zawadik kwa Mungu lakini kiuhalisia ni kwamba ilisaidia ukuhani

3. SURA YA 3:1-17 (7:13-34) SADAKA YA AMANI

a. Utangulizi
(1) kwanini
(a) Sadaka ya ushirika
(b) Sadaka ya agano
(c) sadaka ya jumla
(d) sadaka ya hitimisho
(2) Ilielezea shukrani kwa Mungu kwasababu ya ushirika na Mungu, familia na marafiki.
(3) Mara zote tendo la mwisho katika mfululizo ambamo ndani yake mapatano yalikuwa yamekwishafanyika.
(4) Sadaka ya kuteketezwa ilielezea gharama ya utiifu wakati sadaka ya amani ilielezea furaha na ari ya ushirika na Mungu.
(5) jinsi ya kiume au jinsi ya kike asiye na mawaa
(6) Aina za sadaka
(a) kutoka katika kundi la mifugo; ya kike au ya kiume
(b) Tofauti ambayo ilitengenezwa kati ya kondoo na mbuzi ilikuwa ni kwasababu ya mafuta yaliyokuwa katika mkia wa kondoo
i. mwanakondoo wa kundi la mifugo - jinsi ya kike au ya kiume
ii. mbuzi katika kundi - jinsi ya kike au ya kiume

b. Taratibu
(1) Uwasilishaji wa Sadaka
(a) uwekaji wa mikon juu ya sadaka
(b) iliuwawa mlangoni mwa Hema la Kukutanikia
(c) Utambulisho wa sadaka ulikuwa ule ule kama wa sadaka ya kuteketezwa
(d) Unyunyizaji wa damu kuzunguka madhabahu
(e) Uteketezaji wa sehemu zilizochaguliwa katika madhabahu kwa Mungu
i. mafuta (kondoo-mkia wenye mafuta) iliwakilisha utajiri
ii. figo, maii yaliwakilisha kiti cha nafsi na hisia
iii. sehemu ya mafuta iliwekwa kwenye sadaka ya kuteketezwa ya mtoaji au juu ya mwanakondoo wa asubuhi
(2) Sadaka ya shukrani ilijumuishwa (7:11-14)
(a) Mkate usiotiwa chachu uchanganywao na mafuta
(b) mkate usio tiwa chachu uliwekwa mafuta
(c) unga laini ulichanganywa na mafuta

c. Sehemu ya Kuhani, 7:28-34
(1) Matiti yalienda kwa kuhani kama sadaka ya mganda
(2) Mganda ulijumuisha uwekaji wa sadaka juu ya mikono ya mtoaji na mikono ya kuhani. Ilionesha kwamba Sadaka imetolewa kwa Mungu na baadaye kupokelewa tena na kuhani.

(3) Paja la kulia lilikuwa ni kwa ajili ya kumuweka wakfu kuhani

(4) Sadaka ya Mganda iliinuliwa kwa Mungu na kupokelewa tena na kuhani

d. Sehemu ya Mtoaji, 7:15-18

(1) Sadaka ya shukrani italiwa siku ya utoaji, mstari wa15

(2) Nadhiri (ahadi) au sadaka ya utashi huru italiwa siku ya utoaji sadaka au siku inayofuata, mstari wa 16

(3) Sehemu hii ilikuwa ni vyote ambavyo vilitolewa kwa Mungu na Mungu kwa Kuhani

(4) Mungu kiuwakilishi alikula pamoja na Mtoaji na familia yake na marafiki katika sadaka hii

(5) Sadaka hii iliweka msisitizo kwamba mahusiano ya ushirika yamekwisha rudishwa

4. SURA YA 4:1-5:13 (6:24-30) SADAKA YA DHAMBI

a. Utangulizi

(1) Hii ni sadaka ya kwanza ambamo upatanishi ulikuwa kipengele kinachotawala.

(2) Sadaka hii inaweka upya agano kti ya mwanadamu na Mungu. Inarejesha ushirika.

(3) Sadaka hii inajumuisha:

(a) Dhambi za kutojua

(b) Dhambi za kificho

(c) Dhambi za matamanio

(d) Dhambi za ondoleo

(e) Haikupatanisha dhambi iliyotendwa kwa umakusudi katika uasi dhidi ya Mungu. Hakukuwa na sadaka kwa dhambi ya kukusudia, yenye lengo baya na iliyopangwa kufanyika kabla (kama vile Hes. 15:27-31).

b. Maana

(1) Sadaka hii ilileta upatanisho hukumu na adhabu kwa ajili ya dhambi.

(2) Hii ilijumuisha neema kwa upande wa Mungu na imani kwa upande wa mwanadamu.

(3) Hakuna sadaka inayoweza kufanikisha chochote kwa kuwa tu ni taratibu za sadaka, Ilikuwa inapewa uwezo na imani ya mtoaji anapofanya kile kitendo.

(4) Pia, sadaka ilikuwa ni zaidi ya maelezo ya mtoaji. Ilifanikisha lengo fulani kwa ajili yake. Iliweka upya mahusiano na Mungu

(5) Ibada ilikuwa ni namna iliyotolewa na Mungu kwa ajili ya urejesho, na sio mbadala wa imani binafsi ya binafsi.

(6) Mungu anachukia kitendo chochote cha kidini kisichosindikizwa na imani, Isa. 1:10-20; Amosi 5:21-24; Mika 6:6-8.

c. Taratibu

(1) kwa ajili ya Kuhani Mkuu, mistari ya 3-12

(a) Kuhani Mkuu- kuhani aliyepakwa mafuta

i. Dhambi inayowapelekea watu katika kutenda mabaya

ii. Dhambi yenye asili ya binafsi

iii. kuhani mkuu, hali akiwa mwakilishi wa kiroho wa jamii. Ikiwa angetenda dhambi, wote walionekana wenye dhambi katika yeye (kama vileJoshua 7; Warumi 5:12 na kuendelea).

(b) Taratibu

i. Kuhani Mkuu alileta mwanakondoo asiye na mawaa madhabahuni.

ii. Aliweka mikono juu ya kichwa chake

iii. Kuhani Mkuu alimchinja mnyama
iv. Kuhani Mkuu alinyunyiza damu mbele ya pazia mara 7
    a) hii ilitakasa Hema
    b) kiuwakilishi hii ilifungua njia kwenda kwa Mungu
    c) damu iliwekwa kwenya mapembe ya madhabahu ya uvumba
    d) damu iliyobakia ikimwagwa nje kwenya msingi wa madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa
v. iliweka mafuta yote yateketezwe katika madhabahu
vi. Sehemu iliyobakia ya mnyama ingechukuliwa nje ya kambi sehemu iliyosafi, mstari wa 12, Hapo, majivu yangemwagwa nje ya madhabahu.

(2) Kwa ajili ya Mataifa, mstari wa 13-21
  (a) Walikuwa wametenda dhambi pale ambapo matakwa ya sheria yalikuwa hayajatimizwa, mistari ya 13-21.
  (b) Taratibu
    i. Wazee walileta mwanakondoo asiye na mawaa.
    ii. Wazee waliweka mikono ya kichwa chake.
    iii. Wazee walichinja mnyama
    iv. Kuhani Mkuu alinyunyiza damu kwenye pazia mara 7
        a) hii ilisafisha Hema
        b) kiuwakilishi ilifungua njia kwa Mungu
        c) damu iliwekwa juu ya pembe ya uvumba wa madhabahu
        d) mabaki yalimwagwa kwenye msingi wa madhabahu ya sadaka
    v. Vyote vilitolewa juu ya madhabahu
    vi. Wanyawa wote waliosalia walipelekwa nje ya kambi sehemu safi, mstari wa 12, ambapo majivu yalimwagwa nje ya madhabahu. Hapo mabaki ya mnyama yalichomwa

(3) Kwa kiongozi, mistari ya 22-26
  (a) Kiongozi (mtawala) mistari ya 22-26
    i. Kiongozi wa kabila
    ii. Mtu mwenye kuwajibika katika jamii
    iii. Mzee
  (b) Taratibu
    i. Kiongozi alileta mbuzi wa kiume (mzee, mbuzi mwenye manyoya mengi) kuelekea madhabahuni.
    ii. kiongozi aliweka mikono juu ya kichwa chake.
    iii. Kiongozi alimchinja mnyama.
    iv. Kuhani Mkuu aliweka damu juu ya pembe za madhabahu ya kuteketeza-sehemu ya damu ilimwagwa chini ya madhabahu ya kutolea sadaka.
    v. Mafuta yote yalichomwa juu ya madhabahu.
    vi. Makuhani walikula sehemu ya nyama iliyobakia.

(4) Kwa ajili ya mtu mmoja mmoja, mistari ya 27-35
  (a) kwa mtu binafsi - alipojua kwamba alikuwa ametenda dhambi alitakiwa kutoa sadaka hii
  (b) Taratibu
    i. Mtu alileta mbuzi wa kike au mwanakondoo wa kike.

ii. Mtu aliweka mikono yake juu ya kichwa chake.
iii. Mtu alimchinja mnyama.
iv. Kuhani aliweka damu juu ya pembe za madhabahu ya sadaka-mabaki yakimiminwa katika msingi wa madhabahu.
v. Mafuta yote yaliwekwa juu ya madhabahu na kuchomwa.
vi. Kuhani alikula mabaki ya nyama.

(5) Taratibu maalum zilizojumuisha sadaka ya dhambi, 5:1-13 (Hizi zinaonekana kujumuisha dhambi za kukusudia dhidi ya mwenza wa agano)
(a) Ikiwa shahidi hatokei na kushuhudia (kushindwa kutoa taarifa), 5:1
(b) Kugusa mnyama aliye najisi, 5:2
(c) Kugusa mwanadamu najisi, 5:3
(d) Kuzungumza bila kufikiri kwa kuapa, 5:4
(e) sadaka kwa dhambi hapo juu:
i. ngo'ombe au kondoo wa kike
ii. Njiwa wawili au hua
iii. Efa 1/10 unga wa Efa

(6) Taratibu za utoaji wa ibada, 6:24-30
(a) Kuhani angekula kile kinachobakia.
(b) Ikiwa nguo ingeshika damu, nguo zilitakiwa kuoshwa
(c) Ikiwa damu ingebaki kwenye chungu, chungu kilitakiwa kuvunjwa.
(d) Ikiwa chombo cha shaba kingeshika damu, chombo kilioshwa.
(e) Ikiwa damu ya sadaka ya kuteketezwa ililetwa ndani ya Mahali Patakatifu nyama ilitakiwa kuchomwa na kutoliwa na kuhani.

(7) umuhimu wa sadaka ya dhambi
(a) Hakukuwa na sadaka kwa ajili ya dhambi iliyopangwa-ni kwa ajili ya dhambi ya bahati mbaya tu au dhambi za kutojua kwamba kifanywacho ni dhambi, 5:15, 18.
(b) Msamaha ulijumuisha nini:
i. sehemu ya mtu ni imani
ii. Sehemu ya Mungu ni rehema

5. SURA YA 5:14-19 SADAKA YA HUKUMU AU MAKOSA

a. Utangulizi

(1) Wakati Sadaka ya dhambi ilishughulikia dhambi iliyotendwa, sadaka ya hukumu iliangalia madhara yaliyofanywa na mwenza wa kiagano na urejesho ambao ungewezekana kutendeka.
(2) Sadaka za dhambi na makosa zilikuwa kitu kile kile kinachofanana.
(3) Haki za mtu zilielezewa katika Amri Kumi (Kutoka. 20; Kumb.5).
(a) Nyumba
(b) kupata mali
(c) uhai
(4) Sadaka hii inasisitiza madhara yaliyofanyika kwa ndugu yetu katika kutenda dhambi na urejesho wa gharama ya kile ambacho kilikuwa kimeharibiwa pamoja na zaidi ya sehemu ya 1/5.

b. Dhambi zilizohitaji Sadaka

(1) Dhidi ya Mungu au kile ambacho ni mali yake

(a) malimbuko
(b) mzaliwa wa kwanza, 14-16
(c) zaka
(d) sadaka zilizotolewa vibaya
(e) dhabihu za thamani ya chini

(2) "Ikiwa mtu atatenda dhambi na kufanya chochote kati ya vitu ambavyo BWANA ameamuru visifanywe, japo anajua, bado atakuwa hatiani na atastahili adhabu."

F. Sadaka za kale zilitolewa kwa sababu kadhaa:
a. kupoza Mungu mwenye hasira
b. kumlisha Mungu
c. kuwa na Ushirika na Mungu
d. tendo la sifa
e. namna ya hitaji la msamaha au upatanisho

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI (muktadha)

A. AINISHO FUPI:
1. Sura za 1-16 -- Namna gani twaweza kumuendea Mungu Mtakatifu?
2. Sura za 17-26 -- Je mtu anawezaje kuendelea katika ushirika pamoja na Mungu Mtakatifu?

B. Matumizi ya mwandishi mwenyewe ya kanuni ya utangulizi, "Na Bwana akamwambia Musa (au Haruni) akisema..."
1. Hii ingeweza kumaanisha kwamba vitu vya kliufunuo vilitolewa kwa muda.
2. Maeneo ambayo kanuni hii inatokea: 1:1-3:17; 4:1-5:13; 5:14-19; 5:20-26; 6:1-11; 6:12-16; 6:17-7:21; 7:22-38; 8:1-10:20; 11:1-47; 12:1-8; 13:1-59; 14:1-32; 14:33-57; 15:1-33; 16:1-34; 17:1-16; 18:1-3; 19:1-37; 20:1-27; 21:1-24; 22:1-16; 22:17-25; 22:26-33; 23:1-8; 23:9-22; 23:26-32; 23:33-44; 24:1-23; 25:1-26:46; 27:1-34;

C. MUHTASARI ULIOKUZWA:
1. Kuondolewa kwa unajisi, sura za 1-16
a. Sheria za Sadaka, 1:1-7:38
(1) Sadaka ya Kuteketezwa, sura za 1:3-17 & 6:8-13
(2) Sadaka ya chakula, sura za 2:1-17 & 6:14-23
(3) Sadaka ya amani, sura za 3:1-17; 7:33 & 7:11-21
(4) Sadaka ya dhambi, sura za 4:1; 5:13 & 6:24-30
(5) Sadaka ya hukumu, sura za 5:14-6:7; 7:1-10
(a) Dhambi isiyo ya kukusudiwa dhidi ya agano la YHWH, 4:1-35; 5:14-19
(b) Dhambi ya kukusudia dhidi ya mwenza wa kiagano, 5:1-13; 6:1-7 (Sura za 1-6:7 kwa ajili ya watu; sura za 6:8-7:36 kwa ajili ya makuhani)

b. Kuwekwa wakfu/Kutakaswa kwa Makuhani, 8:1-10:20
(1) Maandalizi ya kupakwa mafuta, 8:1-5
(2) Kunawa, kuvaa na kupakwa mafuta, 8:6-13
(3) sadaka ya kupakwa mafuta, 8:14-32

(4) Musa anampatia Haruni maelekezo, 9:1-7
(5) Haruni na wana wanaanza, 9:8-21
(6) Haruni anawabariki watu na YHWH
(7) Dhambi za Nadab na Abihu, 10:1-3
(8) Hatima yao na kuondolewa, 10:4-7
(9) Kutokunywa mvinyo wakati wakiwa katika zamu zao, 10:8-11
(10) Sehemu ya Kuhani ya sadaka, 10:12-20

c. Najisi na Isiyo najisi, sura za 11-15
(1) Wanyama, sura ya 11 (kama vile Kumb. 14:6-20)
(2) Kuzaliwa kwa mtoto, sura ya 12
(3) magonjwa ya ngozi, sura za 13-14
(a) kwa mwanadamu, 13:1-46
(b) katika nguo, 13:47-59
(c) kusafishwa, 14:1-32
(d) nyumbani, 14:33-53
(e) kwa ufupi, 14:54
(4) Kutakaswa na uchafu utokao katrika mwisli (wanaume na wanawake), sura ya 15

d. Siku ya Upatanisho (Yom Kippur), siku ya mwisho wa mwaka wa kusafishwa, sura ya 16 (Hii inaonekana kuwa kilele cha sura za 1-16)
(1) maandalizi ya kikuhani, 16:1-4
(2) Sadaka ya dhambi kwa ajili ya Kuhani Mkuu, 16:5-10
(3) Taratibu, 16:23-28
(4) Utungwaji wa mwisho wa mwaka, 16:29-34

2. Urejesho wa Utakatifu na Ushirika pamoja na Mungu, sura za 17-26
a. Damu za ki-dhabihu, 17:1-16
b. Viwango vya kidini na kimaadili, 18:1-20:27
(1) kujamiiana
(2) Dhambi za kujamiiana
(3) Adhabu, sura ya 20
c. Utakatifu wa Makuhani, 21:1-22:33
d. Utakatifu wa siku za karamu za mwisho wa mwaka, 23:1-24:23
(1) Sabato, 23:1-3
(2) Pasaka na Mikate Isiyotiwa chachu, 23:5-8
(3) Malimbuko, 23:9-14
(4) Mavuno, 23:15-24
(5) Pentekoste, 23:23-25
(6) Siku ya Upatanisho, 2 3:2 6-3 2 (siku ya kufunga tu)
(7) Hema (Hema), 23: 33-43
e. Miaka maalum, 25:1-55
(1) Ya kisabato, mistari ya 2-7
(2) Jubilee, mistari ya 8-55
(a) Kuangalia kutenda sawasawa, mistari ya 8-12
(b) Madhara, mistari ya 13-34
(c) Kila mtu wa kiagano alistahili kuwa huru, mistari ya 35-55
f. Baraka za Kiagano na Laana, 26:1-46

2. Kiambatisho (viapo), 27:1-34
    a. Mtu, mistari 1-8
    b. Wanyama, mistari 9-13
    c. Makazi, mistari ya 14-15
    d. Ardhi, mistari ya 16-25
    e. Malimbuko ya kwanza, mistari ya 26-27
    f. Kitu cha kutolewa, mistari ya 28-39
    g. Zaka, mistari ya 30-34

VIII. KWELI KUU

A. Kitabu cha mambo ya Walawi kinahusika na msingi wa kisheria kwa ajili ya maisha ya uraia na kidini wa taifa la Israeli na kazi za ukuhani. Inatoa mwongozo wa matumizi ya Hema yanayofunuliwa katika Kut. 25-40.

B. Inaelezea namna gani mtu mwenye dhambi anaweza kumsogelea Mungu Mtakatifu na pia namna gani anaweza kuendeleza ushirika. "Utakatifu" ni msingi wa kitabu (kama vile 11:44 {Mt. 5:48}).

C. Maajabu ya maajabu, Mungu anatamani kwamba mwanadamu mdhambi amwendee yaya na ametoa njia, mfumo wa utoaji sadaka.

D. Tabia ya YHWH inafunuliwa:
    A. Katika kutoa mfumo wa kidhabihu, kama vile sura za 1-7 (Neema)
    B. Katika matendo ya kihistoria, kama vile sura za 8-10 (Haki)
    C. Katika kuendelea kwake katika uwepo pamoja na watu (Uaminifu)

IX. MANENO/AU TUNGO NA WATU WA KUTAMBUA KWA MUHTASARI


A. Maneno na Tungo
    1. kupatanishwa, 1:4; 4:26 (NASB & NIV)
    2. Manukato yaburudishayo, 1:9,1 3, (NIV, Manukato Yaburudishayo)
    3. bila kukusudia, 4:1,22,27; 5:15-18; 22:14 (NASB & NIV)
    4. Urejesho wenye riba, 6:5 (NASB & NIV)
    5. sadaka ya mganda, 7:30 (NIV, mganda)
    6. takatifu (kadosh), 11:44 (NASB & NIV)
    7. ukoma, 13:1 na kuendelea, (NIV, magonjwa ya ngozi ya kuambukiza)
    8. mwanambuzi wa kafara, 16:8 (NASB & NIV)
    9. mapepo ya mbuzi, 17:7 , (NIV, sanamu za mbuzi)
    10. utambuzi, 19 :26 (NIV , kuloga)
    11. jubilei, 25:30 (NASB & NIV)

B. Watu wa kuwatambua kwa muhtasari
    1. Nadabu na Abihu, 10:1
    2. Azazeli, 16:8, 10 (NIV, kwa ajili ya kafara )
    3. Moleki, 18:21; 20:2


X. MAENEO YA KI-RAMANI – HAKUNA

XI. MASWALI YA KIMAUDHUI YA MWANAFUNZI

1. Mfumo wa kidhabihu unawakilisha nini? Kwanini "damu" inatajwa mara kwa mara, (3:17; 7:26; 17:11)?
2. Ni kwa namna gani kifo cha mnyama kinapelekea kusamehewa dhambi ya mwanadamu?
3. Kwa tatu kati ya sadaka tano ni za kujitolea?
4. Watoto wa Haruni walifanya nini ambacho kilisababisha wastahili kifo?
5. Kwanini kuna utofautiano kati ya wanyama walio najisi na wasio anajisi?
6. Nini kilicho cha kipekee kuhusu Siku ya Upatanisho kati ya jozi zote za karamu za Israeli?
7. Nini ni kweli juu ya Mwaka wa Sabato mna Mwaka wa Jubilei?


MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE
KAS
MAGH
MASH
KUS

# PALESTINA




VIPIMO KATIKA MAILI

# UTANGULIZI WA HESABU

I. JINA LA KITABU

A. Katika Kiebrania (MT) jina hili ni "Jangwani." Hili si neno la kwanza bali liko katika sentensi ya kwanza, neno la tano.

B. Katika toleo la LXX hili linaitwa "Hesabu" kwa sababu ya sensa iliyochukuliwa mara mbili kwenye sura ya 1-4 & 26.

II. URASIMISHAJI

A. Nini sehemu ya kwanza ya sheria ya Kiebrania inayoitwa "Torati" au "mafundisho" au "sheria."

B. Sehemu hii inafahamika kamaVitabu Vitano vya Kwanza vya Biblia (magombo matano) kwenye toleo la LXX.

C. Wakati mwingine huitwa "Vitabu vitano vya Musa" kwa lugha ya Kiingereza.

D. Inahusisha mwendelezo wa maelezo ya Musa kutoka wakati wa uumbaji kupitia maisha ya Musa, kitabu cha Mwanzo –Kumbukumbu la Torati.

III. AINA YA UWASILISHAJI - Kitabu hiki kinafanana sana na kitabu cha Kutoka. Huu ni muunganiko wa masimulizi ya kihistoria na utungaji wa sheria kama vile mashairi ya kale ya utabiri wa Balaamu (kama vile Hes. 23-24).

IV. UANDISHI

A. Hiki ni kitabu cha kwanza cha Torati kilichotaja chanzo kilichoandikwa, "kitabu cha vita vya *YHWH*,"21:14-15. Hii kwa dhahili inaonyesha kwamba Musa alitumia baadhi ya maelezo yaliyoandikwa.

B. Kitabu hiki kinaeleza kwamba Musa aliweza kuandika matukio ya kipindi cha kutangatanga jangwani.

C. Kitabu cha Hesabu pia kinatoa mifano kadhaa ya dhahili ya ongezeko la mhariri (inawezekana Yoshua au Samueli): 1. 12:1,3 2. 13:22 3. 15:22-23 4. 21:14-15 5. 32:33 ff 6. 32:33ff.

D. Kwa ndani kabisa Musa anarejelewa kwenye mtu wa tatu isipokuwa katika dondoo lengwa. Hii inadokeza kwamba Musa alitumia msaada wa waandishi ili kukusanya hizi taarifa.

E. Inatia shauku kutambua kwamba kitabu cha Hesabu kinahusisha pamoja na wingi wa fasihi mbili kwa wasio Wayahudi: (1)shairi la kudhihaki la Waamoni katika 21:27-30 (huenda mstr. 30 ilikuwa ni nyongeza kwa Waisraeli);na (2) Mazungumzo ya Balaamu na Balaki, Mfalme wa Moabu katika 23-24. Walitenda kuonyesha maandiko yalitumika au vifaa vya kuandikia pamoja kwenye mpangilio wa kitabu (kama vile *The Book of the Wars of the Lord*.).

V. TAREHE

A. Kitabu chenyewe kinatupatia tarehe:
   1. 1:1; 10:10 inasema ulikuwa mwezi wa pili wa mwaka wa pili baada ya Uhamisho toka Misri. Baada ya hili kulikuwa na kipindi cha miaka 38 cha kutangatanga jangwani.
   2. 9:1 inasema ulikuwa ni mwezi wa kwanza wa mwaka wa pili baada ya safari ya kutoka Misri.

B. Muda kamili wa Uhamisho huu haujulikanihili. Labda mwaka 1445 K.K. au mwaka 1290 K.K.

VI. VYANZO VYA UTHIBITISHO WA MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. Kuna vitu vinne vya kipekee kutoka kitabu cha Hesabu vinavyoaksi desturi za Kimisri:

1. Mpangilio wamakabila katika kambi za Waebrania (Hes. 2:1-31; 10:11-33) na mpangilio wa kutembea wa makabila (Hes. 1-7). Hii inafaa kabisa kwa amri iliyotumiwa na Ramesesi II katika mapambano yake ya kijeshi ya Shamu yanayofahamika kutokana na maandiko ya Armarna. Maelezo haya ya Wakaanani, kutoka kipindi cha mwaka 1300 K.K., yanaelezea kijamii, kisiasa na muunganiko wa kidini kati ya Kaanani na Misri. Pia ina umuhimu kwamba mpangilio huu wa Kimisri na kubadilisha mpangilio kama tunavyojifunza kutoka katika sanamu ya kuchonga ya Ashuru millennia ya kwanza K.K..Waashuru walipiga kambi kwa kuzunguka.
2. Baragumu fedha katika kitabu cha Hesabu 10 inaaksi chanzo cha Kimisri. Wataalam wa utafiti wa mambo ya kale walikuta yametajwa kwenye utawala wa Tutankhamun, mnamo mwaka 1350 K.K. Pia hizi tarumbeta za fedha, zilitumika kwa ajili ya kidini na makusudi ya kiraia yalizoeleka kwenye maandiko ya Armarna.
3. Magari ya farasi wa kivita yalitambulishwa Misri na *Hyksos*, Mtawala wa kisemiti wa nasaba ya karne ya 15 na 16. Magari yaliyokokotwa na maksai pia yalikuwa na upekee Misri. Waliyaona kwenye kambi ya kijeshi ya shamu ya Tuthmose III yapata mwaka 1470 K.K. Watu wa kanaani hakuwa na haya magari ya kukokotwa na farasi maksai, kwa sababu inawezekana kanaani ilikuwa na miamba na milima. Magari haya ya kukokotwa ndiyo yaliyotumwa kumchukua Yakobo (Mwa. 45:19, 21, 27). Pia yalitumiwa na Waebrania katika safari ya kutoka Misri (Hes. 7:3,6, 7).
4. Kipengele cha mwisho cha kipekee cha ki-Misri kilichoigwa na Waebrania kilikuwa ni unyoaji mzima wa makuhani (8:7).

B. Sensa mbili zinazopatikana katika sura 1-4 na 26 zinafanana katika:

1. Vibao vya Mari kutoka miaka ya 1700 K.K.
2. maelezo kutoka kipindi cha utawala wa zamani wa Misri, mwaka wa 2900 - 2300 K.K.

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI (Muktadha)

A. Muhtasari mfupi unaosisitizwa kwenye mpangilio wa Kijiografia:

1. matayarisho katika Mlima. Sinai kwa ajili ya safari ya kwenda Nchi ya Ahadi, 1:1-10:10.
2. safari ya kwenda Nchi ya Ahadi, 10:11 - 21:35
   a. kwenda Kadeshi, 10:11-12:16
   b. katika Kadeshi, 13:1-20:13
   c. kutoka Kadeshi, 20:14-21:35
3. matukio kwenye Uwanda wa Moabu, 22:1-36:13

B. Muhtasari Kamili

1. R.K. Harrison, *Introduction to the Old Testament*, kr. 614-615.
2. E. J. Young, *An Introduction to the Old Testament*, kr. 84-90.
3. Toleo la NIV Study Bible, kr. 187-188.

C. Mojawapo ya ugumu wa uchambuzi wa kitabu cha Hesabu ni taarifa yake inayotumiwa kuandikia maandiko kidogo ya jamii ngeni; yaani,mchanganyiko wa sheria na simulizi na kuhusika kwake na maandiko mbalimbali. Baadhi ya nadharia zenye kuhusiana na muundo wake ni:

1. Kwa namna iliyo dhahiri hii ilitumia utetezi wa "nadharia ya kumbukumbu," J.E.D.P. kukigawa kitabu kuwa katika namna isiyo ya kihistoria, vyanzo visivyo vya Musa.
2. J.S. Wright anapendekeza mkusanyiko wa maandiko ya Musa mwishoni mwa maisha yake kwenye majadiliano na waandishi. Sifa ndogo ndogo za kitabu cha Hesabu zinanukuliwa kimuhtasari lakini zinawakilisha wakati wa maisha ya Musa.
3. Gordon J. Wenham (*Tyndale Commentary on Numbers*, kr. 14-18) anashauri kutumia mfanano wa maandiko ya Biblia toka katika kitabu cha Kutoka, Walawi na Hesabu, na kuwahusisha na safari tatu: (1) Bahari ya Shamu kwenda Sinai; (2) Sinai kwenda Kadeshi; na (3) Kadeshi kwenda Moabu. Kwa

kufanya haya yote maandiko yanahusisha "safari" na "kusimama" ni ushahidi unaokuwa alama mfanano. Zaidi sana anahusisha mfanano huu katika Mwa. 1-11; Mwa. 12-50 na Kumb. Huu unaonekana kuwa wa ahadi sana. Huu unatuonyesha kwamba waandishi wa Mashariki ya Kale ya Karibu wana muundo wa fasihi au mwelekeo ambao unathibiti muundo wa fasihi yao lakini haujulikani kwetu sisi kama watu wa Magharibi.

VIII. KWELI KUU

A. Huu ni mwendelezo wa masimulizi ya kihistoria yanayoanzia katika kitabu cha Mwanzo. Lakini ni lazima ikumbukwe kwamba hii sio "historia ya magharibi" bali ni historia ya kithiolojia ya Mashariki ya Karibu. Matukio hayakuandikwa katika mfuatano wa maelezo bali yanachaguliwa ili kumfunua Mungu na tabia ya Israeli.

B. Inaonyesha tabia ya Mungu:
1. Uwepo wake ulionekana mawinguni:
   a. Wingu likatua juu ya "Patakatifu pa Patakatifu" pa Hema ya kukutania, 9:15. Mungu alilikubali na utaratibu wake kama njia na sehemu kwa ajili ya Mungu na mwanadamu kukutania!
   b. Wingu liliwaongoza watu, 9:17-23. Mungu alikuwa pamoja nao, na kuwaongoza kwa uwepo wake.
   c. Wingu liliunganisha uwepo wa Mungu uliomfunua yeye kwa Musa, 11:17, 25; 16:42-43.
   d. Wingu lilikuwa ni kielelezo cha uwepo wa Mungu kwenye hukumu kama vile ufunuo, 12:1-8;14:10.
   e. Wingu lilikuwa ni kielelezo kinachoonesha uwepo wa Mungu sio tu Israeli bali kwa mataifa yanayoizunguka, 14:14; 23:21.
   f. Uwepo wa Mungu ni kielelezo katika wingu wakati wa Uhamisho na kipindi cha Kutangatanga Jangwani kipindi walisimamishwa kama Waisraeli kuingia Nchi ya Ahadi lakini bado Mungu aliendelea kuwa kielelezo pamoja nao kama maana ya Sanduku, 35:34.
2. Neema yake na rehema katika:
   a. Uwepo wake endelevu pamoja nao katikati ya manung'uniko yao na kukataliwa kwa viongozi wake,11:1; 14:2,27,29,36; 16:11,42; 17:5; 20:2; 21:5.
   b. Utoaji wa mahitaji muhimu kwa ajili yao humo jangwani:
      (1) maji
      (2) chakula
         (a) manna (kila siku, isipokuwa siku ya Sabato)
         (b) kutetemeka kwa hofu (mara mbili)
      (3) mavazi ambayo hawakuyavua kamwe
      (4) Wingu:
         (a) kivuli
         (b) nuru
         (c) kuongozwa
         (d) Ufunuo
   c. Kumsikiliza mpatanishi wake Musa:
      (1) 11:2
      (2) 12:13
      (3) 14:13-20
      (4) 16:20-24
      (5) 21:7
3. Haki yake (Utakatifu) katika:
   a. hukumu ya Israeli ya miaka 38 ya kipindi cha kutangatanga jangwani (14).
   b. hukumu ya Musa iliyosababisha asiweze kuingia nchi ya ahadi (20:1-13; 27:14; Kumb.3:23-29).
   c. Kifo cha Korani na viongozi wa Reubeni, (16:1-40).
   d. Mapigo kwa ajili ya watu waliokataa uongozi wa Musa na Haruni, (16:41-50).
   e. Ibada ya sanamu katika Shitimu ilikuwa ni hukumu ya kifo iliyotolewa na Mungu kwa wakosaji katika mkono wa Walawi, (25).

C. Kama Israeli walivyodumisha makubaliano ya Agano katika Mlima. Sinai, kumwamini *YHWH* na utiifu wa nidhamu kwa Neno lake yakiwa ni mambo ya muhimu.

IX. MANENO NA/AU TUNGO NA WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHTASARI

A. Maneno na Tungo (NASB):

1. Hema ya kukutania, 1:1 (NASB na NIV)
2. Fidia, 3:46 (NIV, komboa)
3. Mnadhiri, 6:2 (NASB na NIV)
4. Mgeni aketie, 9:14 (NIV, mgeni)
5. Wingu, 9:15 (NASB na NIV)
6. "wafuasi waliokuwa kati yao," 11:4 (NASB na NIV)
7. "wakararua nguo zao," 14:6 (NASB na NIV)
8. vishada, 15:38 (NASB na NIV)
9. *Sheol,* 16:30 (NIV, kaburi)
10. ng'ombe mke mwekundu, 19:2 (NASB na NIV)
11. nyoka za moto, 21:6 (NIV, nyoka wenye sumu)
12. mji wa makimbilio, 35:6 (NASB na NIV)
13. kisasi cha damu, 35:19,21 (NASB na NIV)

B. Watu wa kuwatambua kwa muhtasari:


1. mwanamke Mkushi, 12:1 (NIV, "mke wake Mkushi")
2. Anaki, 13:28,33
3. Myebusi, 13:29
4. Kora, 16:1 (NIV, "Korathi")
5. Balaamu, 22:5
6. Baali, 22:41

X. Maeneo ya kiramani (kwa hesabu)


1. bonde la Eshkoli, 13:23 (kaskazini mwa Hebroni)
2. Njia kuu ya mfalme, 20:17
3. Mlima. Pisga, 21:20
4. Mto Arnoni, 21:24
5. Mto Yaboki, 21:24
6. Ashuru, 24:22
7. Shitimu, 25:1
8. Bahari ya Kinerethi, 34:11 (NIV, "Bahari ya Kinerethi")

XI. MASWALI YA KIMAUDHUI KWA MWANAFUNZI

1. Kwa nini kabila la Lawi halitajwi miongoni mwa makabila mengine, 1:49?
2. Ni kwa namna gani Walawi wanahusiana na mzaliwa wa kwanza, 3:12-13?
3. Elezea kipimo cha uzinzi, 5:16 na kuendelea.
4. Taja yanayohitajika katika nadhiri ya Mnazareti, 6:1 na kuendelea.
5. Ni kwa namna gani unaweza kuifafanua sura ya 4:3 na 8:24?
6. Je, Musa aliandika 12:3?
7. Kwa nini Mungu alikichagua miaka 40 ya kipindi cha kutangatanga?
8. Neno hili "siodhamiriwa" linamaanisha nini kwenye uhusiano wa dhambi na sadaka kama unavyopatikana kwenye sura ya 15?
9. Ni nini dhambi ya Musa katika sura ya 20? Matokeo yake yalikuwa yapi?
10. Je, ni kweli punda wa Balaam aliongea? 22:28. Ni kwa namna gani Balaamu alimshauri Balaki kwamba aiangamize Israeli?


MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE
KAS
MAGH
MASH
KUS

# PALESTINA




VIPIMO KATIKA MAILI

# UTANGULIZI WA KUMBUKUMBU LA TORATI

I. UMUHIMU

A. Hiki ni moja ya vitabu vya Agano la Kale vilivyonukuliwa mara kwa mara katika Agano Jipya (Mwanzo, Kumbukumbu la Torati, Zaburi, na Isaya). Kitabu cha Kumb. Kinanukuliwa mara 83.

B. Lazima hiki kilikuwa moja ya vitabu vya Agano la Kale vilivyopendelewa na Yesu:

1. Alikuwa akikinukuu kitabu hiki kwa kurudia rudia wakati alipojaribiwa na Shetani huko jangwani (Mt. 4:1-16; Luka 4:1-13).
2. Yamkini haya ni maelezo mafupi yaliyo nyuma ya Hotuba ya huko Mlimani, Mt. 5-7.
3. Yesu anainukuu Kumb. 6:5 kama amri kuu sana, Mt. 22:34-40; Mk. 12:28-34; Lk. 10:25-28.
4. Yesu anakinukuu kipengele hiki cha Agano la Kale (Mwa.- Kumb.) mara kwa mara sana kwa sababu Wayahudi wa siku zile waliichukulia hii kama kipengele cha sheria za kidini.

C. Huu ni mfano wetu mkuu katika Maandiko ya ufasiri upya wa ufunuo wa awali uliofunuliwa na Mungu kwa hali mpya. Mfano wa hili unaweza kuwa tofauti ndogo kati ya Amri Kumi zilizo katika Kut. 20 dhidi ya Kumb. 5. Kutoka 20 ilikuwa wakati wa Kipindi cha Kutangatanga Jangwani ambapo Kumb. 5 ilikuwa ikiwaandaa watu kwa ajili ya maisha ya Kanaani.

D. Kitabu cha Kumbukumbu la Torati ni, kwa maelezo yake yenyewe, mfululizo wa ujumbe uliotolewa na Musa ili:

1. Kuyasimulia matendo ya uaminifu wa Mungu kwa Israeli;
2. Kuisisitiza Sheria iliyotolewa Ml. Sinai;kwa mara nyingine;
3. Kuzifasiri maana zake kwa maisha ya ukulima humo Kanaani;
4. Kuziandaa taratibu za kulitengeneza upya Agano wawapo katika Nchi ya Ahadi (Yoshua);
5. Kuchukua kumbukumbu ya kifo cha Musa na mabadiliko ya nguvu ya Yoshua

E. Kitabu cha Kumbukumbu la Totati pia ni kitovu cha masemezano ya sasa miongoni mwa wanathiolojia kuhusiana na uundwaji wake wa kifasihi. Wasomi wa sasa wanagawanyika katika nadharia zake za mpangilio wa Vitabu Vitano vya Musa.

II. JINA LA KITABU

A. Katika Kitabu cha Waebrania majina ya vitabu vya Musa ni moja ya maneno kumi ya kwanza, mara nyingi ni neno lao la kwanza:

1. Mwanzo, "Hapo mwanzo"
2. Kutoka, "Basi majina"
3. Mambo ya Walawi, "Bwana akamwita"
4. Hesabu, "katika bara"
5. Kumbukumbu la Torati, "Haya ndiyo maneno"

B. Katika Buku la Sheria za Kiyahudi (Mishnah Hattorah juu ya 17:18) hii inaitwa "marudio ya sheria."

C. Katika tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale, hii inaitwa Tafsiri ya Maandiko ya Agano la Kale ya Kiebrania kwenda Kiyunani (LXX) iliyoandikwa miaka 250 K.K., inaitwa "sheria ya pili" kwa sababu ya tafsiri isiyo sahihi ya 17:18.

D. Kutokana na Toleo la Kilatini la Jerome tunalipata jina la Kiingereza ambalo analiita "sheria ya pili" (Kumb-ndogo).

III. URASIMISHAJI – Hiki ni kitabu chenye kuihitimisha Torati na chenye kuunda migawanyiko mitatu ya kwanza ya sheria za kidini za Kiebrania.

A. Torati au Sheria – Mwanzo –Kumbukumbu la Torati

B. Manabii:
1. Manabii wa Kale -- Yoshua-Wafalme (isipokuwa Ruthu)
2. Manabii wa Baadaye -- Isaya-Malaki (isipokuwa Danieli na Maombolezo)

C. Maandiko:
1. Majabali (magombo 5):
   a. Wimbo Ulio Bora
   b. Mhubiri
   c. Ruthu
   d. Maombolezo
   e. Esta
2. Danieli
3. Fasihi ya Hekima:
   a. Ayubu
   b. Zaburi
   c. Mithali
4. 1 & 2 Mambo ya Nyakati

IV. AINA YA UWASILISHAJI

A. Kitabu cha Kumbukumbu la Torati ni mfululizo wa jumbe, zenye utangulizi jumuishi na ufafanuzi fungaji wa kifo cha Musa, kwamba Musa alipewa upande wa mashariki mwa Mto Yordani kabla ya Israeli kuingia Nchi ya Ahadi.

B. Pia katika hiki kuna wimbo wa kale /zaburi iliyotungwa na Musa, sura za 31:30-32:43

C. Kama ilivyo Mwa. 49, Kumb. 33 huu ni unabii kuhusu wana wa Yakobo.

D. Kitabu hiki kinayo maelezo yahusuyo kifo cha Musa, sura za 34.

V. UANDISHI

A. Mapokeo ya Kiyahudi:
1. Mapokeo ya kale yanakiri kwamba mwandishi alikuwa Musa.
2. Hili linaelezwa katika:
   a. Buku la Sheria za Kiyahudi- Baba Bathra 14b
   b. Mishnah
   c. Mahubiri Yoshua Mwana wa Sira 24:23 (yaliyoandikwa mnamo 185 K.K.)
   d. Philo wa Iskanda

e. Flavius Josephus

3. Maandiko yenyewe:
   a. Waamuzi 3:4 na Yoshua 8:31
   b. "Musa akazungumza":
      (1) Kumb. 1:1, 3
      (2) Kumb. 5:1
      (3) Kumb. 27:1
      (4) Kumb. 29:2
      (5) Kumb. 31:1, 30
      (6) Kumb. 32:44
      (7) Kumb. 33:1
   c. "YHWH akazungumza na Musa":
      (1) Kumb. 5:4-5, 22
      (2) Kumb. 6:1
      (3) Kumb. 10:1
   d. "Musa aliandika":
      (1) Kumb. 31:9, 22, 24
      (2) Kutoka 17:14
      (3) Kutoka 24:4, 12
      (4) Kutoka 34:27-28
      (5) Hesbu 33:2
   e. Yesu ananukuu au kudokeza kutoka katika Kumbukumbu la Torati na kueleza "Musa aliamuru/"Musa aliandika":
      (1) Mathayo 19:7-9; Marko 10:4-5 - Kumb. 24:1-4
      (2) Marko 7:10 - Kumb. 5:16
      (3) Luka 16:31; 24:27, 44; Yohana 5:46-47; 7:19, 23
   f. Paulo anamsawiri Musa kama mwandishi:
      (1) Warumi 10:19 – Kumb. 32:21
      (2) I Kor. 9:9 - Kumb. 25:4
      (3) Gal. 3:10 - Kumb. 27:26
      (4) Matendo ya Mitume 26:22; 28:23
   g. Petro anamsawiri Musa kama mwandishi katika hotuba yake ya Siku ya Pentekoste – Matendo ya Mitume 3:22
   h. Mwandishi wa Kitabu cha Waebrania anamsawiri Musa kama mwandishi - Waebrania 10:28; Kumb. 17:2-6

B. Wanazuoni wa kisasa

1. Wanathiolojia wengi wa karne za 18 na 19, waifuatishao nadharia izungumziayo uandishi wa aina mbalimbali ya Graf-Wellhausen (J.E.D.P.), inadai kwamba kitabu cha Kumbukumbu la Torati kiliandikwa na kuhani/nabii wakati wa utawala wa Yoshua katika Yuda kukubaliana na matengenezo yake mapya ya kiroho. Hii ingweza kumaanisha kwamba kitabu kiliandikwa kwa jina la Musa mnamo 621 K.K.
2. Haya yanajikita juu ya:
   a. II Wafalme 22:8; II Nya. 34:14-15. “Nimekiona kitabu cha torati katika nyumba ya Bwana.
   b. sura ya 12 inajadili juu ya eneo moja la Hema na Hekalu;
   c. sura ya 17 inajadili juu ya mfalme aliyefuatia;

d. ni kweli kwamba tendo la uandishi wa kitabu kwa jina la mtu aliyepita lilikuwa la kawaida katika Mashariki ya Karibu ya Kale na katika mizunguko ya Kiyahudi;
e. kuna ufanano wa mtindo, misamiati na sarufi kati ya Kumb na Yoshua, Wafalme na Yeremia;
f. Kitabu cha Kumbukumbu la Torati kinachukua kumbukumbu ya kifo cha Musa, sura ya 34;
g. kuna nyongeza za kihariri za waziwazi zilizofuatia ndani ya Vitabu Vitano vya Musa:
   (1) Kumbukumbu la Torati 3:14
   (2) Kumbukumbu la Torati 34:6
h. Wakati mwingine tofauti zisizoelezeka zilizo katika matumizi ya Uungu: El, El Shadai, Elohimu, YHWH, katika mwonekano wa muktadha isiyo unganishwa na vipindi vya kihistoria.

VI. TAREHE

A. Ikiwa hiki kiliandikwa na Musa bado kuna uwezekano wa aina mbili unaohusiana na wakati na muda wa Kuhamishawa kutoka Misri:
   1. Ikiwa I Wafalme 6:1 inamaanisha kuchukuliwa kifasihi na kisha mnamo mwaka 1445 K.K. (karne ya 18 ya utawala wa Thutmose III na Amenhotep II):
      a. Toleo la LXX linazungumzia miaka 440 badala ya miaka 480.
      b. Idadi hii inaweza kuviakisi vizazi na si miaka (kiuwakilishi).
   2. Ushahidi wa utafiti wa mambo ya kale uhusuo mwaka 1290 K.K. Uhamisho (karne ya 19 utawala wa Kimisri):
      a. Seti I (1390-1290) aliyahamisha makao makuu toka Thebes kwenda eneo la bonde - Zoani/Tanis.
      b. Ramesesi II (1290-1224):
         (1) Jina lake linajitokeza katika mji uliojengwa na watumwa wa Kiebrania, Mwa. 47:11; Kut. 1:11;
         (2) Huyu alikuwa na mabinti 47;
         (3) Huyu hakunufaishwa na mwanae wa kwanza.
      c. Miji yote ya Palestina iliyokuuwa imezungushiwa kuta iliharibiwa na kujengwa upya mnamo mwaka 1250 K.K.

B. Nadharia ya wataalamu wa sasa ya uandishi wa namna mbalimbali:
   1. Y (YHWH) 950 K.K.
   2. E (Elohim) 850 K.K.
   3. JE (muunganiko) 750 K.K.
   4. K (Kumbukumbu la Torati) 621 K.K.
   5. M (Makuhani) 400 K.K.

VII. VYANZO VYA KUTHIBITISHA MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. Makubaliano ya Wahiti ya milenia ya 2 K.K. yanatupatia mfumo wa kale, wa historia ya sasa wenye kufananishwa na muundo wa Kitabu cha Kumbukumbu la Torati (pamoja na Kut. -Law. na Yoshua.24). Mwelekeo wa mkataba huu ulibadilishwa na milenia ya 1 K.K. Hili linatupa ushahidi wa kihistoria wa kitabu cha Kumbukumbu la Torati.
   Kwa usomaji zaidi unaohusu eneo hili, angalia G.E. Mendenhall's *Law and Covenants in Israel and the Ancient Near East.*

B. Uelekeo wa Wahiti na ufanano wake wa Kumb:
   1. Dibaji (Kumb. 1:1-5, utangulizi wa mnenaji, YHWH)
   2. Kuyarudia matendo ya Mfalme yaliyopita (Kumb. 1:6-4:49 Matendo ya Mungu yaliyopita kwa Israeli)

3. Maneno ya makubaliano (Kumb. 5-26):
    a. Jumuisho (Kumb. 5-11)
    b. Maalumu (Kumb. 12-26)
4. Matokeo ya Makubaliano (Kumb. 27-29):
    a. Manufaa (Kumb. 28)
    b. Matokeo (Kumb. 27)
5. Ushahidi wa Uungu (Kumb. 30:19; 31:19, pia 32, wimbo wa Musa wenye kutenda kazi kama ushahidi):
    a. nakala ihusuyo Uungu iliyokuwa ndani ya hekalu;
    b. nakala iliyokuwa mikononi mwa mtumishi iliyopaswa kusomwa kwa mwaka;
    c. upekee wa makubaliano ya Wahiti kutoka Ashuru ya baadaye na makubaliano ya Shamu yalikuwa :
        (1) pitio la kihistoria la matendo ya mfalme yaliyopita;
        (2) kipengele cha mara kwa mara.

VIII. VIPENGELE VYA KIFASIHI (muktadha)

A. Utangulizi wa kitabu, 1:1-5

B. Hotuba ya Kwanza, 1:6-4:43 (Matendo ya YHWH yaliyopita kwa siku za leo):

C. Hotuba ya Pili, 4:44-26:19 (Sheria ya YHWH kwa siku za leo na siku zote):
1. Kwa ujumla – Amri Kumi (5-11)
2. Mifano ya kipekee na matumizi (12-26)

D. Hotuba ya Tatu, 27-30 (Sheria ya YHWH kwa wakati ujao 27-29):
1. Tendo la kulaani (27)
2. Baraka (28)
3. Pitio la Agano (29-30)

E. Maneno ya Musa ya Mwisho, 31-33:
1. hotuba ya "Maagano" , 31:1-29
2. Wimbo wa Musa, 31:30-32:52
3. Baraka za Musa 33:1-29

F. Kifo cha Musa, 34

IX. KWELI KUU

A. Maandalizi ya mwisho kabla ya kuingia katika Nchi ya Ahadi. Agano la Mungu pamoja na Ibrahimu (Mwa. 12:1-3) nchi ya ahadi na uzao. Agano la Kale linasisitiza juu ya nchi ya ahadi.

B. Musa anawaandaa watu kwa ajili ya maisha ya kujikita katika kilimo dhidi ya maisha ya kuhama hama. Anafanya marekebisho ya Agano la Sinai kwa ajili ya Nchi ya Ahadi.

C. Kitabu hiki kinasisitiza juu ya uaminifu wa Mungu katika wakati uliopita, wakati uliopo, na wakati ujao. Hili agano, hata hivyo,si amrishi! Lazima Israeli iitikie na kuendelea katika imani, toba na utii. Ikiwa hatafanya hivyo laana zilizo katika sura za 27-29 zinajitokeza kwa uhalisia.

X. WATU, MANENO NA/AU VIFUNGU VYA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

A. Maneno na Vifungu:
1. " nawashuhudizia mbingu na nchi hivi leo," 4:26 (NASB na NIV)

2. "nawapatiliza wana uovu wa baba zao...," 5:9 (NIV, "hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, "... nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao..," 5:10 (NIV, "nami navionyesha upendo maelefu ya vizazi")
3. "Sikiza," (Shema) 6:4 (NASB na NIV)
4. "Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako," (maelekezo) 6:8 (NIV, "kama ishara ya")
5. "yaandike juu ya miimo ya nyumba yako," (*mezuza*) 6:9 (NIV, "juu ya malango")
6. "kitu cho chote katika kitu kilichoharimishwa" *herem*, 13:17 (NIV, "wale wayashutumuyo mambo")
7. "jeshi la mbinguni," 17:3 (NIV, "nyota za mbinguni")
8. "ampitishaye mwanawe au binti yake kati ya moto," 18:10 (NIV, "dhabihu")
9. mtu alogaye, 18:11 (NASB na NIV)
10. uliowakomboa, 21:8 (NASB na NIV)
11. " hampendi," 21:15 (NIV, "si kwa ajili ya wengine")
12. " aliyetundikwa," 21:23 (NASB na NIV)
13. " mshahara wa mbwa," 23:18 (NIV, "ujira wa...malaya wa wanaume")
14. " hati ya kumwacha," 24:1 (NASB na NIV)
15. " usijipake mafuta," 28:40 (NIV, "usitumie mafuta")


B. Watu wa kuwatambua kimuhtasari:
1. Anakim, 1:28 (NIV, "wa-Anaki")
2. Warefai, 3:11 (NIV, "Warefai")
3. Wahiti, 7:1
4. Asherimu, 7:5 (NIV, "fito za shera")
5. Nabii, 18:15-22
6. Yeshuruni, 32:15; 33:5, 26

XI. MAENEO KWA RAMANI (Kwa hesabu)
1. Ml. Horebu, 1:2,6,19; 4:10,15
2. Ml. Seiri, 1:2,44; 2:1,4,5,8,12,22 ( aina ya mlima)
3. Kadeshi Barnea, 1:46; 32:51 (NIV, "Kadeshi")
4. Bashani, 1:4; 3:1,3,4,10,11,13; 4:43,47
5. Elati, 2:8 (Ezioni-Geberi)
6. Ml. Hermoni, 3:8,9; 4:48
7. Ml. Ebali, 11:29; 27:4,13
8. Ml. Gerizimu, 11:29; 27:12
9. Ml. Hori, 32:50 (Yebel Haruni)

XII. MASWALI YA KI-MAUDHUI KWA MWANAFUNZI
1. Ni kwa namna gani kitabu cha Kumbukumbu la Torati kinatofautiana na Hesabu (Aina)?
2. Kwa nini Musa anairudia historia ya kitabu cha Kutoka?
3. Kwa nini kuna rejea nyingi za kuwafundisha watoto wako, (4:9; 6:7, 20-25; 11:19; 32:46)?
4. Ni kwa namna gani toleo la kitabu cha Kumbukumbu la Torati na Amri Kumi za Mungu ni tofauti na kitabu cha Kutoka 20?
5. Kwa nini waliambiwa kuzivunja zibomosheni nguzo zao na kuyakata Maashera yao (7:5)?
6. Ni kwa namna gani 10:12-21 inatoa sifa pambanuzi za kitabu cha Kumbukumbu la Torati?
7. Kwa nini sura za 27-29 ni muhimu sana katika kulifasiri Agano la Kale zima?
8. Nani aliyechukua kumbukumbu ya kifo cha Musa (34)?


KAS
MAGH
MASH
KUS
MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE

# PALESTINA



# UTANGULIZI WA YOSHUA

I. JINA LA KITABU

A. Jina la kitabu linakuja kutoka kwa aliyemrithi Musa na muhusika mkuu wa kitabu.

B. Jina lake linaundwa na maneno mawili ya Kiebrania:
   1. YHWH (J ikiwa na irabu)
   2. wokovu (Hoshea)

C. Hii hakika ni jina lile lile la Kiebrania kama Yesu (Mt. 1:21).

II. URASIMISHAJI

A. Yoshua ni kitabu cha kwanza ya sehemu ya Kanoni ya Kiebrania ijulikanayo kama "Manabii."

B. Sehemu hii imegawanyika katika sehemu kuu mbili:
   1. manabii wa kale ambayo inajumuisha - Wafalme (isipokuwa Ruthu).
   2. manabii wa baadaye ambao ilijumuisha Isaya - Malaki (isipokuwa Danieli na Maombolezo).

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Vitabu hivi vya kihistoria vya watu wa Mungu ambayo imeanzia Mwanzo. Sio historia yenye mtiririko wa kimagharibi bali ni historia ya kithiolojia yenye kubagua nini cha kusimulia na nini cha kuacha. Haimaanishi kwamba inamaanisha sio kweli au sahihi lakini inamaanisha kwamba waandishi walichagua matukio fulani ili kufundisha ukweli wa kithiolojia kuhusu Mungu, mwanadamu, dhambi, wokovu, n.k.Kwa namna hii ni sawa na Injili na Matendo ya Mitume katika Agano Jipya

B. Historia kwa ajili ya Wayahudi haikuwa ya kimzunguko kama ya majirani zake ikijikita katika mizunguko ya asili bali ilikuwa "ya kimatukio."Ilikua yenye lengo na makusudi. Mungu alikuwa akitembea katika lengo aliloliweka hapo kabla, yaani ukombozi wa ulimwengu ulioanguka (Mwa. 3:15).

IV. UANDISHI

A. Mwandishi wa kidesturi ni Yoshua:
   1. jina lake kwa asili lilikuwa Hoshea (wokovu), Hes. 13:8.
   2. Musa andiye aliyelibadili jina lake kuwa Yoshua (YHWH “ni” wokovu), Hes. 13:16.
   3. kwasababu zisizoojulikana jina lake linatamkwa kwa namna tofauti tofauti nne:
      a. *yeshoshu'a*, (kawaida) Yosh. 1:1
      b. *yehoshu'a*, Kumb. 3:21
      c. *hoshe'a*, Kumb. 32:44
      d. *yeshu'a*, Neh. 8:17

B. BabaBathra 14b anasema kwamba Yoshua aliandika kitabu isipokuwa kwa masimulizi ya kifo chake ambayo yalinukuliwa na kuhani aitwaye Elieza, 24:29-30 na kwamba mwanaye Finehasi (Kumb. 25:7-13; 31:6-8; Yosh. 22:10-34), alimaliza kitabu chake ambacho kinanukuu kifo cha Elieza, 24:31-33.

C. Mtu aitwaye Yoshua:
   1. alizaliwa utumwani huko Misri
   2. moja ya wapelelezi kumi na mbili; ni yeye tu na Kalebu walioleta taarifa yenye imani (Hes. 14:26-34)

3. Msaidizi mwaminifu wa Musa katika safari yote kutokea Misri. Alikuwa ni yeye pekee aliyepanda na Musa juu ya Mlima Sinai (nusu ya safari - Kut. 24:13-14).
4. Kamanda wa jeshi la Israeli (Kut. 17:8-13)
5. aliongoza jeshi la Kanaani kama mbadala wa Musa (Kumb. 31:23)

D. Baadhi ya Ushahidi wa uandishi wa Musa:
1. Kitabu kinazungumzia Yoshua akiandika agano la Mungu na watu, 24:26, hivyo tunajua aliandika.
2. Ni nyaraka yenye ushuhuda wa macho wa dhahiri:
    a. "sisi," 5:1 (utofautiano wa MSS)
    b. "Yoshua akawatahiri," 5:7-8
    c. kukutana kwa Yoshua binafsi na Malaika wa BWANA, 5:13-15
    d. "Yeye (Rahabu) ameishi kati ya Israeli hata leo," 6:25 (Huu si uhariri wa baadaye bali ushuhuda wa macho wa kisasa)
3. alitumia baadhi ya vyanzo vilivyoandikwa:
    a. kitabu cha Yashari, 10:13 (II Sam. 1:18)
    b. "katika kitabu," 18:9
4. uorodheshaji sahihi wa majina ya miji ya kale ambayo yanashabihiana na mwandishi wa kisasa na sio uhariri wa baadaye:
    a. Yerusalemu ikiitwa Yebusi, 15:8; 18:16, 28
    b. Hebroni ikiitwa Kiriath-arba, 14:15; 15:13,54; 20:7; 21:11
    c. Kiriath - yearimu inaitwa Baalah - 15:9, 10
    d. Sidoni ikirejerewa kama mji mkuu wa Foenike, sio Tiro, 11:8; 19:28, ambayo baadaye ilikuwa mji mkuu.
5. Yoshua kama vitabu vitano vya Torati, lina nyongeza baadhi zilizohaririwa:
    a. kifo cha Yoshua
    b. Vita ya baadaye ya Hebroni, 14:6-15; 15:13-14
    c. vita ya baadaye ya Debiri, 15:15,49
    d. uhamiaji wa Dani wa kusini, 19:47
    e. kauli "hata leo hii" inatokea mara nyingi kitu kinachoonesha uhariri uliofanywa hapo baadaye, 4:9; 5:9; (6:25); 7:26 (mara mbili); 8:28-29; 9:27; 10:27; 13:13; 14:14; 15:63; 16:10; 22:3

E. Uanazuoni wa Kisasa:
1. tazama ufanano kati ya Vitabu Vitano vya Musa na Yoshua:
    a. Staili ya uandishi
    b. Misamiati

2. Toleo la Documentary Hypotheses la J, E, D, P inaangalia kitabu kuandikwa muda mrefu sana kwa mikono mingi:
    a. chanzo J kiliandika sehemu za sura za 1-12 ambazo zinajikita katika mapigano binafsi (950-850 K.K.)
    b. chanzo E kiliandika sehemu za sura za 1-12 ambazo zinajikita katika kampeni ya pamoja (750 K.K).

c. A muunganiko wa J & E unatokea mnamo 650 K.K. ambayo sehemu kubwa ya J haikuzimuisha
d. Kitabu kiliharitiwa tena na makuhani/manabii wa enzi za Yosia aliyeandika Kumbu kumbu la Torati. Mtu huyu au kundi linaitwa chanzo cha Kumbu kumbu la Torati. Chanzo hiki pia kiliandika Kumbu kumbu la Torati. Kuimarisha mabadiliko ya Yosia mnamo mwaka 621 K.K. kwa kuweka shabaha kwa Yerusalemu kama madhabahu pekee ya kweli.
e. Ile chanzo P kilikuwa kundi la makuhani walioandika sura ya 13-21 mnamo mwaka 400 K.K.
f. bado maongezeko zaidi yalifanywa katika karne ya 3 K.K

3. Tazama mapendekezo ya nadharia! Tazama namna ikatavyo andiko kutoka katika mazingira yake ya kihistoria. Jaribio lake la kisasa kuchambua maandiko ya kale katika ufahamu wa nadharia za kiuandishi wa kisasa. Hatahivyo lazima isemwe:
   a. Mwandishi wa kitabu cha Yoshua hatajwi.
   b. Kifo cha Yoshua kama Musa linaandikwa katika kitabu.
   c. Kuwekuwepo na uhariri unaoendelea wa vitabu vya Agano la Kale.
   d. Tunakubali mchakato wa uundwaji ambao ulipelekea Agano la Kale kuwa na uvuvio.
   e. Ushashidi dhidi ya Vitabu Tisa vya Musa. (Mwa. - Yosh.):
      (1) Katika desturi za Kiyahudi kuna utofautiano wa kidhahiri kati ya vitabu vitano vya Musa (Vitabu Vitano vya Musa) na Yoshua anaanza na "Manabii" ambayo ni sehemu ya Kanoni ya Kiebrania:
         (a) BenSira the author of Ecclesiasticus, mwandishi wa Ecclesiasticus, iliyoandikwa mnamo mwaka 185 K.K, inatusaidia kupata utofautiano, 48:22-45:12.
         (b) Falvius Josephus katika kitabu chake Contra Apioness1:7ff anatengeneza utofauti.
         (c) Sehemu ya ufungaji ya Andiko la Kimasoteri (MT) Vitabu vitano vya Musa inatengeneza utofautiano.
         (d) Sehemu ya kila Wiki ya usomaji wa Biblia ya Sinagogi iliita "the Haphtaroth" inapotutengenezea tofauti.
         (e) Kitabu cha Kisamaria kilichukua Vitabu Vitano vya Musa kama maandiko lakini si kitabu cha Yoshua.
      (2) ushahidi wa ndani (Young, ukur.158):
         (a) Kuna matumizi maalum ya uwakilishi wa binafsi katika Yoshua ambayo haipo katika Vitabu Vitano vya Musa.
         (b) Mji wa Yeriko unatamkwa tofauti.
         (c) Jina kwa ajili ya Mungu, "Mungu wa Israeli," inatokea katika Yoshua mara 14 lakini halipo katika Vitabu Vitano vya Musa.
   f. Lazima tukiri kwamba kuna mengi tusiyoyajua juu ya uundwaji wa vitabu hivi vya Agano la Kale katika hali yake ya sasa.

V. TAREHE

A. Kitabu hiki kinashughulikia vita ya Nchi ya Ahadi. Kwakuwa hatuna uhakika juu ya tarehe za Safari ya kutoka Misri na Kipindi cha Utangaji wa Jangwani, hatuna uhakika juu ya tarehe ya vita:
   1. 1445 - 40 — mnamo mwaka 1400 K.K. (I Wafalme. 6:1)
   2. 1290 - 40 — mnamo mwaka 1250 K.K. (akiolojia)

B. Yoshua aliandikwa au kuhaririwa katika kipindi cha Waamuzi; miji fulani ilibadilishwa majina yake baada ya utawala wa Israeli. Moja ya mfano mmojawapo ni mji wa Wakanaani wa Zefa ambao baadaye ulibadilishwa na kuitwa Hormah, Waamuzi 1:16-17. Hatahivyo jina la baadaye linasomwa tena katika Yoshua, 12:14; 15:30; 19:4.

C. R. K.Harrison anabashiri na kudhania kwamba liliandikwa wakati wa utawala wa Daudi kwa kufanywa na Samweli na kwamba Samweli anaweza kuwa chanzo cha desturi za Shiloh (kama vile *Introduction to the Old Testament*, ukur. 673.

VI. VYANZO VINAVYOTHIBITISHA MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. Akiolojia imeonesha kwamba miji mikubwa yenye kuta kbwa ya Kanaani iliharibiwa na ikiajengwa mnamo mwaka 1250 K.K:
1. Hazori
2. Lakishi
3. Betheli
4. Debiri (hapo kabla ikiitwa Kerioth Sepher au Kirath Sepher, 15:15)

B. Akiolojia imekuwa ikishindwa kuthibitisha au kukataa habari ya kibiblia ya kuanguka kwa Yeriko. Hii ni kwasababu eneo liko katika mazingira mabaya:
1. hali ya hewa/eneo
2. kujengwa upya kwa eneo la kizamani kwa kutumia vitu vya zamani zaidi
3. kutojulikana  kwa tarehe za wajenzi

C. Akiolojia imepata madhabahu juu ya mlima Ebali ambayo inaweza kuwa imeunganishwa na Yoshua 8:30-31 (Kumb. 27:2-9). Hii ni sawasawa na maelezo yanayopatikana katika Mishnah (Lijitabu la desturi za Sheria za kiyahudi).

D. Maandiko ya Ras Shamra yanayopatikana katika Ugariti yanaonesha maisha ya Wakanaani na dini ya mnamo miaka ya 1400 K.K:
1. asili ya kuabudu miungu mingi (desturi za ustawi)
2. El alikuwa mungu mkuu
3. El mjakazi wake El alikuwa Ashera (baadaye anakuwa suria wa Baali)
4. mtoto wao alikuwa Baali (Haddadi), mungu wa dhoruba
5. Baali alifanyika "mungu mkuu" wa ibada za wakanaani. Anati alikuwa mjakazi wake.
6. Aina za sherehe zilikuwa sawasawa na Isisi na Osiria wa Misri
7. Ibada za Baali zilijikita katika maeneo ya mahali pamoja “maeneo muhimu” au jukwaa la kwenye jiwe (ukahaba wa ibada).
8. Baali aliwakilishwa kwa nguzo ya mawe iliyoinuliwa (ishara ya mungu), wakati Ashera au Astarte aliwakilishwa kwa mbao iliyopinda ya gogo nene, au mti ambao bado mupo hai ambao uliwakilisha "mti wa uzima."

E. Akiolojia imethibitisha kwamba Falme kubwa za eneo (Wahiti, Wamisri na Mesopotamia) hawakuwa na uwezo na kushawishi katika Palestina wakati wa kipindi hiki kilichojulikana kama Kipindi cha Shaba cha NLate (1550 - 1200 K.K.).

F. Orodha sahihi ya majina ya miji ya kale yanashabihiana na mwandishi wa kisasa na sio mhariri wa baadaye:
   1. Yerusalemu iliitwa Yebusi, 15:8; 18:16,28 (15:28 inasema Wayebusi bado waliendelea kubaki katika sehemu ya Yerusalemu)
   2. Hebroni iliitwa Kiriath-arba, 14:15; 15:13,54; 20:7; 21:11
   3. Kiriath-yearim inaitwa Baalah, 15:9,10
   4. Debiri inaitwa Kiriath-sannah, 15:49
   5. Sidoni ilirejerea mji mkubwa wa Foenike, sio Tiro, 11:8; 13:6; 19:28, ambao baadaye ulikuja kuwa mji mkuu.

G. Yoshua 24 hakika unashabihiana na mkataba wautaratibu wa Wahiti (kama Kumbu kumbu la Torati) wa Milenia ya Pili K.K.

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI (muktadha)

A. mwenendo wa kijiografia unatengeneza uainisho wa kitabu:
   1. unaanza katika uwanda wa Moabu, 1-2
   2. kuvuka kwa Mto Yordani mpaka Gilgali karibu na Yeriko, 3-4
   3. Kampeni ya kijeshi ya Kanaani kati, 5:1-10:15
   4. Kampeni ya kijeshi ya Kanaani kusini, 10:16-43
   5. kampeni ya kijeshi ya Kanaani kaskazini, 11:1-23
   6. mgawanyo wa kijiografia wa nchi kati ya makabila, 12-21

B. Muhtasari mfupi:
   1. Utawala wa Kanaani, 1-11
   2. kugawanya kwa Nchi ya Ahadi kati ya Makabila, 12-21
   3. maneno ya mwisho na kifo cha Yoshua, 22-24

VIII. KWELI KUU

A. Kuonesha uweza wa Mungu na uaminifu kwa ahadi Yake kwa Ibrahimu (Mwa. 12:1-3) juu ya nchi (Mwa. 15:16).

B. Inaendeleza historia ambayo ilianza huko Mwanzo na kuletwa katika kipindi kipya. Wakati huu uhusiano wa kihiari wa kimakabila ulikuwa kiunganishi cha muhimu sana. Hakukuwa na serikali kuu.

C. Dhana ya "Vita vitakatifu" (herem- "vilivyo chini ya kikwazo") vinaonekana vya ukatili sana kwetu lakini Mungu aliwaonya waisraeli dhidi ya dhambi za Wakanaani. Kama ambavyo Mungu aliwaondoa katika nchi kwasababu ya dhambi zao, pia atawaondoa Wayahudi kwa dhambi hizo hizo (Uhamishoni, kwa Ashuru na Babeli).

IX. MANENO NA/AU TUNGO NA WATU WA KUTAMBUA KWA MUHTASARI


A. Maneno na/au tungo:
   1. vivukoni 2:7 (NASB & NIV)
   2. visu vya mawe ya gumegume, 5:2 (NASB & NIV)
   3. "nchi ijaayo maziwa na asali," 5:6 (NASB & NIV)
   4. "vua viatu vyako," 5:15 (NIV, “ondoa viatu vyako”)
   5. "takatifu" (*kadosh*), 5:15

6. "chini ya vikwazo," (*herem*), 6:17 (NIV, "kutolewa")
7. "jua linasimama huko Gibeoni," 10:12 (NASB & NIV)
8. "wakanyage wafalme hawa shingoni mwao," 10:24 (NASB & NIV)
9. (miji ya kilawi), 21:1-3 (NIV, “Musa lituamuru kwamba mtupatie sisi miji tuishi ndani yake”)
10. "mtumishi wa Bwana," 24:29 (NASB & NIV)


B. Watu wa kutambuliwa kwa muhtasari:
1. Rahabu, 2:1
2. "kiongozi wa majeshi ya Bwana," 5:14 (NIV, "kamanda wa jeshi la BWANA,")
3. Akani, 7:1
4. Selofehadi, 17:3
5. Finehasi, 22:12

X. MAENEO KI-RAMANI (kwa hesabu)
1. Bahari Kuu, 1:4
2. Shitimu, 2:1
3. Adamu, 3:16
4. Ai, 7:2
5. Gibeoni, 9:3
6. Negebu, 11:16
7. Araba, 11:16
8. Heshboni, 12:5
9. kitabu cha Wamisri, (*wadi al ‘arish*), 15:4 (NIV, “wadi ya Misri”)
10. bonde la Hinnom, 15:8 (NIV, “Bonde la Ben Hinnom”)
11. Shekemu, 17:7
12. Megiddo, 17:11
13. Shilo, 18:1
14. Beersheba, 19:2

XI. MASWALI YA MWANAFUNZI YA KIMAUDHUI YANAYOHITAJI MAJIBU KWA MUHTASARI
1. Ni kwa namna gani Mungu anamtia moyo Yoshua kama alivyofanya kwa Musa (1:1 na kuendelea; 5:13-15)?
2. Elezea namna gani Wana wa Israeli walitakiwa kuvuka Yordani kwa imani (3).
3. Kwanini Manna ilikata?
4. Kwanini jeshi la Israeli lilishindwa huko Ai?
5. Ni kwa namna gani Wagibeoni walimfanyia ujanja Yoshua?
6. Je ni hakika kwamba Sura ya 10 ni muujiza? Kwanini/Kwanini sio?
7. Elezea uhusiano kati ya miji ya Kilawi na miji ya makimbilio.
8. Tatizo gani linalotokea katika sura ya 22?


KAS
MAGH
MASH
KUS
MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE

# PALESTINA



# UTANGULIZI WA WAAMUZI

I. JINA LA KITABU

A. Jina linatoka katika neno la kiebrania "*shophetim*" ambalo linamaanisha "kusuluhisha mgogoro." Neno hili la Kiebrania ni sawa na:
   1. neno la kifoenike "regent (mshauri)"
   2. neno la ki-Akkadia "ruler (mtawala)"
   3. neno la ki-Kushi, "hakimu mkuu"

B. Lilifasiriwa katika LXX kama "*krital* (mwamuzi)" au hakimu.

C. Jina letu la Kingereza lilitoka katika Kilatini "*judicum* (kuamua kwa sheria)."

D. Neno la Kingereza linapotosha kwasababu watu hawa hawatendi kazi kimahakama lakini ni viongozi wenye uwezo wa kubadilika kimaamuzi wa eneo fulani walioinuliwa na Mungu na kupewa uwezo na Roho Mtakatifu (3:10;6:34; 11:29; 14:6,19; 15:14), kushughulikia makusudi fulani ya kuwaokoa watu wake kutoka wa mtesi wa kigeni (kama vile 2:16). Jina zuri linaweza kuwa "Waokoaji."

II. URASIMISHAJI

A. Hiki ni kitabu cha pili cha mgawanyo wa pili wa Kanoni ya Kiebrania. Inaitwa Manabii.

B. Mgawanyo wa pili una migawanyo midogo miwili:
   1. manabii waliotangulia ambao tunaita vitabu vya kihistoria: Yoshua - Wafalme (isipokuwa Ruthu)
   2. manabii waliofuatia ambao tunawaita manabii: Isa. - Mal. (isipokuwa Dan. na Maombolezo.)

III. AINA YA UWASILISHAJI - Hiki kimsingi kinaitwa simulizi ya kihistoria

IV. UANDISHI

A. Biblia yenyewe iko kimya

B. Baba Bathra 14b inasema kwamba Samweli alikiandika kitabu kinachobeba jina lake na Waamuzi na Ruthu.

C. Kitabu kinachukua muda wa kipindi cha miaka mingi, hivyo hakiwezi kuwa na mwandishi shuhuda wa macho mmoja

D. Kitabu kimekusanya yawezekana kutoka:
   1. vyanzo kadhaa vya kuandikwa visivyotajwa kama vile:
      a. "The book of the Wars of the Lord (Kitabu cha Vita za Bwana)" ikiwa ni moja ya chanzo cha kihistoria kinachotajwa katika Hes. 21:14
      b. "The book of Jashar (Kitabu cha Yashari)" ambacho ni chanzo kingine cha kihistoria kinachotajwa katika Yoshua 10:13 na II Samweli 1:18
   2. Yawezekana vyanzo vingine kadhaa vya mdomo. Historia sahihi za midomo zilikuwa zimezoeleka katika Mashariki ya Kale ya Karibu ambapo nyaraka za kuandikwa zilikuwa ghali sana na ngumu kubeba. mfano huo ungekuwa:
      a. "Mambo ya Nyakati ya Samweli muonaji,…..Nabii Nathan,……Gadi muonaji" katika 1 Nyakt. 29:29

E. Inavyoonekana kwamba mtunzi wa asili aliandika wakati wa mwanzo wa Ufalme ulioungana:

1. Betlehemu inatajwa mara kumi yawezekana ikiaksi siku za Daudi (kama vile 17:7,8,9; 19:1,2,18 [mara mbili]).
2. Maandiko kadhaa yanaaksi kipindi cha kifalme kwa tungo "siku hizo hakukuwa na mfalme katika Israeli"(kama vile 17:6; 18:1;19:1;21:25). Kulikuwa na Wafalme katika mataifa yanayozunguka mji katika mataifa mengine, ingawa sio katika Israeli.

F. Kuna ushahidi wa mhariri wa baadaye:

1. 18:30 inaaksi:
    a. Uhamisho wa Ashuru wa makabila kumi ya kaskazini mnamo mwaka 722 K.K.
    b. yawezekana kutekwa kwa Sanduku na Wafilisti katika siku za Eli, I Sam. 1-7.
2. Desturi za Kiyahudi kwamba Yeremia na/au Ezra mwandishi alihariri sehemu za Agano la Kale. Uuundwaji wa Agano la Kale katika muundo wake wa kisasa umepotezwa kwetu. Hatahivyo hii haiathiri uvuvio wake wa Kiungu wa vitabu hivi vya Agano la Kale.

V. TAREHE

A. Ingawa vimeandikwa na mtungaji yawezekana wakati wa utawala wa Daudi hii haimaanishi kwamba nyaraka za kihistoria hazitokani na vyanzo vya shuhuda wa macho. Kuna mifano miwili mizuri ya hili:

1. Katika 1:21 Wayebusi bado wanashikilia ngome ya ndani ya Yebusi (baadaye Yerusalemu). Daudi hawezi kuteka ngome hii mpaka 2 Sam. 5:6 na kuendelea.
2. Katika 3:3 Sidoni, sio Tiro, inaorodheshwa kama mji mkuu wa Foenike.

B. Kitabu kinachukua kipindi cha muda mara tokea baada ya utawala wa Yoshua mpaka kuzaliwa kwa Samweli. Tarehe za Mwanzo zinategemea tarehe za Kutoka (1445 K.K. au 1290 K.K), 1350 K.K. au 1200 K.K. Tarehe ya mwisho ingeweza kuwa mnamo mwaka 1020 K.K., ambao ni mwanzo wa utawala wa Sauli (Bright).

C. Ikiwa mtu anajumlisha muda wote unaotolewa kwa Waamuzi, inakuja kati ya miaka 390-410. Hii haiwezi kuchukuliwa kwa mtiririko wa mfuatano wa matukio kwasababu kuanzia 1 Wafalme 6:1 Biblia inasema kwamba kulikuwa na miaka 480 kati ya Safari ya Jangwani na Ujenzi wa Hekalu la Sulemani, mnamo mwaka 965 K.K. Hii inamaana kwamba Waamuzi kimsingi walikuwa viongozi wa mahali pamoja na kwamba muda wao lazima unaingiliana.

VI. MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. Mwanzoni sura za Waamuzi zinatuonesha sisi namna gani utawala wa Yoshua ulikuwa una mipaka. Yoshua kimsingi aliushinda mji mkuu wa Wakanaani uliowekewa uzio wa kuta na uwezo wao wa kijeshi. Mungu aliacha kazi kubwa ya makazi kwa kila kabila katika maeneo yao wenyewe, 2:6. Mbinu hii ilikuwa ni kukijaribu kizazi kipya cha Waisraeli ambao walikuwa hawajapata nafasi ya kuona miujiza na maajabu ya Mungu ya Safari ya Jangwani na Uweza wa kutawala vita, 2:1-10; 3:1.

B. Kizazi kipya kiliwekwa katika jaribu, 2:11 na kuendelea 3:7,12; 4:1; 6:1; 10:6; 13:1. Mungu aliwarejea watu wake kwa kutuma mtesi wa kigeni kuwaadhibu watu wake. Watu walitubu na kumlilia Mungu kwa ajili ya msaada. Mungu aliwatumia "mkombozi." Alafu kwa kipindi fulani cha miaka nchi ilikuwa shwari. Huu utaratibu kimsingi ambao unaelezea kitabu cha Waamuzi, 2:6-16:31. ("Dhambi, Huzuni, Sala, Wokovu.")

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI

A. Inaonekana kwamba muda wa Waamuzi kithiolojia unaelezewa kwa namna mbili tofauti tofauti. Hii mitazamo mitatu inatengeneza uainisho wa kitabu:
1. matokeo ya ushindi wa Yoshua
2. hitaji la wakombozi
3. mifano ya ukanaji imani

B. ainisho fupi la Muhtasari wa Kitabu:
1. hadithi fupi ya ushindi, 1:1-2:5
2. dhambi, hukumu na ukombozi wa watu wa Mungu, 2:6-16:31
3. mifano mitatu ya dhambi ya watu wa Mungu ambayo inafunua hali ya hewa ya kimaadili ya siku:
   a. ibada za sanamu za Mika, 17
   b. Uhamaji wa Dani, 18
   c. Dhambi ya kingono ya Gibea, 19-21

C. Waamuzi wakuu na adui zao

| JINA | ANDIKO | ADUI | MUDA wa AMANI (1) au MUDA wa HUKUMU (2) |
|---|---|---|---|
| 1. Othnieli | 3:7-11 | Mesopotamia (Cushan-Rishathaim) | Miaka 40 (1) |
| 2. Ehud | 3:12-30 | Moabu (Egloni) | Miaka 80 (1) |
| 3. Deborah (Barak) | 4:1-24 (riwaya)<br>5:1-31 (ushairi) | Mkanaani (Yabin na Sisera) | Miaka 40 (1) |
| 4. Gideoni | 6-8 | Mmidiani na Muamaleki | Miaka 40 (1) |
| 5. Yefta | 10:17-12:7 | Muamoni(& Efraimu) | Miaka 6 (2) |
| 6. Samsoni | 13-16 | Mfilisti | Miaka 20 (2) |

D. Waamuzi wadogo:

| Jina | Andiko | Adui | Muda wa Hukumu |
|---|---|---|---|
| 1. Shamgar | 3:31 | Wafilisti | ? |
| 2. Tola | 10:1-2 | ? | miaka 23. |
| 3. Yairi | 10:3-5 | ? | miaka 22. |
| 4. Ibzan | 12:8-10 | ? | miaka 7. |
| 5. Eloni | 12:11-12 | ? | miaka 10. |
| 6. Abdoni | 12:13-15 | ? | miaka 8. |

E. Abimeleki, 9:1-57:
1. huyu alikuwa mwana wa Gideoni aliyempata kwa mjakazi

2. aliathiri mji mmoja tu, Shekemu
3. yeye ni tofauti na waamuzi wengine

VIII. KWELI KUU

A. Kitabu hiki kwa dhahiri kinaonesha matokeo endelevu ya Anguko:
   1. Kila kizazi kilichofuatia kilivunja Agano na kufuata miungu ya Ustawi ya Wakanaani.
   2. Hata katika Nchi ya Ahadi pamoja na kuwepo kwa makabila yaliyotolewa na Mungu kuwashinda Wafilisti.

B. Mungu alitumia watu Wapagani kuhukumu watu Wake (baadaye Shamu, Ashuru na Babeli). Hii inaaksi kulaaniwa kwa sehemu ya Kumb. 27-29.

C. Kitabu hiki kinaonesha hitaji la mfalme wa haki kuongoza makabila yaliyoungana.

D. Kitabu hiki kinaendeleza historia ya watu wa Kiyahudi ambayo ilianza katika Mwanzo.

IX. MANENO NA/AU TUNGO NA WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHTASARI

A. Maneno na Tungo:
   1. kata vidole gumba vyaona vidole vyao vikubwa vya miguuni, 1:7 (NASB & NIV)
   2. kupuliza pembe, 3:27 (NIV, "...baragumu")
   3. konzo la ng'ombe, 3:31 (NASB & NIV)
   4. nabii mke, 4:4 (NASB & NIV)
   5. makusanyo, 8:2 (NASB & NIV)
   6. "Mwaloni wa Muonenimu" (*terebinth*), 9:37 (NIV, "Mti wa mtabiri")
   7. Shibbolethi, 12:6 (NASB & NIV)
   8. "kila mtu alitenda kile kilichokuwa sawa machoni pake mwenyewe" 17:6; 18:1; 19:1;21:25 (NIV, "kila mtu akatenda kama alivyopendezwa yeye mwenyewe")
   9. "mungu ya ndani,"(*teraphim*), 18:17 (NIV, "miungu ya nyumbani")
   10. "watu mabaradhuli" (*beliali*), 19:22 (NIV, "watu waovu")

B. Watu wa kuwatambua kwa muhtasari:
   1. Sisera, 4:2
   2. Baraki, 4:6
   3. Yaeli, 4:17
   4. Yerubbaali, 6:32; 7:1(NIV, "Yerub-baali")
   5. Abimeleki, 9:1
   6. Kemoshi, 11:24
   7. Dagoni, 16:23


X. MAENEO YA KI-RAMANI (kwa hesabu)

1. Miji ya mitende, 1:16; 3:13
2. Aradi, 1:16 13
3. Betheli, 1:22
4. Megiddo, 1:27
5. Gezeri, 1:29
6. Acco, 1:31
7. Hazori, 4:2
8. Rama, 4:5
12. Shekemu, 9:1
13. Mizpa, 10:17
14. Mto Arnoni, 11:13
15. Mto Yabbok, 11:13
16. Timnah, 14:1
17. Ashkeloni, 14:19
18. Gaza, 16:1
19. Shilo, 18:31

9. Mlima Tabori, 4:6
10. Mto Kishoni, 4:7
11. Bonde la Yezreeli, 6:33
20. Yebusi, 19:10
21. Gibea, 19:12


XI. MASWALI YA KIMAUDHUI YA MWANAFUNZI

1. Kwanini hadithi za ushindi katika Yoshua 1-12 ni tofauti sana na Waamuzi 1-2?
2. Kwanini Makabila ya Israeli yalitakiwa kuwauwa Wakanaani wote na kutokufanya nao maagano?
3. Kwanini baadhi ya Waamuzi wanaitwa Wakubwa na baadhi wanaitwa Wadogo?
4. Kwanini Sura za 4 – 5 zinazungumzia Mungu kutumia uongozi wa kike?
5. Kwanini Mungu alimtaka Gideoni kupunguza jeshi lake katika sura ya 7?
6. Je sadaka ya mtoto wa Yefta ilimwendea Mungu (11:30-40)?
7. Ni kwa namna gani Mungu anaweza kumtumia Mtu mwenye tamaa kama Samsoni?
8. Kwanini ilikuwa ni dhambi kwa kabila la Dani kutafuta eneo lingine?




MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE

# PALESTINA




VIPIMO KATIKA MAILI

# UTANGULIZI WA RUTHU

I. JINA LA KITABU

Kitabu kinapewa jina kulingana na wahusika wake wakuu, Ruthu, Wamoabi na wazao wa kike wa Daudi na Yesu, Mt. 1:5.

II. URASIMISHAJI

A. Kitabu hiki ni sehemu ya mgawanyo wa tatu wa Kanoni ya Kiebrania iitwayo "Maandiko."

B. Pia ni sehemu ya kundi maalumu la vitabu vitano vidogo viitwavyo Megilloth au "Magombo Matano." Kila moja ya vitabu hivi vidogo: Ruthu, Esta, Muhubiri, Wimbo uliobora, Maombolezo vinasomwa siku za karamu tofauti. Ruthu kinasomwa wakati wa Pentekoste au Karamu za Majuma.

C. Toleo la LXX linaweka Ruthu baada ya Waamuzi. Josephus katika *Contra Apion*, 1:8, anasema kwamba kulikuwa na vitabu 22 tu katika Agano la Kale. Hii ingeweka mamlaka kwamba Waamuzi na Ruthu vilihesabiwa kama kitabu kimoja. Hivyo, ujumuishwaji wake katika sehemu ya "Maandiko" inaweza kuwa ilikuja baadaye (Jerome).

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Kitabu hiki kwa dhahiri ni simulizi za kihistoria, kinachosimuliwa kupitia mazungumzo ya pande mbili. Kitabu kinaundwa na mistari 85; kati ya hesabu hii, 50 ni mazungumzo ya pande mbili. Mwandishi huyu alikuwa msimuliaji mzuri sana wa hadithi.

B. Baadhi ya Wanazuoni wanahisi kitabu hiki ni tamthiliya, siyo historia kwasababu ya:
1. maana zake za uwakilishi za majina ya wahusika
   a. Mahlon = ugonjwa
   b. Chilion = kupoteza
   c. Orpah = shingo-ngumu
   d. Naomi = utamu wangu
2. namna isiyo ya kawaida kwamba wahusika wote ni wa kuheshimika
3. imani kali na yenye nguvu ya kidini inayoonyeshwa na wahusika katika kipindi cha Waamuzi, 1:1

IV. UANDISHI

A. Kama ilivyo juu ya vitabu vingi vya Agano la Kale mwandishi wake hajulikani.

B. Baba Bathra 14b anasema Samweli aliandika kitabu chake na Waamuzi na Ruthu. Kwakuwa Ruthu 4:17,22 inamaanisha kwamba Daudi alikuwa akijulikana sana kitu kinachoonekana kuelekea lakini haiwezekani.

C. Ruthu 4:7 inaonesha baadaye mwandishi au mhariri kwa tungo "Hii ilikuwa desturi katika nyakati za kale."

V. TAREHE

A. Matukio ya hadithi yanatokea wakati wa Kipindi cha Waamuzi, 1:1 (1350 au 1200 K.K mpaka 1020 K.K.). Hii ndio maana yawezekana toleo la LXX linakiweka kitabu baada ya Waamuzi.

B. Lazima ilikuwa imetokea wakati wa kipindi cha amani kati ya Israeli na Moabu:
   1. hii inashangaza juu ya ufahamu wa Waamuzi 3:12-30
   2. Hatahivyo, lazima kulikuwa na nyakati za amani, I Sam. 22:3-4 (yaani Sauli).

C. Lini kitabu kiliandikwa?:
   1. Tarehe ya kuandikwa ni dhahiri wakati wa utawala wa Daudi, 4:17,22. Historia ya hadithi inathibitishwa na ukweli kwamba Wamoabu katika uzao wa Daudi walikuwa kitu cha ziada kwake! (kama vile Kumb. 23:3)
   2. Staili na misamiati ya Ruthu inafanana na Samweli lakini sio Mambo ya Nyakati

VI. VYANZO VINAVYOTHIBITISHA MAZINGIRA YA KIHISTORIA - sehemu pekee ya kitabu hiki ambayo imepatikana katika ugunduzi wa ki-akiolojia ni kuhamishwa kwa ndala kama ishara ya kisheria ya kuhamishwa kwa haki za urithi. Desturi hiyo hiyo imepatikana katika Mbao za Nuzi. Hizi mbao za Akkadia za tokea milenia ya pili ya kipindi cha K.K ambacho tunakiita Kipindi cha Mababa wa Imani.

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI (Muktadha)

A. Familia ya Naomi inakimbia hukumu ya Mungu juu ya Israeli na kukimbilia Moabu ambapo watu wote wanakufa, 1:1-5
B. Naomi anarudi Betlehemu pamoja na mkamwana wake wa kabila la Moabu, 1:6-22
C. Ruthu anakutana na Boazi katika uvunaji wa ngano. Anakuwa mkarimu kwake, 2:1-23
D. Naomi na Ruthu wanapanga kumtongoza Boazi na wanafanikiwa, 3:1-18
E. Boazi anachukua juhudi ya kuwa mposaji kwa ajili ya mbadala wa Naomi, 4:1-22

VIII. KWELI KUU

A. Tabia ya utauwa ya mwamini wa Mataifa, 1:16-17;
B. Tabia ya utauwa ya wanawake. Wote wa kiyahudi na Mataifa;
C. Ukoo wa Mfalme Daudi na Mfalme Masihi unajumuisha wanawake wa kigeni, Mt. 1:5, Lk. 3:32, na ulikuwa ni mpango wa Mungu.

IX. MANENO NA/AU TUNGO NA WATU WA KUWATAMBUA

A. Maneno na Tungo:
   1. Wafrati, 1:2; 4:11 (NASB & NIV)
   2. Mara, 1:20 (NASB & NIV)
   3. Mwenye Nguvu (*El Shaddai*), 1:20 (NASB & NIV)
   4. "ambaye umekuja kukimbilia chini ya mbawa zake," 2:12 (NASB & NIV)
   5. efa, 2:17 (NASB & NIV)
   6. ndugu wa karibu zaidi (*go'el*), 2:20; 3:9; 4:14, (NIV, “ndugu wa karibu”)
   7. (ndoa ya kijadi ya kurithiana), Kumb. 25:5-10
   8. "funua miguu yake," 3:4,7-8,14 (NASB & NIV)
   9. "mtu huvua kiatu chake na kumpatia mwenzake," 4:7 (NASB & NIV)


B. Watu wa kuwatambua:
   1. Elimeleki, 1:2
   2. Yesse, 4:22

X. MAENEO YA KI-RAMANI (kwa hesabu)

1. Moabu, 1:1
2. Betlehemu, 1:2


XI. MASWALI YA KIMAUDHUI KWA MWANAFUNZI

1. Nini kusudi la kitabu hiki katika Kanoni ya Kiebrania?
2. Kwanini familia ilikimbia Israeli?
3. Elezea namna neno *go'el* (ndoa za kijadi) linavyohusiana na desturi za ndoa za kijadi za kurithiana.
4. Kwanini Kitabu hiki kilikuwa ni dhihaka kwa Daudi?




MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE

# PALESTINA



# UTANGULIZI WA 1 SAMWELI & 2 SAMWELI

I. JINA LA KITABU

A. Kilipewa jina kutokanana muhusika wake mkuu, Samweli. Jina lake linamaanisha:
1. "Jina Lake ni El," kurudi Shem,
2. "Muulizaji juu ya El," (kama vile 1 Samweli 1:20)

B. Yeye alikuwa:
1. mwamuzi - 1 Sam. 7:6, 15-17
2. nabii - 1 Sam. 3:20 (manabii kiasili walikuwa wanaitwa"waonaji," 1 Sam. 9:9; 1 Nyakt. 29:29
3. kuhani - 1 Sam. 10:8; 16:5

II. URASIMISHAJI

A. Hii ni sehemu ya pili ya mgawanyiko wa kanoni ya Kiebrania iitwayo manabii. Sehemu imegawanyika katika sehemu mbili:
1. manabii wa kwanza ambao inajumuishwa Yoshua - Wafalme (isipokuwa Ruthu)
2. manabii wa mwisho ambao inajumuisha Isaya - Malaki (isipokuwa Danieli na Maombolezo)

B. Kiasili 1 & 2 Samweli kilikuwa kitabu kimoja katika kanoni ya Kiebrania:
1. Baba Bathra 14b (dokezo la kufungia la MT linatokea tu mwishoni mwa 2 Samweli)
2. Eusebius *Ecclesiastical History*. VII:25:2

C. Tafsiri ya Agano la Kale ya Kiyunani (LXX) iliikigawa kitabu katika sehemu mbili, yawezekana kwasababu ya urefu. Pia ilitoa jina vitabu vya kihistoria:
1. 1 Samweli - I Book of Kingdoms (katika Kilatini, 1 Wafalme)
2. 2 Samweli - II Book of Kingdoms (katika Kilatini, 1 Wafalme)
3. 1 Wafalme - III Book of Kingdoms (katika Kilatini, 2 Wafalme)
4. 2 Wafalme - IV Book of Kingdoms (katika Kilatini, 4 Wafalme)

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Hii kimsingi hadithi ya maisha ilijikita kuwa simulizi ya kihistoria.

B. Hii ilimaanisha kilinukuu desturi za kihistoria na matukio ambayo ki-umuhimu ilitetea waaminio wote!

C. Hii sio historia ya kisasa ya kimagharibi bali historia ya kale yakimashariki. Ilijikita katika matukio yaliyochaguliwa kuzungumzia kweli za kithiolojia. Hivyo ni sawasawa na Injili na Matendo ya Mitume ya Agano Jipya. Lazima ifasiriwe katika ufahamu wa: (1) uchaguzi; (2) uasilishaji; (3) upangaji na (4) chini ya uvuvio.

Hatahivyo, lazima pia iwekwe wazi kwamba Waebrania na Wahiti walikuwa wanahistoria walio sahihi zaidi. Watu wengine walijaribiwa kutia chumvi ushindi na kuweka kando.

D. Utajiri wa Fasihi ya Mashariki ya Karibu sasa inapatikana kwa wanazuoni kupitia akiolojia ya kisasa iliyotoa ufahamu wa msingi katika uandishi wa Samweli, hasa 1 Sam. 15 - 2 Sam. 8. Mnamo miaka ya 1200 K.K. Nyaraka ya Kihiti iitwayo "Apology of Hallusitis" ina ufanano mwingi na Samweli. Kimsingi ni ulinzi wa ufalme mpya ili kwamba mtawala mpya asishtakiwe na uchukuaji wa kisheria wa utawala wa mwingine, (*Zondervan Pictorial Encyclopedia*, vol.5 ukur. 259-260):
1. inaweka mkazo wa matukio ambayo yalipelekea mfalme mpya
2. mara kwa mara ilijumuisha muhtasari wa matukio badala ya mtiririko wa kimakini
3. kidhahiri inaonesha kukosa sifa kwa watawala waliotangulia
4. kinaonesha ushindi wa kijeshi wa mtawala mpya

5. inafunua umaarufu unaokua wa mtawala mpya
6. inaandika ndoa muhimu za kihistoria za mtawala mpya
7. inaweka msisitizo wa kujizatiti wa kidini na utambuzi wa kitaifa wa mtawala mpya
8. muhtasari wa utawala wa mfalme mpya pamoja na Baraka zake za kimungu na ushindi wake wa kiuongozi

IV. UANDISHI

A. Desturi ya Kiyahudi siku zote ilithibitisha kwamba Samweli alikuwa mwandishi:
   1. BabaBathra 14b inasema kwamba Samweli alikiandika kitabu ambacho kinabeba jina lake na pia Waamuzi na Ruthu.
   2. Kitabu chenyewe kinasema kwamba Samweli alikiandika (kama vile 1 Sam.10:25 [hii mara zote hufikiriwa kama sura za kwanza 12 mpaka ya 15]).
   3. Wanazuoni wa baadaye pia walitambua kwamba kama Kumbu kumbu la Torati na Yoshua, kitabu hiki kinaandika, 1 Sam. 25:1; 28:3, na pia kinaandika matukio marefu baada ya kifo chake. Hivyo wanapendekeza kwamba:
      a. yawezekana Sera ya mwandishi, 2 Sam. 8:17, alikimalizia kitabu
      b. yawezekana Abiathari kuhani ndiye aliyekimalizia kitabu
      c. yawezekana Zabudi, mwana wa Nathani nabii (NIV), alikitunga (kama vile 1 Wafalme 4:5)

B. Uanazuoni wa kisasa:
   1. inatambuliwa kwamba maudhui ya vitabu yanatoka kwa shuhuda wa macho juu ya matukio (Bright).
   2. Pia inatambuliwa kwamba vyanzo vilitumika:
      a. "kitabu cha Yashari)," 2 Sam. 1:18
      b. mambo ya nyakati ya Samweli, 1 Sam. 10:25; 1 Nyakati 29:29
      c. mambo ya Nyakati ya nabii Nathani na Gadi, 1 Nyakati 29:29
      d. mambo ya Nyakati nyingine, 1 Nyakati 27:24
      e. wanazuoni wengi wa kisasa wanapenda kudhani kwamba Samweli, Nathani na Gad (1 Nyakati 29:29) walikuwa waandishi wa hadithi tatu ambazo ziliunganishwa na Zabudi, mwana wa Nathani (1 Wafalme 4:5), ambao pia walikuwa na nafasi ya kupata nyaraka za kimahakama.
   3. Pia kua ushahidi wa wahariri wa baadaye baada ya siku za Samweli kukuzwa katika tungo "mpaka leo hii," (kama vile 1 Sam. 5:5; 6:18; 27:6; 30:25; 2 Sam. 4:3; 6:8; 18:18).
   4. Kuna ushahidi kwamba mhariri huyu au wahariri waliishi na kufanya kazi baada ya Ufalme ulioungana kugawanyika katika mwaka 922 K.K. (Bright) au 930 K.K. (Harrison & NIV) au 933 K.K. (Young) katika makabila kumi ya kaskazini yaitwayo Israeli, Efraimu au Samaria na Kusini matatu yaitwayo Yuda (kama vile 1 Sam. 11:8; 17:52; 18:16; 27:6; 2 Sam. 5:5; 24:1).
   5. Samweli ni mfano mzuri wa nini wanazuni wakosoaji wa kisasa wanaona kama ishara ya fasihi ya utungwaji:
      a. mwisho wa familia ya Eli kama kuhani:
         (1) 1 Samweli 2:31 na kuendelea
         (2) 1 Samweli 3:1 na kuendelea
      b. kwa mafuta kwa Sauli:
         (1) siri, 1 Samweli 9:26-10:1
         (2) hadharani (mara mbili), 1 Samweli 13:14; 15:23

c. utangulizi wa Daudi kwa Sauli:
   (1) 1 Samweli 16:21
   (2) 1 Samweli 17:58
d. Daudi anatoroka katika makazi ya Sauli:
   (1) 1 Samweli 24:3
   (2) 1 Samweli 26:5
e. Maagano ya Daudi na Yonathani:
   (1) 1 Samweli 18:3
   (2) 1 Samweli 20:16, 42
   (3) 1 Samweli 23:18
f. Daudi kwenda kwa Gathi:
   (1) 1 Samweli 21:10
   (2) 1 Samweli 27:1
g. mchinjaji wa Goliathi:
   (1) Daudi- 1 Samweli 17:51
   (2) Elhanan - 2 Samweli 21:19
   (3) 1 Nyakati 20:5 inaonekana kuonesha kwamba Goliathi na ndugu yake (Lahmi) walirejerea kwa pamoja
h. kuachwa kwa Sauli:
   (1) 1 Samweli 24:3 na kuendelea
   (2) 1 Samweli 26:5 na kuendelea
i. kama kwa ulinganifu na/au utatu R.K. Harrison anasema, "Lazima ikumbukwe tena kwamba utofautiano usiothibitishwa katika hadithi za kibiblia ni matokeo ya moja kwa moja ya kusoma kwa kutotilia maanani au wakati mwingine uwasilishaji uliokosewa kwa kutokuwa makini kwa maandiko ya Kiebrania..ambayo kwa kusema ukweli yapo tu katika fikra hatarishi ,"*Introduction to the Old Testament*, kur.703.

6. Lazima tukiri kwamba uandishi haujulikani (E.J. Young) na pia mchakato wa utungwaji wa vitabu hivi vya Agano la Kale haujulikani. Hatahivyo lazima tuelezee kwamba:
   a. mchakato uliongozwa na Mungu;
   b. matukio kiukweli ni ya kihistoria na sio ya kufikirika;
   c. matukio yana msukumo wa kithiolojia.

V. TAREHE

A. Wakati matukio yakitokea
   1. 1 Samweli inachukua kipindi cha muda tokea kuzaliwa kwa Samweli, 1105 K.K (NIV) mpaka kifo cha Sauli kama (1011/10 Harrison & NIV; 1013 Young; 1000 Bright).
   2. 2 Samweli inachukua kipindi cha muda tokea kifo cha Sauli kama mnamo mwaka 1011 K.K. mpaka mwisho wa utawala wa Daudi (971/70 Harrison; 973 Young; 961 Bright). Suleimani alianza kutawala mnamo mwaka 969 K.K

B. Wakati kitabu kilipoandikwa
   1. 1 Samweli 11:8; 27:6 inaonesha kwamba angalau baadhi ya kitabu kiliandikwa katika wakati wake tokea baada ya Ufalme ulioungana kuvunjika mnamo mwaka 922 K.K. au 930 K.K.
   2. Tungo inayojirudia, "mpaka leo hii," inaonesha kwamba:

   a. baadhi ya kitabu iliandikwa muda mrefu baada ya matukio:1 Sam. 5:5; 6:18; 27:6; 30:25; 2 Sam. 4:3; 6:8; 18:18.
   b. vyanzo ambavyo vilikuwa vimetumika ilijumuisha tungo hii.
3. Moja ya tatizo la uwekaji tarehe kwa kipindi hiki ni andiko la 1 Sam. 13:1 ambalo linatoa tarehe ya utawala wa Sauli lakini likiwa limeharibiwa katika kuelezwa. Hesabu dhahiri inakosekana.

VI. MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. 1 Samweli inaendelea historia ya uasi na kumomonyoka kwa maadili ya kipindi cha Waamuzi:
   1. dhambi, uvamizi, maombi kwa ajili ya msamaha na mkombozi wa Mungu inaweka alama ya Waamuzi 1-17
   2. mifano mitatu ya mmomonyoko wa maadili inaorodheshwa katika Waamuzi 18-21

B. Ilikuwa ni muda wakati falme kubwa za Mesopotamia na Misri hazikuwa na nia ya kujitanua:
   1. Misri:
      a. Mfalme wa mwisho wa kikabila wa ki-Misri wa ufalme katika XX (1180-1065 K.K., Bright) alikuwa Rameses XI
      b. Toleo la Ufalme wa XXI (usio wa ki-Misri) iitwayo "Tanite" ulikuwa mnamo miaka ya 1065 - 935 K.K (Bright)
   2. Ashuru ilikuwa katika anguko baada ya Tiglath-Pileser I (1118-1078 K.K., Bright)

C. Wafilisti kwa kiwango kikubwa (Watu wa Bahari wa Aegea), alijaribu kuvamia Misri mnamo mwaka 1300 K.K. lakini walishindwa. Waliishi katika pembe ya kusini magharibi mwa Palestina mnamo mwaka 1250 K.K. Walikuwa wamekuza teknolojia ya chuma tokea Wahiti na walikuwa na uwezo kuanzisha wenyewe katika mzunguko wa miji mitano: Ashkeloni, Ashdodi, Ekroni, Gathi na Gaza. Ilipangwa kama miji ya Kiyunani kila mfalme wake. Walikuwa maadui wakubwa wa Wana wa Israeli katika nyakati za ufalme wa kwanza.

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI (Muktadha)

A. Uainisho mfupi wa Wahusika Wakuu:
   1. Eli na Samweli, 1 Sam. 1-7
   2. Samweli na Sauli, 1 Sam. 8-15
   3. Sauli na Daudi, 1 Sam. 16 - 2 Sam. 1
   4. Utawala wa Daudi, 2 Sam. 2-12
   5. Daudi na waliomfuatia katika utawala, 2 Sam. 13-20
   6. Vitu vya zaidi juu ya Daudi na utawala wake, 2 Sam. 21-24

B. 1 & 2 Samweli inaonekana kuainishwa na mwandishi/mhariri kwa kujumuisha muhtasari:
   1. 1 Samweli 7:15-17
   2. 1 Samweli 14:49-51
   3. 2 Samweli 8:15-18
   4. 2 Samweli 20:23-26

C. Uainisho wa ndani:
   1. angalia R.K. Harrison, *Introduction to the Old Testament*, kur. 695-696

2. angalia E.J. Young*, An Introduction to the Old Testament*, kur. 180-187
3. angalia NIV Study Bible, kur. 373 na 422

VIII. KWELI KUU

A. Samweli anaandaa jukwaa kwa ajili ya kutengeneza ufalme kama Musa anavyoandaa jukwaa kwa ajili ya kutengeneza taifa:
   1. Musa alitabiiri Israeli kuwa na mfalme katika Kumb. 17:14-20 ambapo anaelezea nini ambacho mfalme wa haki anatakiwa kufanya na afanye.
   2. Kuna mvutano katika 1 Samweli juu ya mfalme:
      a. vipengele hasi:
         (1) walimkataa *YHWH* kama Mfalme, 1 Sam. 8:7; 10:19
         (2) walitaka mfalme "kama mataifa yanayozunguka," 1 Sam. 8:5; 12:19-20
         (3) Ilimkera Samweli; alijiskia yaeye binafsi kukataliwa, 1 Sam. 8:6
      b. vipengele chanya:
         (1) *YHWH* alitimiliza unabii Wake katika Kumbu kumbu la Torati kwa kuwapa mfalme, 1 Sam. 8:7,9,22, "sikia sauti ya watu"
         (2) mwambie mfalme mpya miongozo ya kiutauwa, 1 Sam. 8:9 (Kumb. 17:14-20)
         (3) mfalme atawaokoa watu wake, 1 Sam. 9:16 (kama mwamuzi katika kuitikia maombi ya watu, kama vile 1 Sam. 12:13)

B. Samweli anaandika mageuzi ya nguvu ya kiroho kutoka kwa Kuhani Mkuu na Hema kwa msemaji anayeibuka wa kinabii. Hii inaweza kuwa mwitikio wa:
   1. Hukumu ya Mungu juu ya Eli na familia yake, 1 Sam. 2:22-3:18
   2. hitaji kwa ajili ya uwiano kati ya muundo na taratibu za makuhani na imani igusayo ya kibinafsi yenye mlengo wa manabii
   3. wote makuhani na manabii ni wasuluhishi wa kiagano kwa watu kama kundi moja
   4. Sauli alimtazamia Samweli wakati Daudi alimtazamia Nathani na Gadi kuyag’amua mapenzi ya Mungu

C. 2 Samweli inaandika:
   1. wema wa Mungu kwa Daudi
   2. uimara wa Daudi na udhaifu wake
   3. Hukumu ya Mungu juu ya Daudi kwasababu ya dhambi yake na athari zake juu ya:
      a. taifa
      b. famia ya Uria
      c. mwana wa Betsheba
      d. wana wa Daudi

D. 1 & 2 Samweli inaendeleza historia ya watu wa Mungu ambayo ilianza katika Mwanzo.

IX. MANENO NA TUNGO NA WATU WA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

A. Maneno na Tungo:
   1. 1 Samweli:
      a. naivera ya kitani, 2:18,28 (NASB & NIV)
      b. "pembe yangu imetukuka," 2:1, 10 (NASB & NIV)
      c. "toka Dani mpaka Beer-Sheba," 3:20 (NASB & NIV)

d. "BWANA wa MAJESHI akaaye juu ya Makerubi"4:4, (NIV, "BWANA Mwenye nguvu yeye ambaye ametukuka juu ya Makerubi")
e. "kila mtu hemani kwake," 4:10 (NASB & NIV)
f. majipu ya dhahabu, 6:4 (NIV, "uvimbe wa dhahabu")
g. Ebenezeri, 7:12 (NASB & NIV)
h. "mtu aupendezaye moyo wake," 13:14 (NASB & NIV)
i. "hakuonekana mhunzi yeyote katika nchi yote ya Israeli," 13:19 (NASB & NIV)
j. "kutii ni bora kuliko dhabihu," 15:22 (NASB & NIV)
k. "BWANA akaghairi..." 15:35 (NIV, "...huzunika")
l. "roho mbaya kutoka kwa BWANA ikamtahayarikisha," 16:14 (NIV, "ikamtesa")
m. "kuyaacha mate yake kuanguka juu ya ndevu zake," 21:13 (NASB & NIV)

2. 2 Samweli:
a. the book of Jashar (kitabu cha Yashari), 1:18 (NASB & NIV)
b. Millo, 5:9 (NIV, "toka pande za ndani")
c. akawazuilia, 8:4 (NASB & NIV)

B. Watu wa kuwatambua kwa muhtasari:
1. I Samweli:
a. Hanna, 1:1
b. Hofni & Finehasi, 1:3
c. Ikabodi, 4:21
d. Kishi, 9:1
e. Yonathani, 14:1; 19:1
f. Mikali, 14:49
g. Abneri, 14:50
h. Goliati, 17:4
i. Doegi, 21:7
j. Abiathari, 22:20
k. Mwanamke mwenye pepo wa utambuzi Endori, 28:7 (NIV, "kupitia...huko Endori")
l. Abigaili, 30:5

2. 2 Samweli:
a. Ish-boshethi, 2:8
b. Yoabu, 2:13
c. Amnoni, 3:2
d. Absalomu, 3:3
e. Adoniya, 3:4
f. Mephiboshethi, 4:4
g. Uza, 6:3
h. Uria, 11:3
i. Tamari, 13:5
j. Zadoki, 15:24
k. Shimei, 16:5

X. MAENEO YA KI-RAMANI (kwa hesabu)

A. 1 Samweli:

1. Kiriath-yearimu, 6:21
2. Rama, 7:17
3. Beersheba, 8:2
4. Yabesh-gileadi, 11:1
5. Pango la Adulamu, 22:1
6. Nobu, 21:1
7. Engedi, 23:29
8. Siklagi, 30:1
9. Mlima Gilboa, 31:8

B. 2 Samweli:

1. Ashkeloni, 1:20
2. Hebroni, 2:3
3. Yezreeli, 2:9
4. Gezeri, 5:25
5. Dameski, 8:5
6. Raba, 12:27
7. Tekoa, 14:2
8. Kiwanja cha kupuria cha Arauna, Myebusi, 24:16 (Yerusalemu)


XI. MASWALI YA MWANAFUNZI YA KIMAUDHUI

A. 1 SAMWELI:

1. Kwanini kuzaliwa kwa Samweli kunaandikwa na sio kule kwa Sauli au Daudi?
2. Kwanini Mungu alimkataa Eli na Familia yake?
3. Kwanini Finehasi na Hofni wachukue Sanduku la Agano vitani?
4. Kwanini Samweli alikuwa mwenye hasira kwamba watu walimuuliza mfalme?
5. Kwanini Sauli alikataliwa kama mfalme?
6. Elezea "roho mbaya kutoka kwa BWANA."
7. Kwanini Sauli alijaribu kumuua Daudi?
8. Kwanini Sauli alimtembelea mwanamke mwenye pepo wa utambuzi wa Endori?
9. Sauli alikufaje?


B. 2 SAMWELI:

1. Kwanini Daudi alipata kuwa mwenye hasira juu ya kifo cha Ishiboshethi?
2. Kwanini Daudi alipata hasira juu ya kifo cha Abneri?
3. Kwanini Daudi alimsaidia Mephiboshethi?
4. Kwanini Mungu Mungu alimuua Uza?
5. Kwanini ahadi za Mungu kwa Daudi katika sura ya 7 ni muhimu sana?
6. Kwa namna gani dhambi ya Daudi pamoja na Bethsheba iliathiri familia yake?
7. Elezea tofauti kati ya Zadoki na Abiathari.
8. Kwanini Mungu alikuwa na hasira kwa kuwahesabu watu?




MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE

# PALESTINA



# UTANGULIZI WA 1 & 2 WAFALME

I. JINA LA KITABU

A. Kama 1 & 2 Samweli na 1 & 2 Mambo ya Nyakati, 1 & 2 Wafalme kiasili vilikuwa kitabu kimoja katika Kiebrania. Kiliitwa "*Melakim*" au Wafalme. Kilipata haya maelezo yake kutoka kwenye ukweli kwamba inachukua historia ya wafalme wa Yuda na Israeli.

B. Kama 1 &2 samweli na 1 & 2 Mambo ya Nyakati, 1 & 2 Wafalme kwanza kilikuwa kimegawiwa katika vitabu viwili na toleo la LXX. Inavyoonekana, hii ilifanyika kwasababu ya urefu wa vitabu hivi. Visingeweza kutosha gombo moja kwasababu ya uzito na unene wa ngozi. Andiko la kwanza la Kiebrania kugawa kitabu halikuwepo mpaka mnamo mwaka 1448 B.K.

C. Jina la vitabu hivi limekuwa:
1. katika Kiebrania - "Wafalme"
2. katika LXX - III & IV Kingdoms (III & IV Falme)
3. katika Vulgate - III & IV Wafalme (1 & 2 Samweli vilikuwa I & II Falme na Wafalme)

II. URASIMISHAJI

A. Vitabu hivi ni sehemu ya mgawanyo wa pili wa kanoni ya Kiebrania iitwayo "manabii."

B. sehemu imegawanyika katika sehemu kuu mbili:
1. manabii wa hapo mwanzo ambao wanajumuishwa Yoshua - Wafalme, isipokuwa Ruthu,
2. manabii wa baadaye ambapo inajumuisha Isaya - Malaki, isipokuwa Danieli na Maombolezo.

C. Orodha ya vitabu katika Kiebrania cha Agano la Kale inaweza kuwa iliathiriwa na udini wa Kiebrania. Kuna barua 22 zilizo katika alfabeti za Kiebrania. Kwa kuunganisha vitabu kadhaa, kuna vitabu 22:
1. Waamuzi na Ruthu
2. Samweli
3. Wafalme
4. Mambo ya Nyakati
5. Ezra - Nehemia
6. Yeremia na Maombolezo
7. Manabii wadogo wadogo kumi na mbili.

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Vitabu hivi kimsingi ni simulizi za kihistoria zikiwa na nukuu zinazojirudia rudia kutoka:
1. kumbukumbu za mahakama
2. manabii

B. Mtu anapolinganisha vitabu vitatu vya Samweli, Wafalme na Mambo ya Nyakati, aina tofauti za simulizi za kihistoria huibuka:
1. Samweli kimsingi ni maisha ya mtu. Inajikita kwa wahusika wakuu:
   a. Samweli
   b. Sauli
   c. Daudi
2. Wafalme kimsingi ni tungo za:
   a. kumbukumbu za mahakama za kifalme:

(1) “kitabu cha Mambo ya Nyakati ya Sulemani,” 1 Wafalme. 11:41
(2) “kitabu cha mambo ya Nyakati ya wafalme wa Yuda,” 1 Wafalme 14:29; 15:7,23
(3) “kitabu cha mambo ya Nyakati ya wafalme wa Israeli,” 1 Wafalme 14:19; 15:31.

b. nyaraka za kinabii:
(1) Eliya
(2) Elisha
(3) Isaya (sura ya 36-39)
(4) ushahidi kwa kumbukumbu za kinabii na kihistoria zinavyoonekana katika Mambo ya nyakati:
(a) 1 Nyak. 29:29
(b) 2 Nyak. 9:29
(c) 2 Nyak. 12:15
(d) 2 Nyak. 13:22
(e) 2 Nyak. 26:22

3. Mambo ya Nyakati kimsingi ni uwasilishaji wenye ubaguzi chanya baguzi ya kithiolojia ya wafalme wa
   a. Ufalme ulioungana.
   b. Wafalme wa Yuda.

IV. UANDISHI

A. Biblia yenyewe iko kimya juu ya uandishi wa 1 & 2 Wafalme kama ilivyo katika wingi wa vitabu vya manabii wa hapo kwanza.

B. Baba Bathra 15a anasema Yeremia aliandika kitabu chake, kitabu cha Wafalme na Maombolezo:
1. Hii yawezekana kwasababu ya umalizio wa 2 Wafalme, 24:18-25:30 ni ufanano kabisa katika Kiebrania kwa Yeremia 52.
2. Iko wazi kwamba mwandishi alikuwa shuhuda wa anguko la Yerusalemu.

C. Kiuhalisia vitabu hivi ni kazi ya mtunzi na sio mwandishi.

D. sharti ikumbukwe kwamba mtunzi alitumia vyanzo kadhaa:
1. Chanzo cha kwanza ilikuwa ni maandiko. Mara kwwa mara ananukuu na kutengeneza maelezo kwa Kumbukumbu la Torati na baadhi ya Manabii.
2. Kuna vyanzo kadhaa vilivyoandikwa hasa na kupewa majina:
   a. "Kitabu cha Matendo ya Sulemani," 1 Wafalme 11:41
   b. "Kitabu cha Mambo ya Nyakati ya Wafalme wa Yuda," 1 Wafalme 14:29; 15:7,23
   c. "Kitabu cha Mambo ya Nyakati ya Wafalme wa Israeli," I Wafalme 14:19; 15:31
   d. Kuna pia kutajwa katika 1 Nyak. 29:29 juu ya simulizi za kuandikwa za manabii: Samweli, Nathan na Gadi. Hii inaonesha kwamba desturi za kinywa zilikuwa zikiandikwa.

E. Kuna baadhi ya nyongeza za uhariri katika 1 & 2 au mtunzi ananukuu tungo "hata leo hii" kutoka vyanzo vyake:
1. 1 Wafalme8:8
2. 1 Wafalme 9:21
3. 1 Wafalme 12:19

4. 2 Wafalme 8:22

V. TAREHE

A. matukio ya kitabu yanachukua kipindi cha muda:
   1. kutoka kifo cha Daudi na mwanzo wa utawala wa Sulemani:
      a. Bright - 961 K.K.
      b. Harrison - 971/970 K.K.
      c. Young - 973 K.K.
      d. NIV - 970 K.K.
   2. mpaka utawala wa mfalme wa Babeli Evil Merodach, pia kijulikana kama Amel-Marduk, 562-560 K.K. (Bright)
   3. lakini kitabu cha 2 wafalme hakitajimfalme Koreshi wa Umedi-Uajemi "Mkuu" ambaye jeshi lake liliharibu mji wa Babeli mnamo mwaka 539 K.K.

B. Kitabu kiliandikwa au kutungwa wakati fulani au mara muda mfupi baada ya uhamisho wa Babeli.

C. Urefu wa miaka ya utawala wa Mfalme alipoongezwa pamoja ni miaka mingi kushabihiana na muda wa majira ya vitabu. Kumekuwepo na majibu kadhaa ya pendekezwayo:
   1. hesabu zinazotajwa hazingatii utawala wa wenza wa kipamoja.
   2. Kulikuwa na kalenda mbili zilizotumika:
      a. Kalenda takatifu ilianza katika anguko.
      b. kalenda ya kidini ilianza wakati wa kipupwe.
   3. Wakati hesabu ya Wafalme na Mambo ya Nyakati vinapolinganishwa, ni wazi kwamba baadhi ya makosa ya kiuandishi yametokea.

VI. VYANZO VINAVYOTHIBITISHA MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. Archaeological EvidenceUshahidi wa ki-akiolojia:
   1. Mesha Stele, pia lijulikanalo kama Jiwe la kimoabu, kumbukumbu ya uasi wa Mesha, Mfalme wa Moabu, dhidi ya Israeli punde baada ya Mfalme Omri (876-869 K.K., Bright; 874/3 K.K., Harrison [kama vile 2 Wafalme 3:4]).
   2. Black Obelisk wa Mfalme wa Ashuru, Shalmaneser III (859-824 K.K.,Bright & Harrison):
      a. Vita ya Qarqar mnamo 853 K.K.vilivyofanyika Mto Orontes. Taarifa kutoka Back Obelisk ya Shalmaneser III inamuita Ahabu Muisraeli na kumpa sifa yeye kama nguvu kubwa ya kijeshi (pamoja na Shamu, kama vile 1 Wafalme 22:1). Vita hii haiandikwi katika Agano la Kale.
      b. Kinaonesha mfalme anayefuata wa Israeli, Yehu (842-815 K.K, Bright [kama vile 2 Wafalme 9-10]), akitambua na kutengeneza mahusiano na Ashuru. Hii pia haiandikwi katika kumbu kumbu za Agano la Kale.
   3. Muhuri wa Ajasper ulipatikana huko Megiddo tokea muda wa Yeroboamu II (786-746 K.K., Bright; 782-753 K.K., Harrison) anamtaja Yeroboamu.
   4. Khorsabad Annals anaelezea utawala na anguko la Samaria kwa Sargon II (722-705 K.K.) mnamo mwaka 722 K.K. (kama vile 2 Wafalme 17).
   5. Simulizi ya Senakeribu juu ya uvamizi wa Yerusalemu mnamo mwaka 701 K.K. wakati wa utawala wa Hezekia (715-687 K.K., Bright [kama vile 2 Wafalme. 18:13-19:37, Isa. 36-39]).

6. Kwa kutumia tarehe za uthibitisho wa tarehe (nyaraka za Ashuru na Agano la Kale) wa: (1)Vita vya Qarqar (Shalmaneser III dhidi ya Israeli na Shamu) 853 K.K.; na (2) kupatwa kwa jua (mu-Ashuru Eponym anaorodhesha Ishdi-Sagale 763 K.K.); (3) kufanya masuluhisho kwa Shalmaneser III (841 K.K); tarehe za matukio katika Wafalme inaweza ikathibitishwa.

B. Toleo la A Brief Historical Survey of the Powers of Mesopotamia (likitumia tarehe ambazo kimsingi zimejikita juu ya *John Bright's A History of Israel,* ukur. 462ff.):
   1. Ufalme wa Ashuru (Mwa.10:11):
      a. Dini na tamaduni zilishawishiwa na Ufalme wa Kisumeri/Babeli.
      b. Orodha ya watawala inayosemekana kuwepo na tarehe zinazosadikia:
         (1) 1354- 1318 Asshur -Uballit I:
            (a) alitawala mji wa Wahiti wa Kakemishi
            (b) alianza kuondoa ushawishi wa Wahiti na kuruhusu Ashuru kupanuka
         (2) 1297-1266 Adad-Nirari I (mfalme mwenye nguvu)
         (3) 1265-1235 Shalmaneser I (mfalme mwenye nguvu)
         (4) 1234-1197 Tukulti-Ninurta I - mtawala wa kwanza wa ufalme wa Babeli kuelekea kusini
         (5) 1118-1078 Tiglath-Pileser I - Ashuru inakuwa taifa lenye nguvu kubwa huko Mesopotamia
         (6) 1012- 972 Ashur -Rabi II
         (7) 972- 967 Ashur -Resh-Isui II
         (8) 966- 934 Tiglath-Pileser II
         (9) 934- 912 Ashur -Dan II
         (10) 912- 890 Adad- Nirari II
         (11) 890- 884 Tukulti-Ninurta II
         (12) 883- 859 Asshur-Nasir-Apal II
         (13) 859- 824 Shalmaneser III Vita ya Qarqar mnamo mwaka 853
         (14) 824-811 Shamashi-Adadi V
         (15) 811-783 Adad- Nirar i III
         (16) 781-772 Shalmaneser IV
         (17) 772-754 Ashur -Dani III
         (18) 754-745 Ashur-Nirari V
         (19)745-727 Tiglath-Pileser III:
            (a) aliiitwa kwa jina lake la kiti cha utawala wa Kibabeli, Puli, katika 2 Wafalme 15:19
            (b) mfalme mwenye nguvu sana
            (c) alianza sera ya kuwahamisha watawaliwa
            (d) mnamo mwaka 735 K.K. kulikuwa na uundwaji wa "Shirikisho la watu wa Shamu-Waefraimu"ambalo lilikuwa ni jaribio la kuunganisha rasilimali jeshi inayopatikana ya kuvuka Mataifa ya Yordani kutoka maziwa makuu ya Frati mapaka Misri kwa ajili ya kusudi la kupunguza nguvu ya kijeshi inayoinuka ya Ashuru. Mfalme Ahazi wa Yuda alikataa kujiunga na alivamiwa na Israeli na Shamu. Aliandika kwenda kwa Tiglath- Pileser III kupata msaada dhidi ya ushauri wa Isaya (kama vile 2 Wafalme 16; Isa. 7-12).
            (e) Mnamo 732 Tiglath-Pileser III alivamia na kutawala Shamu na Israeli na kuweka mfalme wa mpito katika kiti cha utawala wa Israeli, Hoshea (732-722). Maelfu ya

Wayahudi kutokea Ufalme wa Kaskazini walipelekwa uhamishoni Media (kama vile 2 Wafalme 15).

(20) 727-722 Shalmaneser V

(a) Hoshea anatengeneza ubia pamoja na Misri na anavamiwa na Ashuru (kama vile 2 Wafalme 17)

(b) aliuvamia mji wa Samaria mnamo mwaka 724 K.K.

(21) 722-705 Sargon II:

(a) Baada ya miaka mitatu ya kuuzunguka mji ulioanzishwa na Shalmaneser V, mtawala wake aliyefuata Sargon II alitawala mji mkuu wa Israeli, Samaria. Zaidi ya watu 27,000 walihamishiwa Medi.

(b) ufalme wa Wahiti pia unatawaliwa.

(c) Mnamo mwaka 714-711 umoja mwingine wa mataifa yanayozunguka Yordani na Misri yakaaksi dhidi ya Ashuru.Ushirika huu unajulikana kama "Uasi wa Ashdadi." Hata Hezekia wa Yuda kiasili alijumuishwa. Ashuru alivamia miji kadhaa ya Wafilisti.

(22) 705-681 Senekarebu:

(a) Mnamo mwaka 705 ushirika mwingine wa mataifa ya Yodani na Misri yakaasi baada ya kifo cha Sargon II. Hezekia kwa ukamilifu wote alisaidia uasi huu. Senakeribu alivamiwa mnamo mwaka 701.Tendo la uasi lilipingwa lakini Yerusalemu iliachwa na usaiddizi wa Mungu (kama vile Isa. 36-39 na 2 Wafalme 18-19).

(b) Senekaribu pia alizima uasi huko Elamu na Babeli.

(23) 681-669 Esarhaddon:

(a) mtawala wa kwanza wa Kiashuru kushambulia na kutawala Misri

(b) alikuwa na huruma kuu pamoja na Babeli na kujengwa upya kwa mji wake mkuu

(24) 669-663Ashurbanipal:

(a) pia aliitwaOsnappar katika Ezra 4:10

(b) Kaka yake Shamash-shum-ukin alifanywa mfalme wa Babeli. Hii ilileta miaka kadhaa ya amani kati ya Ashuru na Babeli lakini kulikuwa na mwendelezo wa uhuru ambao ulivunjika mnamo mwaka 652 ukiongozwa na kaka yake.

(c) Kuanguka kwa Thebesi, 663 K.K.

(d) Kushindwa kwa Elamu, 653, 645 K.K.

(25) 633-629 Asshur-Etil-Ilani

(26)629-612 Sin-Shar-Ishkun

(27) 612-609 Asshur-Uballit II: - aliwekwa kama mfalme huko uhamishoni Harani baada ya anguko la Asheri mnamo mwaka 614 K.K. na Ninawi mnamo mwaka 612 K.K.

2. Ufalme mpya wa Babeli:

a. 703-? Merodach-Baladan - alianza mapinduzi kadhaa dhidi ya utawala wa Ashuru

b. 652 Shamash-shum-ukin:

(1) Mwana wa Esarhaddon na kaka wa Asshurbanipal

(2) alianza mapinduzi dhidi ya Ashuru lakini alishindwa

c. 626-605 Nabopolassar:

(1) alikuwa mfalme wa kwanza wa ufalme wa kisasa wa Babeli

(2) alivamia Ashuru kutoka kusini wakati Cyaxares wa Medi alivamia kutoka kaskazini mashariki

(3) mji mkuu wa kale wa Ashuru, Asshur ulianguka mnamo mwaka 614 na mji mkuu mpya wenye nguvu wa Ninawi ulianguka mnamo mwaka 612 K.K.

(4) Mabaki ya jeshi la Ashuru walikimbilia kurudi Harani. Hata walidiriki kupandisha mfalme mpya.

(5) Mnamo mwaka 608 Pharaoh Necho II (kama vile 2 Wafalme 23:29) alienda kaskazini kusaidia mabaki wa jeshi la Ashuru kwa kusudi la kutengezeza ukanda wa usalama dhidi ya taifa na nguvu inayokua ya Babeli.Yosia, mfalme mtauwa wa Yuda (kama vile 2 Wafalme 23), walipinga mapinduzi ya jeshi la Misri kupitia Palestina. Kulikuwa na waskemishi wadogo wadogo huko Megiddo. Yosia aliumizwa na kufa (2 Wafalme 23:29-30). Mtoto wake Yehoazi alifanywa mfalme. Pharaoh NechoII alifika akiwa amechelewa kuzimisha uharibifu wa majeshi ya Ashuru huko Harani. Aliyakabili majeshi ya kibabeli kwa kuongozwa na mtoto wa mfalme Nebukadneza II na walishindwa vibaya mnamo mwaka 605 K.K. huko Kakameshi juu ya Mto Frati.

Alipokuwa akirudi Misri alisimama Yerusalemu na kupitia mji. Alimtoa Yehoazi na kumuondoa baada ya miezi mitatu tu. Akamweka mwana mwingine wa Yosia, Yehoakini katiki cha Enzi (kama vile 2 Wafalme 23:31-35).

(6) Nebukadneza II alifukuza jeshi la kimisri kusini kupitia Palestina lakini alipokea neno la kifo cha baba yake na kurudi Babeli. Baadaye mwaka huo huo alirudi Palestina. Alimuacha Yehoakim katika utawala wa kiti chake cha Yuda lakini akapeleka uhamishoni maelfu kadhaa wa raia mna wajumbe kadhaa wa familia ya kifalme. Danieli na rafiki zake walikuwa sehemu ya uhamisho huu.

d. 605-562 Nebukadneza II:

(1) Tokea mwaka 597-538 Babeli ilikuwa na utawala wote juu ya mji wa Palestina.

(2) Mnamo mwaka 597 uhamisho mwingine ulitokea Yerusalemu (2 Wafalme 24). Alikufa kabla ya kuwasili kwa Nebukadneza II. Mwanaye Yehoakini alikuwa ni mfalme pekee kwa miezi mitatu wakati alipopelekwa uhamishoni kwenda Babeli. Watu elfu kumi wakiwemo Ezekieli, walipelekwa kimakazi karibu na Jiji la Babeli kando ya Mfereji wa Mto Kebari.

(3) Mnamo mwaka 586, baada ya mwendelezo wa ushawishi na Misri, Mji wa Yerusalemu uliharibiwa tiki tiki (2 Wafalme 25) na uhamisho mkubwa ukatokea. Zedekia alitawala badala ya Yehoakini, aliyepelekwa uhamishoni na Gedelia kuteuliwa kuwa mtawala.

(4) Gedelia aliuwawa na majeshi ya kiutawala ya Kiyahudi. Majeshi haya yalikimbilia Misri na kumlazimisha Yeremia kwenda pamoja nao (605, 596, 586, 582) na kuhamisha Wayahudi waliobakia waliopatikana.

e. 562-560 Evil-Merodack, pia ajulikanaye kama Amel-Marduk - Alimuachilia Yehoakini kutoka gerezani lakini alitakiwa kuendelea kuishi Babeli (kama vile 2 Wafalme 25:27-30; Yer. 52:31).

f. 560-556 Neriglissar - Alikuwa ni kamanda wa Nebukadneza aliyeuharibu Yerusalemu.

g. 556 - Labaski-Marduk – Alikuwa mwana wa Neriglissar lakini alipigwa risasi baada ya miezi tisa tu.

h. 556-539 Nabonidasi:
   (1) Nabonidasi hakuwa na mahusiano na nyumba ya kifalme hivyo alioa binti wa Nebukadreza II.
   (2) Alitumia muda wake mwingi katika kujenga hekalu kwa ajili ya mungu mwezi "Sin" huko Tema. Alikuwa mwana wa kuhani mke wa mungu huyu. Hii ilimsababishia uadui na makuhani wa Marduk, mungu mkuu wa Babeli.
   (3) Alitumia muda wake mwingi kujaribu kuzima mageuzi na kuimarisha ufalme.
   (4) Aliondoka Tema na kuachia mambo ya nchi kwa mwanawe, Belshazzar, katika mji mkuu wa Babeli (kama vile Dan.5).

i. ? - 539 Belshazzar (mtawala mwenza) - Mji wa Babeli ulianguka kwa haraka kwa Jeshi la Uajemi chini ya Gobryas wa Gutium kwa kuhamisha maji ya mto Frati na kuingia mjini bila kupingwa. Makuhani na watu wa mji waliwaona watu wa Uajemi kama wakombozi na warejeshaji wa Marduk. Gobryas alifanywa Gavana wa Babeli na Koreshi II. Gobryas anaweza kuwa Mede wa Dario Mede wa Dan. 5:31; 6:1. “Dario” maana yake “mtukufu.”

3. Ufalme wa Umedi-Uajemi: Pitio la Kukua kwa Koreshi II (Isa. 44:28; 45:1-7):
   a. 625-585 Cyaxares alikuwa mfalme wa Medi iliyomsaidia Babeli kumshinda Ashuru.
   b. 585-550 Astyages alikuwa mfalme wa Medi. Koreshia alikuwa mjukuu wa Mandane.
   c. 550-530 Koreshi II wa Ansham alikuwa mfalme wa mpito aliyepindua:
      (1) Nabonidasi, mfalme wa Babeli aliyemuunga mkono Koreshi.
      (2) Koreshi II alimvua madaraka Astyages.
      (3) Nabonidasi ili kuweza kurejesha nguvu ya kijeshi, alifanya ushirika pamoja na:
         (a) Misri
         (b) Croesus, Mfalme wa Lydia (Asia Ndogo)
      (4) 547 - Koreshi II aliukabili Sardi (mji mkuu wa Lydia).
      (5) 539 - Mnamo Nov. 2, Gobryas wa Gutium, pamoja na jeshi la Koreshi, waliichukua Babeli bil kipingamizi. Alifanywa gavana wa Babeli.
      (6) 539 - Mnamo Oktoba Koreshi II "Mkuu" binafsi aliingia kama mkombozi. Sera yake ya ukarimu kwa makundi ya kitaifa yakirejeshewa miaka ya uhamisho kama sera ya kitaifa.
      (7) 538 - Wayahudi na wengine waliruhusiwa kurudi nyumbani na kujenga mahekalu yao ya asili.
      (8) 530 - mwana wa Koreshi, Cambyses II, alitawala baada yake.
   d. 530-522 utawala wa Cambyses II
      (1) aliongeza ufalme wa Wamisri mnamo mwaka 525 K.K. kwenye Ufalme wamedi-Uajemi;
      (2) alikuwa na utawala mfupi:
         (a) baadhi wanasema kuwa alijiuwa;
         (b) Herodi anasema kwamba alijikata na upanga wake mwenyewe wakati akipanda katika farasi wake na kufariki kutokana na maambukizi.
      (3) utawala mfupi wa mwamedi wa uongo – 522

e. 522-486 Dario I (Hystapis) alianza kutawala
   (1) Hakuwa natokea uzao wa kialme bali kamanda wa kijeshi.
   (2) Alipangilia Ufalme wa Uajemi akitumia mipango ya Koreshi kwa ajili ya Maakida (kama vile Ezra 1-6; Hagai; Zekaria).
   (3) alianzisha ushirika kama wa Lydia.

f. 486-465 Utawala wa Ahausuero I:
   (1) alizima mapinduzi ya Ki-Misri
   (2) Alitarajia kuvamia Uyunani kutimiza ndoto ya Uajemi lakini alishindwa katika vita ya Thermopoly mnamo mwaka 480 K.K. na Salamis mnamo mwaka 479 K.K.
   (3) Mume wa Esta aitwaye Ahausuero katika Biblia, aliuwawa mnamo mwaka 465 K.K.

g. 465-424 Artashtaza I (Longimanus) alitawala (kama vile Ezra 7-10; Nehemia; Malaki):
   (1) Wayunani waliendelea mbele mpaka kukabiliana na Vita vya Wao kwa wao vya Pelopasania
   (2) Uyunani inagawanya (Wa-Athene – wa-Pelopanisi)
   (3) Vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Wayunani vilimalizika baada ya miaka 20
   (4) wakati wa kipindi hiki Jamii ya Kiyahudi ilitiwa nguvu
   (5) utawala mfupi wa Ahausuero II na Sekydianos – 423

h. 423-404 Dario II (Nothos) anatawala

i. 404-358 Artashtaza II (Mnemoni) alitawala

j. 358-338 Artashtaza III (Ochos) alitawala

k. 338-336 Arses alitawala

l. 336-331 Dario III (Codomannus) alitawala

4. Pitio la Misri:
   a. Hyksos (Mfalme wa-Kichungaji – Watawala wa Kisemiti)-1720/10-1550
   b. Ufalme wa 18 (1570-1310):
      (1) 1570-1546 Amosisi
         (a) aliifanyaThebesi kuwa mji mkuu
         (b) aliivamia Kanaani kusini
      (2) 1546-1525 Amenophis I ( Amenhotep I)
      (3) 1525-1494 Thutmosis I
      (4) 1494-1490 Thutmosis II – alimuoa binti wa Thutmosis I , Hatshepsut
      (5) 1490-1435 Thutmosis III (mpwa wa Hatshepsut)
      (6) 1435-1414 Amenophis II ( Amenhotep II)
      (7) 1414-1406 Thutmosis IV
      (8) 1406-1370 Amenophis III ( Amenhotep III)
      (9) 1370-1353 Amenophis IV (Akhenaten)

(a) aliabudu jua, Aten
(b) alianzisha muundo wa kuabudu mungu mkuu (imani kwa mungu mmoja)
(c) Barua za Tel-El-Amarna ziko katika kipindi hiki

(10) ? Smenkhare
(11) ? Tutankhamun (Tutankhaten)
(12) ? Ay (Aye-Eye)
(13) 1340-1310 Haremhab

c. Ufalme wa 19 (1310-1200):
(1) ? Rameses I (Ramses)
(2) 1309-1290 Seti I (Sethos)
(3) 1290-1224 Rameses II (Ramses II)
(a) kutoka katika ushahidi wa kiakolojia na yawezekana zaidi Farao wa kutoka
(b) alijenga miji ya Avaris, Pithom na Ramses kwa watumwa wa Habaru (yawezekana M-semiti au Mwebrania)
(4) 1224-1216 Marniptah (Merenptah)
(5) ? Amenmesses
(6) ? Seti II
(7) ? Siptah
(8) ? Tewosret

d. Ufalme wa 20 (1180-1065):
(1) 1175-1144 Rames es III
(2) 1144-1065 Rameses IV – XI

e. Ufalme wa 21 (1065-935)
(1) ? Smendes
(2) ? Herihor

f. Ufalme wa 22 (935-725 - Libya):
(1) 935-914 Shishak (Shosenk I au Sheshong I)
(a) alimlinda Yeroboamu I mpaka wakati wa kifo cha Sulemani
(b) Aliitawala Palestina kwa karibia miaka 925 (kama vile 1 Wafalme 14-25; 2 Nyak. 12)
(2) 914-874 Osorkon I
(3) ? Osorkon II
(4) ? Shoshnek II

g. Ufalme wa 23 (759-715 - Libya)

h. Ufalme wa 24 (725-709)

i. Ufalme wa 25 (716/15-663 - Ethiopia/Nubi):
(1) 710/09-696/95 Shabako (Shabaku)
(2) 696/95-685/84 Shebteko (Shebitku)
(3) 690/689, 685/84-664 Tirhakah (Taharqa)
(4) ? Tantamun

j. Ufalme wa 26 (663-525 - Saitiki):
(1) 663-609 Psammetichus I (Psamtik)
(2) 609-593 Neco II (Necho)
(3) 593-588 Psammetichus II (Psamtik)
(4) 588-569 Apries (Hophra)

(5) 569-525 Amasis
(6) ? Psammetiko III (Psamtik)
k. Ufalme wa 27 (525-401 - Kiajemi):
(1) 530-522 Cambyses II (mwana wa Koreshi II)
(2) 522-486 Dario I
(3) 486-465 Ahausuero I
(4) 465-424 Artashtaza I
(5) 423-404 Dario II
*kwa utofatiano wa mtiririko angalia *Zondervan's Pictorial Bible Encyclopedia*, vol. 2 ukur. 231.

5. Pitio la Uyunani:
a. 359-336 Philip II wa Makedonia:
(1) aliijenga Uyunani
(2) aliuwawa mnamo mwaka 336 K.K.
b. 336-323 Iskanda II "Mkuu" (Mwana wa Philipo):
(1) alimpiga Dario II, Mfalme wa Uajemi wakati wa vita vya Isus
(2) Alikufa mnamo mwaka 323 K.K. huko Babeli kama homa akiwa na umri kati ya miaka 32/33.
(3) makamanda wa Iskanda waliugawa ufalme wake wakati wa kifo chake:
(a) Cassender - Makedonia na Uyunani
(b) Lysimicus – Thrace
(c) Seleucus I - Shamu na Babeli
(d) Ptolemy - Misri na Palestina
(e) Antigonus - Asia Ndogo (hakukaa muda mrefu)
c. Wa-Seleucids dhidi ya wa-Ptolemi kwa ajili ya kuitawala Palestina:
(1) Shamu (Watawala wa-Seleucid):
(a) 312-280 Seleucus I
(b) 280-261 Antiochus I Soter
(c) 261-146 Antiochus II Theus
(d) 246-226 Seleucus II Callinicus
(e) 226-223 Seleucus III Ceraunus
(f) 223-187 Antiochus III the Great
(g) 187-175 Seleucus IV Philopator
(h) 175-163 Antiochus IV Epiphanes
(i) 163-162 Antiochus V
(j) 162-150 Demetrius I
(2) Wamisri (Watawala wa ki-Ptolemi):
(a) 327-285 Ptolemy I Soter
(b) 285-246 Ptolemy II Philadelphus
(c) 246-221 Ptolemy III Evegetes
(d) 221-203 Ptolemy IV Philopator
(e) 203-181 Ptolemy V Epiphanes
(f) 181-146 Ptolemy VI Philometor
(3) Pitio fupi:

(a) 301- Palestina chini ya Ptolemy kwa miaka 181.
(b) 175-163 Antiochus IV Epiphanes, mtawala wa nane wa-Seleucid, walitaka kuwa-wasilisha Wayahudi kwa nguvu inapobidi:
   i. walijenga kumbi za sarakasi
   ii. walijenga madhabahu za kipagani za Zeus Olympius katika Hekalu
(c) 168 – Disemba 13 - kuckuliwa mateka kwa kuchinjwa katika madhabahu huko Yerusalemu kulikofanywa na Antiochus IV Epiphanes. Baadhi wanachukulia hii kuwa "chukizo la uharibifu" katika Danieli 8.
(d) 167- Mattathias, kuhani huko Modini, na wana wa kuasi. Watoto wajulikanao zaidi katika watoto wake alikuwa Yuda Makabayo, "Yuda, Mpigiliaji mfano wa nyundo."
(e) 165- Disemba 25 - Hekalu linawekwa wakfu upya. Hii inaitwa *Hanukkah* au "Sherehe ya Mianga."

6. Kwa mjadala mzuri wa matatizo ya uwekaji tarehe, taratibu na nadharia angalia *The Expositors Bible Commentary,*vol. 4 kur. 10-17.

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI (Muktadha)

A. Kuna utaratibu wa kidhahiri wa taarifa ambayo mwandishi anatoa kwa kila mfalme wa kaskazini na kusini.Siku zote taarifa juu ya Wafalme wa Yuda ni kamilifu (inatoka dokezo za darasani za Dr. Huey's SWBTS):
   1. tarehe ya utawala wa mfalme inaratibiwa na jozi kinzani kaskazini au kusini;
   2. jina la mfalme;
   3. jina la baba yake;
   4. umri wake wakati akichukua utawala;
   5. umri wa utawala wake;
   6. eneo la makazi yake;
   7. jina la mama yake;
   8. baadhi ya taarifa juu ya utawala wake;
   9. muhtasari juu ya maisha yake;
   10. simulizi ya kifo chake;
   11. Mara kwa mara #4 & #7 zinaondolewa kwa Wafalme wa Israeli

B. Kuna njia kadhaa tofauti tofauti za kuainisha nyaraka hizi ndefu za kihistoria kwa muhatasari:
   1. kwa kuangalia wahusika wakuu:
      a. Daudi/Sulemani
      b. Rehoboamu/Yeroboamu I
      c. Ahabu (Yezebeli)/Eliya
      d. Eliya/Elisha
      e. Hezekia/Isaya
      f. Yosia/Farao Neco
      g. Yehoiakimu/Yehoiakini/Nebukadneza
   2. kwa mataifa yaliyoshiriki:
      a. ufalme uliounganika
      b. Israeli/Yuda
      c. Shamu

d. Ashuru
e. Babeli

C. Kwa ainisho zaidi kimaelezo angalia:
1. E.J. Young, *An Introduction to the Old Testament*, kur.190-200
2. R.K. Harrison, *Introduction to the Old Testament*, kur.720-721
3. NIV Study Bible, kur. 468-469

VIII. KWELI KUU

A. Hii sio historia ya kimagharibi bali historia ya kithiolojia ya kale ya kimashariki:
1. Wafalme wote wa kaskazini wanashutumiwa kwasababu ya ndama za dhahabu zilizowekwa na Yeroboamu I kumuwakilisha YHWH.
2. Kuna viongozi wenye nguvu zaidi wa kaskazini, Omri na Yeroboamu II wanatazamwa kwa namna fupi na hakuna mafanikio yao ya kisiasa na kijeshi yanayotajwa.
3. Wafalme wa kusini ambao wanapewa kipinzdi kirefu cha matazamio ni Hezekia na Yosia. Wanatajwa kwasababu ya uaminifu wao kwa Agano la Musa na kujaribu kwao kufanya mageuzi ya kiroho.
4. Mfalme mwingine pekee ambaye anapewa hadhi ya muda mrefu ni Manase, mwana wa Hezekia. Lakini hii ni kwasababu anatofautiana haswa na baba yake na anachukua taifa na kuliingiza katika dhambi kubwa.

B. Wafalme wanaendeleza maudhui ya Samweli.Wanatengeneza historia ya vipindi. Kuibuka kwa unabii kwa makuhani kunaendelea. Manabii wasioandikwa wa Eliya na Elisha wanachukua sehemu ya moja ya tatu ya 1 & 2 Wafalme!

C. Wafalme inaonesha kutoka kando kunakoendelea kwa Watu wa Mungu kutoka Agano la Musa. Hii inapelekea mambo yanayoangusha Samaria kwa dhambi (722 K.K.) kuanguka kwa Yerusalemu (586 K.K). Hii haikutokea kwa sababu ya udhaifu wa *YHWH* dhambi ya watu wa Mungu na viongozi wao! Uaminifu wa kiagano lilikuwa jambo kuu. *YHWH* allikuwa mwaminifu! Sulemani, Yuda na Israeli hawakuwa!

IX. MANENO NA/ AU TUNGO NA WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHTASARI

A. 1 WAFALME:
1. Maneno na Tungo:
a. "kama Mungu aishivyo," 1:29 (NASB & NIV)
b. "umpandishe juu ya nyumbu wangu," 1:33 (NASB & NIV)
c. "akazishika pembe za madhabahu," 1:50; 2:28 (NASB & NIV.
d. Yakini na Boaz, 7:21 (NASB & NIV)
e. "akanyosha mikono yake," 8:22 (NASB & NIV)
f. "kidole changu cha mwisho ni kinene zaidi kuliko kiuno cha baba yangu" 12:10 (NIV,"...kinene kuliko kiuno cha baba yangu")
g. Ndama wa dhahabu, 12:28 (NASB & NIV)
h. "wakiruka ruka madhabahuni...wakijikata wenyewe" 18:26,28 (NIV, "wakicheza..na kujikata ...")

i. "muda wa sadaka ya jioni," 18:36 (NIV, “wakati wa sadaka”)
j. "sauti ya kupuliza kwa taratibu" 19:12 (NIV, "sauti ya taratibu ya upole")

2. Watu wa kutambua:
    a. Abishagi, 1:3
    b. Shimei, 2:8
    c. Hiramu, 5:1, 7:13
    d. Malkia waSheba, 10:10
    e. Ashtoreth, 11:5
    f. Moleki, 11:7
    g. Shishaki, 11:40
    h. Omri, 16:16
    i. Nabothi, 21:1
    j. Mikaya, 22:24

B. 2 WAFALME
1. Maneno na tungo:
    a. "magari na farasi wa moto," 2:11; 6:17 (NASB & NIV)
    b. "alifanya maovu mbele za BWANA," 3:2 (NIV, “...macho ya...”)
    c. "funga mshipi wa" 4:29 (NIV, "chomoka vazi lako katika mkanda wako")
    d. "mavi ya njiwa 6:25 (NIV, "mavi ya njiwa")
    e. "nyoka wa shaba ambayo Musa aliitengeneza," (*nehshtan*) 18:4 (NASB & NIV)
    f. "akafanya mfereji wa bwawa" 20:20 (NIV, "...mfereji")
    g. "majeshi ya mbinguni" 21:3 (NIV, "majeshi ya nyota")
    h. "Kitabu cha Sheria," 22:8 (NASB & NIV)
    i. Topheth, 23:10 (NASB & NIV)
    j. "bahari ya shaba," 25:13 (NASB & NIV)
2. Watu wa kuwatambua:
    a. Gehazi, 4:11
    b. Naamani, 5:1
    c. Athaliah, 11:1, 3
    d. Pul, 15:19
    e. Senakeribu, 18:13
    f. Manase, 21:1
    g. Huldah, 22:14
    h. Neco, 23:29
    i. Yehoakini, 24:8
    j. Seraya, 25:18
    k. Gedalia, 25:22

X. MAENEO KATIKA RAMANI (kwa hesabu)

A. 1 Wafalme:
1. En-rogel, 1:9 (Yerusalemu)
2. Gihon, 1:33 (Yerusalemu)
3. Anathoth, 2:26
4. Ghuba ya Misri, 8:65 (NIV, “*wadi ya Misri*”)


5. Megiddo, 9:15
6. Ezion-geberi, 9:26
7. Shekemu, 12:1
8. Penueli, 12:25
9. Ghuba ya Kidroni, 15:13 (NIV, *"Bonde la Kidroni*")
10. Chinneroth, 15:20 (NIV, "*Kinnereth*")
11. Samaria, 16:24
12. Mlima KarmelI, 18:20
13. Ghuba ya Kishoni, 18:40 (NIV, "*Bonde la Kishoni*")
14. Yezreeli, 18:45

B. 2 Wafalme:
1. Ekroni, 1:2
2. Mito ya Abanah na Pharpar, 5:12
3. Dothani, 6:13
4. Sela, 14:7
5. Elath, 14:22
6. Lakishi, 18:14
7. bonde la wana wa Hinnomu, 23:10 (NIV, "...*ya Ben Hinnomu*")
8. Megiddo, 23:30
9. Riblah, 25:6


XI. MASWALI YA KI-MAUDHUI YA MWANAFUNZI

A. 1 WAFALME:
1. Orodhesha baadhi ya sababu kwanini kulikuwa na matatizo mengi katika familia ya Daudi.
2. Kwanini Sulemani alikuwa na wanawake wengi? Ni kwa namna gani walimuathiri katika umri wake wa uzee?
3. Kwanini kiasi kikubwa na maelezo mengi yanatolewa juu ya Hekalu?
4. Kwanini Ufalme uliounganika ulivunjika?
5. Elezea ibada ya Baali/Ashera.
6. Nini maana ya kithiolojia ya 22:18-23?

B. 2 WAFALME:
1. Elezea maana ya 5:15-18.
2. Elezea maana ya 19:19.
3. Orodhesha nguvu ya Hezekia na dhambi ya Manase
4. Ni kwa nani tungo ya (22:8), "nimekipata kitabu cha Sheria" inarejerea?
5. Je Agano la *YHWH* lilikuwa la kimasharti au lisilo na masharti?


KAS
MAGH
MASH
KUS
MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE

# PALESTINA




VIPIMO KATIKA MAILI


# WAFALME WA UFALME ULIOGAWANYIKA

| WAFALME WA YUDA(I NYA. 3:1-16; MT. 1:6-11) | | | | | WAFALME WA ISARELI | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MAJINA NA TAREHE** | **BRIGHT** | **YOUNG** | **HARRISON** | **MAANDIKO YA BIBLIA** | **MAJINA NA TAREHE** | **BRIGHT** | **YOUNG** | **HARRISON** | **MAANDIKO YA BIBLIA** |
| Rehoboamu | 922-915 | 933-917 | 931/30-913 | 1 Fal. 11:43-12:27; 14:21-31 2 Nya. 9:31-12:16 | Yerohoboam I | 922-901 | 933-912 | 931/30-910/09 | 1 Fal.11:26-40; 12:12-14:20 |
| Abiya (Abiyamu) | 915-914 | 916-914 | 913-911/10 | 1 Fal.14:31-15:8 2 Nya.11:20,22 | | | | | |
| Asa | 913-873 | 913-873 | 911/10-870/69 | 1 Fal.15:8-30; 16:8,10,23,29; 22:41,43,46 Yer.41:9 | Nadabu | 901-900 | 912-911 | 910/09-909/08 | 1 Fal.14:20; 15:25-31 |
| | | | | | Baasha | 900-877 | 888-887 | 886/85-885/84 | 1 Fal.15:16-16:17; 2 Fal. 9:9 2 Nya. 16:1-6 Yer. 41:9 |
| Yehoshefati | 873-849 | 873-849 | 870/69-848 | 1 Fal.15:24; 22:1-51 2 Fal.3:1-12; 8:16-19 1 Nya.3:10 2 Nya. 17:1-12:1 | Ela | 877-876 | 888-887 | 886/85-885/84 | 1 Fal.16:8-14 |
| (Yehoramu kaimu mwenza) | ----------- | ----------- | 853-848 | 1 Fal.22:50 2 Fal. 1:17; 8:16; 12:18 | Zimri (kamanda wa jeshi) | 876 | 887 | 885/84 | 1 Fal.16:9-20 2 Fal.9:31 |
| | | | | | Omri (kamanda wa jeshi) | 876-869 | 887-877 | 885/84-874/73 | 1 Fal.16:15-28 2 Fal.8:26 Mika 6:16 |
| Yehoramu | 849-842 | 849-842 | 848-841 | | | | | | |
| Ahazia | 842 | 842 | ------------- | | 1 Nya.21:1-20 Mathayo 1:8 | 869-850 | 876-854 | 874/73-853 | 1 Fal.16:29-22:40 |
| | | | | 2 Fal.8:24-9:29 2 Nya. 22:1-9 | Ahabu | 850-849 | 854-853 | 853-852 | 1 Fal.22:40,41, 49,51-53 2 Nya.18:1-3,19 |
| Atalia (malkia) | 842-837 | 842-836 | 841-835 | | Ahazia | 849-842 | 853-842 | 852-841 | 2 Fal.1:17;3:1-27;8:16-9:29 |
| Yoashi | 837-800 | 836-797 | 835-796 | 2 Fal.8:26; 11:1-20 2 Nya.22:2-23:21 | Yehorumu | 842-815 | 842-815 | 841-814/13 | 1 Fal.19:16-17 2 Fal.9:1-10:36 15:12 2 Nya.22:7-9 Hosea 1:4 |
| Amazia | 800-783 | 797-779 | 796-767 | 2 Fal.11:2-3; 12:1-21 2 Nya.22:11-12; 24:1-27 | Yehu (kamanda wa jeshi) | | | 798-782/81 | |
| (kaimu | ---------- | ----------- | 791/90-767 | | | 801-786 | 798-783 | | 2 Fal.13:9-13,25 2 Nya.25:17-25 |


| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| mweza wa Uzia) | | | | 2 Fal.12:21;<br>14:1-22<br>2 Nya. 25:1-28 | | | | | Hosea 1:1<br>Amosi 1:1 |
| | | | | | | | | 793/92-<br>782/81 | 2 Fal.13:13;<br>14:16,23-29<br>Hosea 1:1 |
| (kaimu<br>mwenza wa<br>Yothamu) | 750-742 | ----------- | 750-740/39 | 2 Nya.26:1-23<br>Hosea 1:1<br>Amosi 1:1<br>Zakaria 14:5 | Yehosa | ----------- | ---------- | 782/81-753 | Amosi 1:1;<br>7:9-11 |
| | | | | | | | | 753-752 | |
| Yothamu | 742-735 | 740-736 | 740/39-<br>732/31 | | | 786-746 | 783-743 | | 2 Fal.15:8-12 |
| | | | | | | | | 752 | |
| | | | | 2 Fal.15:7,<br>32-38 | (kaimu<br>mwenza wa<br>Yer. II) | 746-745 | 743 | | 2 Fal.15:10,<br>13-15 |
| (kaimu<br>mwenza wa<br>Ahazi) | ----------- | ----------- | 744/43-<br>732/31 | | | 745 | 743 | 752-742/41 | 2 Fal.15:14,<br>16-22 |
| | | | | 1 Nya. 5:17 | Yeroboamu II | | | | |
| Ahazi | 735-715 | 736-728 | 732/31-<br>716/15 | 2 Nya.26:23-<br>27:9<br>Isa.1:1;7:1<br>Hosea 1:1<br>Mika1:1 | Zakaria | 745-738 | 743-737 | 742/41-<br>740/39 | 2 Fal.15:23-26 |
| (kaimu<br>Hezekia) | ---------- | ----------- | 729-716/15 | 2 Fal. 15:30-<br>16:20<br>2 Nya.27:9-<br>28:27 | Shalumu | 738-737 | 737-736 | 740/39-<br>732/31 | 2 Fal.15:27-31<br>16:5<br>2 Nya.28:6<br>Isa.7:1 |
| Hezekia | 715-687 | 727-699 | 716/15-<br>687/86 | Isa.1:1; 7:1ff;<br>14:28;38:8<br>Hosea1:1<br>Mika1:1 | Menahemu | 737-732 | 736-730 | 732/31-<br>723/22 | 2 Fal.17:1-18 |
| (Kaimu<br>mwenza wa<br>Manase) | ----------- | ----------- | 696/95-<br>687/86 | 2Fal.16:20;<br>18:1-20,21<br>2 Nya. 28:27-<br>32:33<br>Mith.25:1 | Pekahia | 732-724 | 730-722 | 722 K.K | |
| Manase | 687/86-<br>642 | 698-643 | 687/86-<br>642/41 | Isa.1:136:1-39:8<br>Hosea 1:1<br>Mika 1:1<br>Mt.1:9-10 | Peka | 724 K.K | 722 K.K | | |
| Amoni | 642-640 | 643-641 | 642/41-<br>640/39 | 2 FAL. 20:21-<br>21:18;<br>23:12,26;24:2 | Hosea | | | | |
| Yosia | 610-609 | 640-609 | 640/39-609 | | | | | | |
| | | | | 2 Nya.32:33-<br>33:20<br>Yer.15:4ff<br>2 Fal.21:18-26 | Samaria<br>kuangukia<br>mikononi mwa<br>Shamu | | | | |
| Yehoahazi | 609<br>(miezi 3) | 609 | 609 | 2 Nya. 33:20-25<br>Yer.1:2<br>Zef.1:1<br>1 Fal.13:2-3 | | | | | |
| Yehoiakimu | 609-598 | 609-598 | 609-597 | 2 Fal.21:24;<br>22:1-23:30<br>2 Nya.33:25-<br>35-27 | | | | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Yehoiakini<br><br>Zedekia<br><br>Kuanguka kwa Yerusalemu mikononi mwa Babeli | 598/97 (miezi 3)<br><br>597-586<br><br>586 K.K | 598<br><br>598-587<br><br>587 K.K | 597<br><br>597-587<br><br>587 K.K | Yer.1:2<br>Zef.1:1<br>Mat.1:10-11<br><br>2 Fal.23:30-34<br>2 Nya.36:1-4<br><br>2 Fal.23:34-24:6,19<br>2 Nya.36:4-8<br>Yer.1:3;<br>22:18-23<br>25:1ff<br>26:1ff;27:1ff<br>35:1ff; 36:1ff<br>Dan.1:1-2<br><br>2 Fal.24:17-25:7<br>25:27-30<br>2 Nya.36:8-9<br>Yer.52:31<br>Ezek.1:2<br><br>2 Fal.24:17-25:7<br>2 Nya. 36:10-11<br>Yer.1:3; 21:1-7;<br>24:8-10<br>27:1ff; 32:4-5;<br>34:1-22;<br>37:1-39:7;<br>52:1-11<br><br>Kitabu cha Maombolezo | | | | | |

**Kwa ajili ya mjadala mzuri juu ya matatizo uwekaji tarehe angalia E. R. Thiele, *The Mysterious Numbers of the Hebrew Kings.***


MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE
MAGH
KAS
KUS
MASH

# PALESTINA




VIPIMO KATIKA MAILI

# UTANGULIZI WA 1 & 2 NYAKATI

I. JINA LA KITABU

A. Jina la kitabu kwa Kiebrania ni "maneno (matukio) ya siku (miaka)." Hii inaonekana kutumika kwa namna ya matukio ya miaka. Maneno haya haya yanatokea katika jina la vitabu kadhaa, 14:19,29; 15:7,23,31;16:5,14,20,27; 22:46.Tungo yenyewe inatumika zaidi ya mara thelathini katika 1 & 2 Wafalme na siku zote inatafsiriwa "mambo ya nyakati."

B. Toleo la LXX ilikiita "vitu vilivyoondolewa (juu ya Wafalme wa Yuda)." Hii inamaanisha kwamba Mambo ya Nyakati ni kwa Samweli na Wafalme na kile kinachozungumzwa na Injili ya Yohana kwa Vitabu vyote vya Injili.

C. Jerome, katika fasiri yake ya Kilatini, Vulgate, alikiita "Mambo ya Nyakati ya historia yote takatifu" kwasababu uzao wake unarudi nyuma mpaka kwa Adamu na vitabu vyenza vya Ezra/Nehemia inahusiana na Kipindi baada ya Uhamisho.

D. 1 & 2 Nyakati kiasili ilikuwa kitabu kimoja katika Kiebrania ambavyo vilikuwa vimegawanywa na toleo la LXX, kama ilivyokuwa kwa Samweli na Wafalme.

II. URASIMISHAJI

A. Hiki ni kitabu cha mwisho cha sehemu ya “maandiko" kanoni ya kiebrania. Hii inamaanisha ni kitabu cha mwisho cha Biblia ya kiebrania.

B. nafasi yake katika kanoni ya kiebrania inamaanisha:
   1. utungwaji wake wa baadaye;
   2. asili yake ya kimutahsari;
   3. kilionekana kama kiambatisho;
   4. kilikubaliwa katika kanoni kiiwa kimechelewa.

C. Toleo la LXX lilikiweka baada ya Wafalme na baada ya Ezra. Inashangaza kwamba Ezra/Nehemia anawekwa kabla ya Mambo ya Nyakati, Yawezekana kwasababu ya asili yake ya kimutahsari.

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Kitabu hiki ni simulizi ya kihistoria lakini katika maana maalumu ya kichaguzi ya kithiolojia.

B. Kinaondoa vipengele kanushi vingi zaidi vya utawala wa :
   1. Daudi
   2. Sulemani
   3. Wale Wafalme wa Yudea "watauwa":
      a. Asa
      b. Yehoshefati
      c. Uzia
      d. Hezekia
      e. Yosia

IV. UANDISHI

A. Biblia yenyewe iko kimya juu ya uandishi wake.

B. Baba Bathra 15a anasema kwamba Ezra aliandika kizazi cha Mambo ya Nyakati yeye mwenyewe. Hii imetafsiriwa kwa njia mbili:
   1. Ezra aliandika Mambo ya Nyakati
   2. Ezra alimalizia historia iliyoanzwa katika Mmamo ya Nyakati katika siku zake mwenyewe

C. Ezra 1:1-4 na 2 Nyakati 36:22-23 ni sawasawa katika Kiebrania. Wote wawili Young na Harrison wanasema kwamba Mambo ya Nyakati iliandikwa kwanza. Sehemu hii ilithibitisha kwa mbinu ya kiuandishi iliyotumiwa na waandishi wa kibabeli "vivutio" au mtindo wa aina yake. Mbinu haionekani katika maandiko ya Kiyahudi. Hii ingemaanisha kwamba Ezra alikuwa akitumia Mambo ya Nyakati kama utangulizi wa kihistoria kwa kazi yake mwenyewe ambayo iliendeleza historia ya Wayahudi.

D. Mwandishi/Waandishi wa Mambo ya Nyakati na Ezra/Nehemia wana lengo linalofanana la kithiolojia na mtazamo:
   1. shabaha ju ya Hekalu na ukuhani (haswa orodha ya Walawi)
   2. matumizi yaliyopitiliza ya kumbukumbu za kitakwimu na vizazi
   3. misamiati na staili za kifasihi
   4. lazima isemwe, nazo pia zinatofautiana:
      a. kuna kutajwa majina kunakotofautiana
      b. Mambo ya Nyakati inajikita katika uzao wa Daodi wa kifalme wakati Ezra/Nehemia inajikita juu ya agano la Musa

E. William Albright anaweka sifa uandishi wa Ezra kati ya miaka 428 na 397 K.K. Mapinduzi ya Ezra yanapatikana katika Ezra 7-10 yanayotokea mnamo 458- 457 K.K. chini ya Artashtaza I.

F. Mambo ya Nyakati kinatumia vyanzo vingi:
   1. Maandiko yaliyoandikwa hapo kabla:
      a. Mambo ya Nyakati inatumia nusu ya Samweli na Wafalme au karibia vyanzo vilevile.
      b. 1 Nyakati inaonekana kujua baadhi ya maandiko ya Agano la Kale hasa:
         (1) Mwa. 35:22 -- 5:1
         (2) Mwa. 38:7 -- 2:3
         (3) Mwa. 38:30 -- 2:4,6
         (4) Mwa. 46:10 -- 4:24
         (5) Mwa. 46:11 -- 6:16
         (6) Mwa. 46:13 -- 7:1
         (7) Mwa. 46:21 -- 7:6,12
         (8) Mwa. 46:24 -- 7:13
         (9) Ruthu 4:18-21 -- 2:11-13
         (10) 1 Sam. 27:10 -- 2:9, 25-26
         (11) 1 Sam. 31:1-6 -- 10:1-12
      c. Utangulizi wa NIV Study Bible kwa Mambo ya Nyakati kama vyanzo:

(1) Vitabu vitano vya Musa
(2) Waamuzi
(3) Ruthu
(4) 1 Samueli
(5) Wafalme
(6) Zaburi
(7) Isaya
(8) Yeremia
(9) Maomboalezo
(10) Zekaria

2. nyaraka za kihistoria zilizoandikwa tokea ufalme uliogawanyika.
   a. yawezekana nyaraka rasmi za kimahakama:
      (1) Mambo ya Nyakati ya Mfalme Daudi, 1 Nyakati. 27:24
      (2) kitabu cha wafalme wa Yuda na Israeli, 2 Nyakati 16:11; 25:26; 28:26; 32:32
      (3) kitabu cha wafalme wa Israeli na Yuda, 2 Nyakati 27:7; 35:27; 36:8
      (4) kitabu cha Wafalme wa Israeli, 1 Nyakati 9:1; 2 Nyakati 20:34
      (5) maneno ya wafalme wa Israeli, 2 Nyakati. 24:27; 33:1
   b. manabii:
      (1) matendo ya Daudi, 1 Nyakt. 29:29:
         (a) Mambo ya Nyakati ya Samweli, Muonaji
         (b) Mambo ya Nyakati ya Nathani, nabii
         (c) Mambo ya Nyakati ya Gadi, muonaji.
      (2) matendo ya Sulemani, 2 Nyakati. 9:29:
         (a) kumbukumbu za Nathani nabii
         (b) unabii wa Ahija Mshilo
      (3) matendo ya Yeroboamu 1 katika maono ya Iddo muonaji, 2 Nyakati 9:29
      (4) matendo ya Rehoboamu katika 2 Nyakati 12:15:
         (a) kumbukumbu za Shemaiya nabii
         (b) Iddo muonaji
      (5) Matendo ya Abiya katika 2 Nyakati 13:22 yaliyoandikwa na Iddo nabii
      (6) Matendo ya Yehu katika 2 Nyakati 20: 34 yaliyoandikwa na Mwana wa Hanani
      (7) Matendo ya Manase katika 2 Nyakati 33:19 yaliyoandikwa na Hozai (LXX "muonaji")
   c. kumbukumbu za vizazi vya kikabila:
      (1) Simeoni, 1 Nyakati 4:33
      (2) Gadi, 1 Nyakati 5:17
      (3) Benjamini, 7:9
      (4) Asheri, 7:40
      (5) Israeli yote, 9:1
      (6) walinzi wa Kilawi wa lango, 9:22 (maana ikiwa kila mgawanyiko wa kilawi pia ulikuwa na kumbukumbu [kama vile 1 Nyakati 23:1 na kuendelea; 28:13; 2 Nyakati 35:4]).
   d. vyanzo vya kigeni:
      (1) barua za Senakarebu, 2 Nyakati. 32:17-70
      (2) Matamko ya Koreshi, 2 Nyakati 36:22-23

G. Kama Ezra-Nehemia, Mambo ya Nyakati anaorodhesha vizazi vya watu kadhaa. Baadhi ya hizi zinakua katika wakati ujao baada ya vzazi vine ampaka sita. Kumekuwa na njia mbili za kushugulikia hili:
   1. hizi zilikuwa nyongeza za kihariri;
   2. Hizi ni familia za kisasa, sio vizazi.

V. TAREHE

A. Kuna maandiko mawili katika Mambo ya Nyakati ambayo yanamaanisha kipindi baada ya kurudi kwa maandiko ya Mambo ya Nyakati:
   1. 1 Nyakati 3:19-21. Hii ni orodhaya vizazi vya Zerubbabeli:
      a. baadhi wanasema mapaka vizazi vya sita
      b. wengine wanasema vizazi viwili tu vikifuatiwa na orodha ya familia nne za familia za Daudi waliokuwa wa kisasa wa uzao wa aina mbili za Zerubabeli - Pelatia na Jeshaya (Young & Harrison)
      c. toleo la LXX linakuza orodha ya uzao wa Zerubabeli mpaka kizazi cha kumi na moja (hii inaonesha kuhuishwa kwa uhariri)
   2. 1 Nyakati 3:22-24 - hii ni orodha ya vizazi vya Shekania vinavyotajwa katika mstari wa 21:
      a. baadhi wanasema orodha ni ya vizazi vinne (NIV Study Bible)
      b. ikiwa hii ndivyo ilivyo sasa tarehe ya mwandishi (mhariri) inakuzwa kutoka kizazi cha Zerubbabeli katika 3:19-21
   3. 2 Nyakati 36:22-23:
      a. hii pia inamtaja Koreshi II na tamko lake ambalo liliruhusu watu wote waliotawaliwa kurudi nyumbani ikijumuisha Wayahudi
      b. Koreshi II analitoa tamko lake mnamo 538 K.K. Kurudi kwa kwanza kulichukuliwa mara moja na mwana wa mfalme wa Yudea aliyeteuliwa gavana, Sheshbazzar. Alianza kulijenga upya Hekalu lakini hakulimaliza. Baadaye, chini ya Mfalme wa Uajemi Dario 1, wengine walianza kurudi chini ya Zerubabeli wa uzao wa Daudi na Yoshua kama mzao wa Kuhani Mkuu. Walimaliza kulijenga upya Hekalu mnamo mwaka 516 K.K. kukiwa na kutiwa moyo na Haggai na Zekaria.

B. Tokea vizazi vya kitabu tarehe ya mtungaji inaonekene kuwa kati ya mnamo miaka ya 500-423 K.K. Tarehe hii ya kimatukio inajumuishwa kwasababu inaonekana kuwa maelezo mapya kabisa ya kihistoria ya Agano la Kale. Dario II alivikwa taji mnamo mwaka 428 K.K. Anatajwa katika 12:22. Pia desturi zianasema kwamba Agano la Kale la kanoni ilihitimishwa mnamo muda huu.

C. 1 Nyakati ilichukua kipindi kile kile kama 1 & 2 Samweli, hatahivyo, uzao wake unarudi nyuma mpaka kwa Adamu. 2 Nyakati inachukua kipindi kile kile kama 1 & 2 Wafalme lakini kinapanuliwa, karibia mpaka muda wa Koreshi II.

VI. KUTHIBITISHA MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. Kuna tofauti za dhahiri kati ya uwasilishaji wa kihistoria wa Samweli na Wafalme na ya Nyakati:
   1. Hesabu katika Nyakati ni kubwa (Young, kur. 394-400)
      a. Hii kijumla ni kweli ukilinganisha na 1 Nyakati 21:5 ikiwa pamoja na Sam. 24:9

b. mara kwa mara Mambo ya Nyakati ilikuwa na hesabu ndogo ukilinganisha na 1 Wafalme. 4:26 pamoja na 1 Nyakati 9:29
c. mengi zaidi ya matatizo mengi pia yanapatikana katika fasiri ya LXX ambayo inamaanisha kupanga tarehe kabla ya mwaka 250 K.K.
d. E.R. Thiele, katika kitabu chake cha kihistoria, *The Mysterious Numbers of the Hebrew Kings,* 1954, 1965, inaelezea tofauti kwa:
   (1) mifumo miwili ya uwekaji tarehe:
      (a) mwaka wa ukamilishaji;
      (b) mwaka usio wa ukamilishaji.
   (2) Upatanishao wa pamoja

2. Mambo ya Nyakati inaelezea vipengele chanya vya wafalme wa Yuda wa ukoo wa Daudi
3. Mambo ya Nyakati inaondoa sehemukubwa ya nyaraka kanushi juu ya Daudi na Sulemani. Hatahivyo kama Young anavyoweka wazi (kur. 395-398), pia kinaondoa karibia kila kitu kuhusu maisha yao ya usiri, sio tu zile mbaya lakini pia baadhi ya vipengele chanya.
4. Mambo ya Nyakati pia inaondoa rejea zote kwenye Ufalme wa Kaskazini. Sababu haijulikani. Wengi wanadhania ilikuwa ni kwasababu Wafalme wote wa Kaskazini walishutumiwa kwasababu ya ndamu wa dhahabu waliowekwa huko Dani na Betheli. Kusini kulichukuliwa kuwa uzao wa kweli, wa kiuaminifu wa Daudi tu (wa-Kimasihi).

B. Uhabiti wa historia ya Mambo ya Nyakati inatabia ya kukubaliwa:
1. katika vitu vya kizazi ambavyo vinafananishwa na:
   a. Samweli
   b. Magombo ya Bahari ya Chumvi
   c. toleo la LXX
2. Wakati wa nyaraka za kivcizazi vya Mambo ya Nyakati inafananishwa katika Mwanzo na Hesabu katika Maandiko ya ki-Masoreti na Vitabu vitano vya Torati vya Ki-samaria, uthabiti wake wa kihistoria inapewa mashiko

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI (muktadha)

A. Ainisho fupi:
1. nyaraka za vizazi tokea Adamu mpaka Sauli, 1 Nyakati 1:1-9:44
2. Utawala wa Daudi, 1 Nyakati 10:1-29:30
3. Utawala wa Sulemani, 2 Nyakati 1:1-9:31
4. Utawala wa Wafalme wengine wa Yudea kwenda Uhamishoni na kwa Koreshi, 2 Nyak. 10:1-36:23

B. Kwa uainisho wa ziada angalia:
1. E.J. Young, *An Introduction to the Old Testament*, kur. 401-402
2. R.K. Harrison, *Introduction to the Old Testament*, kur. 1152-1153
3. NIV Study Bible, kur. 581-582

VIII. KWELI KUU

A. Hii ni historia baguzi ya kithiolojia ya Yuda kwa kutumia ila ikipanua simulizi sambamba katika 1 & 2 Samweli na 1 & 2 Wafalme.


B. Hii iliandikwa kwa jamii ya baada ya uhamisho ambao kwa shauku walihitaji kujua kwamba Mungu wa Agano alikuwa bado Mungu wao. Hekalu (kwakuwa kulikuwa na kubisha) lilikuwa shabaha ya Agano lililofanywa upya na Mungu. Agano lilikuwa bado ni la kimasharti juu ya utii wa maelekezo ya Ki-Mungu kupitia Musa.

C. kimsingi inajikita juu ya ahadi za Mungu na mwanawe inayopatikana katika 2 Samweli 7:
   1. anashughulikia bila ujumuishi pamoja na wana wa Daudi na katika kilele cha Masihi Mfalme
   2. kinatoa simulizi chanya ya utawala wa Daudi, Suleimani na Wafalme wa Yuda "watauwa"
   3. kinaweka kumbukumbu marejesho ya Waebrania kwa Yerusalemu inayofanywa na Koreshi II, 36:22-23
   4. kinaweka msisitizo wa Mfalme wa ukoo wa Daudi (Masihi). Njia moja hii ilikamilishwa ilikuwa kupitia kuweka kumbukumbu ya utawala wa Daudi wa "kutauwa", Sulemani na wafalme watauwa wa Yuda. Tumaini hili pia linaelezewa katika Zekaria na Malaki.

D. Pia kuna msisitizo juu ya watu wote wa Mungu kuunganishwa. Hii inaonekana kwa matumizi ya neno la kiujumuishi "Israeli wote" (kama vile 1 Nyakati 9:1;11:1-3,4; 12:38; 16:3; 18:14; 21:1-5; 28:1-8; 29:21,23,25; Nyakati 1:2; 2:8; 9:30; 10:1,16; 12:1; 18:16; 28:23; 29:24; 30:1,6,25-26; 34:7,9,33).


E. Vizazi vinatumika:
   1. kama zile katika Ezra na Nehemia kuoneshwa kwamba Israeli iliyorejeshwa kisheria ni Israeli ya zamani
   2. kuweka muhtasari historia ya Waebrania kurudi kwa Adamu

   *Kwasababu 1 & 2 Nyak. Kimsingi ni matukio yale yale kama 1 & Samweli na 1 & 2 Wafalme, hakutakuwa na Istilahi, ramani au maswali kwa vitabu hivi viwili!




MASHARIKI YA KARIBU YA KALE

# PALESTINA



# UTANGULIZI WA EZRA

I. JINA LA KITABU

A. Ezra na Nehemia viko katika kitabu kimoja katika Kanoni ya Kiebrania (MT).Baba Bathra 15a. iliviita Ezra.
   1. Hii si kawaida kwasababu ni dhahiri kwamba vyote vinajumuisha orodha ya uzao: Ezra 2:1 na kuendelea na Nehemia 7:6-20.
   2. Kwasababu orodha japo ina utofautiano kidogo kimsingi ni vile vile, maana yake ni kwamba kiasili vilikuwa viwili.
   3. Hii inathibitisha kwa matumizi ya sehemu za "Mimi" katika zote Ezra 7-10 na Nehemia.

B. Yawezekana viliunganishwa kwasababu ya huduma ya Ezra (Ezra 7-10) inaendelea katika Nehemia 8-10.

C. Majina ya Ezra na Nehemia vinatofautiana kati ya fasiri za kale:

| LXX | Vulgate | Wycliffe & Coverdale English | Kingereza cha Kisasa |
|---|---|---|---|
| Esdra B (Beta) | Esdras I | I Ezra | Ezra |
| Esdra C (Gamma) | Esdras II | II Ezra | Nehemia |
| Esdra A (Alpha) | Esdras III | ----- | I Esdras (isiyo rasmi) |
| | Esdras IV | ----- | II Esdras isiyo rasmi |

D. Andiko la kwanza la Kiebrania kugawa vitabu hivi mnamo mwaka 1448 B.K. katika uhariri wa MT.

II. URASIMISHAJI

A. Kitabu cha Ezra ni sehemu ya mgawanyo wa tatu wa kanoni ya Kiebrania iitwayo "Maandiko."

B. Kiliwekwa katika MT kabla ya Mambo ya Nyakati. Huu ulikuwa ni mpangilio usio kuwa wa kawaida. Mpangilio wa mfuatano unatakiwa uwe wa Mambo ya Nyakati, alafu Ezra/Nehemia. Kuna nadharia kadhaa (kama vile Nehemia, II. B).

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Masimulizi ya kihistoria ni riwaya ya moja kwa moja

B. Inajumuisha nukuu nyingi kutoka katika nyaraka zingine:
   1. Uajemi
   2. Kiyahudi

IV. UANDISHI

A. Baba Bathra 15a inasema kwamba Ezra aliandika kitabu hiki lakini hii haimaanishi kwamba aliandika Nehemia pia. Ukweli ni kwamba, vyanzo vingine vya Kiyahudi (Gemara) vinasema kwamba Nehemia alikimalizia (Ezra -Nehemia). Madokezo ya mwisho ya MT yanapatikana tu mwishoni mwa Nehemia.

B. Josephus katika *Contra Apion* yake, 1:8, na Melito wa Sard ananukuliwa na *Eusebius', Ecclesiastical History* IV:26, wote wanaelezea uandishi wa Ezra.

C. Sehemu ya Ezra ambayo inajishughulisha na maisha ya Uandishi wa maisha ya Ezra (sura za 7-10) imeandikwa katika nafasi ya kwanza,7:27-28; 8:1-34; 9:1 na kuendelea. Ezra alikuwa kuhani wa ukoo wa Sadoki na mwandishi wa mahakama ya kiajemi wa Artashtaza (465-424 K.K.).

D. Kuna ufanano mwingi kati ya Ezra/Nehemia na Mambo ya Nyakati:
   1. ufungaji wa 2 Nyakati 36:22-23 karibia ni sawa na kufanana na Ezra 1:1-4 kiebrania
   2. vyote vina mtazamo unaofanana wa kithiolojia:
      a. inajikita katika hekalu na ukuhani (haswa orodha ya Walawi)
      b. matumizi mapana ya kumbukumbu za kitakwimu na uzao
   3. misamiati yao na staili ya kifasihi
   4. vyote viwili vinatumia Kiebrania cha kisasa
   5. hatahivyo lazima isemwe pia kuna tofauti za wazi zinazoonekana:
      a. katika kutaja majina ya kifalme;
      b. Ezra na Nehemia anajikita juu ya agano pamoja na Musa wakati 1 & 2 Nyak.vinajikita juu ya agano pamoja na Daudi.

E. Origen (185-253 B.K), msomi Mkristo wa Iskandria, alikuwa wa kwanza kugawa kitabu katika vitabu viwili vya Ezra na Nehemia. Jerome alifanya hivyo hivyo katika fasiri yake ya Kilatini ya Vulgate.

F. Maandiko ya kwanza ya Kiebrania kugawa kitabu yalikuwa mnamo mwaka 1448 B.K. Inavyoonekana kwa muda huu shauku ya Kiyahudi kuwa na vitabu 22 katika Agano la Kale kulinganisha barua 22 za alfabeti za Kiebrania ilikuwa imekwisha kupita.

G. Mwandishi/mmtungaji alitumia vyanzo vingi:
   1. Nyaraka za Kiajemi
   2. kumbu kumbu za Kiyahudi:
      a. orodha ya vyombo kutokea hekalu la *YHWH* ambayo yalikuwa katika Babeli, 1:9-11; 7:19-20
      b. orodha ya wa uhamishoni warudio, 2:1-70; 8:1-20
      c. uzao wa Ezra, 7:1-5
      d. orodha ya wale wanaojumuishwa katika ndoa za mchanganyiko, 10:18-43

V. TAREHE

A. Ezra alikuwa kuhani wa ukoo wa Sadoki (7:2) na mwandishi katika utawala wa Artashtaza I (465-424 K.K.):
   1. Ezra alikuja Yerusalemu katika mwaka wa saba wa Artashtaza I, 458 K.K., kukiwa na wimbi la kurudi kwa wana wa uhamisho wa Kiyahudi.
   2. Nehemia alikuja Yerusalemu katika mwaka wa ishirini wa Artashtaza I, 445 K.K., kama gavana wa uajemi.

B. Inaonekana kwamba vizazi vya Ezra/Nehemia vinaweka mwandishi au mtungaji mwishoni mwa karne ya 5 K.K:
    1. hii ni kudhani kwamba 1 Nyakati 3:15-24 inaorodhesha vizazi vine baada ya Zerubabeli, wala sio sita;
    2. hii ni kudhani kwamba Yadua wa Nehemia 12:10-11 alikuwa:
        a. sio Yadua Yule Yule ambaye Josephus anamuweka katika wakati wa Iskanda Mkuu (336-323 K.K.);
        b. au kwamba uzao huu uliongezwa na mhariri baada ya ile ya asili kuondolewa ili kuhuisha taarifa;
        c. au kwamba alikuwa mdogo sana katika siku za Nehemia na aliishi katika siku za Iskanda.

C. Hii ingeweka uandishi wa historia hizi zinazofanana juu ya:
    1. 440 K.K.kwa ajili ya Ezra
    2. 430 K.K kwa ajili ya Nehemia
    3. 400 K.K. kwa ajili ya Mambo ya Nyakati

VI. VYANZO VINAVYOTHIBITISHA MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. Muundo wa nyaraka katika Ezra unafuata utaratibu na staili ya nyaraka za rasmi za kipindi cha Kiajemi:
    1. tamko la Koreshi (fasiri ya Kiebrania), 1:2-4. (juu ya kurudi Yerusalemu)
    2. mashtaka ya kisheria yaliyoletwa na Rehumu kwa Artashtaza I, 4:7-16. (juu ya kuta za Yerusalemu)
    3. mwitikio wa Artashtaza I, 4:17-22
    4. mashataka ya kisheria yaliyoletwa na Tattenai kwa Dario I, 5:6-17
    5. mwitikio wa Dario wa I (kuhusu Hekalu):
        a. nukuu za matamko ya Koreshi, 6:2-5
        b. mwitikio wa binafsi wa Dario kwenda kwa Tattenai, 6:6-12,13
    6. tamko la Artashtaza kwenda kwa Ezra, 7:12-26

B. Mafunjo ya Elephantine (408 K.K) yalithibitisha historia ya Ezra/Nehemiah kwa kumtaja Sanballat (Sin-Uballit katika kibabeli),Neh. 2:10,19; 4:1. Pia yalielezea aina ya Kiaramu cha Kifalme.

C. Mabakuli kadhaa ya shaba yalipatikana huko Succoth ambayo yaliandikwa "kwa mwana wa Geshemu aitwaye Qainu," ambayo inaonesha historia ya Geshimu, Muarabia, Ezra/Nehemia, aliyetawala ufalme wa Kedari (kama vile Neh. 2:19; 6:1,6).

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI (muktadha)

A. kurudi mapema Yerusalemu, 1:1-2:70
    1. Katika utawala wa Koreshi (550-530 K.K) Sheshbazzar aliteuliwa kuwa gavana, 5:14. Alikuwa mtawala wa Yuda, 1:8, yawezekana mwana wa kiume wa Yehoakini. Alirudi Yerusalemu akiwa na hazina za Hekalu, 1:1-11. Aliweka msingi wa Hekalu lakini hakuweza kuumaliza, 5:13-17.

    2. Katika utawala wa Koreshi na Dario (4:5, 522-486 K.K) Zerubbabeli aliyekuwa wa ukoo wa Daudi alikuwa ameteuliwa gavana. Alirudi pamoja na Yoshua (au Yeshua) wa ukoo wa Kuhani Mkuu wa Mwisho, kwenda Yerusalemu, 2:1-70.

B. Kuna kuanzishwa kwa ibada ya *YHWH* katika Yerusalemu na Zerubabeli na Yoshua, 3:1-6:22
   1. Karamu za Vibanda na sadaka za mara kwa mara zilianza, 3:1-13
   2. matatizo ya kisiasa katika kumaliza miradi ya ujenzi, 4:1-24:
      a. hekalu, 1-5, 24
      b. kuta za Yerusalemu, 6-23
   3. Manabii wanahamasisha ujengwaji mpya lakini sharti wasubiri uthibitisho rasmi wa Kiajemi, 5:1-17
   4. Tamko la Koreshi lilipatikana na ruhusa rasmi ilitolewa kulijenga upya Hekalu, 6:1-22

C. Kurudi kwa mara ya tatu chini ya Mwandishi Ezra, 7:1-10:44
   1. uzao wa Ezra na kurudi kwa Yerusalemu, 7:1-10
   2. Barua ya Artashataza kwa Ezra, 7:11-26, na maombi yake ya shukurani, 7:27-28
   3. kurudi, 8:1-36
   4. tatizo la ndoa mchanganyiko, 9:1-10:44

VIII. KWELI KUU

A. Ezra/Nehemia vinaendeleza historia kipindi cha Kiajemi cha baada ya uhamisho ambapo 2 Nyakati inaisha

B. Inaonesha uthibitisho wa kikabila wa uhaisho urudio kwa:
   1. vizazi vya kikabila kiupana;
   2. migawanyo ya kilawi ya kiupana;
   3. kutengwa kidini kwa waliorudi katika kuhusiana na mataifa yanayowazunguka.

C. Mungu amejieneza upya kiagano pamoja na uzao wa Yakobo

D. Inaonesha maendeleo ya utaratibu mpya wa kuabudu ambao unajikita katika masinagogi ya maeneo ya mahali na waandishi. Hii hasa haikuacha ibada za Hekalu katika Yerusalemu.

IX. MANENO NA/AU TUNGO NA WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHTASARI

A. Maneno na/au tungo:
   1. "kutimiliza neno la Bwana kwa kinywa cha Yeremia," 1:1 (NIV, “kusema...”)
   2. "Mungu wa Mbinguni," 1:2 (NASB & NIV)
   3. "kila mtu ambaye roho ya Mungu imehimizwa," 1:5 (NIV, “...moyo wa Mungu umeenda hapo kabla”)
   4. "nyaraka katika nyumba ya Mungu," 1:7 (NIV, “...ikimilikiwa na hekalu...”)
   5. Urim na Thumim, 2:63 (NASB & NIV)
   6. "jimbo mbele zaidi ya Mto," 4:16 (NIV, “Frati”)
   7. dhiraa, 6:3 (NIV, “miguu”)
   8. kitabu cha Musa, 6:18 (NASB & NIV)
   9. mwandishi, 7:6 (NIV, “mwalimu”)
   10. Nethinim, 7:24 (NIV, “watumwa wa hekalu”)

B. Watu wa kutambua kwa muhtasari:

1. Koreshi, 1:1
2. Mithredathi, 1:8; 4:17
3. Sheshbazza, 1:8,11; 5:14
4. Zerubabeli, 2:2
5. Yeshua, 2:2
6. Ahausiero, 4:6 (NIV, Ahausiero)
7. Osnappa, 4:10 ( NIV, Ashurbanipal)

X. MAENEO KI-RAMANI (kwa hesabu)

1. Mto Frati
2. Yerusalemu
3. Samaria
4. Ekibatana, 6:2


XI. MASWALI YA KI-MAUDHUI YA MWANAFUNZI

1. Ni kwa namna gani Sheshbazza na Zerubabeli wanahusiana?
2. Je 3:6 inapingana na 5:16?
3. Kwanini orodha katika Ezra 2 inatokea upya katika Neh. 7?
4. Nini tabia ya jina la kiajemi la mungu katika kutumiwa mara kwa mara katika vitabu vya baada ya uhamisho kwa kutumia *YHWH*?
5. Manabii Haggai na Zekaria waliotajwa katika 5:1, waliwatia moyo watu kufanya nini?
6. Kwanini tamko la Koreshi lilikuwa na umuhimu sana kwa Wayahudi?
7. "Ndoa mchanganyiko"? Zilikuwa ni nini? Kwanini zilikwa muhimu sana kwa Ezra na Nehemia?




MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE

# PALESTINA



# UTANGULIZI WA NEHEMIA

I. JINA LA KITABU

A. Ezra- Nehemia ni kitabu kimoja katika MT kilicho na jina la Ezra. Dokezo za mwisho za MT zinatokea tu mwishoni mwa Nehemia.

B. Kwa mjadala kamili wa majina tofauti tofauti kitabu hiki kilivyoitwa katika LXX na Vulgate (kama vile Utanguizi wa Ezra, I.)

C. Jina Nehemia linamaanisha "YHWH amefariji."

II. URASIMISHAJI

A. Kitabu cha Ezra-Nehemia ni sehemu ya tatu ya kanoni ya Kiebrania iitwayo "Maandiko."

B. kinakuja kabla ya "Mambo ya Nyakati" ambayo inashangaza kwakuwa kihistoria/kimfuatano inalazimika kuwa simulizi ya kihistoria ya Mambo ya Nyakati. Baadhi wamejaribu kuelezea hii kwa:
   1. Mambo ya Nyakati ni muhtasari kutokea Adamu kwenda kwa Koreshi.
   2. Ezra-Nehemia zilikubalika kwanza kama rasmi.
   3. Mambo ya Nyakati  inawekwa mwsho kwasababu Wayahudi walitaka kanoni iishie katika dokezo chanya (tamko la Koreshi).
   4. Hakuna mtu ajuaye vigezo au mantiki ya uundaji wa sehemu ya "maandiko" ya kanoni ya Kiebrania.

C. Uhariri wa kwanza wa Kiebrania wa MT kuvigawa ulikuwa mnamo mwaka 1448 B.K.

D. Hatahivyo, ni wazi kutokana na ushahidi wa ndani kwamba kiasili vilikuwa vitabu viwili:
   1. orodha pana ya vizazi ya Ezra inarudiwa katika Neh. 7:6-70. Majina yanatamkwa tofauti kidogo;
   2. kuna sehemu ya “Mimi” katika Ezra 7:27-28; 8:1-34; 9:1 na kuendelea na sehemu za “Mimi” katika Nehemia.

E. Kwanni waliunganishwa?
   1. wanatengeneza historia moja.
   2. Imeelezewa kwamba sababu kwanini Ezra-Nehemia ziliunganishwa katika kanoni ya Kiebrania ilikuwa ni kuwa na hesabu ya vitabu katika Agano la Kale kuweka sawa hesabu konsonanti katika alfabeti za Kiebrania. Hii ilimaanisha kwamba vitabu vifuatavyo viliunganishwa:
      a. Waamuzi na Ruthu
      b. Samweli
      c. Wafalme
      d. Mambo ya Nyakati
      e. Ezra – Nehemia
      f. Yeremia-Maombolezo
      g. Manabii wadogo Kumi na mbili
   3. Huduma ya Ezra ambayo inaanza katika Ezra 7-10 na kuendelezwa katika Neh. 8-10.

F. Uhariri wa kwanza wa Kiebrania wa MT kuwagawa ilikuwa mwaka 1448 B.K.

G. Inafurahisha kwamba mrasimishaji wa mwanzo wa Kishamu Theodore wa Mopsuestia (kiongozi wa Antiokia shule ya ufasiri) aliondoa Mambo ya Nyakati, Ezra na Nehemia kutoka katika orodha yao ya vitabu vilivyovuviwa.

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Angalia Ezra IV, D (ufanano kati ya Ezra, Nehemia na Mambo ya Nyakati)
B. Angalia Ezra IV, G (matumizi ya nyaraka)

IV. UANDISHI

A. Baba Bathra 15a anasema kwamba Ezra-Nehemia ni kitabu kimoja kilichoandikwa na Ezra.

B. Gemara anasema kwamba Nehema alimsaidia kuandika kitabu (Ezra/Nehemia).

V. TAREHE

A. Wasomi wa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20 B.K waliamini vitabu vya Ezra-Nehemia na Mambo ya Nyakati kuwa vimeandikwa katika karne ya nne K.K:
   1. Mzao wa Yoshua Kuhani Mkuu aliyemsindikiza Zerubabeli katika kurudi kwake mara ya pili (chini ya Koreshi) alikuwa Yaddua; bado anatajwa katika Nehemia 12:10-11, 22.
   2. Wao wanaelezea kwamba huyu Yadua alitajwa na Josephus (Antiquities, XI:302-7) kama Kuhani Mkuu (351-331 K.K) katika muda wa uvamizi mkubwa juu ya Palestina wa Iskanda Mkuu 333-332 K.K.;
   3. Hii inaunganisha pamoja na vizazi sita vya Zerubabeli vinavyo-jiorodhesha katika 1 Nyak. 3:19-24;
   4. wasomi wengi zaidi hawa pia walishikilia msimamo kwamba Ezra alirudi katika utawala wa Artashtaza (404-358 K.K.) wakati Nehemia alirudi katika utawala wa Artashtaza (465-424 K.K);
   5. Neh. 12:26, 47 inaonesha mhariri/mtungaji wa baadaye .

B. Baadaye karne ya 20 wasomi wenye mlengo wa mabadiliko wameelezea tarehe kwa vitabu hivi vitatu kuwa ni karne ya tano K.K:
   1. Yadua wa Neh. 12:10-11,22 yawezekana alikuwa:
      a. mdogo sana wakati anapotajwa na aliishi maisha marefu zaidi sana. Hatajwi kama Kuhani Mkuu katika Nehemia;
      b. sio Yadua Yule Yule bali mjuu kwa majina yale yale (kama vile *the Expositor's Bible Commentary*, vol. 4 kur. 596-586);
      c. Josephus kimakosa amefupisha kipindi cha Kiajemi kwasababu majina ya watawala wa kiajemi yanarudiwa katika karne ya tano na ya nne K.K.:
         (1) Artashtaza
         (2) Dario
   2. uzao wa Zerubabeli katika 1 Nyak. 3:19-24 unaenda kwa:
      a. vizazi viwili (Young & Harrison)
      b. vizazi vinne

3. Hakuna maelezo ya kihistoria juu ya matukio makubwa ambayo yaliathiri Palestina katika karne ya nne K.K.:
    a. Uvamizi mkubwa wa Iskanda (333-332 K.K)
    b. uasi uliokanyagwa na Artashataza III (358-338 K.K)
4. Inawezekana kwamba hata Yadua yuko pamoja na Iskanda Mkuu kwamba orodha hii walikuwa walawi waliongezwa na mwandishi wa badaye (Young). Kunaweza kuwa na ushahidi wa mwandishi katika tungo "siku za Nehemia," Neh. 12:26,47.
5. Ezraa na Nehemia wanawasilishwa kama kuwa pamoja katika Yerusalemu;pasipo kutenganshwa na ufalme:
    a. usomaji wa sheria, Neh. 8:9;
    b. uwekaji wakfu wa kuta wa Yerusalemu, Neh. 12:26,36.

VI. VYANZO KUTHIBITISHA MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. Mafunjo ya Elephantine (408 K.K.) yanaorodhesha majina ya watukadhaa yanayotajwa katika Ezra/Nehemia:
1. Sanballat, mtawala wa Samaria, Neh. 2:10,19; 4:1;
2. Johanani, mjukuu wa Eliashibu Kuhani Mkuu, Nehemia 12:10-11, 22, 23;
3. Kutajwa kibayana kwa watu hawa kunathibitisha kwamba Ezra na Nehemia waliishi na kufanya kazi wakati wa utawala wa Artashasta I (464-424 K.K).

B. Mafunjo ya kisamaria yanatupatia sisi orodha ya watawala wa Samaria tokea kwa Sanbalati M-Horowitz kuelekea kwenye uharibifu wa mji wa Iskanda Mkuu mnamo mwaka 332 K.K. Yanaonesha pia kwamba matukio ya Nehemia 13:28 na matukio yanayofanana yanakumbukwa na Jesephus wakati wa kipindi cha Sanballati III sio sawasawa.

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI (muktadha)

A. Nehemia anazijenga upya kuta za Yerusalemu (kufanywa kwa mji kuwa mdogo zaidi), 1:1-7:73:
1. utangulizi katika nafsi ya kwanza, 1:1-2:20;
2. kuta ukijengwa kwa siku 52, 3:1-6:19;
3. kaka wa Nehemia, Hanani, anawekwa juu ya mji, 7:1-73.

B. Mageuzi ya kiroho ya Ezra (mwendelezo wa Ezra 7-10), 8:1-10:39:
1. Ezra anasoma sheria na watu wanaitikia, 8:1-9:4;
2. Pitio la matendo ya YHWH kwa niaba ya Wayahudi, 9:5-31;
3. Watu wanajifunga wenyewe kwa viapo kwa kuabudu YHWH na kusaidia Hekalu Lake, (kufanywa upya kiagano) 9:32-10:39.

C. Mageuzi ya kiutawala ya Nehemia, 11-13:
1. Kurudi kwa mara ya kwanza kwa Nehemia huko Yerusalemu, 11-12:
    a. kuanzishwa kwa watu wa Yerusalemu, 11:1-36;
    b. orodha ya makuhani na Walawi, 12:1-26, 44-47;
    c. kuwekwa wakfu kwa kuta za Yerusalemu, 12:27-43.
2. kurudi kwa mara ya pili kwa Nehemia huko Yerusalemu, 13:1-31
    a. uvunjwaji wa agano, 13:1-5
    b. mageuzi, 13:6-31:

(1) Tobia akiondolewa katika vyumba vya Hekalu, 13:4-5, 8-9;
(2) sadaka za Hekalu, 13:10-14;
(3) ndoa mchanganyiko, 13:1-3, 23-29;
(4) utoshelevu kwa ajili ya Hekalu, 13:30-31.

VIII. KWELI KUU

A. Kitabu hiki kinaendeleza historia ambayo ilianza katika Ezra. Vyote vinaandika kuanzishwa upya kwa jamii ya Agano katika Nchi ya Ahadi.
B. Kama Ezra alivyohusika na maisha ya jamii mpya kiagano na kiroho, Nehemia alikuwa anaguswa na:
    1. ukuta wa kiulinzi kuzunguka mji;
    2. kipengele cha kiutawala cha mji.

C. Wote Ezra na Nehemia wanahusika na uaminifu wa kiagano (kwa mujibu wa Musa). Dhambi za watu wa Mungu isipokuwa kwa ibada za sanamu zinaendelezwa na jamii ya baada ya uhamisho.

IX. MANENO na/au TUNGO NA WATU WA KUTAMBULIWA KWA MUHTASARI

A. Maneno na Tungo:
    1. mnyweshaji, 1:11 (NASB & NIV)
    2. Nisan, 2:1
    3. "ikiwa mbwamwitu akirukia juu yake angevunja ukuta wao wa jiwe chini," 4:3 (NIV, “ikiwa hata mbwamwitu akirukia juu yake, angevunja kuta wao wa mawe chini”)
    4. "binti zetu wanalazimishwa kwenda katika kifungo," 5:5 (NIV, “...tayari wamekwisha tumikishwa”)
    5. "nalikunguta mbele ya mavazi yangu," 5:13 (NIV, “...mapindo ya vazi langu”)
    6. nguzo ya wingu, 9:12 (NASB & NIV)
    7. mkate wa wonyesho, 10:33 (NIV, “mkate ulioandaliwa mezani”)
    8. mwendelezo..., 10:33 (NIV, “kawaida”)
    9. malimbuko ya kwanza, 10:35 (NIV, “malimbuko ya kwanza”)
    10. wakapiga kura kumtoa mmoja kati ya kumi kuishi Yerusalemu, 11:1 (NASB & NIV)
    11. "kitabu cha Musa," 13:1 (NASB & NIV)

B. watu wa kutambua kwa muhtasari:
    1. Hanani, 1:2
    2. Tobia muamoni, 2:10,19
    3. Sanballati the mu-heroni, 2:10,19
    4. Geshemu, muarabu, 2:19
    5. Asafu, 11:17
    6. Yeduthun, 11:17
    7. Artashtaza I, 13:6

X. MAENEO KI-RAMANI

1. Susa, 1:1
2. Ashdodi, 4:7
3. “Chephirimu, katika uwanda wa Ono,” 6:2 (NIV, “vijiji uwandani mwa Ono”)


XI. MASWALI YA KI-MAUDHUI YA MWANAFUNZI

1. Kwanini Nehemia ni mwenye huzuni?
2. Alionyeshaje huzuni yake?
3. Kwanini Nehemia alichukua wanajeshi wa Kiajemi (2:9) lakini Ezra alishindwa?
4. Nini lilikuwa jukumu la kimsingi la Nehemia?
5. Kwanini Wayahudi masikini walikuwa na hasira juu ya Wayahudi matajiri (sura ya 5)?
6. Ainisha sura ya 9 kwa mujibu wa matendo ya Mungu kwa jamii ya watu Wayahudi.
7. Orodhesha tabia za Mungu katika 9:17 na kwa muhtasari zielezee.
8. Kwanini hakukuwa na yeyote aliyetaka kuishi Yerusalemu (sura ya 11)?
9. Kwanini Nehemia alikuwa anatatizwa sana na ndoa mchanganyiko?




MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE

# PALESTINA



# UTANGULIZI WA ESTA

I. JINA LA KITABU

A. Kimepewa jina kutokana na Malkia wa Uajemi.

B. Jina lake katika kiebrania ni Hadasah ambalo linamaanisha thamani (2:7). Neno hili ni la kiishara kati ya Wayahudi juu ya furaha (Zek 1:8).

C. Jina lake katika kiajemi lilimaanisha "nyota."

II. URASIMISHAJI

A. Kitabu hiki kilipata tabu kujumuishwa katika kanoni ya Kiebrania:
   1. yawezekana kwasababu haitaji:
      a. jina lolote la Mungu;
      b. Hekalu;
      c. Sheria ya Musa;
      d. sadaka;
      e. Yerusalemu
      f. maombi (ingawa inamaanishwa).
   2. Magombo ya bahari ya chumvi yaliyopatikana mnamo mwaka 1947 yana nakala (katika yote au sehemu) ya kila kitabu cha Agano la Kale isipokuwa Esta
   3. Esta kama Ruthu hainukuliwi katika Agano Jipya
   4. kimepata mapitio mchanganyiko kutoka kwa wafasiri:
      a. Lijitabu la sheria za Kiyahudi za Yerusalemu (Megilla 7a) inasema kwamba sehemu ya "Manabii" ya kanoni ya kiebrania na sehemu ya "Maandiko" inaweza kufika mwisho lakini sio Torati na Esta. Wasingeweza kupotea kamwe (ikichukuliwa kutokea E. J. Young);
      b. Maimonides, mfasiri wa Kiyahudi wa Nyakati za Kati (1204 B.K) anasema kwamba ilikuwa inafuatia Sheria ya Musa kwa umuhimu;
      c. Martin Luther, mwanamageuzi wa ki-Protestanti, alisema inatakiwa kuondolewa kutoka katika Kanoni kwasababu ilikuwa imekaa kiyahudi sana (alizungumzia hili pia juu ya Yakobo na Ufunuo).
   5. kilikuwa ni kitabu kimojawapo kilichoshindaniwa kwenya mijadala huko Jamnia na Mafarisayo baada ya mwaka 70 B.K.
   6. mwandishi wa "Ecclesiasticus," pia alikiita "Hekima ya Ben Sira" aliandika mnamo mwaka 180 K.K., hakuwahi kuzungumzia  Esta hata kidogo.
   7. Inaonekana kujumuishwa katika kanoni ya Kiyahudi kuelezea asili ya karamu zisizo za Musa za Purimu (9:28-31). Katika 2 Makabayo 15:36 Purim inaitwa "Siku ya Mordekai."

B. Kitabu cha Esta ni orodha ya magombo matano iitwayo *Megilloth*. Vitabu hivi vitano vidogo: Ruthu, Muhubiri, Wimbo uliobora, Maombolezo na Esta, ni sehemu za sehemu ya "Maandiko" ya kanoni ya Kiebrania. Kila moja husomwa katika sherehe tofauti na nyingine. Esta husomwa wakati wa Purimu.

C. Andiko la Esta lina tofautiana sana kati ya MT na LXX. LXX ni refu zaidi na linajumuisha maombi ya Modekai na Esta.Haya yameongezwa kama msaada kwa ajili ya kitabu kukubaliwa katika kanoni ya Kiyahudi.

D. Mabaraza ya kanisa ya Hippo (393 B.K.) na Carthage (397 B.K.) kukiri sehemu ya Esta katika Biblia ya Mkristo.

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Ni simulizi ya kihistoria (katika 10:2 msomaji anatiwa moyo kusoma kwa ajili yake mwenyewe hadithi ya Modekai katika kumbukumbu za kimahakama za Kiajemi.)

B. Baadhi wangeweza sema hadithi za kihistoria (riwaya) kufunua kweli ya kiroho
   1. matumizi ya sitiari ya kinyume
   2. mpangilio wa matukio wenye umakini
   3. wahusika wakuu wasiojulikana katika historia

IV. UANDISHI

A. Kumekuwepo nadharia nyingi juu ya uandishi wa kitabu hiki kijulikanacho:
   1. Rabbi Azarias anasema kwamba Yoakini Kuhani Mkuu wakati wa utawala wa Dario I, mnamo miaka ya baadaye ya karne ya sita K.K., alikiandika;
   2. Lijitabu la sheria za Kiyahudi, Baba Bathra 15a, anasema kwamba watu wa Sinagogi aliandika wajibu wa Esta. Hii ilikuwa dhahiri kundi la viongozi katika Yerusalemu iliyoanzishwa na Ezra ambalo baadaye alikuja kuwa Baraza la Wazee wa Sinagogi. Ingawa neno "kuandika" linatumika kumaanisha: "iliyohaririwa," "kutungwa," au "kukusanywa";
   3. IbenEsra, Clement wa Iskandria na Josephus (Antiquities, 11:6:1) anasema kwamba Modekai alikiandika lakini Esta. 10:3 inaonekana kukinzana na hii (mpaka ilivyoongezwa na mhariri wa baadaye);
   4. Isidore na Augustine wanasema kwamba Ezra alikiandika.

B. Ni dhahiri kwamba hakuna ajuaye. Inaonekana hakika kwamba ilikuwa ni uhamisho wa Kiyahudi huko Uajemi uliokuwa ukijua mahakama ya Kiajemi.

C. Huyu mwandishi asiyejulikana alitumia vyanzo:
   1. Kumbukumbu za Mordekai, 9:20;
   2. nyaraka za kihistoria za Uajemi, 2:23; 3:14; 4:8; 6:1; 8:13; 10:2;
   3. yawezekana desturi za kinywa, hasa juu ya kile kilichotokea katika majimbo;
   4. kile ambacho "kitabu" hasa 9:32 kinarejerea hakijulikani bado.

V. TAREHE

A. Kitabu hiki kinamtaja Mfalme wa Kiajemi aitwaye Ahausiero, ambaye katika Kiajemi humaanisha "mtu mwenye nguvu." Wanazuoni wengi wanakubaliana kwamba mfalme huyu ni mfalme ajulikanaye katika historia kwa jina la Kiyunani la Ahausuero 1 (486-465 K.K)

B. Toleo la LXX na Josephus, hatahivyo "Artashtaza" ambaye ni jina la mrithi wa Ahausuero aitwaye Atashtaza I (465-424 K.K)

C. Esta, sura ya kwanza, inaweza kuaksi kipindi cha mpango wa Uajemi kuvamia Uyunani. Tunajua kutokea katika historia ya Heroditus, (2:8) kwamba Uajemi ilimvamia Uyunani na ilikataliwa mnamo mwaka 480 K.K. Anasema kwamba mfalme wa Uajemi alirudi nyumbani na kuchukua muda mwingi zaidi pamoja na haremu wake (9:108).

D. Kuhusu mtiririko wa Kibiblia hii ingeweza kuweka kitabu cha Ezra sura ya 6 na 7. Kuna ombwe la miaka katika simulizi za wakati huu 57. Mtu aitwaye Ezra hatambulishwa mpaka sura ya 7.

E. Esta 10:1-3 inamaanisha muda baada ya kifo cha Ahausuero. Alipigwa risasi mnamo mwaka 465 K.K.

F. Tarehe katika karne ya tano ya baadaye K.K. inaonekana kushawishi:
   1. muundo wa Kiebrania katika Ezra ni kama ule wa Mambo ya Nyakati, Ezra na Nehemia;
   2. juu ya uwepo wa maneno ya mkopo ya Kiajemi;
   3. maarifa ya mwandishi wa desturi za Kiajemi na maisha ya kimahakama. Mfano ungekuwa 1:6-8, 10.

VI. VYANZO VINAVYOTHIBITISHA MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. mbao za kimaandiko kutoka Nippur zilizoandikwa wakati wa utawala wa Atarshtaza I (465-424 K.K.) zinathibitisha uwepo idadi kubwa ya watu wa Kiyahudi huko Mesopotamia baada ya kurudi zikiruhusiwa na Koreshi II mnamo mwaka 538 K.K.

B. Historia ya Heroditus:
   1. Historia ya Heroditus juu Ahausuero I inaonekana kushabihiana na hadithi ya Esta:
      a. aliita baraza kupanga uvamizi wa Uyunani;
      b. baada ya kushindwa kwake alichukua muda mwingi pamoja na harem wake;
      c. inaeleza Ahausuero kama mtu asiyeeleweka dikteta na mwenye ari.
   2. Hii hatahivyo inafanya kazi katika njia mbili zote. Heroditus pia anataja majina na kumuelezea mke wa Ahausuero. Jina lake ni Amestris, na alitakiwa kutokea "familia ya watu saba." Mfalme wa Uajemi alikuwa na washauri wa karibu saba (1:14). Heroditus anataja kwamba Amestris aliongozana na Ahausuero I katika kampeni yake ya Kiyunani.

C. Mbao za ki-Elamu za Persepolis (wakati wa utawala wa Dario I na Ahausuero I) zinataja jina la Modekai kama mtu rasmi wa lango.

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI (muktadha)

A. Ainisho la Biblia ya NIV Study ni yenye msaada sana. Inatumia sherehe tatu katika Esta kama muundo kufuatia mtiririko wa hadithi:
   1. Karamu ya Mfalme, 1:1-2:18;
   2. Karamu ya Esta, 2:19-7:10;
   3. Karamu ya Purimu, 8-10.

B. Kwa ainisho zaidi:
   1. NIV Study Bible, ukur. 719
   2. *Expositor's Bible Commentary*, vol. 4, ukur. 796

VIII. KWELI KUU

A. Kidhahiri kitabu kinaelezea kitabu asili ya sherehe zisizo za Musa za kila mwisho wa mwaka wa Purimu (9:28-32). Sherehe zingine zizizo na asili ya Musa za kila mwisho wa mwaka ni Hanukkah. Kuna jedwali zuri ukur. 176 juu ya Biblia ya NIV Study.

B. Ilikuwa ni kutiwa moyo katika uaminifu kwa Mungu wakati wa nyakati za mateso (hasa wale ambaowalibakia uhamishoni).

C. Ni dhahiri inaonesha mkono wa Mungu uongozao katika historia, sio tu kwa Israeli lakini pia Uajemi. Kutokuwepo kwa jina lolote la Mungu na rejea yoyote kwa shughuli za Kiyahudi za kiroho (isipokuwa kufunga) ilikuwa ni fumbo la kifasihi kusisitiza ushawishi wa ajabu na uongozi wa Mungu kwa historia yote ya mwanadamu (4:14).

D. Baadhi wanaona hiki kitabu kama jaribio lingine la shetani kuharibu jamii ya watu wa Agano na hivyo Masihi!:
1. Anguko la Adamu;
2. Malaika kujichanganya na wanadamu (Mwanzo 6);
3. Ibrahimu na Isaka kutoa wake zao;
4. Uharibifu wa watu wa Kiyahudi katika Esta.

IX. MANENO NA/AU TUNGO NA WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHTASARI


A. Maneno na tungo:
1. "wasimamizi wa nyumba saba," 1:10 (NASB & NIV)
2. "maakida saba wa Uajemi na Umedi," 1:14 (NIV, "wenye mamlaka saba...")
3. "iandikwe katika sheria za Waajemi na Wamedi isitanguke," 1:19 (NASB & NIV)
4. masuria, 2:14 (NASB & NIV)
5. Mwagagi, 3:1, 10; 8:5 (NASB & NIV)
6. Puri, 3:7; 9:24 (NASB & NIV)
7. Pete yake mkononi, 3:10; 8:2 (NASB & NIV)
8. maakida, 3:12 (NASB & NIV)
9. "fimbo ya dhahabu," 4:11; 5:2 (NASB & NIV)
10. "mti wa mikono hamsini urefu wake," 5:14; 7:9-10 (NIV, "urefu wa mikono sabini na tano kwenda juu")
11. "siku hizo za Purimu," 9:28-32 (NASB & NIV)

B. Watu wa kutambua:
1. Ahausuero, 1:1 (NIV, "Ahausuero")
2. Vashti, 1:9
3. Mordekai, 2:5
4. Hamani, mu-Agagi, 3:1

X. MAENEO KATIKA RAMANI – hakuna ramani


XI. MASWALI YA KIMAUDHUI YA MWANAFUNZI

1. Kwanini washauri wa mfalme walikasirika sana juu ya Vashti kumkatalia mfalme (1:16-22)?
2. Kwanini Modekai hakumsujudia Hamani?
3. Kwanini Hamani alitaka kuwaharibu Wayahudi wote kwasababu ya Myahudi mmoja asiyetaka kumsujudia yeye?
4. Hamani anatoa sababu gani kwa mfalme kwa kuharibu Wayahudi (sura. 3)?
5. Orodhesha tabia za ibada za huzuni za Wayahudi zinazo orodheshwa katika 4:1-3.
6. Fundisho la kithiolojia la utoshelevu linahusiana kwa namna gani na 4:14?
7. Ni kwa namna gani 8:17 yawezekana kushabihiana na kusudi la kitabu?




MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE

# PALESTINA




VIPIMO KATIKA MAILI

# UTANGULIZI WA FASIHI YA HEKIMA

I. AINA YA UWASILISHAJI

A. Ni aina ya Fasihi ya Kawaida katika Mashariki ya Karibu ya Kale

1. Mesopotamia (I Fal. 4:30; Isa. 47:10; Dan. 2:2)
    a. Sumeria iliendeleza desturi za hekima sehemu zote kimithali na kiutendaji (NIPPUR).
    b. Hekima ya kimithali ya Babebi ilihusianishwa na kuhani/ushirikina. Hii haukutazamiwa kimaadili. Hii haikuboresha aina kama ilivyokuwa katika Israeli.
    c. Pia Ashuru ilikuwana desturi za hekima, mafundisho ya Ahiqari. Huyu alikuwa mshauri wa Senakaribu (704-681 K.K.).
2. Misri (I Fal. 4:30)
    a. "Mafundisho ya Vizier Ptah-hotep" yaliyoandikwa mnamo 2450 K.K. Mafundisho yake yalikuwa katika aya si katika muundo wa kimithali. Haya yaliumbwa kama baba kwa mwana, hivyo hivyo "Mafundisho kwa Mfalme Meri-ka-re," yapata mwaka 2200 K.K.
    b. Hekima ya Amen-em-opet, iliyoandikwa yapata mwaka 1200 K.K., inafanana sana na Mit. 22:17-24:22.
3. Foenike
    a. Gunduzi zilizofanyika huko Ugariti zimeonyesha uhusiano wa karibu kati ya Wafoenike na hekima ya Kiebrania, hasa mizani. Miundo mingi isiyo ya kawaida na maneno adimu katika Fasihi ya hekima ya Kibiblia sasa inaeleweka kutokana na gunduzi za utafiti wa mambo ya kale huko Ras Shamra (Ugariti).
    b. Kitabu cha Wimbo Ulio Bora kinafanana sana na nyimbo za arusi za ki-Foniki ziitwazo *wasps* zilizoandikwa yapata mwaka 600 K.K.
4. Kanaani (Yer. 49:7; Obadia. 8) - Albright ameufunua ufanano kati ya hekima ya fasihi ya Waebrania na Wakanaani hasa maandiko ya Ras Shamra toka Ugarit, iliyoandikwa mnano karne ya 15 K.K.
    a. mara nyingi maneno yenye kufanana hujitokeza kama jozi
    b. kuwepo kwa mkingo
    c. yana maandiko yaliyopanda juu ya mengine
    d. yana mwandiko wa kimziki
5. Fasihi ya Hekima ya Kibiblia inabeba maandiko ya watu kadhaa wasio Waisraeli:
    a. Ayubu toka Edomu
    b. Agur toka Masa (ufalme wa ki-Israeli ulio katika Saudi Arabia (kama vile Mwanzo 25:14 na I Mambo ya Nyakati 1:30)
    c. Lemueli toka Masa

B. Sifa pambanuzi za Kifasihi

1. Tofauti za Awali za aina mbili
    a. kimithali (masimulizi ya kiuhalisia)
        (1) fupi
        (2) ni rahisi kueleweka kitamaduni (tendo la kawaida)
        (3) ni mawazo ya kukemea – semi za ukweli zenye kuzuia
        (4) mara nyingi hutumia tofauti
        (5) kwa ujumla ni za kweli lakini si za mara kwa mara hasa katika kutumika

b. mada maalumu yenye kukuzwa kwa muda mrefu, kazi za kifasihi (hasa zenye kuandikwa) kama Ayubu, Mhubiri na Yona..
   (1) mazungumzo ya mtu mmoja
   (2) majibizano ya watu wawili
   (3) insha
   (4) yanashughulika na maswali na siri kuu za maisha
   (5) washauri walikuwa huru kuitia changamoto theolojia kama ilivyo
c. unafsishwaji wa shairi wa hekima (mara nyingi ni jinsi ya kike). Hili neno hekima lilikuwa la jinsi ya kike.
   (1) mara nyingi katika kitabu cha Mithali hekima inaelezwa kama mwanamke
      (a) kwa uyakini:
         1) 1:20-33
         2) 8:1-36
         3) 9:1-6
      (b) kwa ukanushi:
         1) 7:6-27
         2) 9:13-18
   (2) Katika Mithali 8:22-31 hekima inabainishwa kama mzaliwa wa kwanza wa uumbaji ambapo Mungu aliviumba vyote (3:19-20). Hii inaonekana kuwa usuli wa matumizi ya Yohana ya neno "kujifunza" katika Yohana 1:1 kumrejelea Yesu Masihi.
   (3) pia hili linaweza kuonekana katika Ecclesiasticus 24.

2. Fasihi hii ni ya kipekee toka Sheria na Manabii katika hilo inaonyesha mtu binafsi si taifa. Hapa hakuna madokezo ya kimadhehebu au ya kihistoria. Awali ilijikita katika maisha ya kila siku, mafanikio, furaha, maisha ya maadili.
3. Fasihi ya hekima ya Kibiblia inafanana na ile ya watu wake walioizunguka katika muundo wake lakini si katika yaliyomo. Mungu Mmoja wa Kweli ndiye msingi ambao kwao hekima zote za kibiblia zinajikita (kama vile Ayubu 12:13; 28:28; Mit. 1:7; 9:10; Zab.111:10). (Katika Babeli hii ilikuwa Apsu, Ea au Marduk. Katika Misri hii ilikuwa Thoth.)
4. Hekima ya kibiblia ilikuwa ya kiutendaji sana. Hii ilijikita katika utendaji, si katika ufunuo mahususi. Hii inajikita katika mtu kuwa na mafanikio katika maisha (maisha yote: takatifu na na ya kiulimwengu). Ni ya ki-Uungu "maana ya farasi."
5. Kwa sababu hekima ya fasihi ilitumika kama fikra, uzoefu na ucunguzi wa mwanadamu ilikuwa ni ya kimataifa, tamaduni zenye kubadilika. Huu ulikwa mtazamo wa kidini wa kiulimwengu kuhusiana na Mungu mmoja ambapo mara nyingi hautajwi, kwamba ndiyo uliyoufanya ufunuo wa hekima ya Israeli.

## II. ASILI INAYOWEZEKANA KUWA VYANZO

A. Katika Israeli Hekima ya Fasihi iliendelezwa kama mwanya au usawa kwa miundo mingine ya ufunuo. (Yer. 18:18; Eze. 7:26)
   1. kuhani – sheria - muundo (ushirika)
   2. nabii - maono - shauku (ushirika)
   3. busara - hekima - vitendo, mafanikio ya maisha ya kila siku (mtu binafsi)
   4. Kama ilivyokuwa katika Israeli kuwa kulikuwa na manabii wachache, ndivyo ilivyo, kulikuwa na wanawake wenye busara (kama vile II Sam. 14:1-21; 20:14-22).

B. Aina hii ya fasihi ilionekana kukuzwa:

1. kama ngano au masimulizi ya jadi kwa kuuzunguka moto
2. kama desaturi za kifamilia zilizopitwa na wakati kwa wanaume na watoto
3. iliyoandikwa na kuungwa mkono na Kasri la Kifalme:
    a. Daudi anahusianishwa na Zaburi
    b. Suleimani anahusianishwa na Mithali (I Fal:29-34; Zab. 72 na 127)
    c. Hezekia anahusianishwa na fasihi ya kuihakiki hekima.

III. KUSUDI

A. Kimsingi ni "namna ya" kutumia katika furaha na mafanikio. Kimsingi ni yenyewe binafsi katika mtazamo wake. Hii inajikita katika:
    1. uzoefu wa vizazi vilivyopita,
    2. sababisho na matokeo ya mahusiano katika maisha.

B. Hii ilikuwa namna ya jamii kuiruhusu kweli na kukifundisha kizazi kifuatacho cha viongozi na wenyeji.

C. Hekima ya Agano la Kale, japo mara nyingi haielezi juu ya hili, inamuona Mungu wa Agano nyuma ya maisha yote.

D. Hii ilikuwa changamoto na usawa wa thiolojia ya jadi. Hawa wenye busara walikuwa wanafikiria huru hawakuwa na mipaka ya kweli za kiuandishi. Hawa walithubutu kuuliza, "Kwa nini," "Namna gani," "Nini kama?"

IV. MISINGI YA UFASIRI

A. Semi fupi za kimithali
    1. hutazama mambo ya kawaida ya kimaisha yanayotumika kueleza kweli.
    2. hueleza kweli kuu katika usemi wa kawaida wa kuarifu.
    3. kwa kuwa muktadha hautasaidia kuvitazama vifungu vyenye kufanana katika jambo lile lile.

B. urefu wa vipande vya kifasihi
    1. huakikisha vinaeleza kweli kuu ya fasihi nzima.
    2. havipeleki mistari nje ya muktadha.
    3. hukagua tukio la kihistoria au sababu ya uandishi.

C. Baadhi ya fasiri za kawaida zisizo za kweli (Fee & Stuart, *How to Read the Bible for All It Is Worth*, uk. 207)
    1. Watu hawakisomi kitabu chote cha Hekima (kama Ayubu na Muhubiri.) na kuyatazama kama kweli kuu lakini huzisukuma sehemu za kitabu za muktadha na kukituma kifasihi kwa maisha ya sasa.
    2. Watu hawauielewi upekee wa aina ya fasihi. Hii ni ya fasihi ya Mashariki ya Kale ya Karibu ya kimapatano sana na ya kiishara.
    3. Kitabu cha Mithali ni semi za kweli ya jumla. Hizi ni visafisha ubao si kweli maalumu, katika kila jambo, kila wakati, semi za kweli.

V. MIFANO YA KIBIBLIA

A. Agano la Kale
    1. Ayubu

2. Zaburi 1, 19, 32, 34, 37, 49, 73, 104, 107, 110, 112, 127-128, 133, 147, 148
3. Mithali
4. Muhubiri
5. Wimbo Ulio Bora
6. Maombolezo
7. Yona

B. Urasimishaji Zaidi
   1. Tobiti
   2. Hekima ya Ben Sira (Ecclesiasticus/Mhubiri)
   3. Hekima ya Suleimani (Kitabu cha Hekima)
   4. Makabayo IV

C. Agano Jipya
   1. Mithali na mafumbo ya Yesu
   2. Kitabu cha Yakobo

# UTANGULIZI WA USHAIRI WA KIEBRANIA

I. UTANGULIZI

A. Aina hii ya fasihi inatengeneza 1/3 ya Kitabu cha Agano la Kale. Sana sana hii ni kawaida katika vipengele vya sheria za Kiebrania vya "Manabii" na "Maandiko".

B. Ni tofauti sana na ushairi wa Kiingereza. Ushairi wa Kiingereza unakuzwa kutokana na ushairi wa Kiyunani na Kilatini. Ushairi wa Kiebrania unahusiana sana na ushairi wa Ki-kanaani. Kuna mistari yenye kuwekewa mkazo, mizani au vina katika ushairi wa Mashariki ya Karibu ya Kale.

C. Ugunduzi wa utafiti wa mambo ya kale kaskazini mwa Israeli huko Ugariti (Ras Shamra) umewasaidia wanazuoni kuuelewa ushairi wa Agano la Kale. Ushairi huu wa karne ya 15 K.K. una uhusiano wa mara kwa mara pamoja na ushairi wa kibiblia.

II. SIFA PAMBANUZI ZA USHAIRI KWA UJUMLA

A. Ni mfupi sana.

B. Hujaribu kuzunguza ukweli, hisia au uzoefu katika hali ya kutumia taswira.

C. Hapo awali hauandikwi katika masimulizi. Umeundwa katika namna ya juu sana. Muundo huu unaelezwa katika:

1. mistari yenye ulinganifu (ufanano)
2. katika mbinu za maneno

III. MUUNDO

A. Askofu Robert Lowth katika kitabu chake, *Lectures on the Sacred Poetry of the Hebrews* (1753) alikuwa wa kwanza kutoa sifa pambanuzi za ushairi wa kibiblia kama mistari yenye ulinganifu wa mawazo. Tafsiri nyingi za Kiingereza zinapangwa ili kuonyesha mistari ya ushairi.

1. Maneno yenye kufanana – mstari inaeleza wazo lile lile katika maneno tofauti tofauti:
   a. Zaburi 3:1; 49:1; 83:14; 103:3
   b. Mithali 20:1
   c. Isaya 1:3
   d. Amosi 5:24
2. kinyume–mistari hii inaeleza ukinzani wa mawazo kwa maana ya kutofautisha au kwa kuanza na uyakinifu na ukanushi:
   a. Zaburi 1:6; 90:6
   b. Mithali 1:6,29; 10:1,12; 15:1; 19:4
3. uambatani – mistari miwili au mitatu inakuza wazo - Zab. 1:1-2; 19:7-9; 29:1-2

B. A Briggs katika kitabu chake cha, *General Introduction to the Study of Holy Scripture* (1899) inaendeleza hatua inayofuatia ya uchambuzi wa ushairi wa Kiebrania:

1. ishara – kifungu kimoja kilicho sahihi na cha pili kilicho cha kistiari, Zab. 42:1; 103:3.
2. mwinuko au kilichokaa kama daraja – kifungu hiki kinafungua ukweli katika mtindo wa kufuata mwinuko, Zab. 19:7-14; 29:1-2;103:20-22.
3. uliyokingana ama kupishana–mfuatano wa vishazi, mara nyingi huwa ni vinne vinavyohusiana na muundo wa ndani wa mstari wa 1 hadi 4 na 2 hadi 3 - Zab. 30:8-10a

C. G.B. Gray katika kitabu chake, *The Forms of Hebrew Poetry* (1915) baadaye inaikuza dhana ya vishazi vyenye ulinganifu kwa:
   1. ulinganifu kamili–ambapo kila neno lililo katika mstari wa kwanza linarudiwa au kuwekewa ulinganifu kwa neno lililo katika mstari wa pili - Zaburi 83:14 na Isaya 1:3
   2. ulinganifu ambapo vishazi havina urefu unaofanana - Zab. 59:16; 75:6

D. utaratibu wa aina za sauti
   1. uchezaji katika alfabeti (chemshabongo)
   2. uchezaji katika konsonanti (takriri)
   3. uchezajj katika irabu (mshabaha wa irabu)
   4. uchezaji katika kurudiarudia maneno (mchezo wa maneno)
   5. uchezaji katika sauti za maneno yenye kufanana (tanakali-sauti)
   6. ufunguzi na uhitimishaji mahususi (ujumuishwaji)

E. Kuna aina kadhaa za ushairi katika Agano la Kale. Nyingine ni mada zenye kuhusiana na nyingine zinazounda uhusiano:
   1. wimbo wa kutunukia - Hes. 21:17-18
   2. nyimbo zenye kutenda kazi - (zilizodokezwa lakini hazikuchukuliwa kumbukumbu katika Amu. 9:27); Is. 16:10; Yer. 25:30; 48:3
   3. tumbuizo - Hes. 21:27-30; Is. 23:16
   4. nyimbo za mvinyo - kanushi, Isa. 5:11-13; Amosi 6:4-7 na yakini, Is. 22:13
   5. mashairi ya mapenzi –Wimbo Ulio Bora, arusi yenye kutatanisha - Amu. 14:10-18, nyimbo za arusi - Zab. 45
   6. maombolezo/wimbo wa maziko - (uliodokezwa lakini haukunukuliwa katika II Sam. 1:17 na II Nya. 35:25)II Sam. 3:33; Zab. 27, 28; Yer. 9:17-22; Omb.; Eze. 19:1-14; 26:17-18; Nah. 3:15-19
   7. nyimbo za vita -Mwa. 4:23-24; Kut. 15:1-18; Hes. 16:35-36; Yosh. 10:13; Amu. 5:1-31; 11:34; I Sam. 18:6; II Sam. 1:18; Isa. 47:1-15; 37:21
   8. dua baraka maalumu au za kiongozi - Mwa. 49; Hes. 6:24-26; Kumb. 32; II Sam. 23:1-7
   9. maandiko yenye kuzungumzia ushirikina - Balaamu, Hes. 24:3-9
   10. ushairi mtakatifu – Zaburi
   11. mashairi ya chemsha bongo - Zab. 9,34,37,119; Mit. 31:10 na kuendelea na Maombolezo 1-4
   12. laana - Hes. 21:22-30
   13. mashairi ya dhihaka - Is. 14:1-22; 47:1-15; Eze. 28:1-23

## IV. MWONGOZO WA KUFASIRI USHAIRI WA KIEBRANIA

A. Angalia kitovu cha ukweli wa ubeti au sehemu ya wimbo (hii ni kama aya iliyo katika nathari au lugha ya mjazo.) Toleo la RSV ilikuwa tafsiri ya kwanza ya sasa ili kuutambua ushairi kupitia beti. Zilinganishe tafsiri za sasa kwa ajili ya msaada wa tambuzi.

B. Itambue lugha ya kiishara na kuieleza katika nathari. Kumbuka aina hii ya fasihi ni ya kimaafikiano sana, mengi yanabakizwa kwa ajili ya msomaji kuyajaza.

C. Hakikisha unayahusianisha mashairi yaliyojikita katika jambo la muda mrefu katika muktadha wake wa kifasihi na mpangilio wa kihistoria.
D. Waamuzi 4 na 5 zinasaidia sana katika kuona namna ushairi unavyoieleza historia. Waamuzi 4 ni nathari ama lugha ya mjazo na Waamuzi 5 ni ushairi wa tukio lile lile.
E. Jaribu kuitambua aina ya ufanano uliomo, kwa vyo vyote visawe, ukinyume, au uambatani. Hili ni la muhimu sana.

# UTANGULIZI WA AYUBU

I. JINA LA KITABU

A. Kitabu kimepewa jina la mhusika mkuu. Ayubu ni jina lililozoeleka. Maana yake imekuwa ikitafsiriwa kama:

1. "Baba yu wapi"
2. "adui"
3. "yeye atubuye"

B. Hiki ni kitabu chenye maana, chenye nguvu na cha ubunifu:

1. Luther anasema ni "cha ajabu na hali ya juu sana sio kama kitabu kingine cha Maandiko matakatifu."
2. Tennyson anasema ni "Ushairi mkuu wa kale kama wa kisasa."
3. Carlyle anasema, "Hakuna kilichoandikwa katika Biblia au nje yake chenye thamani sawa nacho."

II. URASIMISHAJI

A. Kipo katika sehemu ya Maandishi ya sheria ya Kiebrania.

B. Kimejitokeza kwenye baadhi ya MSS ya kiebrania baada ya kitabu cha Kumbukumbu la Torati kwa sababu wote Ibrahimu na Ayubu wanafaa katika kipindi cha kihistoria kile kile.

C. Matukio ya kujirudia ya Ayubu kati ya vitabu vya kishairi vya Biblia yameanzishwa na toleo la Kilatini na kuimarishwa na baraza la Trenti.

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Ayubu ni aina ya sehemu ya fasihi iliyozoeleka sana katika Mashariki ya kale ya karibu inayoitwa "Fasihi ya hekima."

B. Kwa sababu kitabu ni shairi la awali na utambulisho usio wa kishairi (1-2) na kufunga (42), kuna mjadala mwingi kati ya wanazuoni juu ya aina yake:

1. masimulizi ya kihistoria
2. uwasilishwaji wa kifilosofia ya kuigiza/dhamira ya kitheolojia
3. mfano

C. Ayubu ana baadhi ya fasihi mfanano (lakini sio kitheolojia) kwa:

1. maandiko ya Sumeria yaitwayo "Sumeria ya Ayubu" yapata kutoka mwaka 2000 K.K.
   a. mtu wa awali kudhihaki
   b. juu ya mateso asiyostahili
   c. kuachwa na Mungu
   d. maombi ya kusikilizwa barazani
   e. kuifunua dhambi
2. maandiko ya Babeli yaitwayo "nitamsifu Bwana wa hekima." Wakati mwingine huitwa "Babeli ya Ayubu" yapata kutoka mwaka 1300-1100 K.K.
   a. mazungumzo ya mtu mmoja ya nafsi ya kwanza
   b. aliyetengwa na miungu na kuachwa na marafiki
   c. urejesho wa mwisho wa afya na utajiri

3. maandiko ya Babeli yaitwayo "Dialogue About Human Misery (mazungumzo juu ya huzuni ya mwanadamu)."wakati mwingine huitwa "Babeli ya Uthiolojia" yapata mwaka 1000 K.K.
    a. kufikiria amri za Mungu juu ya mateso
    b. kati ya mtesekaji na rafiki
    c. rafiki anae linda mitazamo ya kidesturi na mtesekaji kuyalenga kwa wazi matatizo, kama kuimarika kwa uovu
    d. matokeo ya matatizo yote kutoka kushindwa kwa mwanadamu katika lengo moja
4. maandiko ya Misri yaitwayo "Protests of the eloquent Peasant (malalamiko ya ushawishi wa mkulima)."
5. maandiko ya Misri yaitwayo "Dispute with His Soul of One Who is tired of Life (kupingana na nafsi yake yeye aliyechoka kuishi." Pia huitwa "kupingana juu ya kujiua."

D. Kitabu kina aina ya mifano kadhaa. Haifai katika kundi lolote lile.
1. mazungumzo binafsi/mazungumzo ya nafsi
2. mazungumzo ya pande mbili
    a. marafiki
    b. YHWH
3. Riwaya ya wazi na iliyofunga

IV. UANDISHI

A. Kitabu hakijulikani.

B. Baba Bathra 14b anadai kwamba Musa ndiye aliyeandika kitabu. Baadhi ya machapisho ya kiebrania na tafsiri za Kishamu, Peshita, ziliwekwa baada ya Kumbukumbu la Torati.

C. Inawezekana kwamba Mwanafilosofia wa kiyahudi alichukua maisha ya kihistoria ya Ayubu na kuyabadili ili kufundisha Kifilosofia, ukweli wa kitheolojia.

D. Baadhi ya wanazuoni wanadai kwamba shairi, Sura ya 3-41, liliandikwa na mwandishi wa kale ambapo utangulizi usio wa kishairi (1-2) na hitimisho la shairi (42) liliongezwa na mhariri wa mwisho. Hata hivyo, inahitajika kumbukumbu kwamba sisi tuko katika nyakati zetu za kisasa, tamaduni za kimagharibi hazitambui kikamilifu mpangilio wa maandiko na mbinu za mashariki ya kale ya karibu. Kanuni za maadili mema ya Hammurabi yanafungua na kufunga katika shairi na isiyo ya shairi katikati.

E. Mtu aitwaye Ayubu
1. Ayubu ni mtu wa awali wa kihistoria kwa sababu:
    a. anatajwa katika Ezekieli 14:14 , 20 na Yakobo 5:1
    b. jina lake, ingawa hakuwa mtu Yule yule, aliyejitokeza katika maadiko ya ya mkono arna; maandiko ya laana ya Misri; maandiko ya Mari, na maandiko ya Ugaritiki
    c. kipengele cha fedha kinapatikana katika 42:11, *kesitah*, kimetokea pekee zaidi katika Mwa. 33:19 na Yoshua.24:32
2. Ayubu ni dhahili hakuwa myahudi
    a. kutumia majina ya Mungu kiujumla Ayubu na rafiki zake katika mazungumzo yao
        1. *Elohim* (Mungu) sura 1-2 na 20, 28, 32, 34, 38
        2. *El* (Mungu) mara nyingi
        3. *Shaddai* (Mwenyezi) mara nyingi
    b. alionekana kuwa mtu wa hekima kutoka Edomu
        1. Uzi (Mwa. 36:28; Yer. 25:20; Omb. 4:21)
        2. Temani (Mwa. 36:11)

3. linganisha na "mtu wa mashariki" (Ayubu 1:3; Amu. 6:3,33; Isaya. 11:14; Eze. 25:4,10)

V. TAREHE

A. Mpangilio wa kihistoria wa kitabu unafaa kipindi cha mababa wa imani cha millennia ya pili K.K. Baadhi ya mifano inaweza kuwa:
   1. Ayubu alitenda kama kuhani kwa ajili ya familia yake (1:5)
   2. maisha marefu ya Ayubu – miaka 140 na zaidi (42:16)
   3. maisha ya kuhamahama –aina ya mifugo wa wanyama wa kufugwa.
   4. alilaumu vikosi vya Waseba na Wakaldayo (1:15,17)
   5. Ayubu aliishi katika sehemu ya mji kwa mwaka na sehemu ya makundi ya wanyama kwa mwaka.

B. Aina hii inakipa kitabu tarehe ya kipindi cha kuanzishwa kwa fasihi ya hekima. Hii inaweza kuwa kuanzia wakati wa Daudi kupitia Wafalme wa Yuda, hasa Hezekia.

C. R.K. Harrison anaamini tarehe ya kuandikwa kitabu sio baadae mwisho wa karne ya tano K.K. ushahidi unafaa zaidi.

VI. MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. Eneo la Uzi linatia mashaka. Kuna nadharia kuu mbili:
   1. Ni katika nchi ya Edomu
      a. ulifahamika kwa watu wake wenye hekima, Yer. 49:7
      b. mmojawapo wa marafiki watatu alitoka Temani, mji wa Edomu. Ulipewa jina baada ya uzao wa Esau, Mwa. 36:15.
      c. Uzi anatajwa kama uzao wa Seiri mhori, kama vile Mwa. 36:20-30. Watu hawa walikuwa na uhusiano na sehemu ya Edomu.
      d. Uzi anafanana na Edomu katika Omb. 4:21.
   2. Katika eneo la Aramu
      a. Mtindo wa Fasihi ya Kiaramu na maneno yaliyoenea katika Ayubu
      b. uwepo wa waporaji wa Kikaldayo 1:17.
      c. Mwa. 10:23 inaungamanishwa na Uzi na Aramu, kama vile Mwa. 22:20-22.
   3. inawezekana kwamba jina Uzi lilijumuishwa katika makabila kadhaa mashariki mwa Palestina kutoka kaskazini mwa Aramu hadi kusini mwa Edomu.

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI

A. Utangulizi wa Kinathari (baraza la mbinguni ), 1-2

B. Marafiki wa Ayubu, 3-37
   1. Maombolezo ya Ayubu, 3
   2. Kipindi cha mahojiano matatu, 4-31
      a. Mzunguko wa awali, 4-14
         (1) Elifazi, 4-5 (4) Ayubu, 9-10
         (2) Ayubu, 6-7 (5) Sofari, 11
         (3) Bildadi, 8 (6) Ayubu, 12-14
      b. Mzunguko wa pili, 15-21
         (1) Elifazi, 15 (5) Sofari, 20

(2) Ayubu, 16-17 (6) Ayubu, 21
(3) Bildadi, 18
(4) Ayubu, 19

c. Mzunguko wa tatu, 22-31
(1) Elifazi, 22
(2) Ayubu, 23-24
(3) Bildadi, 25
(4) Ayubu, 26
(5) hitimisho la Ayubu, 27
(6) maoni ya mwandishi (sifa ya siri ya hekima), 28
(7) mazungumzo binafsi ya Ayubu, 29-31

3. Maoni ya Elihu, 32-37
a. lugha isiyo ya shairi, 32:1-5
b. shairi, 32:6-37:24

C. Mungu anamjibu Ayubu, 38:1-42:6
1. Mungu anajibu kama muumbaji, 38-39
2. Mungu anajibu kama Hakimu, 40:1-2,6-41:34
3. Ayubu anatubu, 40:3-5 na 42:1-6

D. Hitimisho la lugha isiyo ya kishairi, 42:7-17

VIII. KWELI KUU

A. Kitabu hiki kimeandikwa kuweka uwiano wa theolojia ya maagano ya kitamaduni (Kumb. 27-29) ya kwamba mwenye haki atabarikiwa katika maisha haya na waovu kuadhibiwa katika maisha haya. Theolojia hii ya utamaduni wa Kiyahudi inawasilishwa kwa maongezi ya marafiki watatu wa Ayubu. Pia inatia shauku muhtasari wa majibizano maalumu ya utamaduni unaoletwa kutoka kwa kijana mdogo kama Elihu ambae kwa uwazi anakanusha na kuwasahihisha wote Ayubu na marafiki zake watatu wa kale.

B. Kitabu hiki kinadai kwamba Mungu ni mwenye haki na mwishowe atapangilia vitu sawa sawa, mojawapo ni katika maisha haya (urejesho wa Ayubu, 42:10-17) au wakati ujao (14:7-17; 19:23-27.)

C. Mateso yote sio matokeo ya dhambi binafsi. Hiki ndicho marafiki hawa watatu walichodai (kama vile. 4:7-11; 8:3- 7; 11:13-15; 15:12-16; 22:21-30). Hii sio haki, dunia iliyoanguka. Wakati mwingine waovu hufanikiwa (Zab. 73). Mara nyingi mwenye haki huteseka. Shetani alimshutumu Ayubu kwa kupendelewa kiimani.

D. Kitabu hiki kinatupatia utambuzi wetu katika ufalme wa kiroho. Kuna mshitaki, adui wa mwanadamu aliyechaguliwa. Shetani ni mtumishi wa Mungu, malaika mshitaki katika Agano la kale (kama vile. A.B. Davidson, *An Old Testament Theology*, lililochapishwa na T & T Clark kr. 300-306.) ni vigumu kupangilia kwa nini neno shetani limewekwa wazi katika makala. Yumkini likamaanisha kusudi zaidi ya jina. Mawakala kadhaa tofauti wanaelezewa kama “adui”.

1. Mwanadamu

a. I Sam. 29:4
b. II Sam. 19:22
c. I Fal. 5:4
d. I Fal. 11:14-22, 23-25
e. Zab. 71:13
f. Zab. 109:6, 20, 29

2. Kimalaika
   a. malaika wa Bwana - Hes. 22:21
   b. Shetani - Ayubu 1-2, I Nya. 21:13; Zek. 3:1-2

E. Mungu kamwe hakumfunulia Ayubu sababu iliyokuwa nyuma ya mateso yake. Maisha ni siri. Kumwamini Mungu ni muhimu zaidi kuliko taarifa!

IX. MANENO NA/AU VIFUNGU NA WATU WA KUWATAMBUA KIMUHTASARI (NASB)

A. Maneno na /au Tungo
   1. Asiye na hatia, 1:1; 2:3 (toleo la NASB na NIV)
   2. wana wa Mungu, 1:6; 2:1 (toleo la NIV, "malaika")
   3. kigae, 2:8 (toleo la NIV, "kipande cha chungu kilichovunjika")
   4. Kuzimu, 7:9; 11:8 (toleo la NIV, "kaburi")
   5. mafujo, 8:11 (toleo la NASB na NIV)
   6. Rahabu, 9:13; 26:12-13 (toleo la NASB na NIV)
   7. Abadoni, 26:6; 28:22; 31:12 (toleo la NIV, "uharibifu")
   8. ukombozi, 33:24; 36:18 (toleo la NASB na NIV)
   9. lewiathani, 3:8; 41:1 (toleo la NASB na NIV)
   10. kiboko, 40:15 (toleo la NASB na NIV)
   11. Utheolojia

B. Watu
   1. "watu wa upande wa mashariki," toleo la NASB, (NIV, "watu wote wa mashariki")1:3
   2. Shetani, 1:6
   3. Waseba, 1:15
   4. Wakaldayo, 1:17
   5. Mwenyezi (*Shaddai*), 6:4,14; 13:3; 22:3,26
   6. Elihu, 32:2

X. MAENEO YA KI-RAMANI

1. Uzi, 1:1
2. Temani, 4:1
3. Edomu

XI. MASWALI YA KI-MAUDHUI KWA MWANAFUNZI


1. Ilimaanisha nini kumhofu Mungu? 1:1,9; 28:28
2. Je, Ayubu hakuwa na dhambi (mwelekevu)? 1:1,8,22
3. “Watu wa mashariki" ni watu gani? 1:1

4. Je! ni tendo gani ambalo Ayubu alitenda kama kuhani kwa ajili ya familia yake lilioandikwa katika kitabu? 1:5
5. Shetani alikuwa anajihusisha na nini mbinguni mbele za Mungu? 1:6-12
6. Ni kwa njia gani shetani alimshutumu Ayubu mbele za Mungu? 1:6-12; 2:1-6
7. Je! 14:7-17 na 19:23-29 inafundisha ufufuo wa kimwili, kwa nini au kwa nini isiwe hivyo?
8. Je! Mungu alimjibu majibu Ayubu?
9. Je! Ayubu alikiri kuwa mtenda dhambi? 40:3-5; 42:1-6
10. Ni nini ambacho Mungu aliwaambia watende marafiki watatu wa Ayubu? (42)
11. Ni kwa namna gani Ayubu anaeleza haki yake ilivyoiathiri tabia ya Mungu? 40:8




**MASHARIKI YA KARIBU YA KALE**

# PALESTINA



# UTANGULIZI WA ZABURI

I. JINA LA KITABU

A. Katika kiebrania jina ni "Nyimbo za sifa" au "sifa" (*Tehillim*). Hii inashangaza kwa sababu Zaburi nyingi ni maombolezo au kilio.

B. Katika toleo la LXX jina ni "*psalmos*" ambalo humaanisha "kung'ang'ania." Neno hili la kiyunani limetumia Zaburi katika Luka 20:42; 24:44 na Mdo. 1:20. Sio Zaburi zote zilimaanisha kuimbwa na kiambata cha muziki, bali hili limekuwa jina la kitabu chote katika toleo la LXX.

II. URASIMISHAJI

A. Zaburi ni sehemu ya tatu ya mgawanyo wa sheria za kiebrania ziitwazo "maandiko." Sehemu hii sheria za kiebrania zinaundwa na:
   1. fasihi za hekima
      a. Ayubu
      b. Zaburi
      c. Mithali
   2. vitabu vya karamu (*Megilloth*)
      a. Ruthu
      b. Mhubiri
      c. Wimbo Ulio Bora
      d. Maombolezo
      e. Esta
   3. vitabu vya kihistoria
      a. Danieli
      b. Ezra
      c. Nehemia
      d. Mambo ya Nyakati

B. Zaburi kama mkusanyiko zinapatikana katika toleo la LXX na Magombo ya Bahari ya Chumvi.

C. Kitabu cha Zaburi kimedokezwa mara nyingi katika Agano Jipya zaidi kuliko kingine cha Agano la Kale.

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Muundo huu wa kifasihi umezoeleka katika Mashariki ya Kale ya Karibu. Zaburi za kibiblia zimechangia muundo wa nyimbo za kumsifu Mungu kutoka Babeli, Misri na Kanaani. Wanazuoni wameona muunganiko wa karibu kati ya:
   1. Zaburi 104:20-30 na wimbo wa Kimisri kwa Atoni (karne ya 14 K.K.)
   2. Zaburi 29 inafanana sana shairi la Ugaritiki kwa Baali, isipokuwa kwa majina ya miungu.

B. Wana akiolojia wamevumbua maandiko ya Ras Shamra kutoka katika mji wa Ugariti yanayoonyesha ufanano kati ya shairi la Wakanaani na Zaburi.

C. muundo wa fasihi ni wa aina ya kale ndani ya Israeli:
   1. wimbo wa Musa, Kut. 15:1-17

2. wimbo wa Miriamu, Kut. 15:21
3. wimbo wa Israeli, Hes. 21:17-18
4. wimbo wa Debora, Yuda. 5
5. wimbo wa Hana, I Sam. 2:1-10
6. wimbo wa upinde kutoka katika kitabu cha Yashari, II Sam. 1:17-27

D. Miundo mitatu ya kanuni:
1. Zaburi za sifa – inaelezea sifa kwa kuanza na umuhimu kama "msifu Bwana," "msifuni Bwana," Nk.
2. Zaburi za maombolezo –inaelezea kwa kuanza na kauli ya mnenaji kama "O Bwana," ikifuatiwa na kilio au ombi
3. Zaburi za hekima – inafanana na aina ya fasihi za hekima

IV. UANDISHI

A. Uandishi wa kitamaduni wa Zaburi zilizo nyingi umepewa jina au maandiko ya juu. Kuna njia mbili za kutazama majina haya:
1. walikuwa sehemu ya andiko la kiebrania na, hivyo basi, kuwa rasmi. Hata hivyo, Zaburi iliyopatikana katika magombo ya bahari ya chumvi haina majina haya na maandiko juu yake.
2. hawakuwa asili na kutembea na waandishi na walitazamwa kama tamaduni za kale sio uvuvio wa kweli. Ilionekana kwamba mwishowe wawili kati yao hawakuyakubaIi baadhi ya maandiko ya kisheria:
   a. Jina la Zab. 34 dhidi ya I Sam. 21:10 na kuendelea
   b. Jina la Zab. 56 jina dhidi ya I Sam. 21:10
3. Tatizo lingine ni kwamba kihusishi cha kiebrania "ya" kinaweza kufahamika kwa njia kadhaa:
   a. "iliandikwa na"
   b. "iliandikwa kwa ajili ya"
   c. "iliandikwa kwenda kwa"
   d. "unahusika na muda wa"
   e. "chini ya maelekezo ya"

B. toleo la MT lina jina na maelezo ya waandishi:
1. Daudi, (I Samweli 16:16-18), (MT) mwandishi wa 73; (LXX) mwandishi wa 84; (Toleo la Kilatini) mwandishi wa 53
2. bila jina - 50 zaburi: 1, 2, 10, 33, 43, 71, 91, 93-97, 104-107, 118-119, 135, 137, 146-150
3. Asafu, kiongozi wa waimbaji wa Daudi (I Nya. 15:16-17; 16:5) 12 zaburi: 50, 73-83
4. Wana wa Kora, ndugu waImbaji wa Kilawi (I Nya. 9:19; 15:17) 11 zaburi: 42-49 isipokuwa 43, 84-88 isipokuwa 86
5. Yeduthuni, kiongozi wa waimbaji wa Kilawi, (I Nya. 16:41-42; 25:1-3; II Nya. 5:12) 3 zaburi: 39, 62, 77
6. Sulemani, 2 zaburi: 72, 127. "iliandikwa na," "iliandikwa kwa ajili ya," "iliandikwa kwa," "inawahusu," "katika muda wa," au "chini ya maelekezo ya."
7. Musa, 1 zaburi: 90
8. Mwezrahi (I Nya. 6:33; 15:17)
   a. Ethani, Zaburi 89 (wengine hufikilia Ibrahimu) I Nya. 15:17,19
   b. Hemani, Zaburi 88 (pia mwana wa Kora) I Fal. 4:31; I Nya. 4:31; 15:19

C. Utamaduni wa uandishi kutoka maandiko ya kiyahudi
    1. Baba Bathra 14b - "Daudi aliandika kitabu cha Zaburi kwa msaada wa wazee kumi, kwa msaada wa Adamu, wa kwanza, na Melkizedeki na Ibrahimu na Musa na Hemani na Yeduthuni na Asafu na wana watatu wa Kora"
    2. Baraza kuu la Wayahudi 38b (kitabu cha maadili na sheria) linafikilia kuwa Zab. 139 hadi Adamu na Zab. 110 hadi Melkizedeki

D. Toleo la LXX linafikilia kuwa Zaburi hadi Yeremia, Ezekieli, Hagai na Zekaria (112, 126, 127, 137,146-149)

## V. TAREHE

A. Tarehe ya Zaburi ni ngumu kwa sababu mbili:
    1. zaburi mojamoja ina jambo maalumu ambalo limewasababisha wao kuandikwa
    2. zaburi ilikusanywa kupitia utaratibu wa uhariri katika vitabu vitano

B. Zaburi inahusisha mashairi kutoka vipindi vyote vya maisha ya Israeli:
    1. tamaduni ya kiyahudi inasema:
        a. Adamu aliandika Zab. 139
        b. Melkizedeki aliandika Zab. 110
        c. Ibrahimu aliandika Zab. 89
        d. Musa aliandika Zab. 90
    2. uanazuoni wa kisasa umekigawa Zaburi katika nyakati kuu tatu:
        a. kabla ya uhamisho (vitabu, I, II, na IV)
        b. wakati wa uhamisho (kitabu III)
        c. baada ya uhamisho (kitabu V)

C. Ni dhahiri kwamba Zaburi nyingi zinamtambulisha Daudi:
    1. Daudi alikuwa mtunzi wa muziki, mchezaji na mwimbaji, I Sam. 16:16-18
    2. Alianzisha na kuongoza makundi ya waimbaji wa Kilawi, au waimbaji wa Hekalu, I Nya. 15:1-16:43, 25:1-31; II Nya. 29:25-30
    3. Vitabu viwili vya kwanza vya Zaburi vinamtambulisha yeye, Zab. 72:20
    4. Zaburi zake zimejitokeza katika vitabu vyote Vitano vya zeze la Kiyahudi

## VI. MUUNDO WA MTUNGA ZABURI

A. Hakuna dhamira au mwelekeo wa jumla. Kuna:
    1. utangulizi wa jumla (sifa za mtu mwenye haki) - Zab. 1 na inawezekana Zab. 2
    2. kila kimoja cha mgawanyo wa vitabu vitano pia kina malizia na wimbo wa kumsifu Mungu, 41:13; 72:18-19; 89:52; 106:48
    3. ufungaji wa jumla (wimbo wa kumsifu Mungu) - Zaburi 150

B. Sifa za Vitabu Vitano
    1. Kitabu cha 1 - Zaburi. 1-41
        a. vyote lakini vitabu 4 vinamtambulisha (1, 2, 10, 33)

  b. YHWH kama jina la Mungu mwenye nguvu zaidi, YHWH mara 273 hadi Elohim mara 15
  c. inawezekana siku za Daudi katika vita na Sauli
2. Kitabu cha 2 - Zaburi 42-72 (72:20 inaonyesha uhariri)
  a. Zaburi 42-49 kwa wana wa Kora (isipokuwa 43)
  b. Mungu kama jina la Mungu mwenye nguvu zaidi, Mungu 164 kwa YHWH mara 30
  c. inawezekana siku za Daudi kama mfalme
3. Kitabu cha 3 - Zaburi 73-89
  a. Zaburi 73-83, Asafu
  b. Zaburi 84-88, wana wa Kora (isipokuwa 86)
  c. Zaburi 26 inamtambulisha Daudi
  d. YHWH kama cheo kwa ajili ya Mungu mara 44; Elohim mara 43
  e. inawezekana mgogoro wa Ashuru
4. Kitabu cha 4 - Zaburi 90-106
  a. Zaburi 101, 103 kwa Daudi
  b. Zaburi 90 kwa Musa
  c. Wengine wote hakuna jina
  d. YHWH limetumika mara 104; Elohim mara 7
  e. inawezekana katika mgogoro na Babeli
5. Kitabu cha 5 - Zaburi 107-150
  a. Zaburi 119 ni upana wa fumbo katika neno la Mungu
  b. YHWH mara 236; Elohim mara 7
  c. Zaburi 146-150 ni Zaburi za sifa ambazo zote zinaanza na "Msifuni Bwana"
  d. inawezekana ni tumaini katika Baraka zijazo za Mungu

C. Kubadilisha idadi ya Zaburi
1. MT MSS
  a. Berachothi 9b -- Zaburi 1 na 2 zinahesabiwa kama 1
  b. Sabato 16 – jumla idadi ya zaburi zilikuwa 147 kulingana na miaka aliyoishi Yakobo
2. toleo la LXX
  a. Zaburi 9 na 10 kwa pamoja zinafanya fumbo moja la zaburi
  b. Zaburi 114 na 115 kwa pamoja zote ni Zaburi za haleluya
  c. Zaburi 116 na 147 zimegawanywa katika sehemu mbili kila moja
3. Idadi ya Zaburi yumkini inasimulia mpangilio wa usomaji wa maandiko kila mwaka katika sinagogi la awali

D. mfano wa njia za kukusanya Zaburi katika kundi:
1. kwa dhamira au mada
  a. nyimbo za kumsifu Mungu
    (1) kwa Mungu kama muumbaji, 8, 19, 104, 139, 148
    (2) kwa Mungu kwa ujumla, 33, 103, 113, 117, 134-136, 145-147
  b. nyimbo za shukrani, 9-10, 11, 16, 30, 32, 34, 92, 116, 138
  c. maombolezo/nyimbo za maombolezo/nyimbo za kilio
    (1) kushirikiana, 12, 14, 44, 53, 58, 60, 74, 49, 80, 83, 85, 89, 90, 94, 106, 123,126, 137
    (2) binafsi, 3-7, 13, 17, 22, 25-28, 31, 35, 38-43, 69-71, 86, 88, 102, 109,120, 130, 139-143
  d. nyimbo za kumsifu mfalme

(1) Mungu kama mfalme, 47, 93, 96-99
(2) mfalme wa Israeli au Masihi, 2, 18, 20, 21, 45, 72, 89, 101, 110

e. tenzi juu ya Sayuni, 46, 48, 76, 84, 87, 122
f. nyimbo za kusifu za kawaida ya ibada na Sala
(1) kufanya upya maagano, 50, 81
(2) Baraka za kuhani , 134
(3) juu ya Hekalu, 15, 24, 68
g. tenzi juu ya hekima, 36, 37, 49, 73, 111, 112, 127, 128, 133
h. tenzi juu imani katika uaminifu wa YHWH, 11, 16, 23, 62, 63, 91, 121, 131
i. shutuma juu ya miungu ya uongo na ibada ya sanamu, 82, 115

2. na mwandishi au mnenaji
a. tenzi za Daudi alizitumia kwa YHWH mkuu kama jina la Uungu, Zab. 1-41
b. tenzi za Daudi alizitumia kwa Mungu mkuu kama jina la Uungu, Zab. 51-72
c. tenzi za Kilawi za Daudi na waimbaji
(1) Kora na wana wake, Zab. 42-49, 84-88
(2) Asafu na wana wake, Zab. 73-83
d. nyimbo za wanaosifu, Zab. 111-118, 140-150
e. nyimbo za wageni waendao Yerusalemu kuabudu siku ya sikukuu, Zab. 120-134

3. kwa matukio ya kihistoria katika historia ya Israeli yanasisitizwa kwenye andiko au yaliyomo, Zab. 14, 44, 46-48, 53, 66, 68, 74, 76, 79, 80, 83, 85, 87, 108, 122, 124-126 na 129

E. Zaburi zinazofanana
1. Zaburi 14 na 53 ni ile ile isipokuwa jina la Mungu
a. Zaburi 14 ina YHWH
b. Zaburi 104 ina Mungu
2. Zaburi 103 na 104 ni muunganiko:
a. mwanzo ule ule na mwisho
b. Zab. 103 ina YHWH kama mwokozi na mkombozi
c. Zab. 104 ina Mungu kama muumbaji na mtoa riziki
3. Zaburi 32 na 51 zote zinasimulia dhambi ya Daudi na Bathsheba
4. Zaburi 57:7-11 na 60:5-12 zimeunganishwa kwenye Zab. 108
5. Zaburi 18 imejirudia katika II Sam. 21:1-51

F. Kwa nini Zaburi 150 ziko katika vitabu 5
1. inawezekana zaburi 150 ni sambamba kwa mgawanyo wa sheria za sinagogi 150 kwa ajili ya kusomwa mbele za watu siku za Sabato.
2. inawezekana vitabu vitano ni sambamba na vitabu vitano vya Musa.

VII. MANENO YA KIMUZIKI YALIVYOTUMIWA NA MTUNGA ZABURI

A. maandiko ya maneno ya kimuziki yametumika kuelezea aina tofauti za Zaburi
1. *MIZMOR* humaanisha "kung'ang'ania." Zaburi hizi humaanisha kwamba kuimba na kuambatana na vyombo vya kimuziki. Kuna aina hizi 57.
2. *SHIR* inarejelea aina zote za nyimbo. Kuna aina hizi 30.

3. *MASCHIL* au *MASKIL* ambazo hudokeza ujuzi maalumu wa nyimbo au mafundisho ya zaburi. Kuna aina hizi 30.
4. *MITCHTAM* au *MITKHTAM* – maana ya neno hili linatia mashaka. Inawezekana kutoka asili ya Kiebrania linamaanisha "shaba" au "thamani"; kutoka asili ya Akkadia linaweza kumaanisha "iliyojificha" au "isiochapishwa"; kutoka asili ya Kiarabu inaweza kumaanisha "lipia kosa" au "msamaha." Kuna aina hizi 6.
5. *PALAL* humaanisha ombi. Imetumika kuelezea zaburi za Daudi katika kitabu cha I na II (kama vile Zaburi 72:20). Pia limepatika katika andiko la Zab. 17, 86, 90, 102, 142 na inawezekana katika 122.

B. Kimuziki maneno yanaelezea kucheza au kuimba Zaburi
1. *SELAH* limetumika mara 71 katika zaburi 39 na Hab. 3:3, 9, 13. Maana yake sio dhahili. Kuna nadharia kadhaa:
   a. kutoka toleo la LXX "nafasi kati ya zaburi" kwa ajili ya tafakari au matokeo ya kuvutia
   b. kutoka asili ya kiebrania "kupanda," hivyo basi, mwinuko au ngome
   c. waalimu wa sheria wanasema ni uthibitisho kama "Amina" ambalo humaanisha "daima."
2. *SHIGGAION* au *SHIGIONOTH* limetumika katika Zab. 7 na Hab. 3. Ni maombolezo au kilio kinaelezea huzuni. Ina muundo wa kishairi la hisia za juu sana.
3. *NEGINOTH* limetumika mara 6 na Hab. 3:19. linamaanisha "katika uzi wa vyombo."
4. *SHEMINITH* limetumika mara mbili. Linamaanisha "katika ubeti wenye mistari minane" au "katika minane."ni kinyume cha Alamothi, hata hivyo, inawezekana kwa ajili ya sauti za wanaumme (kama vile I Nya. 15:21).
5. *ALAMOTH* limetumika mara 4. Linarejelea sauti za kwanza za wanawake (kama vile I Nya. 15:20).
6. *MECHILOTH* limetumika mara moja. linamaanisha "kwenye sauti ya vyombo."
7. *GITTITH* limetumika mara 3. linamaanisha "kwenye kinubi."
8. kuna rejea kadhaa zinazotaja ulinganifu wa sauti, Zab. 9, 22, 45, 53, 56, 57-59, 60,62, 69, 75, 77, 80 na 88

VIII. KUSUDI LA ZABURI

A. Israeli waliamini kwamba maisha yote yanasimuliwa kwa maagano na Mungu. Zaburi ni kujiachilia maisha ya mwanadamu kwa hisia za ndani kabisa kwa Mungu.

B. Israeli wanaamini katika Mungu mmoja tu, anayejali. Imani sio kawaida ya ibada na sala za kidini au kanuni za imani lakini binafsi na kila siku. Muundo wa kishairi wa Zaburi unatusaidia sisi kuelezea ucha-Mungu wetu kwa Mungu. Kiongozi wa tabia ya Agano la kale ni Mungu!

C. Zaburi yote yumkini inaanza kama maelezo ya imani ya mtu binafsi ambayo mwishowe yanatumika kwa imani na jamii (kama vile Zab. 23; 139, n.k).

IX. MANENO NA/AU TUNGO NA WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHTASARI

A. Maneno na/au Tungo
1. "tenga" (*kadosh*) 4:3 (toleo la NASB na NIV)
2. "tumaini" (*emeth* 4:5 (toleo la NASB na NIV)
3. "uisawazishe njia Zako" 5:8 (toleo la NASB na NIV)
4. "fadhili" (*hesed*) 6:4 (toleo la NIV, "upendo usio na mashaka")


5. "asiporejea" 7:12 (toleo la NIV, "tulia")
6. "mwana wa adamu," 8:4 (toleo la NASB na NIV)
7. "wokovu," 9:14 (toleo la NASB na NIV)
8. "shimo," 9:15 (toleo la NASB na NIV)
9. "kikombe," 11:6; 75:8 (toleo la NIV, "kundi")
10. "haki," 15:2 (toleo la NIV, "maadili")
11. "kerubi," 18:10 (toleo la NIV, "*cherubim*")
12. "kama miguu ya kulungu," 18:33 (toleo la NIV, "mguu wa Ayala")
13. "mwokozi," 19:14 (toleo la NASB na NIV)
14. "wanalipigia kura," 22:18 (toleo la NASB na NIV)
15. "bonde la uvuli wa mauti," 23:4 (toleo la NASB na NIV)
16. "katika uvuli wa mbawa ," 57:1; 91:4 (toleo la NASB na NIV)
17. "gunia," 69:11 (toleo la NASB na NIV)
18. "kitabu cha uzima," 69:28; 139:16 (toleo la NASB na NIV)
19. "penye utelezi," 73:18 (toleo la NIV, "uwanja wa utelezi")
20. "pembe za uovu," 75:10 (toleo la NASB na NIV)
21. "mahali pa juu," 78:58 (toleo la NASB na NIV)
22. "Rahabu," 89:10 (toleo la NASB na NIV)
23. "naliwakatilia mbali," 118:10,11,12 (toleo la NASB na NIV)
24. "jiwe kuu la pembeni," 118:22 (toleo la NIV, "jiwe kuu")
25. "pembe za madhabahu," 118:27 (toleo la NASB na NIV)

B. Watu
1. Bwana wa majeshi (YHWH Sabboth) NASB, 24:10 (NIV, "Bwana Mwenye nguvui")
2. Yeduthuni, 62 utangulizi (toleo la NASB na NIV)
3. Waishmaeli, 83:6 (toleo la NASB na NIV)
4. Melkizedeki, 110:4 (toleo la NASB na NIV)


X. MAENEO YA KI-RAMANI
1. Sayuni, Zab. 2:6
2. Bashani, 22:12
3. Kadeshi-Barnea, 29:8 (NIV, “Kadeshi”)
4. Ml. Hermoni, 42:6 (toleo la NIV, “kilima cha Hermoni”)
5. Shilo, 78:60
6. Ml. Tabori, 89:12
7. Baali-Peori, 106:28 (toleo la NIV, “ Baali Peori”)

XI. MASWALI YA MJADALA YA KI-MAUDHUI KWA MWANAFUNZI
1. Kwa nini Zab. 2 inafikiliwa kuwa ni ulimwengu, na zaburi ya kimasihi?
2. Elezea tofauti ya sitiari iliyotumika kumwelezea Mungu katika Zab. 18:1-2
3. Taja aina mbili za ufunuo unaopatikana katika Zab. 19 na fafanua.
4. Je! Zab. 22 inaelezea maana ya kinabii?
5. Elezea mpangilio wa kihistoria wa Zab. 32 na 51.
6. Ni nini Zab. 38 inaongelea (kwa maneno yako.)
7. Elezea sitiari ya Zab. 42:1.

8. Elezea 51:11-12 inaongelea juu ya nini.
9. Je! inamaanisha nini kumhofu Bwana? 67:7
10. Ni tatizo gani la uzima katika Zab. 73 la kupambana nalo?
11. Ni muundo gani usio wa kawaida juu ya Zab. 119? Ni nini mada yake kwa ujumla?
12. Ni lipi tatizo la uzima katika Zab. 139 la kuhusika nalo?


MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE
MAGH
MASH
KAS
KUS

# PALESTINA



# UTANGULIZI WA MITHALI

I. JINA LA KITABU

A. Katika Kiebrania jina ni mistari saba ya kwanza na dhamira mst. 7.

B. Katika toleo la LXX hili linaitwa "Mithali za Sulemani."

C. Katika toleo la Kilatini hili inaitwa "kitabu cha mithali."

D. Jina la Kiingereza linatokana na neno la Kiebrania *mashal* ambalo lina maana ya "kuwa kama." Mithali zilikuwa mafupi, japo zilikuwa za kukaripia, semi, mara nyingi zilikuwa za mistari miwili.

II. URASIMISHAJI

A. Ni sehemu ya mgawanyiko wa tatu wa sheria ya Kiebrania inayoitwa "Maandiko."

B. Buku la sheria za Kiyahudi, Baba Bathra 14b, zinasema mpangilio wa vitabu vya hekima ni Zaburi, Ayubu na Mithali. Ilihusisha uandishi wa:

1. kitabu cha Ayubu kwa Musa
2. Zaburi kwa Daudi
3. Mithali kwa Hezekia

C. Waalimu wa sheria wanadai kuwa Sulemani, ambaye alikuwa maarufu kwa hekima yake, aliandika vitabu vitatu:

1. Wimbo uliobora wakati alipokuwa mdogo,
2. Mithali wakati alikuwa na umri wa kati,
3. Mhubiri alipokuwa mzee na mkali. Utamaduni huu unaelezewa kwa kuunganisha vitabu hivi vitatu pamoja katika toleo la LXX.

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Mithali ni aina maalum ya fasihi ya hekima.

B. Kuna aina kadhaa za maneno ya mithali (kama vile Clyde Francisco, *Introducing the Old Testament,* uk. 265).

1. Mithali ya kihistoria - haya ni maneno maarufu yaliyopendwa zamani ambayo yamekuwa ukweli wa sasa.
2. Mithali ya kisitiari - haya ni maneno mawili yanayolingana na vitu:
   a. kutumia ulinganifu, "kama" au "kama"
   b. kwa kutumia ulinganifu tofautishi
3. fumbo - hivi ni vitendawili au fumbo la ubongo.
4. Mithali ya kimafumbo - haya ni ya muda mrefu, kulinganisha zaidi au utofautishaji.
5. Mithali ya mafundisho - haya ni kweli ya kufundisha vijana kwa huduma ya serikali au uongozi.

C. Mithali ina ulinganifu kama Zaburi:

1. Ufanano wa visawe - Mit. 8: 1
2. Ufanano wa kinyume - Mithali. 28: 1
3. Ufanano wa kuunganisha - Mit. 26: 1

IV. UANDISHI

A. Mithali imekuwa ya desturi ya kushikamana na Sulemani, kama Zaburi zilivyokuwa kwa Daudi. Hii ilikuwa kwa sababu Sulemani alijulikana kwa hekima yake (kama vile I Fal 3:12, 4: 29-34; 10: 1), na pia kwa sababu jina la Sulemani limetajwa katika Mit. 1: 1; 10: 1 na 25: 1.

B. Mithali ni matokeo ya mkusanyiko wa uhariri kama Zaburi. Kuna waandishi kadhaa waliotajwa:
   1. Suleimani - 1: 1; 10: 1; 25: 1
   2. wanaume wenye hekima (wenye hekima) - 22:17; 24:23
   3. Aguri - 30: 1
   4. Lemueli - 31: 1

C. Mchakato wa kuhariri katika Mithali unaweza kuonekana katika 25: 1 ambapo inasema kuwa watu wa baraza la Hezekia walikubaliana na mithali ya Sulemani. Inawezekana wengi walikuwa wasimuliaji kabla ya wakati huu.

D. Sura ya 30 na 31 ni kwa watu kutoka Massa. Kuna kutofautiana kati ya watafsiri kuhusu neno hili. Matoleo mengi ya Kiingereza cha kisasa yanatafsiri neno hili kwa "utabiri" au "mzigo."The Jewish Publication Society of America hutafsiri kama jina la mahali. Neno hili *MASSA* linarejelea ufalme wa Ishmaeli huko Saudi Arabia (kama vile Mwa. 25:14 na I Nya 1:30).

E. Kuna kufanana dhahiri kati ya "Maneno ya hekima" 22: 17-24: 22 na "Maagizo ya Amenemope" kutoka Misri yapata mwaka 1200 K.K. Kwa majadiliano kamili angalia John H. Walton, *Ancient Israelite Literature in Its Cultural Context*, Grand Rapids: Zondervan, 1990. kr. 192-197.

V. TAREHE

A. Tarehe ya kitabu hiki ina shida sawa kama Zaburi. Kuna tarehe mbili zinazofikiriwa:
   1. tarehe ya mithali ya mtu binafsi,
   2. tarehe waliyokusanya katika kitabu chetu cha kisheria.

B. Mengi ya mithali inarudi siku za Sulemani, hasa 10: 1-22: 16 na 25: 1-29: 27.

C. Kuna ufanano mwingi kati ya maneno ya Agur katika sura ya 30 na maandiko ya Ras Shamra kutoka Ugaritiki. Maandiko haya yanatoka karne ya 15 K.K.

D. Kitabu cha kisheria cha Mithali, sura ya 1-29, kiliandaliwa wakati wa Hezekia (710-687 K.K.) Sura mbili za mwisho ziliongezwa baadaye.

VI. MAZINGIRA YA KIHISTORIA

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI

A. Jina la kitabu, 1:1-6
B. Dhamira ya maelezo, 1:7
C. Sifa ya hekima (kibinadamu), 1: 8-9: 18
D. Mithali ya Sulemani (mistari tofauti), 10: 1-22: 16
E. Maneno ya mwenye hekima (sawa na hekima ya Misri), 22: 17-24: 22

F. Maneno zaidi ya mwenye hekima, 24: 23-34
G. Mithali ya Sulemani (kiini), 25: 1-29: 27
H. Maneno ya Aguri (jibu kwa wasioamini), 30: 1-33
I. Maneno ya Lemuweli (kutoka kwa mama yake), 31: 1-9
J. Sifa ya mwanamke mwenye kumcha Mungu (husifiwa), 31: 10-31

VIII. KWELI KUU

A. Ingawa si mara nyingi imeelezwa, Mithali msingi wake ni dhana ya kumwamini Mungu mmoja atendae kazi katika uumbaji wote na maisha ya waamini mmoja mmoja (kama vile 1: 7, 3: 5-6, 9:10, 14: 26-27)

B. Aina hii ya fasihi ilikuwa na uwiano (kama vile Yer 18:18, Ezek 7:26):
1. "Sheria" (makuhani)
2. "Manabii" (manabii)

Sio kubadili historia au ibada ya Israeli lakini furaha, maadili na maisha ya mafanikio ya Waisraeli binafsi.

C. Mwanzoni ilikuwa iliyoundwa kufundisha vijana matajiri kwa huduma ya utawalai au uongozi wa jamii (kama vile 1: 8-9).

D. Ni ufahamu unaoongoza kwa kila siku, vitendo, maisha ya kimungu. Inaweza kuwa kama "ufahamu wa farasi wa Mungu."

E. Ni lazima ikumbukwe kwamba Mithali ni kauli ya jumla ya ukweli. Hawana daima kueleza au kuzingatia matatizo au hali ya mtu binafsi.

IX. MANENO NA/AU TUNGO NA WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHTASARI:

A. Maneno na / au Tungo
1. Mithali (*mashal*), 1: 1 (toleo la NASB na NIV)
2. hekima (*hokmah*), 1: 2 (toleo la NASB na NIV)
3. Hofu ya Bwana, 1: 7 (toleo la NASB na NIV)
4. "hekima hupiga kelele mitaani," 1:20 (toleo la NIV, "hekima huita kwa sauti juu ya barabara")
5. "wajinga ... wanadharau ... wapumbavu," 1:22 (toleo la NIV, "rahisi" wale wanaocheka ... wapumbavu ")
6. mwanamke wa ajabu, 2:16 (toleo la NIV," mzinzi ")
7. " yeye ni mti wa uzima, "3:18 (toleo la NASB na NIV)
8. " chukizo kwa Bwana, "3:32; 17:15 (toleo la NIV, "Bwana huchukia")
9. "unywe maji ya birika lako mwenyewe," 5:15 (toleo la NASB na NIV)
10. "ahadi," 6:1 (toleo la NIV, "usalama")
11. Mtu asiye na maana (*belial*), 6:12 (NIV, "mwovu")
12. "Bwana alikuwa na mimi katika mwanzo wa njia yake," 8:22 (toleo la NIV, "Bwana alinipeleka kama mwanzo wa kazi zake")
13. "Kuzimu na Uharibifu vi wazi mbele za Bwana," 15:11; 27:20 (toleo la NIV, "Kifo na Uharibifu ziko wazi mbele ya Bwana")

14. Mkombozi (*Go'el*), 23:11 (NIV, "mlinzi")
15. riba, 28: 8 (toleo la NIV, "riba kubwa" )
16. unabii (massa), 30: 1; 31: 1 (toleo la NASB na NIV)


B. Watu

1. Watu wa Hezekia, 25: 1
2. Aguri, 30: 1
3. Ithieli, Ithieli, na Ukali, 30: 1
4. Lemueli, 31: 1


X. MAENEO YA KI- RAMANI – hakuna

XI. MASWALI YA KIMAUDHUI KWA MWANAFUNZI

1. Nini tofauti kati ya neno la Kiebrania kwa ajili ya "hekima" na "maarifa"?
2. Kwa nini 1:7 ni ya muhimu sana?
3. Kwa nini hekima inajulikana kama mwanamke?
4. Ni sehemu gani ya hekima ilikuwa katika uumbaji? (kama vile 3:19; 8:27)
5. Elezea "njia mbili" (4: 10-19).
6. Elezea maombi ya 30: 7-9.
7. Orodhesha matokeo ya mwanamke mcha- Mungu katika 31: 10-31.


KAS
MAGH
MASH
KUS
MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE

# PALESTINA



# UTANGULIZI WA MUHUBIRI

I. JINA LA KITABU

A. Jina la Kiebrania lilikuwa ni tungo "Maneno ya *Qoheleth*, mwana wa Daudi, mfalme huko Yerusalemu" kutoka 1: 1. Jina lake fupi lilikuwa *Qoheleth*, ambalo lilitumiwa na Sulemani katika I. 8: 1. Ni mshiriki wa kike kutoka kwa *Qahal* ya Kiebrania, "kutaniko" au "kusanyiko."

B. Kitabu kiliitwa "Mhubiri" ambacho ni muundo wa kilatini kutoka toleo la LXX. Hili ni neno la Kiyunani kwa ajili ya "yule anayekusanyika", kutoka katika asili ya "kuita."

C. Neno *Qoheleth* linaweza kumaanisha:
1. Mtu anayekusanya watazamaji, hivyo basi, mwalimu, mhubiri, mtoa mjadala, nk.
2. inawezekana ni sitiari kwa ajili ya mtu anayekusanya ukweli, mwanafilosofia au mwenye ujuzi.

II. URASIMISHAJI

A. Mhubiri ni mfano wa aina ya hekima ya fasihi. Ni matibabu mapana zaidi ya kuhitaji unyeti, kama Ayubu.

B. Ni sehemu ya mgawanyiko wa tatu wa sheria ya Kiebrania inayoitwa "Maandiko."

C. Pia ni sehemu ya makundi maalum ya vitabu vitano vidogo vinavyoitwa *Megilloth* au "magombo matano." Kila kimojawapo husomwa kila mwaka siku ya sikukuu. Kitabu cha Mhubiri kilikuwa kinasomwa katika sikukuu ya vibanda au hema.

D. Kwa sababu ya asili kubwa ya kitabu hiki kilikataliwa na shule walimu wa sheria za kiyahudi wasio taka mabadiliko ya Shammai lakini kilitetewa na shule ya walimu wa sheria ya kiyahudi wapenda mabadiliko ya Hillel. Mjadala huu uliendelea mpaka wakati wa Jamnia baada ya kuanguka kwa Yerusalemu (70-90 B.K).

E. Vitabu kadhaa vya sheria ya Agano la Kale vilikuwa na ugumu kukubaliwa:
1. Mhubiri - uchungu, mbaya, usio wa utamaduni
2. Wimbo bora - uthibitisho wa upendo wa kimwili
3. Esta - hakuna kutajwa kwa Mungu au Hekalu la Kiyahudi au maeneo
4. Ezekieli - hekalu lake tofauti na Musa
5. na kwa kiasi fulani, Danieli. - unabii wa matukio ya siku za mwisho wa sura ya 7-12

F. Mhubiri hatimaye kilikubaliwa kwa sababu:
1. kilikuwa kinahusishwa na Sulemani,
2. kina hitimisho la utamaduni,
3. kinapenda kweli kwa uzoefu wa mwanadamu na inaonyesha mchafuko wa jumuiya ya Kiyahudi ya baada ya uhamisho.

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Mhubiri kama Ayubu lazima Kitafasirike chote. Ni mhimili wa kejeli kupitia sura. 12.

B. Ni lugha-ya kijembe kutazama maisha bila ya Mungu. Tungo muhimu ni "chini ya jua," 1: 3, 9, 14; 2:11, 17, 18, 19, 20, 22; 3:16; 4: 1, 3, 7, 15; 5:13, 18; 6: 1, 5, 12; 7:11; 8: 9, 15, 17; 9: 3, 6, 9, 11, 13; 10: 5; 11: 7; 12: 2 (mara 31).

IV. UANDISHI

A. Ni Kitabu bila jina.

B. Tamaduni za Kiyahudi zinasema ni mojawapo ya vitabu vitatu vilivyoandikwa na Sulemani: (Midrash Shir Rabbah I, 1, dhehebu 10)
1. wimbo ulio bora wakati alipokuwa mdogo,
2. Mithali wakati alikuwa na umri wa kati,
3. Mhubiri wakati alikuwa mzee na mwenye uchungu.

C. Sulemani alizuia kwa hakika maandishi ya sura ya 1-2, kwa sababu ya hekima, utajiri na nafasi yake. Lakini kuna dokezo kwamba yeye sio mwandishi wa kweli:
1. katika 1:12, "Nilikuwa mfalme juu ya Israeli huko Yerusalemu." (toleo la NIV) - kipindi cha mwisho
2. katika 1:16, "... zaidi ya wote waliokuwa juu ya Yerusalemu kabla yangu" (toleo la NASB) - Daudi pekee alikuwa kabla ya Sulemani
3. katika 4: 1-3, 5: 8 na 8 : 9 unyanyasaji wa serikali hujadiliwa lakini hauna matumaini.
4. Jina Sulemani halitokei katika kitabu.

D. Kwa hoja ya kitaalamu ya uandishi wa Sulemani (kama vile *Introduction to the Old Testament*, na C. F. Keil, juzuu 1, kr. 516-529).

E. Baba Bathra 15a alisema watu wa Hezekia waliandika Mithali, Mhubiri na Wimbo ulio bora, lakini kwa kweli hii inamaanisha kuwa walihariri au walikusanya vitabu vya hekima.

F. Jina la *Qoheleth* linaweza kuwa jina sahihi au cheo. Inaonekana kama cheo kwa sababu:
1. lina makala ya wazi katika 7:27 na 12: 8,
2. ni muundo ya kike ambayo inadokeza mamlaka lakini hutumia vitenzi vya kiume,
3. ni neno la kawaida linalopatikana mara saba, katika kitabu hiki pekee.

G. Ni Sehemu pekee ya kitabu kinachofunua mwandishi au mhariri wa mwisho 12: 9-14. Ni wazi yeye ni mjuzi, mwalimu wa hekima.

H. Kinzani dhahiri au vinavyo jipinga vimeelezwa kama:
1. dhihaka, maisha bila Mungu ("chini ya jua")
2. Utamaduni wa hekima ya Kiyahudi na changamoto zake (imedokezwa kukanushwa)
3. Mwalimu wa hekima na mwanafunzi wake mwenye shauku na mjadala (majadiliano)
4. mgogoro ndani ya mtu aliyeanguka (gazeti la uzima)
5. wahariri wa mwisho, mfano, 12: 9-12 (chanya kuelekea *Qoheleth*) na 12: 13-14 (hasi kuelekea *Qoheleth*).

V. TAREHE

A. Kuna mambo mawili yanayohusiana na tarehe ya Mhubiri:

1. Wakati kitabu kilipoandikwa,
2. Wakati kilipowekwa katika muundo wake wa mwisho kisheria.

B. Mpangilio wa kihistoria lazima uwe baada ya siku ya Sulemani. Alitumia kama fasihi kuzuia katika sura ya sura ya 1-2.

C. Muundo wa mwisho wa kitabu unalenga siku za mwisho:
   1. Muundo wa aina ya Kiebrania ni baada ya uhamisho lakini kabla ya 400-300 K.K.
      a. Maneno ya Kiaramu na halisi
      b. muundo wa Kiebrania
   2. kuna ufanano wa fasihi katika fasihi za hekima ya Foinike yapata mwaka 600-400 K.K.
   3. taswira ya Mhubiri imeonekana katika maandishi ya Ben Sirah, Mwalimu, ambayo yaliandikwa yapata mwaka 180 K.K.
   4. Kumekuwa na sehemu kadhaa ndogo za Mhubiri zilizopatikana katika Magombo ya Bahari ya chumvi (4Q). Hizi zimekuwako mwishoni kama karne ya pili K.K.

VI. VIPENGELE VYA KI-FASIHI

A. Kitabu hiki ni vigumu kuelezea. Ni zaidi kama jarida la uzima kuliko muundo wa fasihi. Ni sawa na mafundisho ya waalimu wa sheria yaitwayo "lulu kwenye uzi." Hata hivyo, kuna wazo la kuunganisha, ikiwa si dhamira ya kuunganisha.

B. Inawezekana kuwa kumekuwa na nyongeza za uhariri:
   1. ufunguzi, 1: 1
   2. ujumuishi 1: 2 na 12: 8 inamaanisha 1: 1 na 12: 9-14 ni nyongeza
   3. utangulizi wa aina mbili umeongezwa:
      a. 12: 9-12 (katika nafsi ya tatu)
      b. 12: 13-14 (thiolojia ya kidesturi)

C. Ni wazi kwamba sura ya 1-2 humtumia Sulemani kama kuzuia fasihi.

D. Sura ya 3 ni shairi nzuri juu ya uzoefu wa kawaida wa maisha ya kibinadamu.

E. Ukumbusho hauna maelezo kirahisi!

VII. MASUALA YA KITHIOLOJIA

A. Ukweli wa uwepo wa kitabu hiki katika sheria unaonekana kudokeza kwamba Mungu hamkatai mwaminifu, mwenye shaka.

B. Kuuliza maswali ya kilele hakuzuiliwi.

C. Mhubiri anaamini kuwepo kwa Mungu na imeandikwa ndani ya mkondo wa imani ya Agano la Kale.

D. Uovu ni matokeo ya mwanadamu, sio Mungu (kama vile 7:29; 9: 3).

E. Njia za Mungu haziwezi kujulikana. Mwanadamu lazima ajitahidi kwa kumaanisha katika maisha!

F. Mashaka ya maoni sahihi ya maisha ya baadaye na shaka juu ya uwezo wa mwanadamu kumjua Mungu kabisa, lakini bado Mungu ni mwenye neema.

G. Ulimwengu, kama ulivyo, sio ya haki ya kikatili, kuna ulazima kuwe na kitu kingine zaidi!

H. Kuwa na maudhui na uhai - ni kutoka kwa Mungu. Unaweza Kufurahia popote na wapi. (2:24)

I. Majibu rahisi ambayo hayafai katika uzoefu wa maisha ni majibu "hapana". Tunapaswa kukabiliana na hali halisi ya maana ya uzima ikiwa hakuna Mungu.

VIII. KWELI KUU

A. Lengo lake kuu lilikuwa ni kuonyesha udhaifu wa binadamu kuwa mbali uwepo wa Mungu. Ni njia ya kubadili utoshelevu wa maandiko au uwezo wa kufikiri. B. H. Carroll alisema kuwa katika siku za uaminifu wake, Mhubiri na Ayubu walimfanyia nguvu isiyo ya kawaida juu yake, wakionyesha udhaifu wa uzima na kuelekeza kwa Mungu.

B. Furaha na kuridhika hupatikana katika (2:24; 3: 12-13,22; 5: 18-20; 8:15; 9: 7-9; 12: 13-14):

1. imani na utii kwa Mungu,
2. raha ya nyumbani na familia,
3. kazi ya mtu.

C. Kitabu hiki ni juu yake asadikiye kuwa hatuna habari za baada ya maisha. Hakijibu maswali ya ukweli halisi lakini hakiulizi maswali ya ukweli wa sasa:

1. Kwa Wayahudi, ilionyesha kosa la msingi wa kutia chumvi yaliyotolewa na wasomaji wa tamaduni ("njia mbili").
2. Kwa Wapagani, inaonyesha ufisadi wa maisha ya kidunia bila Mungu.
3. Majibu rahisi kwa maswali ya maisha ni kawaida. Kuna siri hata kwa imani! Ufunuo haufunulii wote!

D. Mwandishi huyu anatumia ufunuo wa asili, sio ufunuo maalum, kuyachambua maisha. Jina la agano la Mungu, YHWH, halionekani katika kitabu. Kama vitabu vyote vya hekima jina la jumla la Mungu, *Elohim*, limetumika.

E. Kitabu hiki kina muundo wa uwiano wa hekima iliyopangwa vizuri ambayo hutoa mafanikio katika maisha. Kuna siri katika maisha, katika asili, katika mwanadamu, kwa Mungu. Ufunguo unapatikana katika imani, sio ujuzi; katika familia sio kumiliki na ni katika Mungu si mtu. Furaha rahisi ya maisha: familia, kazi, marafiki, kupata chakula furaha katika maisha haya. Uzima unaofuata umefunikwa, lakini Mungu yuko hapo!

IX. MANENO /VIFUNGU NA WATU WA KUWATAMBUA KIMUHTASARI

A. Maneno/Vifungu


1. "ubatili wa ubatili" 1:2 (NIV, "sio maana! Sio maana!")
2. "chini ya jua" 1:3 (NASB na NIV)
3. "Katika wingi wa hekima mna wingi wa huzuni" 1:18 (NIV, "maana kwa hekima nyingi huja huzuni nyingi ")
4. "tukio moja la mwisho liwapatalo wote sawasawa." 2:14 (NASB na NIV)
5. "tena ameiweka hiyo milele ndani ya mioyo yao" 3:11 (NASB na NIV)
6. "ili Mungu awajaribu . . ." 3:18 (NASB na NIV)

7. "... Kwa hiyo nikawasifu wafu waliokwisha kufa kuliko wenye uhai walio hai bado..." 4:2-3 (NIV, " bora zaidi kuliko wote ni yeye ambaye bado hawajawahi ")
8. "mche Mungu" 5:7 (NIV, " kusimama kwa hofu ya Mungu ")
9. " Apendaye fedha hatashiba fedha" 5:10 (NASB na NIV)
10. "Usiwe na haki kupita kiasi; Wala usijiongezee hekima mno" 7:16 (NASB na NIV)
11. "Mwenye kuchimba shimo atatumbukia ndani yake" 10:8 (NASB na NIV)
12. "Tupa chakula chako usoni pa maji; Maana utakiona baada ya siku nyingi" 11:1 (NASB na NIV)

B. Watu
1. Qoheleth 1:1
2. mlinzi 12:3-4 (NIV, "watunzaji wa nyumba")
3. Mchungaji mmoja 12:11
4. mwanangu 12:12


X. MAENEO YA KI-RAMANI –hakuna

XI. MASWALI YA MJADALA KWA MWANAFUNZI
1. Nini lengo kuu la kitabu hiki?
2. Kwa nini fasihi ya Sulemani ilizuliwa katika sura ya 1-2?
3. Ni kwa namna gani mtu anafanana na anatofautiana na wanyama? 3:12-22
4. Je! Tunaweza kumjua Mungu?
5. Je, furaha inapatikana wapi?
6. Kitabu hiki kiliandikwa kwa akina nani na kwa nini?




MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE

# PALESTINA




VIPIMO KATIKA MAILI

# UTANGULIZI WA WIMBO ULIO BORA

I. JINA LA KITABU

A. Kitabu hiki, kama vilivyo vitabu vingine vya Agano la Kale kiuhalisia kilipewa jina baada ya maneno machache ya kitabu. Katika kitabu cha Waebrania maneno ya kwanza ni kitabu cha "wimbo ulio bora ambacho ni cha Suleimani", ambapo ni muundo wa Kiebrania wenye sifa za juu sana. Hiki kingeweza kudokeza nyimbo za kifalme zilizo bora zaidi.

B. Pia kitabu hiki kinajulikana kama "Canticles (utunzi wa wimbo)" katika toleo la Kilatini. (*canticum canticoru*

II. URASIMISHAJI

A. Kwa sababu ya muktadha usio wa kawaida wa kitabu hiki hili linatenda kazi kwa ugumu katika kuifanikisha hadhi ya kisheria:

1. shule ya sheria za Kiyahudi ya Shammai (hifadhi) iliyokipinga kitabu
2. shule ya Kiyahudi ya (huru) iliyokiunga mkono kitabu hiki.
3. Katika baraza la Jamnia (90 B.K) bado kitabu kilikuwa kinaendelea kujadiliwa na kuibuliwa maswali kama ya kisheria.
4. Chini ya uongozi wa Rabbi Akiba (Aqiba) baadaye kilikubaliwa kama cha kisheria. Huyu alizungumza haya juu ya kitabu hiki, "kwa ulimwengu wote si kama wenye thamani kama siku ambayo Wimbo Ulio Bora ulitolewa kwa Israeli, kwa maandiko yote ni matakatifu, bali Wimbo Ulio Bora ni patakatifu pa patakatifu."

B. Hiki ni cha kwanza kati ya orodha ya vitabu maalumu kutokana na kipengele cha Maandiko ya sheria za Kiebrania ziitwazo *Megilloth* (magombo matano). Kila kimoja kilikuwa kikisomwa siku ya sikukuu ya mwaka. Kitabu cha Wimbo Ulio Bora kilikuwa kikisomwa wakati wa Sikukuu ya Pasaka:

1. Wimbo Ulio Bora – Pasaka
2. Ruthu – Pentekoste
3. Muhubiri – Vibanda au Mahema
4. Esta – Mavuno
5. Maombolezo – kwa ajili ya Yerusalemu na maangamizi ya Hekalu la Suleimani.

C. Kipengele cha Maandiko ya Kiebrania hakiwezi kukiweka Kitabu cha Wimbo Ulio Bora baada ya kitbu cha Zaburi, kitabu cha Mithali na Ayubu na kabla ya Ruthu, Maombolezo, Muhubiri na Esta. Toleo la Tafsiri ya Kingereza linaufuatisha mpangilio wa LXX.

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Aina ndilo jambo kuu katika ufasiri wa kitabu. Aina ni ya muhimu katika kulitambua kusudio asilia na makusudi ya mwandishi. Kitabu kinaandikwa katika namna ya ushairi.

B. Nadharia ni:

1. Stiari ya Kiyahudi - The Mishnah, Buku la Sheria za Kiyahudi na Targums, vyote vinakiri kwamba kitabu hiki kinaieleza historia ya katika maneno ya upendo wa Mungu kwa Israeli. Israeli ni bibi harusi wa YHWH (kama vile Kut. 34:15-16; Ufu. 17:7; 20:5-6 na Hes. 14:33).
2. Stiari ya Kikristo - Origen, Jerome, Athanasius, Augustine, Thomas Aquinas na Luther wote wanakiri kwamba kitabu hiki kinalieleza kanisa katika maneno ya upendo wa Kristo. Mara nyingi Efe. 5:21-31 inatolewa kama ufanano.
3. Nyimbo za Ndoa za Jadi – Kuna ufanano wenye kufikirika kati ya kitabu hiki na mashairi ya Shamu, yapata miaka 600 K.K., yajulikanayo kama *wasfs*. Bibi harusi na maneno ya kusifu kwa namna ya mabadiliko ya bwana harusi, kwa kuitana “mfalme" na "malkia." Pia kuna baadhi ya ufanano wa mashairi ya kimapenzi ya Kimisri ambapo apendwaye huitwa "dada" (4:9-10,12; 5:1-2). Aina hii ya kusifu kwa uaminifu, kwa wakati mwingine upendo wa mwanadamu ulijulikana vema katika Mashariki ya Karibu ya Kale.
4. Tamthiliya
   a. Kitabu hiki ni mchezo wa kuigiza wenye kupaswa kuigizwa na katika ya waigizaji kadhaa:
      (1) Mfalme,
      (2) msichana wa nchi ya kaskazini,
      (3) mpenzi mwenyeji wa kaskazini,
      (4) kiitikio au harimu ("binti za Yerusalemu").
   b. Mfano wa mkao wa uigizaji huu unaweza kuelezwa toka sura ya 1:
      (1) mist. 2-4b, bibi harusi
      (2) mst. 4c-e, kiitikio (kama vile 2:7; 3:6-11; 5:9; 6:1,13; 8:5,8)
      (3) mist. 5-7, bibi harusi
      (4) mst. 8, kiitikio
      (5) mist. 9-10, bwana harusi
      (6) mst. 11, kiitikio
      (7) mist. 12-14, bibi harusi
      (8) mst. 15, bwana harusi
      (9) mist. 16-17, bibi harusi
   c. Nadharia ya rafiki wa mvulana wa kaskazini inajikita katika:
      (1) mpenzi anaitwa mchungaji, azifuataye kondoo.
      (2) kitabu kinaishia kaskazini si Yerusalemu.
      (3) Harimu inakosolewa, 6:8-9.
   d. Machapisho ya Kiyunani *Sinaiticus* yana vichwa vya habari kwa kila kipengele chenye kuhusiana na bibi harusi na bwana harusi.
5. Fumbo – Nadharia hii inajaribu kuunganisha uhalisia na stiari. Hii inaichukulia kwa umakini furaha ya ujinsia wa mwanadamu na maana ya ndoa ya mke/mme mmoja. Bado hiki kinaonekana kuwa sababu ya kiubainishaji yenye kuhusiana na Israeli.
6. Uhalisia – Nadharia hii inavikiri vipengele vya ujimsia wa mwanadamu aliompa Mungu. Huu unakipeleka kitabu katika sura ya kuwa na uthamani. Mtazamo huu umetetewa na Theodore wa Mosuestia, mmoja wa mwana mwangaza mwenye ufahamu mkubwa wa shule ya ufasiri ya ki-Antiokia.

C. Kitabu hiki si fasihi halisi ya hekima, japo bado inaweza kutenda kazi katika namna ile ile, kuwafundisha vijana. Inaonekana kuwa na kipengele cha maadili chenye kuhusiana na ndoa ya

mke/mme mmoja na usafi na uzuri wa ujinsia wa mwanadamu kwa wakati ufaao, pamoja na mtu mwenye kufaa.

IV. UANDISHI

A. Baba Bathra 15a anasema kuwa Hezekia na watu wake walikiandika kitabu hiki. Kwa uwazi neno "waliandika" linamaanisha:kilichokusanywa au si kuandikwa (kama vile Mit. 25:1).

B. Mara nyingi desturi za Kiyahudi zimekuwa zikikiri kwamba Suilemani alikiandika kitabu hiki:
1. jina lake linajitokeza katika 1:1,5; 3:7, 9, 11; 8:11, 12.
2. hili jina "mfalme" linajitokeza katika 1:4, 12; 7:5.
3. Farasi wa Kimisri wanatajwa katika 1:9 ambapo wanaendana na utawala wa Suleimani (kama vile I Fal. 10:28).
4. mwandishi anayataja maeneo ya kijiografia Palestina, Shamu na maeneo yote ya nga'mbo ya Yordani hata chini ya Araba. Hili linaiakisi mipaka ya kijiografia ya utawala wa Suleimani.
5. Walimu wa sheria za Kiyahudi wanasema kwamba Suleimani alikuwa kijana alipoziandika nyimbo hizi za mapenzi (Wimbo Ulio Bora), wakati alipokuwa kijana alipoziandika mithali (Mithali) na wakati alipokuwa mzee aliuandika wasifu wa vitu vyote( Muhubiri).

C. Baadhi ya sababu za kuupinga uandishi wa Suleimani:
1. Jina la kitabu katika Kiebrania, "Wimbo Ulio Bora wa Suleimani" linaweza kumaanisha:
   a. na Suleimani,
   b. kwa Suleimani,
   c. kuhusu Suleimani,
   d. katika siku zile za Suleimani,
   e. katika tabia ya Suleimani.
2. kitabu kinaishia kaskazini mwa Israeli (7:10-13) na si katika harimu ya humo Yerusalemu.
3. Kitabu hiki kinaonekana kuukiri wema, ukamilifu na furaha ya ndoa ya mke/mme moja. Hili halikidhi maisha ya Suleimani.
4. Kifasihi Suleimani anaweza kuwa bora kuhusiana na kitabu cha Wimbo Ulio Bora kama alivyo katika Muhubiri 1-2 (E. J. Young, *An Introduction to the Old Testament*, uk. 268).

V. TAREHE

A. Kama vilivyo vitabu vingi vya hekima vya Agano la Kale kuna vipengele viwili vya sasa:
1. mazingira halisi ya kihistoria,
2. tarehe na muundo wa kitabu kama inavyojitokeza katika sheria.

B. Mazingira ya kihistoria:
1. Siku zile za Suleimani:
   a. mamlaka ya mfalme kuchukua wake wengi,
   b. kuwepo kwa harimu kama kiitikio,
   c. ujuzi wa upana wa tofauti za maeneo ya kijiografia (pamoja na wanyama na mimea).
   d. Yerusalemu inafananishwa na Tirza, eneo ambalo lilikuwa makao makuu ya Israeli kabla ya Samaria (Omri), 6:4.
2. muundo wa mwisho wa kitabu:

a. muundo wa kiambata husianishi cha jinsi ya kike ni Kiebrania cha hapo awali (kama vile 1:12; 2:7)

b. matumizi ya maneno ya mkopo ya lugha ya Kiaramu

(1) paradiso

(2) kiunga

(3) kitanda

(4) kochi

C. Kutokubaliana kwa wanazuoni wa sasa:

1. J. Young—siku zile za Suleimani
2. W. F. Albright—karne ya tano-ya nne B.K.
3. R. K. Harrison—muundo wa mwisho wa papo kwa papo kabla ya uhamisho

VI. VIPENGELE VYA KIFASIHI

A. Kuna vipengele kadhaa vya kitabu vilivyo vigumu. Mtu anashangaa ikiwa kuna dhamira ambayo hazijaunganishwa au sababu au mtiririko wa mashairi ya mapenzi.

B. Mistari ifuatayo ni ngumu kuifasiri katika mwangaza wa dhamira iliyounganishwa:

1. 2:15
2. 5:7
3. 8:5b-e
4. 8:8-9

C. Njia pekee ya kufasiri kitabu pamoja na dhamira iliyounganishwa ni kutoa madhaanio ya hali ya uigizaji wa watu watatu na kiitikio:

1. mfalme
2. msichana wa nchi ya kaskazini
3. mpenzi wa nchi ya kaskazini
4. harimu kama kitikio

D. Kitabu hiki, kama Esta, hakina lina jina lo lote la Mungu (8:6 inatafsiri kama "miali ya Yahu" katika *Jewish Publications Society of America's translation*).

VII. KWELI KUU

A. Kwa uwazi huu ni ukiri wa usafi na uzuri wa ujinsia wa mwanadamu, 8:6-7. Huu unaweza kuonekana kuwa ukiri dhahiri lakini katika mwanga wa: (1) Dhambi ya Daudi ya uzinzi na matokeo yake ndani ya nyumba yake, na (2) Suleimani kuabudu sanamu uzeeni mwake kwa sababu ya wake zake wa kigeni na dini zao, huu ulikuwa usemi wenye kuhitajika.

Katika mwangaza wa uwili wa dini ya Kiyahudi hakika kweli hii ndiyo inayohitajika sasa. Kiroho hili haliamrishi hali ya kujinyima anasa! Mwili si dhambi katika asili yake.

B. Wengi wamekiona kitabu hiki katika mwangaza wa ufanano wa Agano la Kale wa Mungu kama mume na Israeli kama mke (yaani, fasiri za sheria za dini ya Kiyahudi za kitabu cha Kutoka na Hosea 1-3).

C. Ugumu katika kuzibaini aina zote na sababu za visababishi vikuu humsababisha mtu kuwa makini na fasiri za mfumo fulani wa imani.

D. Kitabu hiki hakina dondoo za kidini au dhamira ya kitaifa. Hili si la kawaida kwa kitabu cha kisheria.

VIII. MANENO/WATU WA KUWATAMBUA KIMUHTASARI


A. Maneno/Kifungu
1. manemane 1:13; 3:6; 4:6,14; 5:1,5,13 (NASB na NIV)
2. "mbweha wadogo," 2:15 (NASB na NIV)
3. "hofu ya kamsa za usiku," 3:8 (NASB na NIV)
4. "malkia... masuria," 6:8,9 (NASB na NIV)
5. Mitunguja, 7:13 (NASB na NIV)
6. muhuri, 8:6 (NASB na NIV)
7. akiwa ni mlango, 8:9 (4:12) (NASB na NIV)


B. Watu
1. "mfalme," 1:4b, 12
2. "Mimi ni mweusi-mweusi," 1:5 (NIV, “Mi mweusi, bado napendeka”)
3. "Ni wapi utakapolisha kundi lako...," 1:7 (NIV, “...malisho...”)
4. "Mimi ni ua la uwandani, Ni nyinyoro ya mabondeni," 2:1
5. "binti za Yerusalemu" 2:7
6. Walinzi, 3:3; 5:7
7. "Mshulami," 6:13

IX. MAENEO YA KI-RAMANI
1. Engedi, 1:14
2. Sharoni, 2:1
3. Lebanoni, 4:8
4. Ml. Hermoni, 4:8
5. Tirzah, 6:4
6. Gileadi, 6:5 (Ml. Gileadi, 4:1)
7. Dameski, 7:4
8. Ml. Karmeli, 7:5

X. MASWALI YA KIMAUDHUI KWA MWANAFUNZI

1. Kwa nini kitabu hiki kiko katika sheria?
2. Ni fasiri gani ya kitabu hiki inayotawala kwa Wayahudi wenyewe? na kwa nini?
3. Hii ni aina gani ya fasihi? Kwa nini hiki kinatengeneza utofauti?
4. Kwa nini jina la Mungu au historia ya Israeli haikudokezwa kamwe katika kitabu?
5. Je! kitabu kina dhima unganishi?
6. “binti za Yerusalemu" ni akina nani?
7. Orodhesha maeneo tofauti tofauti ambayo simulizi hizi zilitokea.


MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE
KAS
MAGH
MASH
KUS


PALESTINA
0 10 20 30 40
VIPIMO KATIKA MAILI

# UTANGULIZI WA UNABII WA AGANO LA KALE

I. UTANGULIZI

A. Kauli ya ufunguzi:

1. Jamii ya waaminio haikubaliani juu ya namna ya utafsiri wa unabii. Ukweli mwingine umewekwa kulingana na nafasi ya mafundisho ya kiyahudi katika karne zote lakini sio hii.
2. Kuna hatua kadhaa zilizowekwa vizuri za unabii wa Agano la Kale :
   a. kipindi kabla ya utawala wa wafalme:
      (1) mtu moja mmoja waitwao manabii
         (a) Ibrahimu - Mwa. 20:7
         (b) Musa - Hes. 12:6-8; Kumb. 18:15; 34:10
         (c) Haruni – Kut. 7:1 (mzungumzaji wa Musa)
         (d) Miriam – Kut. 15:20
         (e) Medadi na Eldadi - Hes. 11:24-30
         (f) Debora - Waamuzi 4:4
         (g) wasiotajwa - Waamuzi 6:7-10
         (h) Samweli- 1 Sam. 3:20
      (2) rejea kwa manabii kama kundi - Kumb. 13:1-5; 18:20-22
      (3) kundi la kinabii au wafua vyuma - 1 Sam. 10:5-13; 19:20; 1 Wafalme 20:35,41; 22:6,10-13; 2 Wafalme 2:3,7; 4:1,38; 5:22; 6:1, n.k.
      (4) Masihi aitwaye nabii - Kumb. 18:15-18

   b. ufalme usioandikwa (zikizungumzia mfalme):
      (1) Gadi - 1 Sam. 22:5; 2 Sam. 24:11; 1 Nyak. 29:29
      (2) Nathani - 2 Sam. 7:2; 12:25; 1 Wafalme. 1:22
      (3) Ahija – 1 Wafalme 11:29
      (4) Yehu – 1 Wafalme 16:1,7,12
      (5) Asiyetajwa jina – 1 Wafalme 18:4,13; 20:13,22
      (6) Eliya – 1 Wafalme 18-2 Wafalme 2
      (7) Mikaya – 1 Wafalme 22
      (8) Elisha – 2 Wafalme 2:8,13

   c. manabii walioandika nyakati za zamani (wakizungumzia taifa pamoja na mfalme): - Isaya - Malaki (isipokuwa Danieli)

B. Maneno ya Kibiblia

1. *Ro'eh* = "mwonaji," 1 Sam. 9:9. Rejea hii yenyewe inaonesha mapito kwenda kwenye neno *Nabi*. *Ro'eh* kutoka neno la jumla "kuona." Mtu huyu alielewa njia za Mungu na mipango aliulizwa kuyatafuta mapenzi ya Mungu katika mambo.
2. *Hozeh* = "mwonaji," 2 Sam. 24:11. Ni msingi wa kisawe cha *Ro'eh*. Ni neno nadra "kuona." Muundo shiriki unatumika zaidi mara kwa mara kurejerea manabii.
3. *Nabi'* = "nabii," neno sawa kabisa la kitenzi cha Akkadia *Nabu* = "kuita" na Kiarabu *Naba'a*= "kutangaza." Hili ni neno la kawaida katika Agano la Kale kumuelezea nabii. Limetumika mara 300. Asili yake hakika haijulikani lakini "kuita" kwa wakati huu inaonekana kuwa uchaguzi sahihi. Yawezekana uelewa bora zaidi unatoka kwa maelezo ya YHWH juu ya mahusiano ya Musa na Farao kupitia Haruni (kama vile Kut. 4:10-16; 7:1; Kumb. 5:5. Nabii ni mtu anayezungumza na Mungu kwa niaba ya watu wake (Amosi 3:8; Yer. 1:7, 17; Ezek. 3:4.
4. Maneno yote matatu yanatumika katika ofisi ya nabii katika 1 Nyak. 29:29; Samweli - *Ro'eh*; Nathani - *Nabi'* na Gadi - *Hozeh.*
5. Tungo, *'ish ha- 'elohim*, "Mtu wa Mungu," pia ni maelezo mapana kwa ajili ya mzungumzaji wa Mungu. Linatumika kama mara 76 katika Agano la Kale kwa namna ya "nabii."

6. Neno "nabii" ni la Kiyunani kwa asili. Linatoka katika: (1) pro = "kabla" au "kwa ajili ya"; (2) phemi = "kuzungumza."

II. MAANA YA UNABII

A. Neno "unabii" lina uwanja mpana wa kimaana katika Kiebrania kuliko katika Kingereza. Vitabu vya historia vya Yoshua mpaka Wafalme (isipokuwa Ruthu) wanatajwa na Wayahudi kama "manabii wa kale." Wote wawili Ibrahimu (Mwa. 20:7; Zab. 105:5) na Musa (Kumb. 18:18) wanatajwa kama manabii (pia Miriamu, Kut. 15:20). Hivyo kuwa makini na maana ya kudhaniwa ya Kingereza!

B. “Nadharia ya unabii” kisheria na kiuhalali inaweza ikapewa maana kama ule uelewa wa historia ambao unakubali maana tu kwa namna ya kuangalia hali ya ki-Mungu, kusudi la ki-Mungu, ushiriki wa ki-Mungu," *Interpreter's Dictionary of the Bible*, vol. 3, ukur. 896.

C. "Nabii sio aidha mwanafalsafa wala mwanathiolojia wa kimfumo, bali mpatanishi wa kiagano anayefikisha neno la Mungu kwa Watu wake ili aiandae baadaye yao kwa kufanya mageuzi kwenye leo yao “Manabii na Unabii*”," Encyclopedia Judaicavol*. 13 ukur. 1152.

III. KUSUDI LA UNABII

A. Unabii ni njia ya Mungu ya kuzungumza na watu wake, kutoa miongozo katika mazingira yao ya sasa na tumaini na kushughulikia maisha yao na matukio ya kiulimwengu. Ujumbe wao kimsingi ni wa kijamii kwa pamoja. Umekusudiwa kukemea, kutia moyo, kutia moyo imani na toba na kutoa taarifa kwa watu wa Mungu kumuhusu Mungu mwenyewe na mipango Yake. Kwa hili lazima iongezwe kwamba mara kwa mara inatumika kiuwazi kufunua uchaguzi wa Mungu wa msemaji (Kumb. 13:1-3; 18:20-22). Hili lazima lichukuliwe katika kilele ingemaanisha Masihi.

B. Mara kwa mara nabii alichukua mgogoro wa kihistoria au kithiolojia wa siku zake na kuuangaza katika mazingira ya siku za mwisho. Mtizamo huu wa nyakati za mwisho wa kihistoria ni wa pekee katika Israeli na namna yake ya uchaguzi wa Ki-Mungu na ahadi za Agano.

C. Ofisi ya nabii inaonekana kuwa katika uwiano (Yer. 18:18) na kuchukua ofisi ya Kuhani Mkuu kama njia ya kujua mapenzi ya Mungu. Ile Urimu na Thummimu ina badilika kuja kwenye ujumbe wa kinywa. Ofisi ya nabii inaonekana pia kupitwa katika Israeli baada ya Malaki. Haitokei tena mpaka miaka 400 baadaye anakuja Yohana Mbatizaji. Haijulikani namna gani kipawa cha Agano Jipya cha "unabii" kinavyohusiana na Agano la Kale. Manabii wa Agano Jipya (Mdo. 11:27-28; 13:1; 14:29,32,37; 15:32; 1 Kor. 12:10,28-29; Efe. 4:11) sio wafunuaji wa ufunuo mpya juu ya maandiko bali wasemaji wa mambo ya mbele juu ya mapenzi ya Mungu katika hali ya Agano.

D. Unabii sio ujumuishi au kimsingi utabiri kwa asili. Utabiri ni moja ya njia ya kuthibitisha ofisi yake na ujumbe wake lakini lazima ieleweke “chini ya 2% ya unabii wa Agano la Kale ni juu ya Masihi. Chini ya 5% hasa inaelezea nyakati za Agano Jipya. Chini ya 1% inahusu matukio ambayo bado hayajatokea.” (Fee & Stuart, *How to Read the Bible For All Its Worth*, ukur. 166.

E. Manabii wanamwakilisha Mungu kwa watu wakati Makuhani wanawawakilisha watu kwa Mungu. Hii ni kauli ya jumla. Kuna upekee kama wa Habakuki, anayemkaribia Mungu kwa maswali.

F. Moja ya sababu ya ugumu wa kuelewa manabii ni kwasababu hatujui namna gani vitabu vyao viliundwa. Haviko katika mpangilio. Vinaonekana kuwa vya kimaudhui lakini siku zote si kama mtu ambavyo angetegemea. Mara kwa mara hakuna mazingira ya udhahiri ya kihistoria, muda uliotengwa au mgawanyo wa wazi kati ya unabii. Vitabu hivi ni vigumu: (1) kusoma kwa mkao mmoja; (2) kuainisha kwa mada; na (3) kutambua ukweli mkuu au kusudio la uandishi katika kila unabii.

IV. TABIA ZA UNABII

A. Katika Agano la Kale kunaonekana kuwa na maendeleo ya dhana ya "nabii" na "unabii." Karibia Israeli kumekuwa ushirika wa manabii, ukiongozwa na kiongozi mwenye nguvu mwenye ushawishi kama vile Eliya au Elisha. Wakati mwingine tungo, "wana wa manabii" ilitumika kuelezea kundi hili (2 Wafalme 2). Manabii walikuwa na tabia kwa miundo ya shauku (1 Sam. 10:10-13; 19:18-24).

B. Hatahivyo kipindi hiki kilipita kwa kasi kwa nabii mmoja mmoja. Kulikuwa na hao manabii (wote wawili wa kweli na wasio wa kweli) waliotambulikana pamoja na Mfalme na kuishi katika jumba la Kifalme (Gadi, Nathani). Pia kulikuwa na wale waliokuwa wakijitegemea, wakati mwingine wakiwa hawajaunganishwa kikamilifu na hadhi ya jamii ya ki-Israeli (Amosi). Walikuwa wote wawili, wa kike na wa kiume (2 Wafalme 22:14.)

C. Nabii mara kwa mara alikuwa mfunuaji wa siku za mbele, zilizotegemea mwitikio wa haraka wa mwanadamu. Mara kwa mara jukumu la nabii lilikuwa kufumbua mpango wa Mungu wa kiulimwengu kwa ajili ya uumbaji wake ambao hauathiriwi na mwitikio wa mwanadamu. Mpango huu wa kiulimwengu ni wa pekee kati ya manabii wa Mashariki ya Kale ya Karibu. Utabiri na uaminifu wa kiagano ni mapacha wa ujumbe wa kinabii (kama vile Fee na Stuart, ukur. 150). Hii inamaanisha kwamba manabii kimsingi ni wa kijamii katika shabaha yao. Wao siku zote japo sio kwa ujumuishi huzungumzia taifa.

D. Nyaraka za kinabii zaidi ziliwasilishwa kwa njia ya mdomo. Baadaye iliunganishwa kwa namna ya maudhui, mpangilio au utaratibu mwingine wa Mashariki ya Karibu ya Kale ambao umepotea kwetu. Kwasababu ilikuwa kwa njia ya mdomo, haijaundwa kama riwaya za kuandikwa. Hii inafanya vitabu kuwa vigumu kusoma moja kwa moja na ngumu kuelewa bila mazingira hasa ya kihistoria.

E. Manabii wanatumia utaratibu kadhaa kufikisha ujumbe wao:
   1. Mazingira ya Kimahakama- Mungu anachukua watu wake kortini, mara kwa mara ni kesi ya talaka ambapo YHWH anamkataa mkewe (Israeli) kwa kukosa kwake uaminifu (Hosea 4; Mika 6).
   2. Nyimbo za misiba - kipimo maalumu cha aina hii ya ujumbe na tabia yake ni "ole" inaifanya kuwa ya kipekee kama muundo maalumu (Isaya 5; Habakuki 2).
   3. Utamkwaji wa Baraka za Kiagano- asili ya kimasharti ya asili ya agano inasisitizwa na matokeo, vyote viwili vizuri na vibaya, vinatamkwa kwa ajili ya wakati ujao (Kumb. 27-28).

V. SIFA ZA KIBIBLIA KWA AJILI YA UTHIBITISHAJI WA NABII WA KWELI

A. Kumbu kumbu la Torati 13:1-5 (utabiri/ishara)
B. Kumbu kumbu la Torati 18:9-22 (manabii wa uong/manabii wa kweli)
C. Mathayo 7 (mtindo wa maisha)
D. 1 Yohana 4:1-6 (shabaha ya kimafundisho)
E. Wote wanaume na wanawake wanaitwa na kuelezwa kama manabii au manabii wa kike
   1. Miriam – Kut. 15
   2. Debora - Waamuzi. 4:4-6
   3. Hulda – 2 Wafalme 22:14-20; 2 Nyak. 34:22-28
F. Katika desturi zilizozunguka manabii walithibitishwa kwa namna ya ubashiri. Katika Israeli ilikuwa:
   1. jaribu la kithiolojia – jina la YHWH
   2. jaribu la kihistoria - utabiri wa uhakika.

VI. MIONGOZO YA ZIADA KWA AJILI YA UFASIRI WA UNABII

A. Tafuta kusudio la asili ya nabii (mhariri) kwa kuzingatia mazingira ya kihistoria na muktadha wa kifasihi wa kila unabii. Siku zote itajumuisha Israeli kuvunja Agano la Musa kwa namna fulani.

B. Soma na fasiri unabii mzima, sio tu sehemu; ainisha kama maudhui. Angalia namna inavyohusiana na unabii mwingine uliopo.

C. Chukulia ufasiri wa kibayana wa ujumbe mpaka kitu katika andiko lenyewe kimejiweka wazi kwako kutoka katika matumizi ya sitiari ya kimafumbo; alafu weka lugha ya kimafumbo katika riwaya .

D. Ainisha tendo la kiuwakilishi kwa mwanga wa mazingira ya kihistoria na kifungu kinachofanana. Kumbuka kuzingatia hili la fasihi ya Mashariki ya Karibu ya Kale si ya kimagharibi wala fasihi ya kisasa.

E. Uuchukue unabii kwa uangalifu:
   1. Je umekusudiwa kwa wakati wa mwandishi pekee?
   2. Je ulitimizwa katika historia ya Israeli?
   3. Je tayari umeshakuwa matukio ya wakati ujao?
   4. Je una utimilizwaji wa kisasa na unangoja utimilizwaji wa baadaye?
   5. Ruhusu waandishi wa Biblia, si waandishi wa kisasa, kuongoza majibu yako.

F. Vitu vya kuzingatia
   1. Je unabii unasifa kwa mwitikio wa kimasharti?
   2. Ni hakika kwa Yule ambaye unabii unaelekezwa (na kwanini)?
   3. Je kuna uwezekano wa utimilizwaji wote wa aina mbili au zaidi wa, Kibiblia na/au kihistoria?
   4. Mwandishi wa Agano Jipya chini ya uvuvio alikuwa na uwezo wa kuona Masihi katika maeneo mengi katika Agano la Kale ambayo hayako wazi kwetu. Wanaonekana kutumia uanishi au mbinu za maneno. Kwakuwa hatuvuviwi, ni bora kuacha mbinu kwao.

VII. VITABU VYA ZIADA


A. *A Guide to Biblical Prophecy* cha Carl E. Armerding na W. Ward Gasque
B. *How to Read the Bible for All It Is Worth* cha Gordon Fee na Douglas Stuart
C. *My Servants the Prophets* cha Edward J. Young
D. *The Expositor's Bible Commentary*, vol. 6 "Isaiah - Ezekiel," Zondervan
E. *The Prophecies of Isaiah* cha J. A. Alexander, 1976, Zondervan
F. *Exposition of Isaiah* cha H. C. Leupold, 1971, Baker
G. *A Study Guide Commentary*, "Isaiah" cha D. David Garl na, 1978, Zondervan

# UTANGULIZI WA ISAYA

I. KAULI YA UFUNGUZI

A. Isaya inanukuliwa mara kwa mara zaidi katika Agano Jipya kuliko nabii mwingine yoyote (zaidi ya mara 411). Ujumbe wake ulikuwa mmoja wa:
   1. Mungu mmoja,
   2. ulimwengu mmoja,
   3. imani moja.

B. Isaya ni kitabu cha kupendeza sana cha ki-Masihi:
   1. wana maalum, sura za 7-14,
   2. wimbo wa Mtumwa, sura za 42:1-9; 49:1-7; 50:4-11; 52:13-53:12,
   3. ufalme wa baadaye wa kimasihi (Nyakati mpya), sura za 56-66

C. E. J. Young, katika *An Introduction to the Old Testament*, amesema:
   1. "Kitabu cha Isaya kinachukuliwa vizuri zaidi kama kitabu cha unabii kuliko vyote vya Agano la Kale" ukur. 168.
   2. "Katika manabii wote wa Israeli, Isaya alielewa kwa ukamilifu zaidi nia ya Mungu na mpango Wake kwa nyakati" ukur. 171
   3. "Katika ufahamu wa kiroho hapingwi katika Agano la Kale lote" ukur. 172

II. JINA LA KITABU

A. Kitabu kinapewa jina kwa jina la mzungumzaji wake wa kinabii.

B. Jina linamaanisha "wokovu wa YHWH" au "YHWH anaokoa." Majina ya Kiebrania ambayo yanaishia na "iah" ni kifupisho cha YHWH, kama ilivyo kwa majina ambayo yanaanza katika Kingereza na herufi "j" na irabu, mfano ni Joshua na Joel.

III. URASIMISHAJI

A. Hiki ni cha kwanza kati ya magombo manne ya manabii wa mwisho:
   1. Isaya
   2. Yeremia
   3. Ezekieli
   4. Kumi na Mbili (manabii wadogo)

B. Kilikubalika mwanzoni na kiukamilifu katika maandiko ya unabii ya waisraeli.

IV. AINA YA UWASILISHAJI

A. Ujuzi wa kifasihi wa Isaya unapita manabii waote wa Agano la Kale. Mbinu zake za maneno na ushairi ni wa kushangaza na wa kuvutia sana. Kitabu sehemu kubwa sana ni ushairi.

B. Ni ngumu kukaa chini na kusoma kitabu cha Isaya chote kwa wakati mmoja. Ni ngumu kuainisha kitabu. Hii ni kwasababu Isaya alikuwa ni muhubiri na si mwandishi au mhariri. Kitabu chake kinaandika jumbe za kuzungumzwa. Zinaunganishwa kwa pamoja, wakati mwingine:
   1. kwa maudhui,
   2. kwa mpangilio,
   3. kwa taratibu za kidesturi za Mashariki ya Karibu ya Kale ambazo ni tofauti na zile za kwetu.

V. UANDISHI

A. Mtazamo wa kiyahudi wa uandishi

1. Ile Talmud Baba Bathra 15a alisema Hezekia na watu wake waliandika (yaani walihariri au walitunga) Isaya, Mithali, Muhubiri na Wimbo ulio bora. Hii inamaaanisha kitabu kizima kinatoka kwa nabii.
2. BenSirah, katika "Ecclesiasticus 49:17-25, kilichoandikwa mnamo mwaka 185 K.K., alisema, "Isaya, mwana wa Amozi," ndiye aliyeandika kitabu (1:1; 12:1; 13:1).
3. 2 Nyakati 32:32 kinashuhudia maono ya Isaya na ufanano katika Wafalme (2 Wafalme. 18:19-20:19.)
    a. Kutoka katika familia tajiri katika Yerusalemu, yawezekana hata binamu wa Mfalme Uzia.
        (1) Baadhi ya ushahidi kwamba "iah,"ni kifupisho cha YHWH, ulifanywa karibia bila ujumuishi kati ya waheshimiwa wa Yuda.
        (2) Isaya kumfikia mfalme pia kunatoa msaada kwa uwezekano wake wa kuwa na muunganiko wa kifamilia.
        (3) Kama vile Talmud, "Meg." 10b
    b. alioa nabii wa kike (8:3)
        (1) mtoto wa kiume wa kwanza, "Shear-Jashub," ambayo inamaanisha "mabaki yatarejea"
        (2) mwana wa kiume wa pili, "Maher-Shalal-Hash-Baz" (8:3) ambayo inamaanisha "haraka haraka, haina baraka"
    c. Isaya alikuwa na huduma ndefu zaidi za kinabii kati ya manabii wote. Alikuwa mzungumzaji wa Mungu katika Yuda tokea utawala wa Yotham (742-735 K.K.) mpaka ule wa Hezekia (715-687 K.K.) pamoja na uwezekano wa kwenda mpaka utawala wa Manase (687-642 K.K.); Manase anawezekana akawa alikuwa mshauri tokea mwaka 696 K.K.
    d. ikiwa 2 Nyak. 26:22 inarejerea kwa Isaya basi alikuwa mwandishi rasmi na mtunzaji wa nyaraka za kiofisi za mfalme.
    e. desturi zinasema alichinjwa kwa msumeno katika vipande viwili wakati wa utawala wa Manase.
4. Moses benSamuel Ibn Gekatilla, mnamo mwaka 110 B.K, alisema kwamba sura za 1-39 ni za Isaya lakini sura za 40-66 ziliandikwa wakati wakipindi cha Hekalu la Pili (Kipindi cha Uajemi, 538-430 K.K.)
5. Ibn Ezra (1092-1167 B.K) kufuatia uongozi wa Gekatilla alikataa sura za 40-66 kuwa za Isaya.

B. Mtazamo wa kiuanazuoni wa kisasa juu ya uandishi
1. muhtasari mzuri wa kisasa unapatikana katika R. K. *Harrison's Introduction to the Old Testament*, Eerdmans, 1969.
2. Mjadala mzuri wa sababu za kiufundi kwa kuelezea waandishi wawili unaweza kupatikana katika S. R. *Drivers' Introduction to the Literature of the Old Testament*, reprint 1972.
3. Hakuna maandiko ya Kiebrania au Kiyunani (LXX) ambayo yamekwisha kupatikana ambayo yanaonesha mgawanyiko katika sura za 1-39 na 40-66.
    a. Kuna nafasi ya mistari miwili mwishoni mwa sura ya 33 katika Magombo ya Bahari ya Chumvi. Hii inamaanisha mgawanyiko katika hatua hii, sio sura ya 39.
    b. Kunaonekana kuwa na muundo wa kimfanano kati ya 1-33 na 34-66. Muundo huu wa aina mbili umejikita katika siku za mwandishi mwenyewe na baadaye, ulikuwa umezoeleka kwa manabii wa Kiebrania (kama vile Ezekieli, Danieli na Zekaria).
4. Uanazuoni wa kisasa hauna ukubaliano kama kwa namna gani waandishi wengi au wapi pa kugawa kitabu.

C. Baadhi ya sababu kwa umoja wa Isaya
1. Maneno ishirini na tano yanapatikana katika sehemu zote mbili za Isaya pasipokupatikana sehemu nyingine yoyote ile katika Agano la Kale (NIV, *Intro. to Isaiah*, ukur. 1014).
2. Jina "Mtakatifu wa Israeli" linatokea mara 13 katika sura za 1-39 na mara 14 katika sura za 40-66 na mara sitini na sita tu katika vitabu vingine vya Agano la Kale.

3. Yesu, katika Yohana 12:38, 40, ananukuu kutoka katika vyote Isa. 53:1 na 6:10 na kuvipa sifa za Isaya.
4. Vifungu kutoka Isa. 40-66 vinapewa sifa za Isaya katika Mt. 3:3; 8:17; 12:17;Lk. 3:4; 4:17;Yn. 1:23; Mdo. 8:28 na Rum. 10:16-20
5. Hakuna ushahidi wa kimaandiko wa ugawanywaji wa kitabu katika sura ya 39 (MT or DSS).
6. Hakuna Historia ya kutajwa ya nabii mkubwa (Diedre-Isaiah) katika karne ya 6. R. K. Harrison, katika *Introduction to the Old Testament,* anaongeza juu ya somo hili,

    "Hoja kutoka muundo wa kifasihi zilikuwa tupu mwishoni mwa karne ya kumi na tisa lakini kwa ufahamu mpana wa maarifa ya lugha za Mashariki ya Karibu ya Kale sasa wamedhania nafasi kubwa yenye umuhimu kidogo. Somo lenyewe la uzingativu wa miundo lilikuwa na mvuto mkubwa kwa washirika wa nadharia ya Graf-Wellhausen ya uanishaji wa kifasihi, ambaye anasema hapa kwa hali ya kutofanana juu ya namna ya kupitia nyaraka zinazohusianishwa na mwandishi wa kibiblia na pia kukataa sehemu za kiwango chake kwasababu ya muundo wa kifasihi na misamiati ya kila sura kutokuwa na mfanano. Inavyoonekana haikutokea kwa wale wachunguzi wa mwanzo kwamba ilikuwa tu inawezekana kugeuza baadhi ya dhana za mtindo wa mwandishi wa kale kutokana na usomaji makini wa nyaraka zote anazopewa, na kwamba kukataliwa kwa sehemu au kwa kiasi kile kungeweza kupitishwa kwa msingi wa baadhi ya mazingira au masharti magumu ya nje." ukur. 776

D. Baadhi ya sababu za uandishi zaidi ya moja wa Isaya.
1. Katika sura za 40-66 jina "Isaya" halitajwi.
2. Sura za 40-66 hazishabihiani na mazingira ya kihistoria ya Isaya.
3. Kunaonekana kuwepo kwa kuchanganya kwa rejea za Isaya na:
    a. uvamizi wa Ashuru, uhamisho na hukumu yao
    b. Uvamizi wa Babeli, uhamisho na hukumu yao.
4. Kwa dhahiri kuna baadhi ya sababu kwa kuwepo kwa nadharia wa waandishi zaidi ya mmoja:
    a. kubadilika kwa mazingira ya kihistoria
        (1) uvamizi wa kabla wa Yuda, 1-39
        (2) uhamisho, 40-55
        (3) baada ya uhamisho wa Yuda, 56-66
        (4) Katika Isaya 1-39 Hekalu halitaweza kamwe kuanguka wakati katika 40-66 ni dhahiri limeanguka. Mwandishi anaonekana kuwa uhamishoni.
    b. kubadilika kwa maneno kunaelezea kuchagua kwa Mungu:
        (1) mwana wa ki-Masihi
        (2) Mtumwa atesekaye
        (3) Israeli kama:
            (a) mke (50:1)
            (b) watumishi wa YHWH (54:17)
5. Wanazuoni wenye msimamo wa Kisasa:
    a. Kauli ya E.J.Young juu ya sura za 56-66 ni ya msaada, "uwezekano mwingine ni kwamba unabii wenye kujaa Roho na uliokusanywa na mhariri kutoka kwa manabii tofauti tofauti wa shule ya Isaya juu ya maudhui ya msingi ya sehemu hii." Ukur. 188
    b. Kauli ya G.R. K. Harrison, "Mwandishi wa sasa anashikilia mtazamo kwamba Isaya kama wengi wao wenye maandiko ya kinabii, anawakilisha mtiririko wa kauli zilizotolewa wakati tofauti na kwa kazi hizo hazibebi hadhi tofauti na zile ambazo zilitolewa kama unabii mwingine wa Agano la Kale. Kwa muunganiko huu ni muhimu kukumbuka kwamba hoja inayojikita juu ya utofauti wa mtindo wa kifasihi unachukuliwa mara moja kwa mjongeo huu wa mwandishi juu ya vipindi tofauti vya shughuli za ubunifu wake. Uhalalishaji kwa uelezeaji wa kazi kama mkusanyo kwa namna bora zaidi ya neno hili unanogeshwa na ufunguzi wa mstari wa unabii ambao unajumuisha kichwa cha kazi na kuzungumza hasa

juu ya nyaraka za ufunuo kwamba Isaya mwana wa Amozi alipokea katika maono juu ya Yuda na Yerusalemu siku za Uzia, Yotham, Ahazi na Hezekia. Kama ilivyo kwa makusanyo mengine ni wazi wa kiushahidi kwamba kitabu kinajumuisha tu uchaguzi wa unabii unaopatikana na mahubiri, na kuna uwezekano mkubwa zaidi kwamba Isaya alizalisha nyaraka zaidi kuliko zilizowekwa katika kitabu chake. Asili ya unabii kama makusanyo inaelezewa zaidi na uwepo wa vielelezo katika Isa. 2:1 na 13:1, ambavyo vinaweza kuwa viliwakilisha au kuashiria uwepo wa, makusanyo ya mwanzo ya unabii wa kuzungumzwa." Ukur. 780

6. muundo wa kifasihi wa sura za 40-66 ni tofauti na sura za 1-39.

E. Maoni ya kuhitimisha ju ya uandishi
   1. Wanazuoni wacha Mungu wanaendelea kukataa juu ya namna kitabu chetu cha Agano la Kale cha Isaya kilitokea na kuwa na muundo wake wa sasa (kama vile DSS na MT). Msisitizo wake mkuu lazima uwekwe juu ya uvuvio na uaminifu wake katika kufunua sifa na makusudi ya YHWH.
   2. Lazima tukatae madhanio ya kwanza ambayo yanakataa ufunuo wa uaminifu wa Mungu. Hii pia inajumuisha kukataa mwanzoni kabisa kwa unabii wa utabiri na ushushwaji wa Agano la Kale kuwa masimulizi ya kibinadamu, ya kihistoria ya maisha ya kawaida.

VI. TAREHE

A. Isaya ni sehemu ya manabii wa karne ya nane
   1. Yona, Amosi, na Hosea huko kaskazini, wakati wa utawala wa Yeroboamu II (786-640 K.K.)
   2. Isaya na Mika huko kusini

B. Alizaliwa mnamo mwaka 760 K.K. na aliitwa kutumika katika nafasi ya unabii mnamo mwaka 742 K.K. wakati Uzia alipokufa (6:1). Uzia pia anaitwa Azaria (783-742 K.K.).

C. Isaya alikuwa na huduma ndefu kutokea kufungwa kwa miaka ya Uzia (783-742 K.K.) mpaka Yotham (742-735 K.K.), Ahazi (735-715 K.K.), Hezekia (715-687 K.K.) na yawezekana Manase (687-642 K.K.).

D. R. K Harrison anasema kwamba kitabu ni makusanyo ya maandiko ya nabii na mahubiri kwa miaka mingi kupia utawala wa wafalme wa Yudea. Hatimaye kilihitimishwa na kuhaririwa baada ya kifo cha nabii, mnamo mwaka 630 K.K.

VII. MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. Manabii wa Karne ya Nane
   1. Nyaraka za kibiblia zinapatikana katika:
      a. 2 Wafalme 14:3-17:6
      b. 2 Nyak. 25-28
      c. Amosi
      d. Yona
      e. Hosea
      f. Isaya
      g. Mika
   2. Muhtasari mfupi wa hali ya kuabudu sanamu kati ya watu wa Mungu inaweza kuonekana katika Hosea
      a. 2:16, "hawataniita Mimi tena Baali"
      b. 4:12-13, " . . . binti wanafanya ukahaba . . ."
      c. 4:17, "Efraimu ameifuata sanamu; mwacheni aende"
      d. 13:2 "watu hubusu ndama!" (ibada)
   3. mazingira ya kijamii
      a. Ilikuwa ni muda wa utajiri wa kiuchumi na upanuzi wa kijeshi kwa wote Israeli na Yuda. Hatahivyo, utajiri huu ulikuwa wa faida kwa tabaka la watu wenye fedha tu. Masikini walinyonywa na kunyanyaswa. Nia kama ilionekana "masikini na wenye nguvu" ikawa kama ibada ya sanamu!
      b. Uimara wa kijamii na mali wa kwa wote Israeli na Yuda inahusiana na visababishi kadhaa:

(1) utawala mrefu na wenye mafanikio wa Yeroboamu II (786-746 K.K.) huko kaskazini na Uzia (783-742 K.K.) huko Kusini.
(2) kushindwa kwa Ashuru na Adad-Nirari III mnamo mwaka 802 K.K.
(3) kutokuwepo kwa migogoro kati ya Israeli na Yuda.
(4) utozwaji kodi na unyonywaji wa njia za kibiashara kutoka kusini mpaka kaskazini kupitia daraja ardhi la Palestina kulisababisha ukuaji wa ghafla wa kiuchumi, hata matumizi ya starehe kwa tabaka la watu wenye mali.

c. Ile "Ostraca ya Samaria" ambayo inawekwa katika tarehe wakati wa utawala wa Yereboamu II inaonekana kuonyesha ushirika wa kiutawala sawasawa na wa Sulemani. Hii inaonekana kuthibitisha kupanuka kwa ombwe kati ya "walio nacho" na "wasiokuwa nacho."

d. Ukosefu wa ukweli wa wenye mali kunawekwa wazi kwa uzuri katika Amosi, ambaye anaitwa "nabii wa haki ya kijamii." Rushwa ya kimahakama na uongopeaji wa uzito wa kibiashara ni mifano miwili ya wazi ya matumizi mabaya jambo ambalo lilikuwa limezoeleka inavyooneakana huko kote Israeli na Yuda.

4. Mazingira ya kidini

a. Ulikuwa ni muda wa shughuli nyingi za kidini za nje japo imani ya mkweli ikiwa ni kidogo sana. Ibada za ustawi za kanaani zilikuwa zimeunganishwa katika dini ya Israeli. Watu walikuwa waabudu sanamu lakini waliita dini ya YHWH. Mwenendo wa watu wa Mungu juu ya muungano wa kisiasa ulikuwa umewaunganisha katika ibada za kipagani na shughuli zake.

b. Ibada ya kuabudu sanamu ya Israeli inatajwa katika 2 Wafalme 17:7-18.

(1) Mst. 8, walifuata matendo ya ibada ya wakanaani.

(a) ibada za ustawi

i) sehemu za juu, mistari ya 9, 10, 11
ii) nguzo za unabii (Baali), mistari 10, 16
iii) Asherim, mstari wa 16 hivi vilikuwa viwakilishi vya mbao vya suria wa kike wa Baali. Walikuwa aidha: nyama za kuchongwa au miti iliyo hai.

(b) Ubashiri, Mstari wa 17 hili linajadiliwa kwa kina katika Law. 19-20 na Kumb. 18.

(2) Mstari wa 16, waliendelea na ibada ya ndama wawili wa dhahabu wakiwakilisha YHWH, waliweka huko Dani na Betheli kwa kufanywa na Yeroboamu I (1 Wafalme 12:28-29).
(3) Mstari wa 16, waliabudu mungu wa anga wa Babeli: jua, mwezi, nyota na vitu vyote vya anga.
(4) Mstari wa 18, waliabudu mungu wa moto wa ustawi wa Foenike, Moleki (kama vile Law. 18:21; 20:2-5).

c. Dini ya kumuabudu Baali (kama vile W. F. Albright's *Archaeology and the Religion of Israel*, ukur. 82 na kuendelea).

(1) Chanzo chetu bora zaidi ni "Baal Epic of Ugarit."

(a) Inamuonesha Baali kama mungu wa majira anayekufa na kufufuka. Alishindwa na *Mot* na kufungwa kwenye ulimwengu wa chini kwa chini. Maisha yote duniani yalikwisha. Lakini alisaidiwa na mungu mke (*Anat*), anainuka na kumshinda *Mot* kila kipupwe. Yeye ni mungu aliyekuwa akiabudiwa na miujiza ya kuigiliza.
(b) Alijulikana kama *Hadad*.

(2) *El* ni mungu mkuu wa madhabahu ya Wakanaani lakini umaarufu wa Baali ulichukua nafasi yake.
(3) Israeli ilikuwa chini wa ushawishi mkubwa zaidi wa Dini ya Baali ya kulazimishwa na Yezebeli aliyekuwa Mfalme wa binti wa Tiro. Alichaguliwa na Omri kwa ajili ya kijana wake Ahabu.

(4) Katika Israeli Baali alikuwa anaabudiwa katika maeneo ya kawaida. Aliwakilishwa kwa jiwe lililoinuliwa. Suria wake Ashera, aliwakilishwa na nyama iliyochongwa iliwakilisha mti wa uzima.

d. Vyanzo kadhaa na aina ya ibada za sanamu vinatajwa.
   (1) Ndama za dhahabu huko Betheli na Dani zilizowekwa na Yeroboamu I kumuabudu YHWH.
   (2) Ibada ya mungu wa ustawi wa Tiro na mungu mke katika maeneo ya juu ya kawaida.
   (3) kuabudu sanamu kwa muhimu kulikujumuishwa katika miunganiko ya kisiasa ya siku hiyo

5. Muhtasari fupi ya uvamizi wa Ashuru na Babeli wakati wa karne ya nane ambayo iliathiri Palestina:
   a. Manabii wa karne ya nne walikuwa macho wakati wa kupanda kwa ufalme wa Hedekeli-Frati wa Ashuru. Mungu angetumia taifa hili katili kuhukumu watu wake hasa Israeli..
      (1) Tukio hasa lilikuwa uundwaji wa muungano wa Yordani kisiasa na kijeshi ikijulikana kama "Shirikisho la Shamu-Efraimu" (735 K.K.). Shamu na Israeli walijaribu kulazimisha Yuda kuwaunganisha dhidi ya Ashuru. Badala yake Ahazi alituma barua kwa Ashuru kwa ajili ya msaada. Ufalme wa kwanza wenye nguvu wa mfalme wa Kiashuru, Tiglath-Pileser III (745 - 727 K.K.), alirejea mrejesho wa tishio la kijeshi ba kuvamia Shamu.
      (2) Baadaye, mfalme wa kupandikizwa wa Ashuru, Hoshea (732-722 K.K.), huko Israeli pia aliasi akiwapendeza Misri. Shalmaneser V (727-722 K.K.) aliivamia Israeli tena. Alikufa kabla Israeli haijatiishwa lakini aliyemfuatia, Sargon II (722-705 K.K.), aliutwaa mji mkuu wa Israeli, Samaria mnamo mwaka 722 K.K. Ashuru alipeleka uhamishoni zaidi ya Waisraeli 27,000 katika tukio hili wakati Tiglath-Pileser alipokuwa amepeleka uhamishoni maelfu hapo kabla mnamo mwaka 732 K.K.
   b. Baada ya kifo cha Ahazi (735-715 K.K.) muungano mwingine wa kijeshi ulitengenezwa na nchi za jangwa la Yordani na Misri dhidi ya Ashuru (714-711 K.K.). Unajulikana kama "Uasi wa Ashdodi." Miji mingi ya Yudea iliharibiwa wakati Ashuru ilipovamiwa tena. Mwanzoni Hezekia alisaidia muungano huu lakini baadaye alijitoa na msaada wake.
   c. Hatahivyo muungano mwingine ulijaribu kuchukua fursa ya kifo cha mfalme mwenye nguvu wa Ashuru, Sargoni II, mnamo mwaka 705 K.K. pamoja na uasi mwingine mwingi ambao ulitokea wakati wote wa ufalme wa Ashuru.
      (1) Hezekia alishiriki kikamilifu wakati wa uasi huu. Kwa mwanga huu wa tishio hili la Senakeribu (705-681 K.K.) alivamia (701 K.K.) Palestina na kuweka kambi karibu na mji wa Yerusalemu (2 Wafalme 18-19; Isa. 36-39) lakini jeshi lake liliharibiwa na Mungu kimiujiza.
      (2) Kuna baadhi ya maswali kati ya wanazuoni juu ya mara ngapi Senakaribu alivamia Palestina (Mfano: John Bright ana uvamizi mmoja mnamo mwaka 701 K.K. na mwingine unaowezekana ni mnamo mwaka 688 K.K. kama vile ukur. 270).
      (3) Hezekia aliachwa kwa mapinduzi ya Kiashuru lakini kwasababu ya maonyesho yake ya kiburi na hazina za Yuda kwa ujumbe wa Ki-Babeli, Isaya alitabiri kuanguka kwa Yuda kwa Babeli (39:1-8). Yerusalemu ilianguka kwa Nebuchadneza mnamo mwaka 587-586 K.K
   d. Isaya pia alitabiri urejesho wa watu wa Mungu chini ya Koreshi II, mtawala wa ki-Medi mwenye asili ya Uajemi (41:2-4; 44:28; 45:1; 56:11). Ninawi ilianguka mnamo mwaka 612 K.K. Babeli lakini mji wa Babeli ulianguka mnamo mwaka 539 K.K kwa jeshi la Koreshi. Mnamo mwaka 538 K.K. Koreshi alitoa tamko kwamba watu wote wa uhamishoni wakiwemo Wayahudi wanaweza kurudi nyumbani. Hata pia alitoa fedha kutoka katika hazina kwa ajili ya kujenga upya mahekalu ya kitaifa.

B. Pitio Fupi la Kihistoria la Nguvu za Mesopotamia (kwa kutumia tarehe zenye msingi wa toleo la John Bright liitwalo *A History of Israel*, ukur. 462 na kuendelea):
   1. Ufalme wa Ashuru (Mwa. 10:11):
      a. dini na desturi zilichagizwa kwa sehemu kubwa na Ufalme wa Ki-Sumeri na Ki-Babeli.
      b. orodha ya watawala wanaodhaniwa na makisio ya tarehe za utawala wao:
         (1) 1354-1318 Asshur-Uballit I:
            (a) alitawala mji wa wa-Hiti wa Karmeshi.
            (b) alianza kuondoa ushawishi wa wa-Hiti na kuruhusu wa-Ashuru kukua.
         (2) 1297-1266 Adad Nirari I (mfalme mwenye nguvu).
         (3) 1265-1235 Shalmaneser I (mfalme mwenye nguvu).
         (4) 1234-1197 Tukulti-Ninurta I - uvamizi wa kwanza wa ufalme wa Babeli huko Kusini.
         (5) 1118-1078 Tiglath-Pileser I - Wa-Ashuru wanakuwa taifa kubwa huko Mesopotamia.
         (6) 1012- 972 Ashur -Rabi II
         (7) 972- 967 Ashur -Resh-Isui II.
         (8) 966- 934 Tiglath-Pileser II.
         (9) 934- 912 Ashur -Dan II.
         (10)912- 890 Adad- Nirari II.
         (11)890- 884 Tukulti-Ninurta II.
         (12)890- 859 Asshur-Nasir-Apal II.
         (13)859- 824 Shalmaneser III. Vita ya Qarqar mnamo mwaka 853
         (14)824- 811 Shamashi-Adad V.
         (15)811- 783 Adad- Nirari III.
         (16)781- 772 Shalmaneser IV.
         (17)772- 754 Ashur -Dan III.
         (18)754- 745 Ashur-Nirari V.
         (19)745- 727 Tiglath-Pileser III:
            (a) aliitwa kwa jina la kiti cha kifalme cha kibabeli, Pul, katika 2 Wafalme 15:19.
            (b) mfalme mwenye nguvu sana.
            (c) alianzisha sera ya kupeleka uhamishoni watu waliotawaliwa.
            (d) Mnamo mwaka 735 K.K. kulikuwa na uundwaji wa "Shirikisho la Shamu-Efraimu" ambalo lilikuwa ni jaribio la kuunganisha rasilimali jeshi lote lililopo la mataifa yanayozunguka Yordani kutoka katika vyanzo vya maji vya Hedekeli mpaka Misri kwa kusudi la kudhoofisha taifa linalokua kwa kasi ya nguvu za kijeshi la Ashuru. Mfalme Ahazi wa Yuda alikataa kujiunga na anavamiwa na Israeli na Shamu. Aliandika kwa Tiglath-Pileser III kwa ajili ya msaada kinyume cha ushauri wa Isaya (kama vile Is. 7-12).
            (e) Mnamo mwaka 732 Tiglath-Pileser III anavamia na kuitawala Shamu na Israeli na anaweka mfalme wa mpito katika ufalme wa Israeli, Hoshea (732-722 K.K.). Maelfu ya Wayahudi wanapelekwa uhamishoni Media (kama vile 2 Wafalme 15-16).
         (20)727- 722 Shalmaneser V. - Hoshea anatengeneza muungano pamoja na Misri na anavamiwa na Ashuru (kama vile Wafalme 17).
         (21)722- 705 Sargon II:
            (a) baada ya miaka mitatu ya kuzungukwa kivita, ulioanzishwa na Shalmaneser V, kamanda wake na mtawala aliyemfuatia Sargon II, anatawala mji mkuu wa Israeli, Samaria. Zaidi ya 27,000 wanapelekwa uhamishoni Media
            (b) Ufalme wa wa-Hiti nao unavamiwa na kutawaliwa.
            (c) in 714-711 muungano mwingine wa mataifa ya Yordani na Misri yaliasi dhidi ya Ashuru. Ushirika huu uliitwa "uasi wa Ashdodi." Hata Hezekia wa Yuda kiasili alishiriki. Ashuru alivamia na kuharibu miji kadhaa ya wafilisti.
         (22)705- 681 Senakeribu:

(a) Mnamo mwaka 705 shirikisho lingine la mataifa ya Yordani na Misri waliasi baada ya kifo cha baba yake, Sargon II. Hezekia aliunga mkono kikamilifu uasi huu. Senakeribu alivamia mnamo mwaka 701. Uasi ulipigwa lakini Yerusalemu iliachwa kwa tendo la Mungu (kama vile Isa. 36-39 na 2 Wafalme 18-19.)
(b) Senakeribu pia anashinda uasi huko Elamu na Babeli.

(23)681-669 Esarhaddon:
(a) mtawala wa kwanza wa Kiashuru kushambulia na kutawala Misri
(b) alikuwa na huruma kuu pamoja na Babeli na kujengwa upya kwa mji wake mkuu

(24) 669-663 Ashurbanipal:
(a) pia aliitwaOsnappar katika Ezra 4:10
(b) Kaka yake Shamash-shum-ukin alifanywa mfalme wa Babeli. Hii ilileta miaka kadhaa ya amani kati ya Ashuru na Babeli lakini kulikuwa na mwendelezo wa uhuru ambao ulivunjika mnamo mwaka 652 ukiongozwa na kaka yake.
(c) Kuanguka kwa Thebesi, 663 K.K.
(d) Kushindwa kwa Elamu, 653, 645 K.K.

(25) 633-629 Asshur-Etil-Ilani
(26)629-612 Sin-Shar-Ishkun
(27) 612-609 Asshur-Uballit II: - aliwekwa kama mfalme huko uhamishoni Harani baada ya anguko la Asheri mnamo mwaka 614 K.K. na Ninawi mnamo mwaka 612 K.K.

2. Ufalme mpya wa Babeli:

a. 703- ? Merodach-Baladan - alianza mapinduzi kadhaa dhidi ya utawala wa Ashuru
b. 652 Shamash-shum-ukin:
(1) Mwana wa Esarhaddon na kaka wa Asshurbanipal
(2) alianza mapinduzi dhidi ya Ashuru lakini alishindwa
c. 626-605 Nabopolassar:
(1) alikuwa mfalme wa kwanza wa ufalme wa kisasa wa Babeli
(2) alivamia Ashuru kutoka kusini wakati Cyaxares wa Medi alivamia kutoka kaskazini mashariki
(3) mji mkuu wa kale wa Ashuru, Asshur ulianguka mnamo mwaka 614 na mji mkuu mpya wenye nguvu wa Ninawi ulianguka mnamo mwaka 612 K.K.
(4) Mabaki ya jeshi la Ashuru walikimbilia kurudi Harani. Hata walidiriki kupandisha mfalme mpya.
(5) Mnamo mwaka 608 Pharaoh Necho II (kama vile 2 Wafalme 23:29) alienda kaskazini kusaidia mabaki wa jeshi la Ashuru kwa kusudi la kutengezeza ukanda wa usalama dhidi ya taifa na nguvu inayokua ya Babeli.Yosia, mfalme mtauwa wa Yuda (kama vile 2 Wafalme 23), walipinga mapinduzi ya jeshi la Misri kupitia Palestina. Kulikuwa na waskemishi wadogo wadogo huko Megiddo. Yosia aliumizwa na kufa (2 Wafalme 23:29-30). Mtoto wake Yehoazi alifanywa mfalme. Pharaoh NechoII alifika akiwa amechelewa kuzimisha uharibifu wa majeshi ya Ashuru huko Harani. Aliyakabili majeshi ya kibabeli kwa kuongozwa na mtoto wa mfalme Nebukadneza II na walishindwa vibaya mnamo mwaka 605 K.K. huko Kakameshi juu ya Mto Frati.

Alipokuwa akirudi Misri alisimama Yerusalemu na kupitia mji. Alimtoa Yehoazi na kumuondoa baada ya miezi mitatu tu. Akamweka mwana mwingine wa Yosia, Yehoakini katiki cha Enzi (kama vile 2 Wafalme 23:31-35).
(6) Nebukadneza II alifukuza jeshi la kimisri kusini kupitia Palestina lakini alipokea neno la kifo cha baba yake na kurudi Babeli. Baadaye mwaka huo huo alirudi Palestina. Alimuacha Yehoakimu katika utawala wa kiti chake cha Yuda lakini akapeleka uhamishoni maelfu kadhaa wa raia mna wajumbe kadhaa wa familia ya kifalme. Danieli na rafiki zake walikuwa sehemu ya uhamisho huu.

d. 605-562 Nebukadneza II:
   (1) Tokea mwaka 597-538 Babeli ilikuwa na utawala wote juu ya mji wa Palestina.
   (2) Mnamo mwaka 597 uhamisho mwingine ulitokea Yerusalemu (2 Wafalme 24). Alikufa kabla ya kuwasili kwa Nebukadneza II. Mwanaye Yehoakini alikuwa ni mfalme pekee kwa miezi mitatu wakati alipopelekwa uhamishoni kwenda Babeli. Watu elfu kumi wakiwemo Ezekieli, walipelekwa kimakazi karibu na Jiji la Babeli kando ya Mfereji wa Mto Kebari.
   (3) Mnamo mwaka 586, baada ya mwendelezo wa ushawishi na Misri, Mji wa Yerusalemu uliharibiwa tiki tiki (2 Wafalme 25) na uhamisho mkubwa ukatokea. Zedekia alitawala badala ya Yehoakini, aliyepelekwa uhamishoni na Gedelia kuteuliwa kuwa mtawala..
   (4) Gedelia aliuwawa na majeshi ya kiutawala ya Kiyahudi. Majeshi haya yalikimbilia Misri na kumlazimisha Yeremia kwenda pamoja nao (605, 596, 586, 582) na kuhamisha Wayahudi waliobakia waliopatikana..

e. 562-560 Evil-Merodack, pia ajulikanaye kama Amel-Marduk - Alimuachilia Yehoakini kutoka gerezani lakini alitakiwa kuendelea kuishi Babeli (kama vile 2 Wafalme 25:27-30; Yer. 52:31).
f. 560-556 Neriglissar - Alikuwa ni kamanda wa Nebukadneza aliyeuharibu Yerusalemu.
g. 556 - Labaski-Marduk – Alikuwa mwana wa Neriglissar lakini alipigwa risasi baada ya miezi tisa tu.
h. 556-539 Nabonidasi:
   (1) Nabonidasi hakuwa na mahusiano na nyumba ya kifalme hivyo alioa binti wa Nebukadreza II.
   (2) Alitumia muda wake mwingi katika kujenga hekalu kwa ajili ya mungu mwezi "Sin" huko Tema. Alikuwa mwana wa kuhani mke wa mungu huyu. Hii ilimsababishia uadui na makuhani wa Marduk, mungu mkuu wa Babeli.
   (3) Alitumia muda wake mwingi kujaribu kuzima mageuzi na kuimarisha ufalme.
   (4) Aliondoka Tema na kuachia mambo ya nchi kwa mwanawe, Belshazzar, katika mji mkuu wa Babeli (kama vile Dan.5).

i. ? - 539 Belshazzar (mtawala mwenza) - Mji wa Babeli ulianguka kwa haraka kwa Jeshi la Uajemi chini ya Gobryas wa Gutium kwa kuhamisha maji ya mto Frati na kuingia mjini bila kupingwa. Makuhani na watu wa mji waliwaona watu wa Uajemi kama wakombozi na warejeshaji wa Marduk. Gobryas alifanywa Gavana wa Babeli na Koreshi II. Gobryas anaweza kuwa Mede wa Dario Mede wa Dan. 5:31; 6:1. “Dario” maana yake “mtukufu.”

3. Ufalme wa Umedi-Uajemi: Pitio la Kukua kwa Koreshi II (Isa. 44:28; 45:1-7):
   a. 625-585 Cyaxares alikuwa mfalme wa Medi iliyomsaidia Babeli kumshinda Ashuru.
   b. 585-550 Astyages alikuwa mfalme wa Medi. Koreshi alikuwa mjukuu wa Mandane.
   c. 550-530 Koreshi II wa Ansham alikuwa mfalme wa mpito aliyepindua:
      (1) Nabonidasi, mfalme wa Babeli aliyemuunga mkono Koreshi.
      (2) Koreshi II alimvua madaraka Astyages.
      (3) Nabonidasi ili kuweza kurejesha nguvu ya kijeshi, alifanya ushirika pamoja na:
         (a) Misri
         (b) Croesus, Mfalme wa Lydia (Asia Ndogo)

   d. 547 - Koreshi II aliukabili Sardi (mji mkuu wa Lydia).
   e. 539 - Mnamo Nov. 2, Gobryas wa Gutium, pamoja na jeshi la Koreshi, waliichukua Babeli bila kipingamizi. Alifanywa gavana wa Babeli.

f. 539 - Mnamo Oktoba Koreshi II "Mkuu" binafsi aliingia kama mkombozi. Sera yake ya ukarimu kwa makundi ya kitaifa yakirejeshewa miaka ya uhamisho kama sera ya kitaifa.

g. 538 - Wayahudi na wengine waliruhusiwa kurudi nyumbani na kujenga mahekalu yao ya asili.

h. 530 - mwana wa Koreshi, Cambyses II, alitawala baada yake.

i. 530-522 utawala wa Cambyses II
   - aliongeza ufalme wa Wamisri mnamo mwaka 525 K.K. kwenye Ufalme waUmedi-Uajemi;
   - baadhi wanasema kuwa alijiua;

j. 522-486 Dario I (Hystapis) alianza kutawala
   (1) Hakuwa anatokea uzao wa kifalme bali kamanda wa kijeshi.
   (2) Alipangilia Ufalme wa Uajemi akitumia mipango ya Koreshi kwa ajili ya Maakida (kama vile Ezra 1-6; Hagai; Zekaria).
   (3) alianzisha ushirika kama wa Lydia.

k. 486-465 Utawala wa Ahausuero I:
   (1) alizima mapinduzi ya Ki-Misri
   (2) Alitarajia kuvamia Uyunani kutimiza ndoto ya Uajemi lakini alishindwa katika vita ya Thermopoly mnamo mwaka 480 K.K. na Salamis mnamo mwaka 479 K.K.
   (3) Mume wa Esta aitwaye Ahausuero katika Biblia, aliuwawa mnamo mwaka 465 K.K.

l. 465-424 Artashtaza I (Longimanus) alitawala (kama vile Ezra 7-10; Nehemia; Malaki):
   (1) Wayunani waliendelea mbele mpaka kukabiliana na Vita vya Wao kwa wao vya Pelopasania
   (2) Uyunani inagawanya (Wa-Athene – wa-Pelopanisi)
   (3) Vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Wayunani vilimalizika baada ya miaka 20
   (4) wakati wa kipindi hiki Jamii ya Kiyahudi ilitiwa nguvu

m. 423-404 Dario II anatawala

n. 404-358 Artashtaza II alitawala

o. 358-338 Artashtaza III alitawala

p. 338-336 Arses alitawala

q. 336-331 Dario III alitawala

4. Pitio la Misri:

   a. Hyksos (Mfalme wa-Kichungaji – Watawala wa Kisemiti)-1720/10-1550 K.K.
   b. Ufalme wa 18 (1570-1310 K.K):
      (1) 1570-1546 Amosis
      (2) 1546-1525 Amenophis I (Amenhotep I).
      (3) 1525-1494 Thutmosis I
      (4) ? Thutmosis II
      (5) ? Hatshepsut
      (6) 1490-1435 Thutmosis III
      (7) 1435-1414 Amenophis II.
      (8) 1414-1406 Thutmosis IV
      (9) 1406-1370 Amenophis III
      (10) 1370-1353 Amenophis IV (Akhenaten)
      (11) ? Smenkhare
      (12) ? Tutankhamun
      (13) ? Ay
      (14) 1340-1310 Haremhab
   c. Ufalme wa 19 (1310-1200 K.K.):
      (1) ? Rameses I
      (2) 1309-1290 Seti I

(3) 1290-1224 Rames ses (Rameses II)
(4) 1224-1216 Marniptah (Merenptah)
(5) ? Amenmesses
(6) ? Seti II
(7) ? Siptah
(8) ? Tewosret

d. Ufalme wa 20 (1180-1065 K.K.):
(1) 1175-1144 Rames es III
(2) 1144-1065 Rameses IV – XI

e. Ufalme wa 21 (1065-935 K.K..):
(1) ? Smendes
(2) ? Herihor

f. Ufalme wa 22 (935-725 K.K - Libya):
(1) 935-914 Shishak (Shosenk I au Sheshong I)
(2) 914-874 Osorkon I
(3) ? Osorkon II
(4) ? Shoshnek II

g. Ufalme wa 23 (759-715 K.K. - Libya)

h. Ufalme wa 24 (725-709 K.K.)

i. Ufalme wa 25 (716/15-663 K.K. - Ethiopia/Nubi):
(1) 710/09-696/95 Shabako (Shabaku)
(2) 696/95-685/84 Shebteko (Shebitku)
(3) 690/89, 685/84-664 Tirhakah (Taharqa)
(4) ? Tantamun

j. ufalme wa 26 (663-525 K.K. - Saitic):
(1) 663-609 Psammetichus I (Psamtik)
(2) 609-593 Neco II (Necho)
(3) 593-588 Psammetichus II (Psamtik)
(4) 588-569 Apries (Hophra)
(5) 569-525 Amasis
(6) ? Psammetichus III (Psamtik)

k. Ufalme wa 27 (525-401 K.K - Uajemi):
(1) 530-522 Cambyses II (mwana wa Koreshi II)
(2) 522-486 Dario I
(3) 486-465 Ahausuero I
(4) 465-424 Artashasta I
(5) 423-404 Dario II

*kwa tofauti za mpangilio, angalia *Zondervan's Pictorial Bible Encyclopedia*, vol. 2 ukur. 231.

5. Pitio la Uyunani:
   a. 359-336 Philip II wa Makedonia:
      (1) aliijenga Uyunani
      (2) aliuwawa mnamo mwaka 336.
   b. 336-323 Iskanda II "Mkuu" (Mwana wa Philipo):
      (1) alimpiga Dario II, Mfalme wa Uajemi wakati wa vita vya Isus
      (2) Alikufa mnamo mwaka 323 K.K. huko Babeli kama homa akiwa na umri kati ya miaka 32/33.
      (3) makamanda wa Iskanda waliugawa ufalme wake wakati wa kifo chake:
         (a) Cassender - Makedonia na Uyunani
         (b) Lysimicus – Thrace

(c) Seleucus I - Shamu na Babeli
(d) Ptolemy - Misri na Palestina
(e) Antigonus - Asia Ndogo (hakukaa muda mrefu)

c. Wa- Seleucid dhidi ya wa-Ptolemy kwa ajili ya kuigawa Palestina
   (1) Shamu (Watawala wa Seleucid):
      (a) 312-280 Seleucus I
      (b) 280-261 Antiochus I Soster
      (c) 261-246 Antiochus II Theus
      (d) 246-226 Seleucus II Callinicus
      (e) 226-223 Seleucus III Ceraunus
      (f) 223-187 Antiochus III Mkuu
      (g) 187-175 Seleucus IV Philopator
      (h) 175-163 Antiochus IV Epiphanes
      (i) 163-162 Antiochus V
      (j) 162-150 Demetrius I
   (2) Watawala wa ki-Misri (wa-Ptolemy):
      (a) 327-285 Ptolemy I Soter
      (b) 285-246 Ptolemy II Philadelphus
      (c) 246-221 Ptolemy III Evegetes
      (d) 221-203 Ptolemy IV Philopator
      (e) 203-181 Ptolemy V Epiphanes
      (f) 181-146 Ptolemy VI Philometor
   (3) Pitio Fupi:
      (a) 301- Palestina chini ya Ptolemy kwa miaka 181.
      (b) 175-163 Antiochus IV Epiphanes, mtawala wa nane wa-Seleucid, walitaka kuwa-wasilisha Wayahudi kwa nguvu inapobidi:
         i) walijenga kumbi za sarakasi
         ii) walijenga madhabahu za kipagani za Zeus Olympius katika Hekalu

VIII. VIPENGELE VYA KIFASIHI

A. Ainisho Fupi
   1. Sura za 1-39 - nabii na nyakati zake
   2. Sura za 40-66 (au yawezekana 40-55 na 56-60) - nyakati mpya

B. Sura za 1-39, mazingira ya kihistoria ya siku za Isaya (kabla ya uhamisho)
   1. Sura za 1-6, chini ya Wafalme Uzia na Yotham
   2. Sura za 7-14, chini ya Mfalme Ahazi
   3. Sura za 15-39, chini ya Hezekia (sura za 36-39 zinafanana na 2 Wafalme 18:13-20:19)

C. Sura za 40-66, ni za uhamisho na kipindi baada ya uhamisho na aina za ufalme ujao.
   1. kama sura za 1-39 zinaaksi mahubiri ya Isaya nan i wazi uwasilishaji wa kinywa, sura za 40-55 zinaaksi mazingira mapya. Hukumu ya Mungu pia imekuja na sasa urejesho ni maudhui makubwa. Kuna dokezo la kimuundo kwamba sura hizi si sana kwa kinywa kama kuandika.
   2. Sura za 1-39 ni wazi zinahusu tishio la Ashuru, na tishio la aina la ki-Babeli hasa katika sura za 13-14, 21 na 39. Sura za 40-55 zinahusu kipindi cha Uajemi na urejesho wa watu wa Mungu kwenye nchi ya Ahadi.
   3. Sura zinazofuata za Isaya, 56-66, ni za matukio ya siku za mwisho, kwa kutumia sitiari za kihistoria kutoka mashariki ya Kale ya Karibu kubashiri ibada ya kiulimwengu kwa mungu mmoja YHWH.

D. Ugumu wa uaninishaji wa Isaya

1. Wasomi wengi zaidi wa kisasa wanagawa kitabu angalau katika sehemu mbili: sura za 1-39 na 40-66. R. K. Harrison: sura za 1-33 na 34-66 kwasababu ya ombwe katika andiko la DSS. Huu mgawanyo wa dhahiri katika DSS kati ya sura za 33 na 34 zimefanya kuinuka kwa mapendekezo kwamba Isaya kilizalishwa na wafuasi katika Juzuu mbili. W.H. Brownlee amependekeza kwamba juzuu mbili zijiangalie zenyewe katika muundo:

| Volume 1: | Volume 2 |
|---|---|
| Sura za 1-5 - uharibifu na urejesho | sura za 34-35 |
| Sura za 6-8 – nyaraka za maisha binafsi | sura za 36-40 |
| Sura za 9-12 - wasaidizi wa Baraka za ki-Mungu na hukumu | sura za 41-45 |
| sura za 13-23 - unabii dhidi ya nguzu za kigeni | sura za 46-48 |
| sura za 24-27 - ukombozi wa jumla na ukombozi wa Israeli | sura za 49-55 |
| sura za 28-31 - mahubiri ya maadili 56-59 | |
| sura za 32-33 - urejesho wa taifa | sura za 60-66 |

2. Baadhi ya shabaha za ainisho juu ya mazingira ya kihistoria wakati wengine wakiweka shabaha juu ya maudhui ya ki-Masihi

| **NIV** | **Leupold** |
|---|---|
| Sura za 7-12 Nabii zinawekwa katika mazingira ya kiaramu na Tishio la Waisraeli dhidi ya Yuda" | "Immanuel Book (Kitabu cha Immanueli)" |
| Sura za 28-33 "Ole Sita: Tano juu ya kukosa uaminifu katika Israeli juu ya Ashuru" | "The Book of Zion (Kitabu cha Sayuni)" (the Cornerstone(Jiwe kuu la Pembeni)) |

3. Baadhi ya mifano ya ukosefu wa uhakika wa vipengele vya kifasihi (sura za 1-12)
   a. Ainisho za Sura 1-12 na E. Y. Young, kur. 211-214:
      (1) 1:1-12:6 Nabii juu ya Yuda na Yerusalemu
         (a) 1:1-31 mashitaka makuu
         (b) 2:1-4:6 utawala wa Masihi na hukumu juu ya watu
         (c) 3:5-30 uovu uzidio juu ya Yuda
         (d) 6:1-13 Maono ya Isaya juu ya Bwana
         (e) 7:1-12:6 Unabii unatajwa wakati wa utawala wa Ahazi.
   b. Ainisho za sura za 1-2 na R.K. Harrison, ukur. 764:
      (1) Nabii juu ya uharibifu na urejesho wa Yuda, sura za 1-5
      (2) Wito wa Isaya; nyaraka za maisha ya mtu binafsi, sura za 6-8
      (3) falme za ulimwengu uliopo na majukumu yao, sura za 9-12
   c. Ainisho za Sura 1-12 na The NIV Study Bible, kur. 1016
      (1) Sura za 1-6
         (a) Utangulizi: mashitaka dhidi ya Yuda kwa kuvunja agano, sura ya 1
         (b) Nidhamu ya baadaye na utukufu wa Yuda na Yerusalemu, sura za 2-4
            i) baraka za baadaye za Yerusalemu (2:1-5)
            ii) nidhamu ya Bwana ya Yuda (2:6-4:1)
            iii) Urejesho wa Sayuni (4:2-6)
         (c) hukumu ya taifa na uhamisho (sura za 5)
         (d) agizo maalumu la Isaya (sura ya 6)
      (2) sura za 7-12
         (a) Ahazi anaonywa kutohofu Wa-Aramu na muungano wa Waisraeli (sura ya 7)
         (b) mwana wa Isya na mwana wa Daudi (8:1-9:7)
         (c) Hukumu dhidi ya Israeli (9:8-10:4)

(d) Ufalme wa Ashuru na ufalme wa nyumba ya Daudi (10:5-12:6)
    i) uharibifu wa Ashuru (10:5-34)
    ii) Uanzishwaji wa ufalme wa nyumba ya Daudi na ufalme wake (sura ya 11)
    iii) Wimbo wa furaha kwa ajili ya Ukombozi (sura za 12)

d. Ainisho la sura ya 1-12 na H.C. Leupold, kur. 38-40:
  (1) Nabii juu ya Yuda na Yerusalemu (sura za 1-12)
    (a) utangulizi: ujumbe halisia wa Isaya (sura 1)
      i. Kichwa cha habari, v. 1
      ii. Mashtaka ya ki-Mungu, mistari ya 2-4
      iii. hali ya uharibifu ya nje ya taifa, mistari 5-9
      iv. hali ya sasa ya ibada isiyo na mguso kama madhara, mistari ya 10-15
      v. kuitwa kutubu, mistari 16-20
      vi. viashiria vya uharibifu katika Yerusalemu, mistari ya 21-33
      vii. Israeli ikikombolewa na hukumu, mistari ya 24-31
    (b) kupitia hukumu mpaka kutimilizwa kwa ahadi za neema za Mungu, sura za 2-6
      i. Ubaadaye wa utukufu wa Sayuni katika nyakati za ki-Masihi, 2:2-5
      ii. usasa wa Sayuni usio na utukufu, 2:6-4:1
        a) maelezo ya thamani za uongo ambazo ndizo zilizopo, mistari ya 6-9
        b) viashiria vya hukumu kali inayotegemewa kuja, mistari ya 10-11
        c) kile siku ya Bwana itakachokifanya kwa thamani zote za uongo, mstari wa 12-17
        d) anguko la sanamu, mistari ya 18-21
        e) hukumu ya Bwana kwa viongozi wasiowajibika, 2:22-3:15
          i) hali yenye matokeo ya uasi wakati Bwana atakapochukua misaada yote 3:1-12
          ii) hatia ya viongozi walioleta janga hili, 3:13-15
        f) hukumu ya Bwana juu ya mizaha na wanawake wambea wa Yerusalemu, 3:16-4:1
        g) Sayuni inatakaswa, 4:2-6
        h) hukumu ya Mungu juu ya watu wake wenye hatia, sura ya 5
          i) mfano wa shamba la mzabibu, mstari wa 1-7
          ii) zabibu chungu zinazozalishwa na Israeli, mistari ya 8-23
          iii) hukumu iliyopo iletwayo na wa-Ashuru, mistari ya 24-30
        i) hukumu ya Israeli ikijumuisha wito wa asili wa nabii, sura ya 6
          i) maono ya nabii, mistari ya 1-3
          ii) mwitikio wa nabii juu ya maono, mistari ya 4-5
          iii) Kuitikia kwake, mistari ya 6-7
          iv) Kupewa kwake agizo, mistari ya 8-9a
          v) Ujumbe wake, mistari ya 9b-13
    (c) The Immanuel Book (Kitabu cha Immanueli) (sura za 7-12)
      i. Ishara ya Immanueli, sura ya 7
          a) tukio sehemu ya juu ya Birika, mistari ya 1-9
          b) mtiririko juu ya tukio, Neno juu ya Immaneli, mistari ya 10-17
          c) mwendelezo zaidi, hali mbaya itabiriwayo juu ya ardhi, mistari ya 18-25
      ii. Nyakati za kuchochea (734-732 K.K.) na namna gani ya kukutana nazo, sura ya 8
          a) kubomolewa kwa Dameski na Shamu, mistari ya 1-4
          b) uvamizi wa Ashuru wa Yuda, mistari ya 5-8
          c) usalama ambao Immanueli anaweza kutoa, mistari ya 9-10
          d) nani na nini cha kuhofia, mistari ya 11-15

e) kusubiria kwa subira kwa imani, mistari ya 16-18
f) kauli mbiu sahihi ya siku, mistari ya 19-22

iii. Mwana mwenye majina manne, 9:1-7
a) muhtasari, mstari wa 1
b) furaha kuu, mistari ya 2-3
c) nini kinaondolewa? Mistari ya 4-5
d) mwandishi wa furaha kuu, mistari ya 6-7

iv. "Mkono Wake umenyooshwa vyema," 9:8-10:4
a) kwasababu ya kiburi na kukosa utakatifu kutakuwepo na kushindwa na adui, mistari ya 8-12
b) kwasababu ya uasi unaoendelea kutakuwana kuondolewa kwa uongozi, mistari ya 13-17
c) kwasababu ya kuendele kwa uovu kutakuwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe, mistari ya 18-21
d) kwasababu ya kukosekana haki, kutakuwepo na siku ya majuto, 10:1-4

v. Ole wale Ashuru, 10:5-34
a) Waashuru wenye viburi wamepotoka katika majukumu yao kwa Mungu, mistari ya 5-11
b) hukumu iliyocheleweshwa itapiga mtawala huyu mwenye kiburi, mistari ya 12-14
c) kiburi chake Ashuru kitateketezwa kama msitu uteketeavyo kwa moto, mistari ya 15-19
d) Baada ya janga la hukumu ya Mungu mabaki ya Israeli watamrejerea Yeye, mistari ya 20-23
e) Sayuni itaokolewa wakati Ahsuru itakapotubu, mistari ya 24-27
f) kuendelea mbele kwa mikakati ya Ashuru kuliko karibia kuchukua Sayuni kunaelezwa kwa maneno ya matamko tokea mbele, mistari ya 28-32
g) Yahweh atakata chini msitu wa wa-Ashuru wenye viburi, mistari ya 33-34
h) Masihi wa Ukoo wa Daudi na kazi yake kubwa ya wokovu, sura ya 11
   i) chombo cha Masihi, mistari ya 1-3a
   ii) Namna yake ya utendaji Kazi, mistari ya 3b-5
   iii) mageuzi ya kutengenezwa hata katika ulimwengu wa asili, mistari ya 6-9
   iv) maelezo ya Kazi Yake kwa namna ya kile atakachofanya kwa Israeli, mistari ya 10-16
i) sifa kwa ajili ya siku inayokuja, sura ya 12
   i) maamuzi ya upande wa Israeli kutoa sifa hizo, mistari ya 1-2
   ii) maelezo ya muhtasari ya Baraka ya siku hiyo, mstari wa 3
   iii) maonyo kutoa sifa za namna hiyo, mistari ya 4-6

IX. KWELI KUU

A. Isaya alishikilia Yuda kwa uaminifu wa Agano la Daudi (2 Sam. 7) lakini pia alirudi nyuma kwenye makusudi ya asili ya agano la Ibrahimu (Mwa. 12:1-3) ambalo lilikuwa Mungu kuchagua Israeli kuuchagua ulimwengu. Ulinganifu wa namna gani utawala huu wa ujumla wa YHWH ulivyokuwa. Mungu si tu atarejesha Israeli bali atapanua ushawishi wake kwa ulimwengu wote!

B. Isaya hasa alitabiri kutokea kwa matukio ya ulimwengu katika yake mwenyewe na wakati ujao ikipelekea urejesho wa ufalme wa Daudi kupitia Masihi wa Mungu (ndivyo pia ilivyokuwa kwa

Mika). Ufalme huuni mtakatifu na wa kiulimwengul (ndivyo pia ilivyo kwa Mika). Hivi vyote ni vipengele vya Mungu mkombozi Mtakatifu mmoja kama anavyoonyeshwa Isaya.

C. Isaya kwa uwazi anaonesha upotovu wa watu wa Mungu katika kuamini kwa vitu vya kidunia, maliza kibinadamu za aliyeanguka.Ukombozi utatoka kwa YHWH tu!

D. Isaya anafunua tabia tatu zenye nguvu zaidi za mpango wa ukombozi wa Mungu:
   1. Masihi ajaye
   2. Masihi kama Mtumishi atesekaye
   3. utawala wa kiulimwengu wa Masihi

X. MANENO/TUNGO NA WATU WA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

A. Maneno na Tungo
   1. "Sikieni, enyi mbingu, tega sikio, Ee nchi", 1:2 (NASB & NIV)
   2. "kama kibanda katika shamba la mizabibu. . .", 1:8 (NIV, "kama kibanda katika shamba la tikiti")
   3. "Huu wingi wa sadaka zenu mnazonitolea una faida gani?. . .", 1:10-15 (NIV, " wingi wa sadaka zenu ")
   4. " njoni, tusemezane . . .", 1:18 (NASB & NIV)
   5. " siku za mwisho . . .", 2:2 (NASB & NIV)
   6. " na mataifa yote watauendea. . .", 2:2-4 (NASB & NIV)
   7. " na pete ", 3:21 (NASB & NIV)
   8. "wingu", 4:5 (NASB & NIV)
   9. "nani atakwenda kwa ajili yetu?", 6:8 (NASB & NIV)
   10. "bikira", 7:14 (NIV, “bikira”)
   11. " wakati ajuapo kuyakataa mabaya na kuyachagua mema. ", 7:15,16 (NASB & NIV)
   12. " bali ni jiwe la kujikwaza na mwamba wa kujikwaa", 8:14 (28:16) (NASB & NIV)
   13. " kwa watu wenye pepo na kwa wachawi; waliao kama ndege na kunong'ona ", 8:19 (NASB & NIV)
   14. "Ashuru! Fimbo ya hasira yangu", 10:5 (NASB & NIV)
   15. "ni mabaki tu watakaorudi. . .", 10:22 (NASB & NIV)
   16. "litatoka chipukizi katika shina la Yese ", 11:1,10 (NIV, "... katika shina")
   17. "hayawani wakali", 13:21; 34:14 (NIV, "hayawani wakali wa nyikani")
   18. " juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini ", 14:13(NIV, " juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini")
   19. "madhabahu katika nchi ya Misri kwa Bwana, na nguzo mpakani mwake kwa Bwana", 19:19 (NIV, katika nchi ya Misri")
   20. Arieli, 29:1-2,7 (NASB & NIV)
   21. "amewaangamiza kabisa", 34:2 (NIV, "amewaangamiza kabisa")
   22. "kulabu yangu katika pua yako", 37:29 (NASB & NIV)
   23. "umezitupa dhambi zangu zote nyuma yako", 38:17 (NASB & NIV)
   24. "neno la Mungu wetu litasimama milele", 40:8 (NASB & NIV)
   25. "Yeye ndiye anayeketi juu ya duara ya dunia", 40:22 (NIV, "Yeye ndiye anayeketi juu ya duara ya dunia")
   26. "Mimi, Bwana, wa kwanza na wa mwisho, mimi ndiye", 41:4; 44:6 (NASB & NIV)
   27. "wala sitazikumbuka dhambi zako", 43:25 (NASB & NIV)
   28. "Je! Yuko Mungu zaidi yangu mimi? Hakika hapana Mwamba", 44:8;45:5 (NIV, " Je! Yuko Mungu zaidi yangu mimi? Hakika hapana Mwamba; mimi sijui mwingine.")
   29. "Mimi naiumba nuru, na kulihuluku giza; mimi nafanya suluhu, na kuhuluku ubaya " 45:7 (NIV, " Mimi naiumba nuru, na kulihuluku giza; mimi nafanya suluhu, na kuhuluku ubaya ")
   30. "Niangalieni mimi, mkaokolewe, enyi ncha zote za dunia. . .", 45:22 (NASB & NIV)
   31. " ya kwamba mbele zangu kila goti litapigwa, kila ulimi utaapa", 45:23 (NASB & NIV)


32. " Kwa ajili ya nafsi yangu, kwa ajili ya nafsi yangu, nitatenda haya. . .", 48:11 (NASB & NIV)
33. "Je! Mwanamke aweza kumsahau mtoto wake anyonyaye.........Naam, hawa waweza kusahau, lakini mimi sitakusahau wewe", 49:15 (NASB & NIV)
34. "Kikombe cha hasira yake", 51:17 (NIV, " Kikombe cha ghadhabu yake ")
35. "Amepigwa na Mungu, na kuteswa.. . .", 53:4 (NASB & NIV)
36. ". . . Lakini Bwana aliridhika kumchubua; Ame*mhu*zunisha", 53:10(NIV," Lakini Bwana aliridhika kumchubua; Amemhuzunisha")
37. "Bali Bwana atakuwa nuru ya milele kwako", 60:19-20 (NASB & NIV)

B. Watu
1. "Mtakatifu wa Israeli" 1:4; 41:8-9; 42:1,19; 43:10
2. "binti wa Sayuni" 1:8
3. "Bwana wa Majeshi" 1:9 (NIV, "Bwana mwenye nguvu")
4. "Tawi la Bwana" 4:2
5. Seraphim 6:2 (NIV, "serafu")
6. Shear-jashub 7:3
7. Immanueli 7:14
8. Maher-shalal-hash-baz 8:3
9. "mwenye nguvu" (El Shaddai) 13:6
10. "Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi" 14:12
11. "yeye atokaye mashariki" 41:2,25 (44:28; 45:1)
12. "Mtumishi wangu" 41:8,9; 42:1,19; 43:10; 52:13
13. Bel...Nebo 46:1
14. walinzi 52:8
15. towashi 56:3

XI. MAENEO YA KI-RAMANI
1. Tarshishi 2:16 (NIV, “meli za biashara”)
2. kabila la Efraimu 7:2
3. Mlima Sayuni 8:18
4. Kabila la Zabuloni 9:1
5. Galilaya 9:1
6. Karkemishi 10:9
7. Sela 16:1; 42:11
8. Zoani 19:13
9. Memphisi 19:13
10. Negebu 21:1 (NIV, “NEGEBU”)
11. Tema 21:14
12. Tiro 23:1
13. Sidoni 23:2
14. Arabah 35:1 (NIV, “jangwa”)
15. Mlima Karmeli 35:2
16. Sharoni 35:2
17. Ararati 37:38
18. Tubali 66:19
19. Yavani 66:19 (NIV, Uyunani)


XII. MASWALI YA KI-MAUDHUI YA MWANAFUNZI
1. Kwanini Mungu awalete watu wake katika mahakama? Ni nini wamefanya? (sura ya 1)
2. Je Mungu hataki sadaka? (1:10-15)
3. Elezea kwanini 5:1-7 ni yenye nguvu na mguso?

4. Kwanini wito wa Isaya haukuandikwa mpaka sura ya 6?
5. Kwanini Isaya hatumii neno la Kiebrania "bikra" katika 7:14?
6. Orodhesha sehemu katika sura ya 7-12 ambapo mtoto anatumika kufunua nyakati mpya.
7. Elezea majina matatu ya makabila ya kaskazini yanayotumiwa katika 9:8-9.
8. Kwanini kuanguka kwa Babeli kunatajwa katika sura ya 13 wakati Ashuru anayezungumzwa na Isaya katika sura ya 10?
9. Ni kwa namna gani Isa. 14 na Ezek. 28 inahusiana na Shetani?
10. Elezea mazingira ya kihistoria ya sura za 36-39
11. Je 40:1-2 ina maana kwamba watu wa Mungu wako uhamishoni? Ikiwa ndivyo, ni kwa namna gani hii inahusiana na uandishi?
12. Ni kwa namna gani Mtumishi wa 42:1 anahusiana na Yesu lakini sio mstari wa 19?
13. Ni kwa namna gani 52:13-53:12 inahusiana na Yesu? kwa Israeli?
14. Ni nini mazingira ya kijiografia ya sura za 56-66?




MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE

# PALESTINA



# UTANGULIZI WA YEREMIA

I. JINA LA KITABU
   A. Kiliitwa jina la nabii.
   B. Jina lake lilimaanisha:
      1. "nguvu za YHWH"
      2. "YHWH huimarisha"

II. URASIMISHAJI
   A. Lilikuwa eneo la "nabii" sehemu ya sheria ya kiebrania.
   B. katika fasihi ya walimu wa kisheria mara nyingi ilikuwa inafikiriwa kuwa manabii wa kwanza(kama vile Mt. 27:9).

III. AINA YA UWASILISHAJI
   A. Kitabu hiki kinaundwa kwa aina kadhaa:
      1. Utamaduni wa sheria ya kiebrania (maono wa Yeremia)
      2. maandiko ya kiebrania (yaliandikwa na Baruki katika mtu wa tatu)
      3. maelezo ya mahubiri ya Yeremia mara nyingi ni katika maandiko (pia kutoka kwa Baruki)
      4. kilio cha mwandishi kwa Mungu katika muundo wa shairi (maungamo ya Yeremia)

   B. Kwa wazi Yeremia inahusisha kwa pamoja unabii ulioandikwa na wa kusimuliwa. Pia kutoka sura ya 36 tunajifunza kwamba baadhi ulitabiriwa/kuandikwa upya.

IV. UANDISHI
   A. Ni dhahili kwamba Yeremia hakuandika sura ya 52 kwa sababu mist. 31-34 inataja matukio ambayo yalitukia katika Babeli. Yeremia alikuwa amechukuliwa kwa nguvu kwenda Misri na vikosi vya waasi wa kiyahudi baada ya kifo cha Gedelia,gavana wa Babeli.
   B. Inawezekana waandishi/wahariri:
      1. Yeremia
      2. Baruki – mwandishi wake
      3. mhariri wa mwisho (Ezra au watu wa sinagogi kuu)

   C. Tunamjua zaidi Yeremia kuliko nabii yeyote:
      1. kutoka ukuhani (uhamishoni) uzao wa Abiathari, I Fal. 2:26-27.
      2. amekulia jirani na Yerusalemu katika Anathothi.
      3. aliitwa na Mungu kama kijana mdogo, 1:2; 25:3 (627 K.K.).
      4. alishawishiwa na kazi, Hosea na Kumbukumbu la torati.
      5. Siku za leo sawa na :
         a. Danieli
         b. Ezekieli
         c. Habakuki
         d. Sefania
         e. Nahumu

      6. Miaka mitano baada ya kuitwa kwake "kitabu cha sheria" kilipatikana katika Hekalu wakati wa matengenezo ya Yoashi. Inashangaza kwamba uhusiano wao kamwe haukutajwa katika maandiko. Kilipopatikana kitabu cha sheria,mfalme alimuuliza nabii wake wa kike aitwaye Hulda (2 Fal. 22:14-20) sio Yeremia.

      7. hisia zake zinaweza kuonekana kwa wazi katika maungamo au kilio chake:
         a. 11:18-12:6
         b. 15:10-21
         c. 17:14-18

d. 18:18-23
e. 20:7-18

8. alichukuliwa mateka kwa nguvu kwenda Misri ambapo aliuwawa na Wayahudi waliokimbilia huko, 43:6.

V. TAREHE

A. Yeremia alizaliwa huko Anathothi yapata mwaka 640 K.K.

B. Kitabu cha Yeremia kiliandikwa katika 1:2 na kufunika kutoka miaka kumi na mitatu ya Yoashi hadi muda wa Gedalia, 627 K.K. - 582 K.K. Inatia mashaka Muda gani Yeremia aliishi Misri na wakimbizi.

C. Makala ya ostrica iliyopatikana huko Lakishi inaelezea kuzingirwa kwake katika mwaka wa 587 K.K. Muundo wa maandiko yake ya kiebrania unafananishwa na Yeremia.

D. Ujumbe wa Yeremia ulilenga katika matukio kutoka kuangamia kwa Samaria (722 K.K.) hadi kuangamia kwa Yerusalemu (586 K.K.).

VI. MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. 686 K.K. - Manase (686-641 K.K.) alikuwa mfalme wa Yuda. Alikuwa mfalme wa Yuda mwovu sana.
B. 664 K.K. – utawala wa Misri ulipata nguvu chini ya Psammetichus (664-610 K.K.).
C. 648 K.K. – kuzaliwa kwa Yoashi.
D. 642 K.K. - Amoni, mfalme wa Yuda aliuwawa na watumishi wake (2 Fal. 21:19-26).
E. 640 K.K. – matokeo ya mwisho utawala wa Ashuru, kifo cha Ashurbanipal.
F. 640 K.K. – Yoashi alikuwa na umri wa miaka minane alipoanza kutawala (2 Fal. 22:1).
G. 628 K.K. – Yoashi alianzisha mabadiliko (2 Nya. 34:3 na kuendelea; 2 Fal. 23).
H. 626 K.K. – wito wa Yeremia (Yer. 1:2).
I. 626 K.K. – Nabopolasari (626-605 K.K.) akawa mfalme wa Babeli mpya.
J. 621 K.K. –kitabu cha sheria kilipatikana toka kwa mfanyakazi aliyekuwa akilitengeneza upya Hekalu (2 Nya. 34:8 na kuendelea; 2 Fal. 22).
K. 614 K.K. –mji mkuu wa Ashuru, Ashuri, ulianguka katika utawala wa Babeli mpya.
L. 612 K.K. – Ninawi, mji wa awali wa Ashuru kuharibiwa na Babeli mpya na Umedi
M. 609 K.K. – Yoashi aliuwawa huko Megido akishindana na Farao Neko II (610-594 K.K.) ambaye alijaribu kuwasaidia mabaki huru wa jeshi la Ashuru (2 Nya. 35:20-24; 2 Fal. 23:28-30).
   - Yehoahazi II (609 K.K.), mwana wa Yoashi, alifanywa mfalme katika sehemu ya baba yake lakini kwa miezi mitatu pekee. Farao Neko alimpeleka Misri.
   - Yehoiakimu (609-598 K.K.) aliwekwa katika kiti cha ufalme wa Yuda na Farao Neko. Aliachwa kwenye kiti cha ufalme wa Yuda na Nebukadnezza II mwaka wa 605 K.K. Baadaye aliasi kwa kufanya ushirikiano na Misri. Mwana wake, Yehoiakimu, alimrithi kwa miezi mitatu na aliwekwa na Nebukadnezza na Zedekia mwaka wa 597 K.K.
N. 605 K.K. –Babeli mpya waliwashinda Wamisri na kuyabakisha majeshi ya Ashuru huko Karkemeshi.
O. 605 K.K. - Nebukadnezza II alipitia Palestina na kudai malipo ya kodi (akimchukua Danieli na uhamisho wa awali.) kulikuwa na vamizi nne zilizoathiri Yuda na Yerusalemu, 605,597, 586 na 582 K.K.
P. 601 K.K. - Nebukadnezza II alipoteza katika vita umiliki wa Misri (kufikia mwisho).

VII. VIPENGELE VYA FASIHI

A. Muundo wa kitabu ni wenye kiini au wa kisasa, sio wa kufuatana. Inawezekana ni mkusanyiko kadhaa wa magombo/ujumbe wa Yeremia, 1-25, 30-33 na 46-51.

B. Toleo la LXX na MT kuna utofauti mkubwa. Zaidi ya maneno 3000 ya MT hayaonekani katika toleo la LXX. Pia mpangilio wa mataifa katika sura 46-51 ni tofauti, kama vile yalivyowekwa katika kitabu baada ya sura 25. Tamaduni zote za MSS zalipatikana katika magombo ya bahari ya chumvi.

C. Ainisho la madhanio (msingi unafuata Harrison na Young):
1. sura ya 1 – wito wa Yeremia na mapatano.
2. sura ya 2-25 – dhambi ya Yuda kutoka miaka ya awali ya huduma ya Yeremia.
3. sura ya 26-29; 34-35 – maisha binafsi ya nabii.
   a. ujumbe wa YHWH kwa Zedekia na maendeleo ya Hanania, 26-29.
   b. Warekabi, 34-35
   c. matukio ya kihistoria kutoka utawala wa Yehoyakimu - Zedekia, na Gedalia hadi Misri, 36-45
4. sura ya 30-33 – ahadi ya urejesho kwa watu wa Mungu:
   a. kimwili
   b. kiroho
5. sura ya 46-51 – unabii dhidi ya mataifa yanayoizunguka (pia sura ya 25:12-38):
   a. Misri - 46 (Isaya 19; Ezek. 29-32)
   b. Filisti - 47 (Amosi 1:6-8; Isaya. 14:29-32; Ezek. 25:15-17)
   c. Moabu - 48 (Amosi 2:1-3; Isaya 15-16; Ezek. 25:8-11)
   d. Amoni - 49:1-6 (Amosi 1:13-15; Ezek. 25:1-7)
   e. Edomu - 49:7-22 (Amosi 1:11-12; Isaya 21:11-12; Ezek. 25:12-14; Obadia)
   f. Shamu - 49:23-27 (Amosi 1:3-5; Isaya 17:1-3)
   g. Arabia - 49:28-33
   h. Elamu - 49:34-38
   i. Babeli - 50-51 (Isaya 13:1-14; Hab. 2:6-17)
6. sura ya 52 – kuangamizwa kwa Yerusalemu (kama vile. II Fal. 24:18-25:30)

D. maelezo yanatia shauku kwamba katika sura ya 1-25 ujumbe wa Yeremia unatambulishwa na tungo "neno la YHWH likanijia" ambapo katika sura ya 26-51 inatambulishwa na "neno la YHWH likamjia Yeremia."

E. Jedwali la unabii wa Yeremia kwa mfalme atawalaye:

| | E. J. Young: | R. K. Harrison: |
|---|---|---|
| 1. | Chini ya Yosia (640 K.K. - )<br>1:1-19; 2:1-3:5; 3:6-6:30;<br>7:1-10:25; 11:1-13:27;<br>14:1-15:21; 16:1-17:27; 18:1-20:18 | <br>1:1-19; 2:1-3:5; 3:6-6:30;<br>7:1-10:25; 18:1-20:18 |
| 2. | Chini ya Yehoahazi (609 K.K.) | |
| 3. | Chini ya Yehoyakimu (609 K.K.)<br>25; 26; 27; 35; 36; 45 11:1-13:14; 14:1-15:21; 16:1-17:27;<br>46-49 2; 23; 25; 26; 35; 36; 45; 46-48 | |
| 4. | Chini ya Yekonia (598 - 596 K.K.) | 31:15-27 |
| 5. | Zedekia (597 K.K.)<br>21:1-22:30; 23; 24; 27<br>28; 29; 30-31; 32; 34;<br>37; 38; 39 | <br>21:1-22:30; 24:1-10; 27; 28; 29;<br>30-31; 32; 33; 34; 37; 38; 39; 49;<br>50:1-51:64 |
| 6. | Chini ya Gedalia<br>40; 41; 42; 43-44:30; | <br>40:1-42:22; 43:1-44:30 |

50-52

7. Kiambatisho cha kihistoria 52:1-34

VIII. DHAMIRA KUU

A. Muda wa hukumu ni sasa kwa sababu Yuda hakutubu! Yeremia alitilia mkazo dhambi, hukumu kisha urejesho; 1:4-10.

B. kawaida ya ibada au utaratibu wa dini pasipo maisha binafsi ya imani katika Mungu ni maangamizo! (sur. 7; Isa. 29:13).

C. Yuda amepoteza matumaini kwa kuzifuata njia za kawaida, ibada ya sanamu na dhambi! Amelivunja agano la Mungu, kielelezo kama makubaliano ya ndoa (kama vile. 2:1-3:5).

D. toba binafsi na imani ni msingi wa maagano mapya ya Mungu (31:31-34) sio imani ya familia (31:29; Ezek. 18).

E. maagano mapya ni ya kudumu (31:35-37) kwa sababu sio katika hali ya matendo ya mwanadamu lakini ni katika nguvu na neema ya Mungu (Ezek. 36:26-27).

IX. MANENO/AU TUNGO NA WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHTASARI (NASB)

A. Maneno na /au tungo
1. nabii, 1:5 (NASB na NIV)
2. ufito wa mlozi, 1:11 (NASB na NIV)
3. kaskazini, 1:13 (NASB na NIV)
4. jifunge viuno,1:17 (NIV, "kaa tayali!")
5. hati ya talaka, 3:8 (NIV, "kibali cha kutengana")
6. "akazini na mawe a miti," 3:9 (NASB na NIV)
7. "govi za mioyo yenu," 4:4 (NIV, "kutahiri mioyo yenu")
8. "zeri katika Gileadi," 8:22 (NASB na NIV)
9. "kukaa nywele zao katika mahekalu," 9:26 (NIV, "katika sehemu zilizotengwa")
10. "kama Bwana aishivyo," 12:16 (NASB na NIV)
11. "kuteka wakati wa adhuhuri," 15:8 (NIV, "wakati wa adhuhuri nitamleta mtekaji")
12. "jeshi lote la mbinguni," 19:13 (NIV, "mng’ao wa majeshi yote")
13. kuangamizwa kabisa, 25:9 (NIV, "kuangamiza kabisa")
14. "vyombo vya nyumba ya Bwana," 27:16 (NIV, "vyombo...")
15. "wakati wa taabu ya Yakobo," 30:7 (NIV, "wakati wa taabu kwa ajili ya Yakobo")
16. agano jipya, 31:31 (NASB na NIV)
17. "walipomkata ndama vipande viwili na wakapita katikati ya vipande vile," 34:18 (NIV, "walimkata ndama katika vipande viwili na kisha kupita katikati yake")


B. Watu
1. Yosia, 1:2,3
2. Yehoyakimu, 1:3
3. Baali, 2:8
4. Manase, 15:4
5. Nebukadnezza. 21:2,7
6. Hanania, 28:1
7. Baruku, 32:12,13,16
8. Moleki, 32:35
9. Warekabi, 35:1 (NIV, “familia ya Warekabi”)
10. Ebed-Meleki, 38:7
11. Gedalia, 39:14 & 40-41
12. Farao Neko, 46:2 (NIV, “Neko”)
13. Kemoshi, 48:7,13,46
14. Ben-Hadadi, 49:27
15. Beli, 50:2; 51:44
16. Merodaki, 50:2


X. MAENEO KI-RAMANI

1. Anathothi, 1:1
2. Kitimu
3. Nofu
4. Shilo, 7:12
5. bonde la wana wa Hinomu, 7:31
6. Sodoma na Gomora, 23:14
7. Tiro, 25:22
8. Lakishi, 34:7
9. Mizpa, 40:6
10. Gibeoni, 41:12
11. Bethlehemu, 41:17
12. Karkemishi, 46:2
13. Betheli, 48:13
14. Hazori, 49:28
15. Elamu, 49:34

XI. MASWALI YA KI-MAUDHUI KWA MWANAFUNZI

1. Kwa nini Yeremia inamuwia vigumu kutoa maelezo?
2. Ni kwa muda gani Yeremia alihubiri?
3. Elezea maono mawili ya 1:11-16.
4. Kwa nini sura ya 2 inawasilishwa kama jambo la sheria? (kama vile. 4-8, 9, 29)
5. Kwa nini sura inawasilishwa kama jambo la talaka?
6. Taja hali nne ambazo zinaonyesha Mungu anadai toba katika 4:1-2.
7. Ni kwa namna gani sura ya 7 na 26 zinahusiana?
8. Je, Yeremia alishutumu utaratibu wa sadaka katika sura ya 7?
9. Kwa nini wenyeji wa mji wa Yeremia walijaribu kutaka kumua yeye? (sura 11-12)
10. Kwa nini 12:14-17 na 16:19-21 ni za muhimu sana?
11. Elezea ni kwa namna gani kundi na dhambi binafsi zinasimuliwa katika 16:10-13
12. Ni kwa namna gani 17:10 inasimulia Gal. 6:7?
13. Fafanua njia tofauti Yeremia alitumia sitiari ya mfinyanzi katika sura 18 na 19


MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE
KAS
MAGH
MASH
KUS


PALESTINA
0 10 20 30 40
VIPIMO KATIKA MAILI

# UTANGULIZI WA MAOMBOLEZO

I. JINA LA KITABU

A. Kwa Kiebrania (MT) jina ni neno la kwanza la kitabu ambacho ni "Ah How" ['*echah*] (kama vile 1: 1, 2: 1, 4: 1). Hii ilikuwa neno la kawaida linalojulikana katika mazishi.

B. Katika Tafsiri ya Bibli ya Agano la Kale kutoka Kiebrania kwenda Kiyunani (LXX) ilikuwa majina "maombolezo" kutoka kwa mizizi ya Kiyunani "kulia kwa sauti."

C. Kitabu cha Sheria za Kiyahudi alikiita "maombolezo."

D. Toleo la Kilatini linasema kuwa "Inajumuisha maombolezo ya Yeremia Mtume."

II. URASIMISHAJI

A. Ni katika orodha maalumu ya vitabu kutoka sehemu ya Maandiko ya Sheria ya Kiebrania inayoitwa *Megilloth* (vitabu vitano). Kila kimoja kilisomwa siku ya sikukuu ya kwanza:

1. Wimbo ulio Bora - Pasaka
2. Ruthu – Pentekosti
3. Mhubiri – Pembe ya Hema
4. Esta – Purimu
5. Maombolezo – Kuanguka kwa Yerusalemu na uaharibifu wa Hekalu la Sulemani

B. Sehemu ya Maandiko ya kifungu cha Sheria ya Kiebrania huweka Maneno ya Wimbo Ulio Bora baada ya Zaburi, Mithali na Ayubu na kabla ya Ruthu, Maombolezo, Mhubiri na Esta. Biblia ya Kiingereza inafuata amri ya LXX.

C. Maombolezo yanasomewa tarehe 9 ya Ab (katikati ya Julai) katika ukumbusho wa uharibifu wa Hekalu la Sulemani na jeshi la Nebukadneza II katika 586 K.K. Katika Ukristo wa baadaye pia ulikumbuka kuanguka kwa Yerusalemu kwa mkuu wa Kirumi, Tito katika 70 B.K.

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Kila sura tano ni tofauti ya uombolezo / ufufuo wa mazishi. Aina hizi za mashairi ni za kawaida katika Mashariki ya Kale ya Karibu, kurudi kwa Sumeri. Kwa Israeli wanaonyesha huzuni juu ya hali ya sasa lakini matumaini ya siku zijazo.

B. Mashairi ya kwanza ya manne ni ya kimafumbo. Kila mstari huanza na barua inayofuata ya alfabeti ya Kiebrania. Hii inaweza kuwa njia ya mfano ya kueleza huzuni kamili.

C. Mashairi ya Kiebrania yanategemea ulinganifu wa mawazo, sio mashairi.

1. Mstari, sio maneno, ni ufunguo wa fasihi.
2. Ulinganifu kawaida ni mistari miwili au mitatu.
   a. sawa kufanana - mistari inaonyesha mawazo sawa kwa maneno tofauti
      (1) Zab. 3:1; 8:40; 83:14; 103:3
      (2) Mith. 20:1
      (3) Maomb. 1:2, 3
      (4) Isa. 1:3
      (5) Amosi 5:24
   b. ulinganifu wa kinyume - mistari ya kuelezea mawazo kinyume na matumizi ya kulinganisha au kusema chanya na hasi ya suala hilo.
      (1) Zab. 1: 6; 90: 6
      (2) Mith. 1:29; 10: 1, 12; 15: 1; 19: 4
   c. ulinganifu wa maandishi - mistari huendeleza mawazo
      (1) Zab. 1: 1-2; 19: 7-9

(2) Maomb. 1: 4

IV. UANDISHI

A. Kitabu chenyewe hakitoi uandishi wo wote. Ni wazi kwamba kimeandikwa na ushahidi wa macho juu ya kuzingirwa na kuanguka kwa Yerusalemu katika 586 K.K.

B. Baba Bathra 15a na Targums ya Yer. 1: 1 huonyesha uandishi kwa Yeremia.

C. Septuagint inafungua kitabu hicho kwa "na ikawa baada ya Israeli kuhamishwa, na Yerusalemu ikaharibiwa, Yeremia akaketi akalia na kuandika kilio hiki juu ya Yerusalemu na kusema ..." Iliiweka kitabu baada ya Yeremia.

D. Vulgate huanza kitabu hicho na, "Inajumuisha kilio cha Yeremia nabii."

E. Peshitta (karne ya 5 K.K tafsiri ya Syriaki) ilisema kitabu "Kitabu cha Maombolezo ya Yeremia Mtume."

F. Ushahidi wa uandishi:

1. kwa Yeremia:
   a. Yeremia anafikiriwa kuwa ndiye mwandishi kwa sababu ya 2 Nyakati. 35:25. Lakini angalia hii ina maana ya kilio kwa Yosia, si Yerusalemu.
   b. Vifungu vingi katika Yeremia husema juu ya kuomboleza kwake juu ya hali ya siku yake, 7:29; 8:21; 9: 1,10,20 (kama vile Maomb. 3: 48-51).
   c. Kuna kufanana kwa msamiati .
   d. Ile"I" ya 3: 1 inaweza kurejerea kwa Yeremia.
   e. Mwandishi alikuwa wazi shahidi wa kuanguka kwa Yerusalemu.
2. dhidi ya Yeremia:
   a. Yeremia anasema Mungu alimtuma Babeli kuhukumu lakini 3: 59-66 inaonekana tofauti.
   b. Yeremia hakutaka kusema ujumbe wa kinabii umekoma, 2: 9c.
   c. Yeremia hakuweza kutetea msaada kutoka Misri, 4:17.
   d. Yeremia hakuweza kumtumaini Zedekia, 4:20.
   e. Mashairi haya ya kwa mafumbo yanajenga sana ambayo ni tofauti kabisa na mtindo wa Yeremia wa kujipenda.
   f. Mtindo wa muundo wa kila shairi 5 pia ni tofauti. Baadhi wana mistari mirefu, baadhi ya muda mfupi. Idadi ya mistari inayoanza na barua hiyo inatofautiana. Mfano hubadilika kutoka kwa shairi hadi shairi. Yote hii inaashiria zaidi ya mwandishi mmoja.

V. TAREHE/MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. Hali ya kihistoria ni kuanguka kwa Yerusalemu kwa jeshi la Babeli katika 586 K.K
B. Kwa mazingira ya kihistoria yanasoma 2 Wafalme 25: 8-12 na Yer. 52.
C. Wengine wanaona kitabu hiki kama kinachohusiana na Wayahudi ambao walibaki Yuda na kila mwaka wakakumbuka kuanguka kwa Yerusalemu, Yer. 41: 4-5.

VI. VIPENGELE VYA KIFASIHI

A. Yerusalemu umefanyika, mke wa mtumwa, sura 1.
B. Uwezo huleta wajibu, ghadhabu ya agano la YHWH, sura ya 2.
C. Maumivu ya kibinafsi, sura ya 3.
D. Uwezo huleta wajibu, watu wa agano wa dhambi, sura ya 4
E. Kuamini na kutumaini katika Agano la Mungu, sura ya 5.

VII. KWELI KUU

A. Mashairi haya yanaonyesha huzuni na hisia ya kupoteza ambayo watu wa Mungu walihisi:

1. kupoteza kwa Yerusalemu,
2. uharibifu wa Hekalu,
3. YHWH kufutilia mbali Agano la Musa. Hizi zilisikika kwa kasi kwa sababu ya ahadi za Mungu katika:
    (a) 2 Sam. 7: 10-16
    (b) Isa. 37: 30-35

B. Mashairi haya yalisisitiza:
    (1) Mamlaka ya kiutawala ya Mungu,
    (2) haki ya Mungu,
    (3) hukumu ya Mungu,
    (4) ahadi za Mungu za kurejeshwa.

C. Yuda imeharibiwa kwa sababu Ilivunja Agano la Musa (Kumb. 27-28). Kushindwa kwa Babeli sio udhaifu wa YHWH, bali dhambi ya watu wake. YHWH ataleta ushindi nje ya nguvu Zake katika wakati ujao (3: 22-23, 25).

D. Ahadi za Mungu zote ni masharti na zisizo na masharti. Dhana ya agano inahitaji mwitikio sahihi.

IX. MANENO NA/AU TUNGO NA WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHTASARI

A. Maneno na/au tungo
1. " wapenzi wake wote"1: 2, 19 (NASB & NIV)
2. "Binti mwanamwali wa Yuda" 1:15 (NASB & NIV)
3. "Kiti cha miguu yake"2: 1 (NASB & NIV)
4. "Bwana amekuwa adui "2: 5 (NIV,"Bwana ni kama adui")
5. "wakapiga makofi yao...wakabusu...wakatingisha vichwa vyao" 2:15 (NIV, "piga makofi...fyonya...tingisha")
6. "Inua mikono yako Kwake" 2:19; 3:41 (NASB & NIV)
7. "Wanawake wanapaswa kula watoto wao"2:20; 4:10 (NASB & NIV)


B. Watu
1. "Mimi ni mwanadamu" 3: 1

X. MAENEO YA KI-RAMANI


1. Yuda, 1: 3
2. Sayuni, 1: 4
3. Yerusalemu, 1: 7
4. Uzi, 4:21

XI. MASWALI YA KI-MAUDHUI KWA MWANAFUNZI

1. Elezea muundo wa maandishi ya Maombolezo.
2. Kitabu hiki cha Biblia kinatusaidiaje kukabiliana na mateso na machafuko?
3. Kitabu kinasema nini sababu ya uhamisho? (1: 5, 18)
4. Je! 2:17 inahusiana na Kumb. 27-28?
5. Kwa nini 3: 19-38 ni muhimu sana?


KAS
MAGH
MASH
KUS
MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE

# PALESTINA



# UTANGULIZI WA EZEKIELI

I. JINA LA KITABU

A. Hiki kinapewa jina baada ya mzungumzaji wake mkuu, nabii Ezekieli.

B. Jina lake linamaanisha "Mungu huimarisha," au "Mungu anaweza kunifanya imara."

II. URASIMISHAJI

A. Kitabu hiki kilikuwa na baadhi ya ugumu uliokuwa ukitegemewa kuwa katika sheria za Kiebrania:
   1. Hekalu la Ezekieli na hatua zake ni tofauti na lile la Musa.
   2. lugha halisi ya mambo yanayoonekana, hasa sura za 1, 8 na 10.

B. Rabbi Hanania mwana wa Hezekia wa shule ya sheria za Kiyahudi ya Shammai, anasemekana kuwa na magudulia 300 ya mafuta ya kumpatanisha Ezekieli na Musa (kama vile Shabb. 14b; Menahuth 45a; Hagigah 13a).

C. Desturi za Kiyahudi zilisema kwamba Eliya alirudishwa kabla ya Masihi, huyu angetatua matatizo yalitokuwepo kati ya Ezekieli na Musa.

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Kitabu hiki kimejumuisha aina nyingi:
   1. unabii (sur. 37)
   2. matukio ya siku za mwisho (sur. 1, 8-10, 38-39, 40-48)
   3. ushairi
   4. nathari au lugha ya mjazo
   5. mifano ya kimaigizo (sur. 4-7, 12)
   6. uainishaji (sur. 16)

B. Namna ya kuzifasiri sura za 40-48
   1. Maelezo ya Ufunguzi
      a. Muktadha wa kifasihi wa sura za 40-48 ni ahadi ya urejesho kama ilivyoandikwa katika sura za 33-39.
      b. Kipengele hiki kinanelezwa katika sampuli ya usanifu - majengo wa hekalu la matukio ya siku za mwisho kama Kut. 25-27 ilivyo kuhusiana na Hekalu.
      c. Maelezo ya kimuhtasari:
         1) Sura za 40-43 — Hekalu linarejeshwa
         2) Sura za 44-46 — taratibu zinarejeshwa
         3) Sura za 47-48 — nchi inafanyiwa marekebisho
      d. Unabii huu unalitumia agano la awali katika ya Mungu na Ibrahimu na uzao wake kuusawiri rejesho wa wakati wa mwisho wa watu wa Mungu.
      e. Kihistoria sura hizi lazima zihusiane  kurudi toka Uhamishoni (43:2). Bado, kwa hali iliyo wazi hili ni tukio la siku za mwisho katika namna Fulani kwa sababu hili haliendani na kipindi kilichofuatia baada ya uhamisho.
   2. Baadhi ya tafsiri zifaazo:
      a. Kamwe haikumaanisha kukamilishwa kifasihi;
      b. Huu ulikuwa unabii shurutushi ambao Wayahudi hawakuuhitikia kama ilivyotakiwa;
      c. Huu ulitimizwa kwa umbali katika kipindi cha kurudi toka Uhamishoni chini ya Zerubabeli na Yoshua;
      d. Huu ulitimizwa wakati wa hekalu la Herode;
      e. Mara nyingi huu ulimaanisha kuwa wa kiishara (kama vile *Prophecy Interpreted* na John Milton);
      f. Huu utakamilishwa katika hekalu la siku za mwisho.

3. Matatizo katika kulitafsiri andiko hili:
   a. Hakuna mpangilio maalumu wa kihistoria kwa sura za 38 na 39 au 40-48. Kwa sababu hakua mpangilio wa kihistoria, kwa vyo vyote katika andiko au historia, watafsiri walio wengi wanaufanya utabiri huu kuwa wa matukio ya siku za mwisho;
   b. Agano Jipya:
      (1) huu unaonekana kuuweka kando mfumo wa kidhabihu wa wakati mwa mwisho ulio katika Ebr. 9 na 10;
      (2) huu unaonekana kuyajumuisha Mataifa ambapo Eze. 40-48 ni ya kizalendo sana.
   c. Yesu anaonekana kuwakataa Wayahudi kama chombo cha ukombozi wa Mungu ndani ya fumbo la wapangaji dharimu (kama vile Mt. 21:33-46; Mk. 12:1-12; Lk. 20:9-19;
   d. Japo naamini kuwa Mungu atalitumia taifa la Israeli katika mazingira ya wakati wa mwisho (kama vile Rum. 9- 11), Naamini kuwa Kanisa ni Israeli ya Kiroho (kama vile Rum. 2:28-29; Gal. 3:1na kuendelea; 6:16; Efe. 2-3.

C. Ezekieli aliziunganisha jumbe zake zilizo nyingi katika muundo wa kiuandishi. Hizi hazikutolewa katika katika masimulizi kama zilivyokuwa zile za Isaya na Yeremia. Hizi zimeundwa vizuri sana.

IV. UANDISHI

A. Uandishi wa kitabu hakuwai kutiliwa mashaka kamwe. Kitabu kizima isipokuwa 1:2-3 kimeandikwa katika nafsi ya kwanza, umoja (tawasifu.)

B. Desturi za Kiyahudi, Baba Bathra 15a, zinasema "watu wa Sinagogi walikiandika kitabu cha Ezekieli na vingine Kumi na Viwili." Kama tulivyo kwisha liona neno "aliandika" lenye kumaanisha alihariri au aliunganisha kwa pamoja.

C. Josephus' *The Antiquities of the Jews*, 10:5:1, anasema kwamba Ezekieli aliandika vitabu viwili. Hiki kinaweza kurejelea sifs bainifu ya muundo wa manabii wengi wa Kiebrania kwa sababu vitabu vyao vimegawanyika kwa urahisi na kwa nusu-nusu. Katika sehemu ya kwanza mazingira ya kihistoria ni zile siku zake. Katika sehemu ya pili sehemu ya kitabu mazingira ni ya wakati ujao (kama vile Isa. 1-39 na 40-66; Dan. 1-6 na 7-12; Zek. 1-8 & 9-14 na Eze.1-32 na 33-48). Hii inaweza kuwa sababu ya Jerome kueleza mashaka yake kuhusu umoja wa Ezekieli. Pia hii ndiyo sababu ya Josephus kufikiri kuwa huyu aliandika vitabu viwili.

D. Wote tunafahamu ya kuwa nabii Ezekieli anatokana na kitabu hiki. Huyu hatajwi mahali po pote pale katika kitabu cha Agano la Kale:
   1. huyu alikuwa kuhani wa uzao wa Zadoki, 1:3,
   2. huyu alioa lakini hakuwa na watoto, 24:16-18,
   3. huyu alichukuliwa mateka na Nebukadneza II wakati alipokuwa na umri wa miaka ishirini na mitano mnamo 597 K.K. kwa makubaliano na Mfalme Ahikamu, 1:1; I Fal. 24:14-16,
   4. huyu alihamishiwa katika makazi ya Kiyahudi ambayo hayakuwa mbali kutoka Babeli katika mfereji wa umwagiliaji uliochimbwa, Chebar, 1:1,3, uitwao Tel-abibu, 3:15,
   5. huyu alihubiri miaka ipatayo ishirini na miwili, 1:1-2; 29:17,
   6. huyu alikuwa na nguvu lakini nabii mwenye huruma, 9:8; 11:13.

V. TAREHE

A. Huyu alizaliwa mnamo 623 K.K. huko Yerusalemu.

B. Ezekieli ni mmoja wa manabii wa karne ya saba: Yeremia, Danieli, Nahumu, Habakuki na Sefania.

C. Wakati wa kipindi cha kushamiri kwa utawala wa ki-Babeli chini ya Nabopolasa na taji ya mfalme Nebukadneza II, Mungu anazungumza kupitia manabii hawa katika maeneo tofauti tofauti:

1. Danieli alichukuliwa mateka na Nebukadneza mnamo mwaka 605 K.K. Huyu alihamishiwa eneo lililoko Babeli, Dan. 1:1.
2. Ezekieli alichukuliwa mateka na Nebukadneza mnamo mwaka 597 K.K. mafundi stadi wapatao 10,000 na Mfalme Ahikamu, II Fal. 24:14-16.
3. Yeremia alibaki Yerusalemu hadi kutokea kwa kifo cha Gedalia.

D. Ezekieli alizipa tarehe nabii zake. Tarehe hizi zinaonyesha kwamba kitabu hiki hakiko katika mpangilio maalumu:

| | Siku | Mwezi | Mwaka wa Uhamisho wa Yehoakimu |
|---|---|---|---|
| 1. maono, 1:1 | 5 | 4 | 13 |
| 2. maono, 1:2 | 5 | 4 | 5 |
| 3. maono, 8:1 | 5 | 6 | 6 |
| 4. maswali ya wazee, 20:1 | 10 | 5 | 7 |
| 5. kuzingirwa kwa Yerusalemu kunaanza, 24:1 | 10 | 10 | 9 |
| 6. unabii dhidi ya Tiro, 26:1 | 1 | ? | 11 |
| 7. unabii dhidi ya Misri, 29:1 | 12 | 10 | 10 |
| 8. unabii dhidi ya Misri, 29:17 | 1 | 1 | 27 |
| 9. unabii dhidi ya Misri, 30:20 | 7 | 1 | 11 |
| 10. unabii dhidi ya Misri, 31:1 | 1 | 3 | 11 |
| 11. unabii dhidi ya Misri, 32:1 | 1 | 12 | 12 |
| 12. unabii dhidi ya Misri, 32:17 | 15 | (12) | 12 |
| 13. kuanguka kwa Yerusalemu, 33:21 | 5 | 10 | 12 |
| 14. maono ya Yerusalemu mpya, 40:1 | 10 | 1 | 25 |

E. Hivyo huduma ya Ezekieli ilianza mnamo mwaka 592 na kuendelea hadi mwaka 570 K.K., yamkini ni muda mrefu sana.

## VI. MAZINGIRA YA KIHISTORIA

## VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI

A. Unabii za Ezekieli zinaweza kugawanyika katika jumbe tofauti tofauti mbili:
1. kabla ya kuanguka kwa Yerusalemu mnamo mwaka 586 K.K. mahubiri yake yalibainishwa kwa wito wa toba kwa sababu ya ujio wa hukumu ya Mungu. (1-32)
2. baada ya kuanguka kwa Yerusalemu mahubiri yake yalibadilika na kuwa katika tumaini, urejesho, msamaha. (33-48)

B. Ainisho Fupi
   1. Wito wake katika huduma, 1-3.
   2. Dhambi ya Watu wa Agano na baada ya kuanguka kwa Yerusalemu, 4-24.
   3. Hukumu ya Mungu juu ya mataifa yaliyozunguka, 25-32
   4. Ahadi ya Mungu ya urejesho kwa watu wake, mji na Hekalu, 33-37.
   5. Ujio wa kihama toka Kaskazini, 38-39.
   6. Maono ya kurejeshwa kwa Hekalu, 40-48.

VIII. KWELI KUU

A. Wayahudi waliteseka kwa sababu ya dhambi zao wenyewe, si udhaifu wa YHWH.

B. Agano la imani ina vyote kipengele cha ushirika na kipengele binafsi. Agano Jipya liliotajwa katika Yer. 31:31-34 kimsingi ni la kibinafsi, kama zilivyo sura za 18 na 33. Pia hili liliwekewa dhamana kwa matendo ya Mungu (kama vile sura za 36-37). Huu ni ulinganifu wenye kufanana kati ya ukuu wa Mungu na majukumu ya kiagano kwa mwanadamu yanayopatikana katika Agano Jipya.

C. Mungu ni mwaminifu juu ya uzao wa Ibrahimu na Daudi. Agano litahimarishwa tena, sura za 37, 40-48. Uhamisho halikuwa tendo la upendo!

D. Matatizo ya Wayahudi hayaishi, sura za 38-39 (kama vile Dan. 7-12). Kuna mapambano yanayoendelea kati ya watu wa Mungu na anguko, ya kiroho, ubinadamu uliojaribiwa (Zab. 2).

IX. MANENO NA/AU VIFUNGU NA WATU WA KUWATAMBUA KIMUHTASARI

A. Maneno na /au Tungo
   1. shekeli, 4:10
   2. zabarajadi, 10:9 (NIV, “zabarajadi”)
   3. "Toboa mahali ukutani mbele ya macho yao, ukachukue vitu kwa kuvipitisha pale," 12:5
   4. mtu mbaya, 13:18 (NIV, “wachawi”)
   5. "jifanyieni moyo mpya na roho mpya," 18:31 (NIV, “pokea moyo mpya na roho mpya”)
   6. "walipitisha motoni," 20:26 na 31
   7. *Bamah,* 20:29
   8. "nitawapitisha chini ya fimbo," 20:37
   9. terafi, 21:21 (NIV “vinyago”)
   10. "watakuondolea pua yako na masikio yako," 23:25
   11. "Ulikuwa ndani ya Adeni, bustani ya Mungu," 28:13
   12. kazi ya matari,
   13. ya daima, 46:15 (NIV, “kila asubuhi kwa sadaka zisizo halali”)


B. Watu
   1. "viumbe hai vinne," 1:5 (NIV, “kwa viumbe hai”)
   2. Mwanadamu, 2:1
   3. Tamuzi, 8:14
   4. kerubi, 10:6
   5. Danieli, 14:14, 20
   6. Ohola na Oholiba, 23:4
   7. wana wa Sadoki, 40:46

X. MAENEO KI-RAMANI
   1. mto Kebari, 1:1 (NIV, “Mto Kebari”)
   2. nchi ya Wakaldayo, 1:3 (NIV, “nchi ya Wababeli”)
   3. Tiro, 26:2 7.

4. Tubali, 27:13 (NIV, “Uyunani”)
5. Tubali, 27:13 Wababeli”)
6. Meshaki, 27:13
7. Soani, 30:14

XI. MASWALI YA KI-MAUDHUI KWA MWANAFUNZI

1. Nini anachokiona Ezekieli katika sura ya 1? Kwa nini haikuwa kawaida katika Babeli?
2. Je! gombo la sura ya 2 linawakilisha nini?
3. Je! natendo ya kiishara ya sura za 4 na 5 yanawakilisha nini?
4. Kwa nini sura ya 8 inatisha sana? Je! hii ilikuwa ya kweli aua ya kiishara?
5. Je! sura za 1 na 11 zinahusianaje?
6. Kwa nini sura ya 18 si ya kawaida sana katika kitabu cha Agano la Kale?
7. N kwa namna gani Shetani alikuwa na uhusiano na Mfalme wa Tiro (28)? Kwa nini sura ya 28 ni maelezo yamhusuyo Shetani?
8. Ni kwa namna gani sura za 36-39 zinahusiana na siku zile za Ezekieli?
9. Ni kwa namna gani 18:30-32 inahusiana na 36:26-27?
10. Hekalu la Ezekieli ni la kiishara au ni halisi?


KAS
MAGH
MASH
KUS
MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE

PALESTINA



# UTANGULIZI WA KITABU CHA DANIELI

I. JINA LA KITABU
   A. Hiki kimeitwa kwa jina  la mzungumzaji wake mkuu na nabii.
   B. Jina lake linamaanisha "Mungu ndiye mwamuzi wangu."

II. URASIMISHAJI
   A. Kitabu cha Danieli ni sehemu ya mgawanyo wa tatu na wa mwisho wa sheria za Kiebrania, "Maandiko."

   B. Hii ni kwa sababu:
      1. Wayahudi walimfikilia huyu kama mzungumzaji, si nabii,.
      2. Hii inaakisi tarehe ya muundo unayofuatia (uhariri).
      3. Hii imebeba sehemu fulani za Kiaramu (2:4b-7:28), kama Ezra.

III. AINA YA UWASILISHAJI
   A. Kama walivyo manabii wengi wa Kiebrania huu ni muungano wa aina nyingi:
      1. Sura 1-6 ni simulizi za kihistoria zilizoandikwa katika nafsi ya tatu. Hizi zinayaakisi maisha na nyakati za Danieli.
      2. Sura 7-12 ni matukio ya baadaye haya mara nyingi yanaelezwa katika taswira ya matukio ya siku za mwisho katika nafsi ya kwanza (kama vile 7:1,9; 8:1; 9:2).

   B. Huu ni mpangilio maalumu wa kihistoria kisha yanayofuatia pia yanapatikana katika:
      1. Isaya, 1-39 na 40-66
      2. Ezekieli 1-32; 33-48
      3. Zekaria 1-8 & 9-14.

   C. Fasihi ya Matukio ya mwisho ni aina ya kipekee ya Kiyahudi. Hii ilikuwa ikitumika mara kwa mara katika hofu kuu kuihakikisha imani ya utawala wa Mungu wa historia na ahadi za ukombozi ujao na baraka.

   D. Hii inaelezwa kwa matumizi ya juu ya lugha za kiishara
      1. rangi,
      2. wanyama,
      3. namba,
      4. maono/ndoto,
      5. upatanisho wa kimalaika,
      6. maneno ya mkusanyiko wa sheria za siri,
      7. uwili ulio dhahiri—kati ya Mungu na uovu.

IV. UANDISHI
   A. Kitabu hiki hakimtaji mwandishi wake. Sura za 1-6 zimeandikwa katika nafsi ya tatu ambapo 7-12 ziko katika nafsi ya kwanza, 7:1,9; 8:1; 9:1.

   B. Desturi za Kiyahudi, Baba Bathra 15zinasema, "watu wa Sinagogi kuu ndiyo waliokiandika kitabu cha Danieli." Hii inamaanisha kuwa walikiariri au kukikakiri. Hii inaweza kuwa sababu ya sifa za baadaye za Kiebrania.

   C. Sababu zifuatazo zinatolewa ili kuiunga mkono aidha tarehe ya mwanzo au tarehe iliyofuatia:
      1. tarehe ya mwanzo (karne ya 7-6 K.K.):

a. kitabu hiki kinadai kuwa mgawanyo wa Danieli, 7:2, 4, 6 na kuendelea, 28; 8:1, 15; 9:1-2; 10:2 na kuendelea 12:4-8.
b. Yesu anaurejerea uandishi wa Danieli, Mt. 24:15.
c. kuwepo kwa maneno ya Kiajemi na Kiyunani hakuonyeshi tarehe iliyofuatia kwa sababu kulikuwa na uhusiano wa kibiashara kati ya nchi hizi katika siku zile za Danieli.
d. theolojia ihusuyo maisha baada ya kifo pia inaweza kuonekana katika kitabu cha Ayubu na baadhi ya Zaburi. Theolojia iliyokuzwa yenye kuhusu malaika inaweza kuonekana katika Zekaria.
e. Kitabu cha Danieli kinakidhi uelewa wetu wa sasa wa kiutafiti juu ya mabaraza ya kifalme ya ki- Babeli na Kiajemi.

2. tarehe iliyofuatia (karne ya 2 K.K.):
   a. kuwekwa katika sheria ya Kiebrania.
   b. kuwepo kwa maneno ya Kiajemi na Kiyunani.
   c. theolojia za maisha ya baada ya kifo na malaika zilizokuzwa.
   d. ubayana wa tabiri hasa sura ya 11, zenye kuhusiana na mapambano ya Seleucid na kwa ajili ya kuitawala Palestina.
   e. ufanano uliopo kati ya Danieli na vitabu vingine vya matukio ya siku za mwisho ya kipindi cha Makabayo.
   f. "makosa" kadhaa na halisi yaliyo katika kitabu:
      1) matumizi ya neno "kikaldayo."
      2) Danieli kama mkaldayo (mwenye hekima).
      3) Belshaza aliyeitwa "mfalme wa Babeli."
      4) Nebukadreza aliyeitwa baba wa Belshaza.
      5) kumtaja "Dario Mmedi,."
      6) Matumizi ya neno la utawala wa Kiajemi, *satrap*.

D. Umoja wa kitabu cha Danieli unaweza kuonekana katika:
1. uhusiano kati ya sura za 2, 7 na ya 8.

| sur. ya 2 | sur. ya 7 | sur. ya 8 |
|---|---|---|
| dhahabu (Babeli) | simba | |
| fedha | dubu | kondoo mume (Uajemi) |
| shaba | chui | beberu (Uyunani) |
| chuma/udongo wa tope | mnyama | |

2. hiki kipengele cha Kiaramu kinajitokeza kutoka 2:4b-7:28.

E. Biblia inazitambulisha falme hizi:
1. neno shahabu la sura ya 2 kama la Babeli, 2:38.
2. maneno kondoo mume ya sura ya 8 kama Uajemi, 8:20.
3. neno beberu la sura ya 8 kama Uyunani, 8:21.
4. hivyo, ufalme wa nne lazima uwe Rumi. Huu ndiyo ufalme ambamo ndaye yake Masihi atatokea (2:34-35,44; 8:35.)

F. Tunafahamu nini kuhusu mtu aitwaye Danieli:
1. alipelekwa uhamishoni mnamo mwaka 605 K.K. 1:1.
2. kutoka katika nyumba ya kitajiri na muhimu humo Yerusalemu, 1:3.
3. mwerevu, 1:4.
4. zawadi maalumu kwa ajili ya kuzifasiri ndoto na maarifa, 5:12, 14.
5. utumishi wa kifalme pande zote:
   a. kwa Mungu, 6:5.

b. kwa mfalme, 6:4.

G. Huyu Danieli wa kitabu cha Agano la Kale si sawa na yule Danieli wa Eze. 14:14, 20 na 28:3. Majina haya yanatamkwa kwa utofauti katika Kiebrania.

V. TAREHE

A. Danieli anapelekwa utumwani kwa amri ya Nebukadneza II katika 605 K.K. (kama vile 1:1).

B. Danieli ni mfasiri wa ndoto na mshauri kwa wafalme wa Babeli na Uajemi hadi kipindi cha Koreshi II, "mkuu" (kama vile 1:21; 6:28; 10:1).

C. Baadhi ya wanazuoni wanaoupinga utabiri wa kinabii wanakanganywa na uthabiti wa undani wa maelezo ya kihistoria wa Danieli wa sura ya 11. Hawa wanakipa tarehe kitabu hiki mara baada ya utabiri wake maalumu wa mwisho, kuhusu Antioko IV Epiphanes (175-164 K.K.).

D. Kwa kuwa kiwakilishi cha nafsi ya kwanza umoja kilikuwa kikitumika hivyo hivyo na mara kwa mara katika kitabu hiki (kama vile 7:1,9; 8:1; 9:1), hii inamaanisha kuwa Danieli ndiye mwandishi wa kitabu ambacho anakiita jina lake, na angeweza kukipa tarehe kitabu hiki ndani ya kipindi cha maisha yake.

VI. VIPENGELE VYA KIFASIHI

A. Maelezo ya Kimuhtasari
1. maisha ya Danieli, 1-6.
2. maono ya Danieli, 7-12.

B. Muhtasari kwa fahirisi
1. Danieli mbele ya Nebukadneza, sura ya 1.
2. ndoto ya Nebukadneza na fasiri, sura ya 2.
3. Sanamu ya shaba ya Nebukadneza na marafiki watatu wa Danieli, sura ya 3.
4. ndoto ya pili ya Nebuchadneza na fasiri yake, sur. ya 4.
5. karamu ya Belshaza na kuanguka kwa mji wa Babeli, sur. ya 5.
6. Dario Mmedi na Danieli ndani ya tundu la simba, sur. ya 6.
7. Maono ya wanyama wa nne, sura. 7.
8. maono ya sur. 7 yanaelezwa na kuwekewa upanuzi, sur. 8.
9. hofu ya Danieli juu ya urejesho wa Yerusalemu lakini anaonyeshwa matatizo yatakayotukia baadaye kwa Wayahudi, sur. 9.
10. utangulizi wa ujumbe wa sura za 11-12, sura za 10
11. mapambano kati ya wa-Seleucid na wa- Ptolemy juu ya Palestina, sura za 11-12.

VII. KWELI KUU

A. Mungu alikuwa/yu katika kuitawala historia; kumtumainia yeye na kubaki katika imani nyakati za magumu.
B. Kuteseka kwa watu wa Mungu (Wayahudi) hakukuwa/hakujatimizwa.
C. Mungu atauimarisha ufalme wa ndani kupitia Masihi.
D. Kutakuwa na ufufuo kwa wote wenye haki na wadharimu.

VIII. MANENO NA/AU VIFUNGU NA WATU WA KUWATAMBUA KIMUHTASARI


A. Maneno na /au Vifungu
1. "lugha ya Wakaldayo" (muundo wa fumbo), 1:4 (NIV, "lugha na fasihi ya Wababeli")
2. " yule wa nne ni mfano wa mwana wa miungu," 3:25 (NASB na NIV)
3. *Mene, Mene, Tekel Upharsin*, 5:25 (NIV, "...*parsin*")
4. " pepo nne za mbinguni," 7:2 (NASB na NIV)


5. "wanyama wakubwa wanne wakatoka baharini," 7:3 (NASB na NIV)
6. "vitabu vikafunuliwa," 7:10 (NASB na NIV)
7. "wakati, na nyakati mbili, na nusu wakati," 7:25 (NASB na NIV)
8. majuma sabini, 9:24 (NIV, "sabini ya sabani")
9. "watu wa mkuu," 9:26 (NIV, "watu wa mtawala")
10. "chukizo la uharibifu," 9:27 (NIV, "bawa la hekalu litasimama kama chukizo"
11. "chukizo la uharibifu," 11:31 (NIV, "chukizo lenye kusababisha uharibifu")

B. Watu
1. Yehoakimu, 1:1
2. Wakaldayo, 2:2 (NIV, "wanajimu")
3. Belteshaza, 2:26
4. mlinzi, naye ni mtakatifu, 4:13 (NIV, "mjumbe")
5. Belshaza, 5:1
6. Dario Mmedi, 5:31-6:1
7. Pembe ndogo, 7:8
8. mzee wa siku, 7:9
9. mwana wa adamu, 7:13
10. Pembe ndogo, 8:9
11. Gabrieli, 8:16
12. Mikaeli, 10:13
13. "mfalme wa kusini," 11:5 (NIV, "mfalme wa Kusini")
14. "mfalme wa kaskazini," 11:6 (NIV, mfalme wa Kaskazini)

IX. MAENEO KI-RAMANI
1. Shinari,1:2 (NIV, Babeli”)
2. Umedi, 8:20
3. Susa, 8:2
4. Elamu, 8:2
5. Uyunani, 8:21

X. MASWALI YA KI-MAUDHUI KWA MWANAFUNZI
1. Ni kwa njia gani tatu neno Mkaldayo limetumika?
2. Ni kwa namna gani maono ya sura ya tatu 2, 7 na 8 yanahusiana?
3. Ni "vitabu" gani vilivyotajwa katika 7:10 na 12:1?
4. Kwa nini sura za 9:24-27 ni ngumu sana kufasirika?
5. Ni mataifa gani mawili yanayohusiana na sura ya 11?
6. Kuna pembe ndogo mbili katika Danieli (7:8 na 8:9), je! zinamwakilisha nani?
7. Ni eneo gani katika kitabu ni suala la ujumla la ufufuo wa wafu waliotajwa?


KAS
MAGH
MASH
KUS
MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE


PALESTINA
0 10 20 30 40
VIPIMO KATIKA MAILI

# UTANGULIZI WA HOSEA

I. JINA LA KITABU

A. Kinatajwa kutokana na Nabii.

B. Jina lake linamaanisha "wokovu." Kiasili lilikuwa jina la Yoshua, Hes. 13:16. Ni jina sawasawa na Hoshea (2 Wafalme 17:1).

C. Yeye alikuwa:

1. Mwana wa Beeri (1:1),
2. Raia wa Israeli (7:5) lakini mji gani hiyo haijulikani,
3. kama Amosi alivyozungumzia hitaji la haki ya kijamii, Hosea alizungumzia hitaji la uaminifu wa agano,
4. amekuwa anaitwa:
   (a) "Yeremia wa Israeli"
   (b) "Mtume wa Yohana wa Agano la Kale"
   (c) "muinjilisti wa kwanza wa Israeli"

II. URASIMISHAJI

A. Kitabu hiki ni sehemu ya"manabii wa mwisho" (Ecclesiasticus 49:10)

B. ni sehemu ya kwanza ya Kumi na Mbili,ya kundi la manabii wadogo (Baba Bathra 14b)

1. kama Isaya, Yeremia na Ezekieli wanafaa kuwa katika gombo moja.
2. kinawakilisha makabila kumi na mbili au uwakilishi wa hesabu ya mpangilio.
3. inaaksi mtazamo wa kijadi wa mpangilio wa kitabu.

C. Mpangilio wa "Kumi na Mbili" au Manabii Wadogo umeunganishwa na wanazuoni wengi kwenye mpangilio wa kimfuatano.Hatahivyo, kuna matatizo na mtazamo huu:

1. vitabu sita vya kwanza ni tofauti kati ya MT na LXX.

| **MT** | **LXX** |
|---|---|
| Hosea | Hosea |
| Yoeli | Amosi |
| Amosi | Mika |
| Obadia | Yoeli |
| Yona | Obadia |
| Mika | Yona |

2. ushahidi wa ndani unamuweka Amosi katika mpangilio kabla ya Hosea.
3. Tarehe ya Yoeli inabishaniwa sana. Namuorodhesha yeye kama nabii wa baada ya uhamisho pamoja na Obadia.

D. Andiko la Hosea yawezekana ni gumu zaidi kati ya vitabu vyote vya Agano la Kale.

1. Sehemu ya hili ni kutokana na asili ya kihisia ya kitabu.
2. Sehemu ni kutokana na unakili wa kiuandishi. Toleo la MT na LXX ni tofauti.
3. Sehemu ni kutokana na tofauti katika Kiebrania kinachozungumzwa kati ya Israeli na Yuda.

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Simulizi yake kihistoria ni ya maisha ya karne ya nane ya manabii wa Israeli (hasa sura ya 1-3).

B. Maisha yake yalitumika kama njia ya masimulizi ya kuonyesha upendo wa Mungu:

1. Mungu kama mpenzi mdogo mwaminifu(1-3)
2. Mungu kama mzazi mwenye upendo (11)
3. Sitiari hizi zilijikita juu ya mkanganyiko wa Israeli wa Baali kama "mume" na "bwana."

C. Kimeandikwa katika vipengele vizuri, vyenye nguvu na ushairi wenye hisia ila ulio achanishwa (sura za 4-14)

IV. UANDISHI

A. Upatanishi siku zote amekuwa Hosea, ingawa tunajua kidogo kuhusu yeye.

B. Baba Bathra 15a anasema watu wa Sinagogi Kuu aliandika "Kumi na Mbili." Hii lazima iwe ni kwa namna ya utungwaji au uhariri.

C. Baadhi wamehoji:
1. rejea kwa Yuda, 1:1; 4:15; 5:5,10,12-14; 6:4,11; 8:14; 11:12,
2. vifungu vya mafanikio ya baadaye na ukombozi,
3. ndoa ya Hosea inaelezewa katika nafsi ya tatu katika sura za 1-2 lakini nafsi ya pili katika sura

D. Majibu kwa mapingamizi:
1. manabii wote wanatazama mgawanyiko kati ya Israeli na Yuda kama makosa. Yuda siku zote huwa inaonekana kama mrithi wa haki wa ahadi za Ibrahimu na Daudi .
2. manabii wanaunganisha hukumu na ahadi ya unabii. Vinaenda pamoja kama ujumbe mmoja wa Kimungu.
3. Hosea kinaweza kuwa kusanyiko la mahubiri yake.

V. TAREHE

A. Hosea ni nabii wa kane ya nane K.K.
1. Isaya na Mika katika Yuda
2. Yona, Amosi na Hosea katika Israeli

B. Hosea alifuatia na kufanana na huduma ya Amosi

C. Tarehe ya mahubiri yake yangekuwa siku za wafalme wanaotajwa katika 1:1:
1. Uzia (wa Yuda)
2. Jotham (wa Yuda)
3. Ahazi (wa Yuda)
4. Hezekia (wa Yuda)
5. Yeroboamu II (wa Israeli)

D. mapendekezo kadhaa ya kiunazuoni:
1. Keil, 790-725 K.K.
   a. 1:4, kilianza kabla ya kuanguka kwa ufalme wa Yehu
   b. 10:14, kipo katika uvamizi wa Shalmaneser V
2. Francisco, 750-735 K.K.
   a. baadaye kidogo kuliko Amosi
   b. siku za mwisho za Yeroboamu II
   c. sio zaidi ya 735 K.K. kwasababu Ashuru alichukua eneo la Gileadi
3. Harrison, kabla ya 722 K.K.
   a. Yeroboamu II anakufa mnamo 753 K.K.
   b. safari inayofanywa na Menahem mpaka Tiglath-pileser III (8:9) mnamo 739 K.K.
   c. matukio ya vita ya washamu-Waefraimu ya 735-734 K.K. ikirejerewa katika 5:8-6:6 (pia Is. 7-14).

d. siku za Hosea zinaelezea rejea kwa Misri katika 7:11; 9:6 na 12:2.

4. La Sor, Hubbard na Bush, 753 – mpaka mnamo 722 K.K.
    a. kilianza kabla ya kifo cha Yeroboamu wa II, 753 K.K.
    b. kinavuka mpaka utawala wa Hezekia
        (1) utawala wenza tokea mnamo 728 K.k.
        (2) mfalme tokea 715 K.K.
    c. amehubiri wakati wa utawala wa Tiglath-pileser III, 745-727 K.K.

VI. MAZINGIRA YA KIHISTORIA

kama vile "Historical Background to the Eighth Century Prophets (Mazingira ya Nyuma ya Kihistoria ya Manabii wa karne ya Nane)" mwanzoni mwa Isaya

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI

A. (Imechukuliwa kutoka *Introduction to the Old Testament* by Clyde Francisco, kur. 150-163)
    1. Utangulizi, 1:1
    2. Mgogoro wa kinyumbani wa Hosea, 1:2-3:5
    3. Sintofahamu ya Mungu na Israeli, 4:1-10:15
    4. Baba na Mwanawe Mkaidi, 11:1-12
    5. Nini kilicho katika jina (Yakobo dhidi ya Israeli) 12:1-15
    6. Kifo cha taifa, 13:1-16
    7. Mbadala wa Hukumu 14:1-9

B. (Imechukuliwa kutoka *Introduction to the Old Testament* na E. J. Young, kur. 252-254)
    1. Mahusiano ya Mungu na watu Wake, 1:1-3:5
    2. Mikondo tofauti ya Nabii, 4:1-14:9
        a. hatia ya makabila ya kaskazini, 4-8
        b. adhabu ya makabila ya kaskazini, 9:1-11:11
        c. baraka za mbeleni kwa watu watubuo, 11:12-14:9

VIII. KWELI KUU

A. YHWH ni Mungu binafsi. Dhambi ni kuwa kinyume na Mungu mwenye upendo, sio tu uvunjaji wa kanuni za kiagano (Amosi)

B. imani ya kibiblia inaweza kupewa tabia bora zaidi kwa sitiari za kati ya familia:
    1. mume (Mungu) - mke (Israeli)
    2. mzazi (Mungu) - mtoto (Israeli)

C. YHWH amechagua kushughulika na mwanadamu aliyeanguka kupitia ahadi, sadaka na agano. Hii inajumuisha tumaini la kibinafsi na utii wa kiagano.

D. Kutotii kiagano kunapelekea katika hukumu. Hukumu siku zote ni kwa kusudi la urejesho. Nidhamu ni kitendo cha upendo wa mzazi (Ebr. 12:5 na kuendelea). Baraka za mbeleni za Israeli zimewekewa masharti katika utii wake wa sasa.

IX. MANENO NA/AU TUNGO NA WATU WA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

A. Maneno na/au Tungo

1. ukahaba, 1:2 (NIV, "mke kahaba")
2. kushindana, 2:2 (NIV, "kemeo")
3. Mikate ya zabibu kavu, 3:1 (NIV, “mitakatifu...”)
4. homeri, 3:2 (NASB & NIV)
5. nguzo takatifu, 3:4 (NIV, "mawe matakatifu")
6. *teraphim*, 3:4 (NIV, "sanamu")
7. "hawamjui Bwana," 5:4, (NIV, "hawamtambui BWANA")
8. "waondoao alama ya mipaka," 5:10 (NIV, "mawe ya mipaka")
9. "Efraimu ajichanganya na mataifa," 7:8 (NASB & NIV)
10. "ndama yako, Ee Samaria," 8:5 (NIV, "sanamu yako ya ndama, Ee Samaria")
11. "umepanda upepo,nao watavuna tufani," 8:7 (NASB & NIV)
12. "mkate wa matanga," 9:4 (NASB & NIV)
13. "Mimi nalimfundisha Efraimu kutembea," 11:3 (NASB & NIV)
14. Wema [*hesed*] 4:1; 6:6; 10:12; 12:6 (NIV, "hakuna uaminifu")

B. Watu

1. Uzia, 1:1
2. Ahazi, 1:1
3. Hezekia, 1:1
4. Yeroboamu mwana wa Yoashi (II), 1:1
5. Gomeri, 1:3
6. Yezreeli, 1:4
7. Lo-ruhamah, 1:6
8. Lo-ammi, 1:9
9. Baali, 2:16 (NIV, "mume wangu")
10. Mfalme Yarebu, 5:13; 10:6 (NIV, "mfalme mkuu")


X. MAENEO YA KI-RAMANI


1. bonde la Ankori, 2:15 (Yosh. 7:26)
2. Gilgali, 4:15
3. Beth-aven, 4:15 (Betheli)
4. Mizpah, 5:1
5. Mlima Tabori, 5:1
6. Gilbea, 5:8
7. Rama, 5:8
8. Adamu, 6:7
9. Gileadi, 6:8
10. Baal-peori, 9:10
11. Lebanoni, 14:6-7

XI. MASWALI YA KIMAUDHUI YA MWANAFUNZI

1. Je Hosea alimuoa kahaba?
2. Je agano la Mungu pamoja na Israeli la kimasharti au lisilo na masharti?

3. Ni kwa namna gani Baali na Gomeri wanahusiana na YHWH na Israeli?
4. Kwanini 6:1-3 ilifikiriwa kuwa toba ya muda ya mpito tu?
5. Kiwakilishi "wa-" kinarejerea watu gani katika 7:4-6 na 8:4?
6. Je 8:13 ni upinganifu ndani ya 11:5?
7. Je Israeli itapelekwa uhamishoni kwenda Misri au Ashuru? Elezea 11:5 ukilinganisha na 7:10, 8:13 na 9:3.
8. Kwanini muungano wa kisiasa ulishutumiwa na manabii wote wa Agano la Kale?


MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE
KAS
MAGH
MASH
KUS


PALESTINA
0 10 20 30 40
VIPIMO KATIKA MAILI

# UTANGULIZI WA YOELI

I. JINA LA KITABU

A. Kiliitwa kwa jina la nabii.

B. Jina lake ni muunganiko wa majina mawili ya Mungu:

1. YHWH - Jina la kiagano la Mungu.
    a. jina lolote la Kiebrania ambalo lilianza na "J" na irabu siku zote ni kifupisho kwa ajili ya YHWH.
    b. Jina lolote la Kiebrania ambalo linaishia na "iah" pia ni kifupisho cha jina la YHWH (Elijah/Eliya).
2. El - Jina la Jumla la Mungu.
3. Kati ya majina haya mawili ya Kiebrania, kitenzi lazima kirejeree YHWH (ni) El.

C. Hili lilikuwa ni jina lililozoeleka la Kiebrania. Kuna zaidi ya kumi na tatu yaliyotajwa katika vitabu vya kihistoria.

II. URASIMISHAJI

A. Kitabu hiki ni sehemu ya mgawanyiko wa kanoni ya Kiebrania iitwayo "Manabii."

B. Kilikuwa ni sehemu ya gombo liitwalo "Kumi na Mbili." Haya yanajulikana kama manabii wadogo kwasababu ya urefu wa maandiko yao

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Hii ni nusu riwaya na nusu ushairi.

B. Yoeli anaonekana kuelezea manabii kadhaa wengine:

1. Yoeli 1:15c - Amosi 4:9; Is. 13:6
2. Yoeli 2:3 - Isa. 51:3 au Ezek. 36:35
3. Yoeli 2:10 - Isa. 13:10
4. Yoeli 3:10 - Isa. 2:4; Mika 4:3
5. Yoeli 3:16 - Amosi 1:2
6. Yoeli 3:18 - Amosi 9:13

C. Umaliziaji wa Yoeli wa taswira unaelezewa kwa namna ya neno la siku za mwisho, "Siku ya BWANA."

D. Nadharia ni kwa namna gani ya kutafsiri pigo la nzige, 1:4; 2:25.

1. kiuwakilishi/kisiari
    a. Targums ya Kiyahudi katika 2:25
        1) watu
        2) lugha
        3) watawala
        4) falme
    b. dokezo la pambizo karne ya 6 MSS ya LXX
        1) Wamisri
        2) Wababeli
        3) Waashuru
        4) Wayunani
        5) Warumi
    c. wafasiri wa Kikristo (karne ya 18)
        1) Waashuru
        2) Wakaldayo
        3) Wamakedonia
        4) Warumi
2. historia ya nyuma
    a. nabii anatumia wakati uliopita wa kitenzi cha kiebrania
    b. hii ilikuwa mbinu ya tabia ya kinabii kuchukua matukio ya m,aisha ya nabii na kuyamulika katika mazingira ya baadaye. Ubaadaye wa Israeli ulitegemea maamuzi ya toba ya imani kwa wakati uliopo
3. Historia ya ubaadaye

a. kuna uvamizi wa kibayana ujao kwasababu ya dhambi za Israeli
b. nzige wanatumiwa kwasababu ya sitiari ya kijeshi inayotumika kuwaelezea:
    1) kuonekana kama punda
    2) kuonekama kama magari za farasi
    3) kutembea kwa utaratibu
c. Yoeli yawezekana anaihusianisha na Ufunuo 9:3-11

4. Matukio ya siku za mwisho
    a. kutajwa kwa "siku ya Bwana" kunatoa ishara ya aina hii ya uwasilishwaji
    b. matumizi ya rangi na wanyama ni wasifu wa aina hii ya uwasilishwaji

IV. UANDISHI

A. Hakuna isipokuwa jina la Nabii na lile la Baba yake ndiyo yanayojulikana, Yoeli, mwana wa Pethuel, 1:1.
B. Kumekuwapo na desturi mbili juu ya nabii:
    1. kutoka kabila la Reubeni (asiye-Epiphania)
    2. kutokea Yuda kwasababu ya maarifa yake ya taratibu za Hekalu

V. TAREHE

A. Hakuna namna inayojulisha tarehe kamili (G. Campbell Morgan alisema kuwa alikuwa ni moja ya manabii wa kwanza kabisa au moja ya manabii wa siku za usoni zaidi):
    1. kutoka ushahidi wa ndani tarehe mbili zimependekezwa:
        a. tarehe za baada ya uhamisho:
            1) lazima ihusianishwe na uvamizi utishiao Yuda kwa sitiari ya pigo la nzige.
            2) 3:2 inamaanisha Israeli imepelekwa uhamishoni tayari. Jina la "Israeli" sasa linatumika kwa ajili ya Yuda, 2:27; 3:1-2,16.
            3) 3:6 inazungumzia biashara ya utumwa ya Kiyunani ambayo inamaanisha tarehe za baada ya uhamishoni.
            4) 3:1, 17 inamaanisha kwamba Yuda tayari imekwisha pelekwa uhamishoni na iko hatarini kuvamiwa tena ikiwa dhambi yake itaendelea.
            5) Hakuna kutajwa kwa Mfalme ambalo linamaanisha mazingira baada ya uhamishoni. Yoeli alizungumza ujumbe wake kwa wazee na makuhani.
            6) wavamizi wanaitwa "watu wa kaskazini" ambalo linamaanisha uvamizi wa Mesopotamia (Ashuru, Babeli, Uajemi) , 2:20.
            7) wasifu wa kuabudu Baali kipindi kabla ya uhamishoni pasipo kutajwa.
        b. tarehe kabla ya uhamishoni:
            1) kunaonekana kuwa na rejea kwa Hekalu, 1:9, 13-14; 2:17.
            2) maadui wanatajwa katika 3:4,6,8 (Foenike, Filistia, Edomu, Sabea) ni kabla ya uhamisho na si miji ya uhamishoni.
    2. kutoka katika ushahidi wa nje:
        a. eneo la kitabu katika kanoni ya Kiebrania inamaanisha tarehe ya kabla ya uhamisho.
        b. Hatahivyo inaweza kuwa iliwekwa baada ya Amosi kwasababu wote wanazungumzia "Siku ya YHWH" na uvamizi wa nzige ni uwakilishi wa hukumu. Pia, ni utembeleo wa Baraka, sio hukumu. Hii inashabihiana na mazingira baada ya uhamishoni.

3. mwandishi anafikiria tarehe za baada ya uhamisho zinashabihiana zaidi na ushahidi.

B. Nadharia juu ya tarehe kwa kujikita katika uvamizi wa Palestina:
   1. Wakati wa utawala wa Yoashi (837-800 K.K.)
   2. Wakati wa utawala wa Uzia (783-742 K.K.)
   3. Wakati wautawala wa Zedekia (598-586 K.K)
   4. Wakati wa muda wa Zerubabeli (598 K.K)
   5. Wakati wa muda wa Malaki (430 K.K.)
   6. uvamizi wa kibaadaye wa watu wa Mungu wa matukio ya siku za mwisho

C. Kuna uhusiano wa kifasihi kati ya:
   1. Yoeli 2:32 na Obadia 17. Wote ni baada ya uhamisho mwanzoni.
   2. Yoeli 3:16 na Amosi 1:2. Yoeli ananukuu manabii wengi sana, yawezekana Yoeli anamnukuu Amosi.

D. John Calvin alitengeneza pointi nzuri juu ya tarehe ya Yoeli,
   "Kama ambavyo hakuna uhakika, ni vizuri zaidi kuacha muda ambamo alifundisha kuwa hivyo; na kama tutakavyooona, hili halina umuhimu mkubwa. Kutokujua muda wa Hosea kungekuwa hasara kubwa kwa wasomaji, kwa sehemu kubwa ambayo ingeweza kuelezewa bila maarifa ya historia; lakini kama ilivyo kwa Yoeli kuna hitaji kidogo kwa ajili ya hili, kwakuwa kuchukua fundisho lake iko wazi ingawa muda wake umekingwa na haujulikani."

VI. MAZINGIRA YA KIHISTORIA — The National Geographic Magazine la Disemba, 1915 (XXVIII, No. 6) inaweka kumbukumbu la Nzige katika Palestina. Makala hii ni ya muhimu kuelewa maelezo ya nabii.

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI
   A. Maono ya pigo la kutisha la nzige kama uwakilishi wa jeshi livamiwalo, 1:1-2:27

   B. Siku ya Bwana itakuwa Baraka sio laana kwa watu wa Mungu watubuo, 2:28-3:21
   (Sefania ni kinyume.)

VIII. KWELI KUU
   A. Nabii anaona matukio ya siku zake.
   B. Yoeli anaitisha siku ya kitaifa ya toba, 1:13-14; 2:12-17.
   C. Ikiwa watu wa Mungu watatubu, Mungu ataleta siku mpya ya utajiri vyote kiroho na mwili. (Kumb. 27-28.)
   D. Mungu atayahukumu mataifa yaliyozunguka mji! 3:1-17
   E. Siku hii mpya ya kufanywa upya kiroho (kama vile 2:28-29) itaathiri:
      1. wanaume na wanawake,
      2. vijana na wazee,
      3. watumwa na walio huru. (kama vile Mdo. 2; Gal. 3:28)
   F. "Siku ya Bwana" ni tungo ya wasifu wa Amosi, Yoeli na Sefania. Namna gani tunaitikia kwa Mungu sasa inaamua ni siku ya Baraka au hukumu.
   G. Wasifu wa Mungu unaelezewa katika 2:13 (kama vile Kut. 34:6; Zab. 103:8-13 na Neh. 9:17).

H. Kumwagwa kwa Roho 2:28-32 kunaaksi kizazi kipya cha Agano (kama vile Yer. 31:31-34 na Ezek. 36:26-27).

IX. MANENO NA/AU TUNGO NA WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHATASARI

A. Maneno na/au Tungo

1. "matawi yake yatakuwa meupe," 1:7 (NASB & NIV)
2. "siku ya Bwana i karibu," 1:15 (NASB & NIV)
3. "pigeni baragumu katika Sayuni," 2:1,15 (NASB & NIV)
4. "rarueni mioyo yenu na si mavazi," 2:13 (NASB & NIV)
5. wema (*hesed*), 2:13 (NIV, "mwingi wa upendo")
6. "nitawamwagieni Roho wangu wanadamu wote," 2:28 (Mdo. 2:16ff.) (NIV, "...juu ya watu wote")
7. "yeyote atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa," 2:32 (Mdo. 2:21; Rum. 10:13.) (NIV, yeyote atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa")
8. "wamewatenga watu wangu," 3:3 (NASB & NIV)
9. "yafueni majembe yenu yawe panga..." 3:10 (NASB & NIV)

B. Watu


1. Mwenye nguvu (*El Shaddai*), 1:15
2. Wa-Sabea, 3:8

X. MAENEO YA KI-RAMANI


1. Tiro, 3:4
2. Sidoni, 3:4
3. Filistia
4. Yavani (Uyunani )
5. Edomu, 3:19
6. Sayuni, 2:1
7. Bonde la Shittimu,. 3:18 (NIV, "...la Acacia")

XI. MASWALI YA KIMAUDHUI KWA MWANAFUNZI

1. Je nzige wa 1:4 ni nzige wa tofauti au wa aina ya hatua tofauti za maisha ya nzige?
2. Kwanini makuhani wanaambiwa waomboleze?
3. Toa maana ya jina la Mungu linavyotumika katika 1:15.
4. Mistari gani miwili katika sura ya 2 inayotumika katika Agano Jipya? na inatumika kwa nani?
5. Je 3:15 ni ya kidhahiri au ya kimafumbo na kwanini?



MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE
KAS
MAGH
MASH
KUS


PALESTINA
0 10 20 30 40
VIPIMO KATIKA MAILI

# UTANGULIZI WA AMOSI

I. JINA LA KITABU

A. Kinaitwa jina kwa jina la nabii wake.
B. Amosi inamaanisha:
   1. "kuwa mzigo."
   2. "kubeba mzigo."
   3. "kustahimilisha."
   4. Desturi moja ya Kiyahudi inaeleza kwamba lilikuwa ni jina kwa wale wote waliopinga ujumbe wake.
C. Jina hili linatokea mahali hapa tu katika Agano la Kale

II. URASIMISHAJI

A. Kitabu hiki ni sehemu ya "manabii wa mwisho."
B. Ni moja ya orodha ya manabii wadogo "Kumi na Mbili,".
C. Kiliwekwa nafasi ya tatu katika manabii wadogo na toleo la MT, ingawa toleo la LXX linakiorodhesha nafasi ya pili.

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Hii ni sehemu ya kwanza ya maandiko ya mabanii.
B. Hiki ni nadharia ya unabii wa Kiebrania iliyokuwa ikikubalika wakati ule. Hiki ni mfano wa ushairi bora kabisa wa Kiebrania na wenye kutumia taswira.

IV. UANDISHI

A. desturi ya Kiyahudi siku zote imeelezea mwandishi kuwa Amosi wa Tekoa.
B. Mtu aitwaye Amosi:
   1. Alikuwa mtu wa kabila la Yudea kutoka Tekoa ambapo ni kama maili tano kusini mashariki mwa Betlehemu.
   2. Hakuwa nabii wala sehemu ya familia ya kinabii au mfua vyuma (kama vile 7:14). Kiasili manabii waliishi katika makundi ya kijamii kwa pamoja. Baadaye baadhi walitambuliwa na jumba la kifalme.
   3. Inavyoonekana alikuwa mchungaji wa "kundi dogo la kondoo" (kama vile 1:1). Neno linalotumika kumuelezea ni nadra japo linatumika kwa kumiliki kondoo (kama vile 2 Wafalme 3:4).
   4. Yeye alikuwa: (1) mmiliki wa miti ya matunda; au (2) "mtunzaji wa miti ya mizeituni" (kama vile 7:14). Hii inaweza kuwa ilijumuisha uhamaji wa kila mwisho wa mwaka. Miti hii inaitwa "mitini." Tunda lake ni sawasawa kabisa kama mtini. Lazima lichomwe kwa kitu chenye ncha ili kuiva vizuri. Hili llikuwa zao muhimu sana kwa watu wa mashariki ya karibu. Daudi aliteuliwa kama mwangalizi maalumu (kama vile 1 Nyakati 27:28).
   5. Desturi ya Kiyahudi inasema alikuwa ni mfanyabiashara mzuri sana. Hii ni tofauti kabisa na mtazamo uliozoeleka leo kwamba alikuwa ni mkulima wa vijijini masikini. Kwasababu ya ubora wa ushairi wake na umahiri wake wa kifasihi, desturi za Kiyahudi ziko sawa kabisa! Kutokea 2 Samweli 14:2ff tunajua kwamba Tekoa ilikuwa inajulikana kwa raia wake wenye

hekima. Alikuwa nabii wa kwanza wa Israeli kuandika ujumbe wake. Tambua nafsi ya kwanza yenye umoja ya kiwakilishi 5:1; 7:1-9; 8:1 na 9:1.

6. Alihubiri kwa ufalme wa kaskazini wa Israeli.Tunajua kwa hakika kwamba Betheli lilikuwa ni eneo la kuhubiria lakini yawezekana kulikuwa na maeneo mengine mengi ya kijiografia katika Israeli.

C. Tatizo la uandishi lina matatizo kwasababu:
   1. kitabu kinamaanisha alikuwa mfanyakazi masikini wa shambani.
   2. mtindo na ushairi ni bora zaidi ikimaanisha kuwa alikuwa mtu mwenye elimu nzuri ya darasani.
   3. Mahubiri yake yanasemekana kutolewa kwa mdomo japo yamewekewa muundo na kuwianishwa ambayo inamaanisha fasihi ya kuandika.
   4. wengi wanadhania Amosi alikuwa na uhariri au msaada wa kiuandishi.

V. TAREHE

A. Inaonekana rahisi kuweka tarehe ya unabii huu mnamo mwaka 750 K.K. pamoja au kutoa miaka 10.

B. Mstari wa kwanza wa Amosi ni mrefu na ulio mzuri zaidi katika kujaribu kuweka kitabu cha Agano la Kale:
   1. Uzia alitawala kutokea mnamo 783-742 K.K. (Bright)
   2. Yeroboamu II alitawala kutokea mnamo mwaka 786-746 K.K. (Bright)
   3. Tetemeko la ardhi pia ni jaribio la kuweka tarehe ya kitabu (kama vile 1:1; 8:8; 9:1,5). Josephus inahusiana na 2 Nyak. 26:16-21 wakati Uzia alipotoa sadaka. Masomo ya akiolojia huko Hazori inadai mnamo mwaka 760 K.K (Yadin, 1964).

C. Katika 5:8 na 8:9 ni kupatwa kunakotajwa. Hii inaweza kuwa sawa na moja iliyotajwa katika nyaraka za Ashuru kama inatokea mnamo Juni 15, 763 K.K., hatahivyo, kuna kukamilika kwingine kwa mzunguko Februari 9, 784 K.K.

D. Kukutana kwa Amosi na Amazia, kuhani mtawala huko Betlehemu chini ya mamlaka ya Yeroboamu II, pia inaweka kitabu hiki (kama vile 7:10-17).

VI. MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. nyaraka zinazofanana kibiblia zinapatikana katika:
   1. 2 Wafalme 14:3-17:6
   2. 2 Nyakati 25-28
   3. Hosea
   4. Isaya
   5. Mika

B. muhtasari mrahisi kabisa ya hali ya kuabudu sanamu kati ya watu wa Mungu inaweza kuonekana katika Hosea:
   1. 2:16, "sitaitwa Mimi tena Baali.”
   2. 4:12-13, "... binti zangu hufanya ukahaba ..."
   3. 4:17, "Efraimu amejiunga na sanamu; Mwacheni"
   4. 13:2, "watu hubusu ndama!" (Ibada)

C. mazingira ya kijamii

1. Ilikuwa ni muda wa utajiri wa kiuchumi na upanuzi wa kijeshi kwa wote Israeli na Yuda. Hatahivyo, utajiri huu ulikuwa wa thamani tu kwa tabaka la wenye utajiri. Masikini walikuwa wakinyonywa bna kutendewa vibaya. Ni karibia ilionekana kwamba "wa chini na bunduki" vilikuwa sanamu za nyongeza!
2. Uimara wa kijamii na mali kwa wote Israeli na Yuda inahusiana na visababishi kadhaa:
   a. Utawala mrefu na wenye mafanikio wa Yeroboamu II (786-746 K.K.) kaskazini na Uzzia (783-742 K.K.) upande wa Kusini.
   b. kuanguka ghafla kwa muda mkwa Misri na Mesopotamia.
   c. kushindwa kwa Shamu na Adad-Nirari III mnamo mwaka 802 K.K.
   d. kukosekana kwa migogoro kati ya Israeli na Yuda.
   e. Utozwaji kodi na unyonyaji wa nji za kibiashara kutokea kaskazini kwenda kusini kupitia daraja la ardhi ya Palestina kulisababisha ukuaji kiuchumi wa ghafla hata matumizi ya ziada sana kwa daraja la watu matajiri.
3. Ile "Ostraca ya Samaria" ambayo inawekwa katika tarehe wakatio wa utawala wa Yereboamu II inaonekana kuonyesha ushirika wa kiutawala sawasawa na wa Sulemani. Hii inaonekana kuthibitisha kupanuka kwa ombwe kati ya "walio nacho" na "wasiokuwa nacho."
4. Ukosefu wa ukweli wa wenye mali kunawekwa wazi kwa uzuri katika Amosi, ambaye anaitwa "nabii wa haki ya kijamii." Rushwa ya kimahakama na uongopeaji wa uzito wa kibiashara ni mifano miwili ya wazi ya matumizi mabaya jambo ambalo lilikuwa limezoeleka inavyooneakana huko kote Israeli na Yuda.

D. mazingira ya kidini
1. Ulikuwa ni muda wa shughuli nyingi za kidini za nje japo imani ya mkweli ikiwa ni kidogo sana. Ibada za ustawi za kanaani zilikuwa zimeunganishwa katika dini ya Israeli. Watu walikuwa waabudu sanamu lakini waliita dini ya YHWH. Mwenendo wa watu wa Mungu juu ya muungano wa kisiasa ulikuwa umewaunganisha katika ibada za kipagani na shughuli zake.
2. Ibada ya kuabudu sanamu ya Israeli inatajwa katika2 Wafalme 17:7-18.
   a. Mst. 8, walifuata matendo ya ibada ya wakanaani.
      1) ibada za ustawi
         (a) sehemu za juu, mistari ya 9, 10, 11
         (b) nguzo za unabii (Baali), mistari 10, 16
         (c) Asherim, mstari wa 16 hivi vilikuwa viwakilishi vya mbao vya suria wa kike wa Baali. Walikuwa aidha: nyama za kuchongwa au miti iliyo hai.
      2) Ubashiri,
         a. Mstari wa 17 hili linajadiliwa kwa kina katika Law. 19-20 na Kumb. 18.
         b. Mstari wa 16, waliendelea na ibada ya ndama wawili wa dhahabu wakiwakilisha YHWH, waliweka huko Dani na Betheli kwa kufanywa na Yeroboamu I (1 Wafalme 12:28-29).
         c. Mstari wa 16, waliabudu mungu wa anga wa Babeli: jua, mwezi, nyota na vitu vyote vya anga.
         d. Mstari wa 18, waliabudu mungu wa moto wa ustawi wa Foenike, Moleki (kama vile Law. 18:21; 20:2-5).
3. Dini ya kumuabudu Baali (kama vile W. F. Albright's *Archaeology and the Religion of Israel*, ukur. 82 na kuendelea).
   a. Chanzo chetu kbora zaidi ni "Baal Epic of Ugarit."

1) Inamuonesha Baali kama mungu wa majira anayekufa na kufufuka. Alishindwa na *Mot* na kufungwa kwenye ulimwengu wa chini kwa chini. Maisha yote duniani yalikwisha. Lakini alisaidiwa na mungu mke (*Anat*), anainuka na kumshinda *Mot* kila kipupwe. Yeye ni mungu aliyekuwa akiabudiwa na miujiza ya kuigiliza.
2) Alijulikana kama *Hadad*.

b. *El* ni mungu mkuu wa madhabahu ya Wakanaani lakini umaarufu wa Baali ulichukua nafasi yake.

c. Israeli ilikuwa chini wa ushawishi mkubwa zaidi wa Dini ya Baali ya kulazimishwa na YezebelI aliyekuwa Mfalme wa binti wa Tiro. Alichaguliwa na Omri kwa ajili ya kijana wake Ahabu.

d. Katika Israeli Baali alikuwa anaabudiwa katika maeneo ya kawaida. Aliwakilishwa kwa jiwe lililoinuliwa. Suria wake Ashera, aliwakilishwa na nyama iliyochongwa iliwakilisha mti wa uzima.

4. Vyanzo kadhaa na aina ya ibada za sanamu vinatajwa.
   a. Ndama za dhahabu huko Betheli na Dani zilizowekwa na Yeroboamu I kumuabudu YHWH.
   b. Ibada ya mungu wa ustawi wa Tiro na mungu mke katika maeneo ya juu ya kawaida.
   c. kuabudu sanamu kwa muhimu kulikujumuishwa katika miunganiko ya kisiasa ya siku hiyo.

E. Mazingira ya Kisiasa Kaskazini

I. Yeroboamu II alikuwa mfalme wa mwisho mwenye nguvu katika Israeli. Alikuwa wanne katika uzao wa Yehu na wa mwisho kwa kutabiriwa kutawala (kama vile 2 Wafalme 10:30). Alikuwa na utawala mrefu na mwenye mafanikio kisiasa (786-746 K.K.).

II. Baada ya kifo cha Yeroboamu II kulikuwa na wafalme sita ndani ya kipindi cha miaka ishirini na tano.

a) Zekaria (2 Wafalme 15:8-12). Aliuwawa baada tu ya miezi sita.
b) Shallum (2 Wafalme 15:13-15). Aliuwawa baada tu ya mwezi mmoja.
c) Menahem (2 Wafalme 15:16-22). Alitawala miaka kumi lakini alilipa kodi kubwa kwa Tiglath-Pileser III.
d) Pekahian (2 Wafalme 15:23-26). Alitawala miaka miwili na kuuwawa.
e) Pekah (2 Wafalme 15:27-21). Alitawala miaka mitano na kuuwawa. Alipoteza miji kadhaa kwa Ashuru.
f) Hoshea (2 Wafalme 15:30, 17:1-6). Alitawala miaka tisa na kupelekwa uhamishoni na Ashuru mnamo mwaka 722 wakati Samaria ilipoanguka.

4. Muhtasari fupi ya uvamizi wa Ashuru na Babeli wakati wa karne ya nane ambayo iliathiri Palestina:

a) Manabii wa karne ya nne walikuwa macho wakati wa kupanda kwa ufalme wa Hedekeli-Frati wa Ashuru. Mungu angetumia taifa hili katili kuhukumu watu wake hasa Israeli. Tukio hasa lilikuwa uundwaji wa muungano wa Yordani kisiasa na kijeshi ikijulikana kama "Shirikisho la Shamu-Efraimu" (735 K.K.). Shamu na Israeli walijaribu kulazimisha Yuda kuwaunganisha dhidi ya Ashuru. Badala yake Ahazi alituma barua kwa Ashuru kwa ajili ya msaada. Ufalme wa kwanza wenye nguvu wa mfalme wa Kiashuru, Tiglath-Pileser III (745 - 727 K.K.), alirejea mrejesho wa tishio la kijeshi ba kuvamia Shamu. Baadaye, mfalme wa kupandikizwa wa Ashuru, Hoshea (732-722 K.K.), huko Israeli pia aliasi akiwapendeza

Misri. Shalmaneser V (727-722 K.K.) aliivamia Israeli tena. Alikufa kabla Israeli haijatiishwa lakini aliyemfuatia, Sargon II (722-705 K.K.), aliutwaa mji mkuu wa Israeli, Samaria mnamo mwaka 722 K.K. Ashuru alipeleka uhamishoni zaidi ya Waisraeli 27,000 katika tukio hili wakati Tiglath-Pileser alipokuwa amepeleka uhamishoni maelfu hapo kabla mnamo mwaka 732 K.K.

b) Baada ya kifo cha Ahazi (735-715 K.K.) muungano mwingine wa kijeshi ulitengenezwa na nchi za jangwa la Yordani na Misri dhidi ya Ashuru (714-711 K.K.). Unajulikana kama "Uasi wa Ashdodi." Miji mingi ya Yudea iliharibiwa wakati Ashuru ilipovamiwa tena. Mwanzoni Hezekia alisaidia muungano huu lakini baadaye alijitoa na msaada wake.

c) Hatahivyo muungano mwingine ulijaribu kuchukua fursa ya kifo cha mfalme mwenye nguvu wa Ashuru, Sargoni II, mnamo mwaka 705 K.K. pamoja na uasi mwingine mwingi ambao ulitokea wakati wote wa uifalme wa Ashuru. Hezekia alishiriki kikamilifu wakati wa uasi huu. Kwa mwanga huu wa tishio hili la Senakeribu (705-681 K.K.) alivamia (701 K.K.) Palestina na kuweka kambi karibu na mji wa Yerusalemu (2 Wafalme 18-19; Isa. 36-39) lakini jeshi lake liliharibiwa na Mungu kimiujiza. Kuna baadhi ya maswali kati ya wanazuoni juu ya mara ngapi Senakaribu alivamia Palestina (Mfano: John Bright ana uvamizi mmoja mnamo mwaka 701 K.K. na mwingine unaowezekana ni mnamo mwaka 688 K.K. kama vile ukur. 270). Hezekia aliachwa mna mapinduzi ya Kiashuru lakini kwasababu ya maonyesho yake ya kiburi na hazina za Yuda kwa ujumbe wa Ki-Babeli, Isaya alitabiri kuanguka kwa Yuda kwa Babeli (39:1-8). Yerusalemu ilianguka kwa Nebuchadneza mnamo mwaka 587-586 K.K.

d) Isaya pia alitabiri urejesho wa watu wa Mungu chini ya Koreshi II, mtawala wa ki-Medi mwenye asili ya Uajemi (41:2-4; 44:28; 45:1; 56:11). Ninawi ilianguka mnamo mwaka 612 K.K. Babeli lakini mji wa Babeli ulianguka mnamo mwaka 539 K.K kwa jeshi la Koreshi. Mnamo mwaka 538 K.K. Koreshi alitoa tamko kwamba watu wote wa uhamishoni wakiwemo Wayahudi wanaweza kurudi nyumbani. Hata pia alitoa fedha kutoka katika hazina kwa ajili ya kujenga upya mahekalu ya kitaifa.

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI

A. Mashitaka dhidi ya mataifa 1:1-2:3 (yawezekana mpaka 2:16)
   1. Shamu (Dameski), 1:3-5
   2. Filistia (Gaza), 1:6-8
   3. Foenike (Tiro), 1:9-10
   4. Edomu, 1:11-12
   5. Ammoni, 1:13-15
   6. Moabu, 2:1-3

B. Mashitaka maalumu dhidi ya watu wa Mungu, 2:4-6:14
   1. Yuda, 2:4-5
   2. Israeli, 2:6-6:14 (muktadha wa hukumu ya Israeli mpaka 6:14)

C. Maono ya hukumu, 7:1-9:10
   1. Nzige, 7:1-3
   2. Moto, 7:4-6
   3. Timazi, 7:7-17

4. Tunda la kipupwe, 8:1-14
5. Uharibifu wa madhabahu, 9:1-10

D. Tumaini la kimasihi, 9:11-15

VIII. KWELI KUU

A. Amosi inahusianisha ghadhabu ya Mungu kwa uvunjaji wa agano la Musa kwa Waisraeli. Tunahitaji kutambua uhusiano kati ya majukumu ya pamoja ya Agano la Kale na imani ya mtu mmoja mmoja. Tuna tatizo la kijamii la dhambi kama Israeli walivyofanya, hatahivyo, mara kwa mara katika fahamu zetu viwango viwili hutokea:
   1. maisha yetu ya binafsi na imani;
   2. maisha yetu ya pamoja ya kijamii ya wazi.

B. Mamalaka ya Mungu duniani kote ni historia ya nyuma ya YHWH kushughulikia hukumu kwa mataifa nje ya Agano la Mungu. Huu ni msingi wa uelewa wa Israeli juu ya imani ya kubudu Mungu mmoja.

C. Sura ya 2:9-12, hukumu ya Mungu lazima ionekane katika mwanga wa matendo yake ya neema katika historia. Uchaguzi wa Mungu na agano pamoja na Israeli linaweka jukwaa kwa ajili ya hukumu kali. Lazima ikumbukwe kwamba "kwake aliepewa vingi, kwake vingi vitatakwa" (kama vile Lk. 12:48)

D. Sura ya 5 inaunganisha imani na maisha bila kuyaachanisha! Amosi anakataa unyanyasaji unaofanywa na matajiri kwa masikini.

E. Israeli inamtumaini kwa makosa katika:
   1. Dini yake (kama vile 4:4-5; 5:21-23).
   2. mafanikio yake ya kiuchumi (kama vile 6:1 na kuendelea).
   3. nguvu yake ya kijeshi, (kama vile 2:14-16; 6:1b, 13).

F. Hati katikati ya kutoamini kwa Israeli kuna tumaini katika agano la Mungu, Mungu masihi, 9:8b-15.

IX. MANENO NA/AU TUNGO NA WATU WA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

A. Maneno na/au Tungo
   1. "tetemeko," 1:1 (NASB & NIV)
   2. ukuta, 1:7 (NIV, "ngome")
   3. fimbo, 1:8 (NASB & NIV)
   4. "choma moto mifupa ya mfalme wa Edomu..," 2:1 (NASB & NIV)
   5. "kwa jozi ya viatu," 2:6; 8:6 (NASB & NIV)
   6. "pembe za madhabahu," 3:14 (NASB & NIV)
   7. "nyumba ya ndovu," 3:15 (NIV, "nyumba iliyopambwa na ndovu")
   8. "nachukia, nakaa sherehe zenu," 5:21 (NASB & NIV)
   9. unono, 5:22 (NIV, "sadaka za ushirika ")
   10. timazi, 7:7 (NASB & NIV)

11. "hatia ya Samaria," 8:14 (NIV, "fedheha ya Samaria")

B. Watu


1. Wanazeti, 2:12
2. Ng'ombe wa Bashani, 4:1
3. Waombolezaji mashuhuri, 5:16 (NIV, "waombolezaji")
4. *Sikkuth*, 5:26 (NIV, "madhabahu")
5. *Kiyyun*, 5:26 (NIV, "kwa kunyonga")
6. Amazia, 7:10
7. Yeroboamu II, 7:10
8. muonaji, 7:12

X. MAENEO KI-RAMANI


1. Karmeli, 1:2
2. Gileadi, 1:3
3. Gaza, 1:6
4. Ashdodi, 1:8
5. Ashkeloni, 1:8
6. Ekroni, 1:8
7. Temani, 1:12
8. Bozrah, 1:12
9. Rabbah, 1:14
10. Betheli, 4:4
11. Gilgali, 4:4
12. Sodoma, 4:11
13. Beersheba, 5:5
14. Hamathi, 6:14
15. Dani, 8:14

XI. MASWALI YA KI-MAUDHUI YA MWANAFUNZI

1. Je Amosi alikuwa mkulima wa kijijini au mfanya biashara mwenye mali nyingi?
2. Je tunawajibika kwa dhambi binafsi za mtu mmoja mmoja au dhambi ya jamii yetu nzima ?
3. Nini msisitizo wa 3:2-8?
4. Kwanini Betheli na Gilgali wanashutumiwa? Kwanini shughuli ya kidini ya 4:4-5 inashutumiwa?
5. Kwanini Mungu alikataa sadaka za Israeli?
6. Kwanini 5:25-26 iwe ngumu sana kufasiri?
7. Je Amosi alikuwa anashutumu mfumo wa utoaji dhabihu?
8. Je Mungu hubadili mawazo Yake?
9. Ni kwa namna gani Toba inahusiana na msamaha? (sura ya 7)
10. Je hukumu ya Mungu ni tukio la mwisho au la papo kwa papo?


MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE
KAS
MAGH
MASH
KUS

# PALESTINA



# UTANGULIZI WA OBADIA

I. JINA LA KITABU
   A. Hiki kiliitwa jina baada ya nabii wake huyu
   B. Jina hili linamaanisha "mtumishi wa YHWH"
   C. Hili lilikuwa jina la kawaida la Kiebrania (kama vile I Fal. 18:3; I Nya. 3:12; 7:3; 8:38; 9:16,44; 12:9; 27:19; II Nya. 17:7; 34:12; Ezra 8:9; Neh. 10:5; 12:25

II. URASIMISHAJI
   A. Kitabu hiki ni sehemu ya kipengele cha manabii waliofuatia" (Ecclesiasticus 49:10)
   B. Hiki kiko katika kipengele cha "wale Kumi na Wawili," kundi la manabii wadogo wadogo (Baba Bathra 14b)
      1. kama vilivyo vitabu vya Isaya, Yeremia na Ezekieli, manabii hawa wanashabihiana na gombo moja la chuo
      2. hawa wanaziwakilisha kabila kumi na mbili za uwakilishi wa namba za ushirika
      3. hawa wanauakisi mtazamo wa kitamaduni wa mfululizo wa vitabu

   C. Mpangilio wa kipengele cha "wale Kumi na Wawili" au Manabii Wadogowadogo umekuwa ukihusianishwa na wanazuoni wengi katika mfululizo wa mfuatano wa matukio. Hata hivyo, kuna matatizo yanayoukumba mtazamo huu:
      1. Vitabu sita vya mwanzo vina tofauti kati ya toleo la MT na LXX.

| MT | LXX |
|---|---|
| Hosea | Hosea |
| Yoeli | Amosi |
| Amosi | Mika |
| Obadia | Yoeli |
| Yona | Obadia |
| Mika | Yona |

      2. Ushahidi wa ndani unamuweka Amosi katika mfululizo ule wa kabla ya Hosea
      3. Tarehe ya Yoeli inajadiliwa kwa kiwango cha juu sana. Hii inamuorodhesha kama nabii wa mwanzo wa kipindi cha baada ya uhamisho sambamba na Obadia

III. AINA YA UWASILISHAJI – unabii wa ushairi wa sasa wa Kiebrania

IV. UANDISHI
   A. Hakuna kinachojulikana kuhusiana na Nabii huyu
   B. Nadharia kadhaa:
      1. Sanhedrin 39b (Buku la Sheria za Kiyahudi) inasema kwamba huyu alikuwa mtumishi wa Mfalme Ahabu katika I Fal. 18:3-16
      2. Asiye-Epiphane (kanisa la mwanzo) katika kitabu chake "Lives of the Prophets" anasema kwamba huyu alikuwa mkuu wa jeshi la Mfalme Ahazia (842 K.K.) katika 2 Fal. 1:12 na kuendelea
      3. John Calvin anasema kwamba huyu alikuwa shahidi wa macho kwa macho wa yale maangamizi ya Yerusalemu (586 K.K. na Nebukadneza II au Babeli)
   C. Jina hili linaweza kuwa cheo.

V. TAREHE
   A. Kiisimu kitabu hiki kinahusiana na Yeremia 49:7-12 (Obad. mist. 1-9) na Yoeli 2:32 (Obad. mst. 10):
      1. E. J. Young anawaweka katika mpangilio huu: Obadia, Yeremia
      2. R. K Harrison anawaweka katika mpangilio huu: Yeremia, Obadia, (450 K.K.) na Yoeli (400 K.K.). Hili linakifanya kitabu hiki kuwa cha kipindi cha mwanzo cha baada ya uhamisho.

3. Keil anawaweka hawa katika mpangilio huu: Obadia, Yoeli, Yeremia

B. Ni dhahiri kuwa kitabu hiki kinahusiana na ujio wa Yuda na mashambulizi ya Yerusalemu yaliyofanywa na Edomu. Baadhi ya tarehe yakini ni:
   1. Yerusalemu iliyotekwa na Shishak, Farao wa Misri katika mwaka wa tano wa Rehoboamu, 922-915 K.K.(kama vile I Fal. 14:25-28; II Nya. 12:2-10).
   2. Yerusalemu iliyotekwa na umoja wa Warabu na Wafilisti katika utawala wa Yehoramu, 849-842 K.K. (kama vile II Fal. 8:20 na kuendelea; II Nya. 21:16-17; 22:1.
   3. Yerusalemu iliyotekwa na Waashuru katika utawala wa Yoashi, 837-800 K.K. (kama vile II Nya. 24:23-24).
   4. Yerusalemu iliyotekwa na Israeli (Yehoashi) baada ya kumwondosha Edomu katika utawala wa Amazia (kama vile II Fal. 14:7-14 (842 K.K.)
   5. Yuda aliyeshambuliwa na Waedomu (kama vile II Nya. 28:17; 19:8-9; II Fal. 16:1-20).
   6. Yerusalemu iliyotekwa na Nebukadneza mara kwa mara, 605, 597, 586, 582 K.K.:
      a. 605 K.K. utawala wa Yehoiakimu (kama vile Dan. 1:1-2)
      b. 597 K.K. utawala wa Yehoiakimu (kama vile II Fal. 24:8-17; II Nya. 36:9-10; Eze.
      c. 586 K.K. utawala wa Zedekia (kama vile II Fal. 24:18-25:21; II Nya. 36:11-21; Maombolezo; Zab. 137:7
      d. 582 K.K. Gedalia Gavana wa ki- Babeli (kama vile II Fal. 25:22-26)

C. Kumekuwa na tarehe mbili zilizoelezwa na wanazuoni:
   1. tarehe ya mwanzo katika utawala wa Yehoramu (849-842 K.K.) kwa sababu:
      a. nafasi ya kitabu katika kipengela cha "wale Kumi na Wawili"
         (1) kundi la karne ya 8: Amosi, Hosea, Mika, (Yoeli?) na Obadia
         (2) kundi la karne ya 7: Nahumu, Habakuki na Sefania
         (3) kundi la kipindi baada ya uhamisho: Hagai, Zekaria na Malaki
      b. kitabu cha Obadia hakiyataji maangamizi ya Hekalu
      c. mataifa yaliyotajwa ni ya kipindi cha kabla ya uhamisho, si kipindi cha baada ya uhamisho
      d. dhambi zinafanana na za wale waliorodheshwa na manabii wa karne ya 8
      e. hakuna maneno ya Kiaramu, semi au maelezo
   2. Tarehe ya baadaye yenye kuhusiana na uvamizi wa Nebukadneza II juu ya Yerusalemu
      a. mist. 11-14 inaonekana kushabihiana na kuanguka kwa Yerusalemu katika 586 K.K.
      b. Edomu ilishiriki katika uvamizi huu
         (1) kufufurahi juu ya anguko la Yuda
            (a) Zab. 137:7
            (b) Omb. 2:15-17; 4:21
            (c) Eze. 36:2-6
            (d) I Esdras 4:45, 50
         (2) ilisaidia katika kuanguka kwa Yuda:
            (a) Eze. 25:12-14
            (b) Eze. 35:1-15

VI. MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. Edomu, Mtendaji wa Unabii, mist. 1-9, 18, 21
   1. Edomu ni taifa la mashariki ya Bahari ya Chumvi toka Esau, ndugu yake na Yakobo (kama vile Mwa. 25-29; 32- 33). Edomu inamaanisha "nyekundu" ambapo Esau inamaanisha "vinyweleo" (kama vile Mwa. 25:25, 30)
   2. Israeli analazimishwa kumheshimu Edomu (kama vile Kumb. 23:7)
   3. Israeli na Edomu wilikuwa na matatizo endelevu:
      a. Hes. 20:14-21
      b. Amu. 11:16-17

c. I Sam. 14:47-48
d. II Sam. 8:14
e. I Fal. 11:14-25
f. II Fal. 14:22; 16:5-6
g. II Nya. 20:10-30; 21:8 na kuendelea
h. Amosi 1:6, 9

4. Nabii nyingine dhidi ya Edomu
   a. Isa. 34:5 na kuendelea; 63:1 na kuendelea
   b. Yer. 49:7-22
   c. Omb. 4:21-22
   d. Eze. 26:12 na kuendelea; 35:1 na kuendelea; 36:2-6
   e. Amosi 1:11-12
5. Edomu anashutumiwa kwa sababu ya:
   a. majivuno yake, mist. 3-4
      (1) katika ulinzi wa kijiografia
      (2) katika miungano ya kisiasa na nguvu ya kijeshi
      (3) katika utajiri wa kibiashara
      (4) katika hhekina ya kitamaduni
   b. machafuko yake juu ya Yuda, jamaa zake, mist. 10-14
      (1) kurahi juu ya kuanguka kwa Yerusalemu (Omb. 2:15-17; 4:21)
      (2) kukwepa kusaidia (mst. 15)
      (3) tendo halisi la kuwaunga mkono maadui (mist. 14)
      (4) kuzichukua mali za Yuda (Yer. 13:19)
   c. kukataa kwake na kumdharau YHWH (mst. 16

B. Edomu ni ishara ya mataifa yote yaliyoasi dhidi ya Mungu na watu wake, mist. 15-21 (kama vile Zab. 2).

C. Utimilifu yakini wa unabii wa-kihistoria
1. maangamizi ya Edomu yaliyofanywa na Babeli ya Sasa yapata miaka 5 baada ya anguko la Yerusalemu, 580 K.K.
2. kumwondosha Edomu toka Petra tendo lililofanywa na Waarabu wa ki-Nabatea yapata miaka 550-449 K.K. (kama vile Mal. 1:2-5).
   Edomu hatajwi katika orodha ya Nehemia ya kuwazingira maadui bali anaondoshwa na makabila ya Waarabu. Edomu alielekea huko Negevu.
3. kumwondosha Edomu tendo lililofanywa na generali wa Iskanda, Antigonus mnamo mwaka 312 K.K. (tendo lililonukuliwa katika Diodorus Seculus)
4. kumwondosha Edomu katika Negevu tendo lililofanywa na Yuda Makabaeus mnamo mwaka 175 K.K. (kama vile. I Wamakayo 5:3,15; II Wamakabayo 10:15; Josephus' *Antiquities of the Jews* 12:8:1; 13:9:1
5. Edomu alilazimishwa kuikubali dini ya Kiyahudi tendo hili lilifanywa na John Hyrcanus mnamo mwaka 125 K.K. Kwa sasa wanaitwa Waidume.
6. Jenerali wa Kirumi, Titus, aliuharibu ushawishi wa Waidume kwa ujumla mnamo mwaka 70 B.K

## VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI

Muhtasari wa maelezo uliochukuliwa toka katika *The New International Commentary* ni mtiririko uhusuo "Yoeli. Obadia, Yona, na Mika" na Allen, uk. 142

A. Maangamizi ya Edomu (2-9)
1. kuanguka kwa Edomu (2-4)
2. ukamilifu wa kutupiliwa mbali kwa Edomu (5, 6)
3. ulaghai wa umoja wa Edomu (7)
4. Edomu kupoteza hekima na mashujaa (8, 9)

B. Edomu kutembea Kinyume (10-14, 15b)
   1. Edomu kutokuwa na udugu (10, 11)
   2. Dharau za Edomu (12)
   3. Kuvamia kwa Edomu (13)
   4. Kuungana kwa Edomu na kulipiza kisasi (14, 15b)

C. Edomu katika siku ya Yahweh (15a, 16-21)
   1. Siku ya Yahweh (15a, 16)
   2. kazi ya mabaki (17, 21)
   3. moto wa Yudea na ubora wa Mwedomu (18)
   4. nchi inarejeshwa (19, 20)

VIII. KWELI KUU

A. Maadui wa Mungu na maadui wa watu wa Mungu ataadhibiwa. Edomu kama aina ya mwenye kuasi, taifa lisilo amini (kama vile mst. 15)
B. Mungu atawatukuza watu wake kulingana na ahadi za agano lake. Utakatifu ndiyo shabaha ya YHWH kwa watu wake.
C. Hali ya kihistoria itageuzwa. Edomu ataangamizwa; watu wa Mungu watabarikiwa.

IX. MANENO NA/AU VIFUNGU NA WATU WA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

A. Maneno na /au Vifungu
   1. "Ujapopanda juu kama tai," 1:4 (NIV, “ujapojenga kiota chako katikati ya nyota”)
   2. "Kwa sababu ya udhalimu aliotendwa ndugu yako Yakobo..." 1:10 (NASB na NIV)
   3. "na kumpa kura juu ya Yerusalemu," 1:11 (NASB na NIV)
   4. "hiyo siku ya Bwana i karibu" 1:15 (NASB na NIV)


B. Watu
   1. Esau, 1:8

X. MAENEO KI-RAMANI


1. Edomu, 1:1
2. Temani, 1:9
3. Ml. Sayuni, 1:17
4. Negevu, 1:19, 20 (au “Negebu”)
5. Shefela, 1:19 (NIV, “vilima”)
6. Gileadi, 1:19

XI. MASWALI YA KI-MAUDHUI KWA MWANAFUNZI

1. Nini wazo kuu la kitabu cha Obadia?
2. Kwa nini Edomu anahukumiwa kwa ukali?
3. Kwa nini Edomu anatumika kama ishara ya kwa mataifa yote?
4. Je! Obadia ananukuliwa au kudokezwa katika kitabu cha Agano Jipya?




MASHARIKI YA KARIBU YA KALE


PALESTINA
0 10 20 30 40
VIPIMO KATIKA MAILI

# UTANGULIZI WA YONA

I. JINA LA KITABU

A. Kitabu kinapewa jina kwa nabii wake

B. Jina lake linamaana ya "hua." Huu ulikuwa ni uwakilishi wa taifa la Israeli:

1. limetumika na muimba zaburi kama chanya, Zab. 68:13; 74:19,
2. limetumiwa na Hosea vibaya, 7:11,
3. limetumika na Wimbo Ulio Bora kama sitiari ya upendo, 2:14; 5:2; 6:9.

II. URASIMISHAJI

A. Kitabu hiki ni sehemu ya "manabii wa mwisho" (Ecclesiasticus 49:10)

B. ni sehemu ya kwanza ya Kumi na Mbili ya kikundi cha manabii wadogo (Baba Bathra 14b)

1. kama Isaya, Yeremia na Ezekieli wanatosha kuwa katika gombo moja.
2. kinawakilisha makabila kumi na mbili au hesabu ya uwakilishi wa ushirika.
3. kinaaksi mtazamo wa kijadi wa mpangilio wa kitabu.

C. Mpangilio wa "Kumi na Mbili" au Manabii Wadogo umeunganishwa na wanazuoni wengi kwa mpangilio wa mfuatano. Hatahivyo kuna matatizo yanayotokana na mtazamo huu:

1. Vitabu vya kwanza sita ni tofauti kati ya MT na LXX.

| **MT** | **LXX** |
|---|---|
| Hosea | Hosea |
| Yoeli | Amosi |
| Amosi | Mika |
| Obadia | Yoeli |
| Yona | Obadia |
| Mika | Yona |

2. ushahidi wa ndani unamuweka Amosi kimapgilio kabla ya Hosea.
3. Tarehe ya Yoeli inabishaniwa sana. Namuorodhesha yeye kama nabii wa baada ya uhamisho pamoja na Obadia.

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Ni tofauti na Manabii Wadogo wengine waliobaki. Ni riwaya isipokuwa 2:2-9.

B. Aina ya uwasilishaji ya Yona imekuwa ikibishaniwa sana.Wanazuoni wengi hawaridhiki na vipengele vya kithiolojia vya miujiza na utabiri :

1. sitiari
2. mafumbo (kwa kutumia kichekesho)
3. uainishi

C. Jina la Yona ni nadra katika Kiebrania kama ilivyo kwa baba yake. Mtu huyu na baba kwa majina haya wanatajwa katika 2 Wafalme 14:25. Aliishi wakati wa Utawala wa Yeroboamu II (783-743 K.K.). Yesu alimrejerea Yona kama mtu wa kihistoria, Mt. 12:39-40; 16:4 na Luka 11:29.

D. Inawezekana kwamba Yona kama Ayubu, kiliandikwa na/au kilikuzwa na mwenye hekima kufundisha kweli ya kithiolojia. Vitabu vingi zaidi vya kinabii vinaweka jumbe za kumbu kumbu za nabii lakini katika Yona ujumbe wa unabii upo katika maneno matano katika 3:4.

IV. UANDISHI

A. Mwandishi ni nabii. Anatambulishwa katika 1:1 kama manabii wengine wadogo.

B. Yona na baba yake, Amittai, yalikuwa majina nadra ya Kiebrania; yote yanatokea katika 2 Wafalme 14:25. Alikuwa nabii kwa Yeroboamu II kutoka kwa Gath-hepher karibu na Nazareti.

C. Inawezekana kwamba wenye hekima wa kiebrania walichukua mfano wa maisha ya kihistoria, kama Ayubu na kukuza kwenye ukweli wa kithiolojia. Yawezekana Yona aliitwa na mfalme wa Israeli ili ajitetee mwenyewe juu ya kuhubiri kwake kwa adui wa Israeli. Yona alikuwa nabii/mwandishi mwaminifu wa kaskazini. Hii inaweza kuelezea kwanini anaonekana akipingana sana katika kitabu. Mwenye hekima yaweza kuwa alisikia utetezi wake na kuona maana ya ujumla na kuandika sehemu ya maisha ya Yona (John Harris, ETBU, 1998).

V. TAREHE

A. Ikiwa mwandishi ni Yona wa 2 Wafalme 14:25 basi tarehe ya kuandikwa ni kabla ya kuanguka kwa Ninawi mnamo mwaka 612 K.K. na wakati wa utawala wa Yeroboamu II (783-743 K.K) sharti kuchagizwa.

B. Mara kwa mara Yona inasemekana kuandikwa kwa kuchelewa japo hii mara nyingi imejikita juu ya:
   1. kukataliwa kwa unabii wa wakati ujao,
   2. kukataliwa kwa vipengele vya nguvu itokayo juu ya kitabu kama historia,
   3. kudhania kwamba inazungumzia fahari ya kitaifa ya baada ya uhamisho na kutokuwepo kwa ujumuishaji.

VI. MAZINGIRA YA KIHISTORIA -- Kuna tarehe mbili katika historia ya Ashuru ambayo inaweza kuwa tukio la toba ya Ninawi.
   1. hali ya kuelekea kuabudu Mungu mmoja wakati wa utawala wa Adad-Nirari III (810-783 K.K.)
   2. pigo kubwa katika Ashuru wakati wa utawala wa Assurdan III (771-754 K.K.)

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI

A. migawanyo ya sura inaonesha muendelezo wa matukio

B. Ainisho fupi
   1. Sura ya 1 - Mapenzi ya Mungu yanakataliwa na badala yake kunakuwa na mapenzi ya Yona. Mungu anashinda!
   2. Sura ya 2 - Yona anatubu (ushairi ulioandikwa kwa njeo ya wakati uliopita na kuonesha ibada katika Hekalu katika Yerusalemu)
   3. Sura ya 3 - Mapenzi ya Mungu yanapokelewa. Ninawi inatubu
   4. Sura ya 4 - tabia ya Mungu inafunuliwa kwa ulinganisho na mtazamo wa Yona na matendo.

VIII. KWELI KUU

A. Katika kitabu hiki Mataifa ni watu wa dini wakati nabii ni muasi
   1. Mabaharia
   2. watu wa Ninawi

B. upendo wa Mungu unaonekana kwa dhahiri katika 3:10 na 4:11. Mungu si tu kwamba anawapenda wanadamu bali pia wanyama, 4:11

C. Waashuru wakatili wanaochukiwa, wanakubalika na YHWH kwa msingi wa toba yao na imani katika yeye, 3:5-9. Hawatakiwi kuwa Wayahudi.

D. Yona anawakilisha wito wa Mungu kwa Israeli kuwa ufalme wa makuhani kwa ulimwengu (kama vile Mwa. 12:3; Kut.19:4-6. Israeli ilifanyika taifa lenye majivuno, kujitenga na ufahari badala ya kiujilisti na lenye ukombozi.

IX. MANENO NA/AU TUNGO NA WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHTASARI

A. Maneno na/au Tungo

1. "Bwana akaamuru samaki mkubwa" 1:17 (NIV, "...akatoa samaki mkubwa")
2. kuzimu 2:2 (NIV, "kaburi")
3. shimo 2:6 (NASB & NIV)
4. "Mungu akaghairi", 3:10 (NIV, "alikuwa na huruma")
5. "wema (*hesed*), 4:2 (NIV, "mwenye upendo")
6. "Bwana akatoa mmea, 4:6 ...mnyoo, 4:7 ...upepo, 4:8 (NIV, "akatoa")
7. "watu wasio jua tofauti ya mkono wa kuume na kushoto", 4:11 (NASB & NIV)
8. "pamoja na wanyama wengi", 4:11 (NIV, "na mifugo mingi pia")

B. Watu


1. Amittai 1:1
2. "Mungu wa mbinguni" 1:9

X. MAENEO KI-RAMANI


1. Ninawi, 1:2
2. Tarshishi, 1:3
3. Joppa, 1:3

XI. MASWALI YA KI-MAUDHUI KWA MWANAFUNZI

1. Je Yona ni mtu wa kihistoria?
2. Kwanini Yona hakutaka kwenda Ninawi?
3. Je samaki mkubwa ni jambo kubwa la utata kiutafsiri? Kwanini au kwanini sio?
4. Elezea asili ya Mungu. (1:9; 4:2)
5. Je muhusika Mkuu ni Yona au Mungu? Kwanini?
6. Ni ujumbe gani kitabu hiki kinatoa kwa Israeli? Je Yona ni kama Israeli?
7. Ni kwa namna gani Yesu alitumia kitabu hiki? (kama vile Mt. 12:38-45)


KAS
MAGH
MASH
KUS
MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE

# PALESTINA



# UTANGULIZI WA MIKA

I. JINA LA KITABU

A. Kitabu kinapewa jina kutokana na nabii wake.

B. Jina lake limefupishwa kutoka katika muundo wa Micaiah (Waamuzi 17:1,4; 1 Wafalme 22:13) ambalo lilimaanisha "nani kama YHWH."

II. URASIMISHAJI

A. Kitabu hiki ni sehemu ya "manabii wa mwisho" (Ecclesiasticus 49:10).

B. Ni kimoja kati ya kikundi cha manabii wadogo "Kumi na Mbili," (Baba Bathra 14b).

1. kama Isaya, Yeremia na Ezekieli wanafaa kuwa katika gombo moja.
2. kinawakilisha makabila kumi na mbili au uwakilishi wa kiishara wa mpangilio.
3. kinaaksi mtazamo wa kidesturi wa kitabu kimpangilio.

C. Mpangilio wa "Kumi na Mbili" au Manabii Wadogo umeunganishwa na wanazuoni wengi kwa mpangilio wa mfuatano. Hatahivyo kuna matatizo yanayotokana na mtazamo huu:

4. Vitabu vya kwanza sita ni tofauti kati ya MT na LXX.

| **MT** | **LXX** |
|---|---|
| Hosea | Hosea |
| Yoeli | Amosi |
| Amosi | Mika |
| Obadia | Yoeli |
| Yona | Obadia |
| Mika | Yona |

5. ushahidi wa ndani unamuweka Amosi kimpangilio kabla ya Hosea.
6. Tarehe ya Yoeli inabishaniwa sana. Namuorodhesha yeye kama nabii wa baada ya uhamisho pamoja na Obadia.

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Ingawa ni kama Amosi katika thiolojia, hakipo katika mtindo. Ingawa Mika sio ushairi uliokuzwa vizuri kama Amosi, kina kauli za namna ya ukali za kweli.

B. Kinaundwa na ujumbe wa hukumu na urejesho ikiwekwa sambamba bila mapito. Ukweli umewekwa katika rangi mbili, nyeupe na nyeusi!

C. Nabii alitoa ujumbe wa upendo, wenye nguvu na wenye maarifa kutoka kwa Mungu wa Agano!

D. Mika ni nabii wa utabiri:

1. kuangukwa kwa Samaria kwa Ashuru, 1:5-7; 6:9-16
2. kuanguka kwa Yerusalemu kwa Babeli, 1:9-16; 3:12; 4:10-12; 6:9-16
3. kurudi kwa watu wa Kiyahudi waliokuwa uhamishoni, 2:12-13; 5:5b-9; 7:7-20
4. sehemu ya kuzaliwa kwa Masihi, 5:2 na ufalme wake wa Kiulimwengu, 5:4
5. imani ijayo ya taifa la Wasioamini, 4:1-5

IV. UANDISHI

A. Kidesturi Mika nabii kutoka Moresheth-gath anaonekana kama mwandishi wa unabii.

B. Wanazuoni wa kisasa wamejaribu kukigawa kitabu cha Mika kati ya waandishi kadhaa kama walivyofanya maandiko ya Musa. Hatahivyo kuna ushahidi wa ndani kwamba kitabu kina umoja:
   1. sura kadhaa zinaanza na neno la Kiebrania "sikilizeni" (*shema,* kama vile Kumb. 6:4), 1:2; 3:1; 6:1.
   2. Sitiari "wachungaji"/"kondoo" zinatumika wakati wote 2:12, 3:2-3; 4:6; 5:1 na kuendelea; 7:14.
   3. kuna maelezo pote katika kitabu kwenda kwa maneno ya manabii wengine wa karne ya nane (kama vile 4:1-3 pamoja na Isa. 1:2-4).

C. Mika kwa njia nyingi ni sawasawa katika utashi na ujumbe kwa Amosi. Nyumbani kwao kumeachana kama maili ishirini tu. Wote walikuwa watu kutoka nje ya miji ambayo haijushughulishi katika mapambano wa kisiasa na nguvu ya mahakama za kifalme kama Isaya.

V. TAREHE

A. Sura ya 1 mstari wa 1 inataja urefu wa muda wa huduma ya Mika: "siku za Yothani, Ahazi na Hezekia."

B. Yeremia 26:18 inasema kwamba alitabiri katika utawala wa Hezekia.

C. Kwakuwa 1:1 inazungumzia Samaria na pia Yerusalemu na 6:1-16 ni tukio la kimahakama linalotabiri kuanguka kwa Israeli, lazima alikuwa ametabiri kabla ya kuanguka kwa Samaria mnamo mwaka 722 K.K.

D. Huduma yake pia ilienda mbali ya kuanguka kwa Samaria. Kitabu kinaonekana kukusanya jumbe katika wakati wake wote wa huduma.

VI. MAZINGIRA YA KIHISTORIA

A. Mika ni nabii wa karne ya nane aliyetenda kazi katika ufalme wa kusini na yule aitwaye Isaya leo.
B. Ulikuwa ni muda wa upanuzi wa kijeshi. Kulikuwa na shughuli nyingi za kidini lakini ilikuwa ni ibada ya Ustawi ya Kikanaani wakitumia jina la YHWH.
C. Ufalme ukuao wa Ashuru chini ya uongozi machachari wa Tiglath-Pileser III uligubikwa na uasi.
D. Kwa ajili ya muhtasari kamili wa ndani wa kihistoria angalia sehemu katika Isaya.

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI

A. Kitabu hiki kinaundwa na wasifu wa mabadiliko ya ghafla: 2:5,12; 3:1; 6:6-8; 7:14-15. Mwandishi anabadilisha kutoka hukumu kwenda kwenye unabii wa wokovu, linganisha 2:10-11 pamoja na 2:12-13.

B. Muhtasari wa msingi
   1. kuja kwa hukumu juu ya watu wa Mungu, 1:1-16
      a. kwenda uhamishoni kaskazini, 1:5-7
      b. uhamishoni kusini, 1:9-16 (3:12)
   2. adhabu na urejesho wa watu wa Mungu, 2:1-13
      a. dhambi za kijamii za walio na mali, 1-11
      b. tumaini la baadaye, 12-13

3. uongozi wa wtu wa Mungu unashutumiwa, 3:1-12
    a. viongozi wa kijamii, 1-4, 9, 11
    b. manabii, 5-7, (manabii wa kweli, mst. 8), 11
    c. kuhani, 11
    d. madhara, 12 (4:10)
4. utukufu uliorejeshwa wa baadaye wa watu wa Mungu, 4-5
    a. ukaribisho wa kiulimwengu kwa mataifa yote, 4:1-5
    b. ukaribisho kwa walemavu, waliokataliwa na wadhaifu, 4:6-8
    c. jamii ya watu waaminio ikishambuliwa lakini ikishinda, 4:9-13
    d. kuja kwa Masihi, 5:1-5a
    e. ushindi wa baadaye juu ya Ashuru, 5:5b-9
    f. hukumu ya sasa ya watu wa Mungu, 5:1, 10-15
5. Mungu anawaleta watu wake katika mahakama, 6
    a. nabii anazungumza kwa niaba ya Mungu, 1-5
    b. watu wa Mungu wanaitikia, 6-7
    c. nabii anajibu kwa ajili ya Mungu, 8
    d. Hukumu ya Mungu inaanguka juu ya watu wa mji; aidha Yerusalemu na/au Samaria, 9-16
6. Mungu kuhukumu na Baraka iliyohaidiwa kwa ajili ya watu wa Mungu inaendelea, 7
    a. watu wa Mungu wanaendelea za dhambi za kijamii, 1-6
    b. watu wa Mungu na kiongozi wao wa baadaye atakavyokuja kuwa, 14-20

VIII. KWELI KUU

A. Mika kama Amosi, alishutumu dhambi za kijamii za wenye mali na wenye nguvu.
B. Mika kama Hosea, anahukumu uasi wa kidini wa manabii na makuhani (3:11).
C. Mika alitabiri kuanguka na kwenda uhamishoni kwa wote Israeli na Yuda kwasababu ya kuabudu kwao sanamu na kukosa kwao uaminifu katika agano.
D. Mungu ni mwaminifu. Watu wake wataadhibiwa. Mungu pia ni mwenye neema na mwaminifu kwa watu wake wa Agano (mabaki) watakombolewa na kurejeshwa.
E. Mungu anataka watu Wake kuaksi tabia yake, 6:8 sio taratibu zisizo za kiimani (6:6-7).
F. Israeli, Yuda na Mataifa waaminio watabarikiwa kupitia kuja kwa Masihi akizaliwa huko Betlehemu (5:2). Huyu kiongozi mpya atakuwa kama YHWH (7:18-20).

IX. MANENO NA/AU TUNGO NA WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHATASARI

A. Maneno na/au Tungo
    1. "milima itayeyuka" 1:4 (NASB & NIV)
    2. "jeraha lake halitapona" 1:9 (NASB & NIV)
    3. Watunga kwa ubaya 2:4 (NASB & NIV)
    4. "mnakula nyama ya watu wangu" 3:3 (NASB & NIV)
    5. kubashiri 3:6 (NASB & NIV)
    6. "Sayuniutalimwa kama shamba" 3:12 (NASB & NIV)
    7. "watu...mataifa yatakuja..." 4:1-2 (NASB & NIV)
    8. "watafua panga zao kuwa majembe" 4:3 (NASB & NIV)
    9. "matokeo yake yamekuwako tangu zamani za kale" 5:2 (NIV, "ambaye asili yake ni ya zamani, toka nyakati za kale")
    10. "je nitoe...mzao wa mwili wangu kwa ajili ya roho yangu?" 6:7 (NASB & NIV)

11. Mizani ya udhalimu 6:11 (NIV, "mizani ya uongo")
12. "utazitupa dhambi zao zote katika vilindi vya bahari" 7:19 (NIV, "futa uovu wetu wote katika vilindi vya bahari")

B. Watu


1. Nimrodi, 5:6
2. Balaki, 6:5
3. Balaamu, 6:5
4. Omri, 6:16


X. MAENEO KI-RAMANI

1. Samaria, 1:5
2. Jerusalemu, 1:5
3. Lakishi, 1:13
4. Moresheth-gath, 1:14
5. Mlima Sayuni, 4:7
6. Betlehemu Efrata, 5:2
7. Nchi ya Nimrodi, 5:6
8. Shitimu, 6:5
9. Gilgali, 6:5
10. Bashani
11. Gileadi

XI. MASWALI YA KIMAUDHUI KWA MWANAFUNZI

1. Orodhesha ibada za huzuni za 1:8-16.
2. Miundo yote mitatu ya kinabii (ahadi ya kinabii, tukio la kimahakama, na ombolezo/ombolezo) yanapatikana katika Mika. Toa mifano.
3. Ni kwa namna gani Mika inakuwa kama Amosi?
4. Kwanini Mika ananukuliwa katika Yeremia 26:18?
5. Ni kwa nani msura ya 5:10-15 yanazungumzwa?
6. Orodhesha vitu ambavyo Mungu atafanya kwa ajili ya watu wake katika 7:18-20.


KAS
MAGH
MASH
KUS
MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE


PALESTINA
0 10 20 30 40
VIPIMO KATIKA MAILI

# UTANGULIZI WA NAHUMU

I. JINA LA KITABU

A. Kinaitwa kwa jina la nabii.

B. Jina lake linamaana ya "faraja" au "huruma" (kama vile Is. 57:18).

II. URASIMISHAJI

A. Kitabu hiki ni sehemu ya Manabii Wadogo kwasababu ya urefu wa maandiko yake.

B. Vinaitwa "Kumi na Mbili." Vinawezekana violiwekwa pamoja kwasababu vinafaa kuwa katika gombo moja.

C. Viko katika mgawanyo wa pili wa kanoni ya kiebrania iitwayo "Manabii."

D. Wayahudi walitaka hesabu ya vitabu katika kanoni yao kuwa sawa na hesabu ya konsonanti katika alfabeti zao, hivyo waliunganisha vitabu kadhaa.

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Ni nadharia ya unabii ya kiebrania ya kidesturi (ushairi). Ni moja ya ushairi wenye nguvu zaidi katika Agano la Kale.

B. Nahumu ilikuwa ya pekee na yenye ufundi katika uchaguzi wake wa maneno na nahau. Yeye na Isaya wanachukuliwa washairi wakubwa zaidi wa Manabii. Kuna mahusiano ya kifasihi kati yao:

1. Nahumu 1:4 na Isaya 33:19.
2. Nahumu 1:15 na Isaya 52:7.

C. Nahumu 1:2-8 ni zaburi yenye fumbo. Zaburi yenye ufunguzi ni ya kipekee kati ya manabii wadogo.

IV. UANDISHI

A. Kuna machache yanayojulikana juu ya nabii. Hili ni tukio pekee ya jina lake katika Agano la Kale.

B. Anaitwa Elkoshite ambayo yawezekana kuwa ni jina la sehemu. Kumekuwa na nadharia kadhaa:

1. wanakiweka Galilaya, mji wa Elkosh.
2. Wengineo wanaelezea kwamba Karpenaumu, "nyumba ya Nahumu," ni eneo lakini hakuna uthibitisho wa kiushahidi.
3. Isiyo-Epiphania wanakiweka kusini mwa Yuda, *The Lives of the Prophets*, XVII, mji wa Elkosh karibu na nyumba ya Mika.
4. desturi ya Kiarabu ya karne ya 16 B.K, wanakiweka Iraq (mwana wa wazazi wa uhamishoni). Mji wa Elkosh ni maili 24 kaskazini mwa Ninawi.

V. TAREHE

A. Lazima kiliandikwa kabla ya kuanguka kwa Ninawi, 612 K.K.

B. Kiliandikwa baada ya kuanguka kwa Thebesi (No-amoni) kwa Ashurbanipal mnamo mwaka 663 K.K. (kama vile 3:8 na kuendelea) kwasababu kilitumika kama mfano wa mji ulindwao na maji yaliyotekwa.

C. Yawezekana kiliandikwa mapema baada ya kifo cha Ashurbanipal mnamo mwaka 627 K.K. Alikuwa mfalme wa mwisho mwenye nguvu wa Ashuru na mnamo mwaka 626 K.K, Babeli mpya ilipata uhuru chini ya Nabopolassar.

VI. MUHTASARI MFUPI WA HISTORIA YA ASHURU NA PALESTINA

A. Nahumu kinazungumzia kuanguka kwa Ashuru ambao mji mkuu wake ni Ninawi. Mungu ametumia taifa hili katili kama chombo cha Hukumu yake ya Israeli (kama vile Is. 10:5).

B. Tukio la kwanza kuandikwa katika utawala wa Yehu (842-815 K.K.). Mnamo mwaka 841 K.K. mfalme wa Ashuru, Shalmaneser III (858-824 K.K.), alilazimisha ulipaji wa kodi.

C. Hii iliendelea chini ya Adad-nirari III (810-782 K.K). Dameski ilikamatwa na Yoashi alilazimishwa kulipa kodi.

D. Uvamizi wa kwanza mkubwa na upelekwaji uhamishoni ulitokea katika utawala wa Menahem (752-732 K.K.) kulikofanywa na Tiglath-pileser III (745-727 K.K) mnamo mwaka 732 K.K. Inavyoonekana alikiweka Pekah (740-732 K.K.) pamoja na Hoshea (732-722 K.K.) (kama vile 2 Wafalme 15:29); 1 Nyak. 5:6; 2 Nyak. 30:6,10; Is. 9:1. Huu utawala wa Palestina uliiathiri Yuda kwasababu Ahazi (735-715 K.K) pia alilipa kodi.

E. Hoshea alijaribu kuunda ushirika na Israeli pamoja na Misri na alivamiwa na Shalmaneser V (727-722 K.K.) Samaria, mji mkuu, ulianguka miaka mi 3 kuzungukwa na Sargon II (721-705 K.K.). Israeli ilikimbilia uhamishoni mwa Medea (kama vile 2 Wafalme 17:3-20; 18:20-21; Is. 7:8; 8:4; 10:11; 36:20; Hos. 9:3; 10:6,14; 11:5). Sargon II alivamia na kulazimisha ulipaji kodi kwa Yuda mnamo mwaka 720 K.K. na 712 K.K.

F. Katika Yuda, Hezekia (728-687 K.K) alitawala baada ya Ahazi. Mwanzoni alilipa kodi kwa Sargon II. Baadaye alikataa kodi kwa Ashuru (kama vile 2 Wafalme 18). Yuda ilivamiwa na Senakeribu (704-681 K.K.) mnamo mwaka 701 K.K., lakini alilazimishwa kuondoka na pigo lililosababishwa na Malaika wa Bwana, ambaye aliuwa askari wa Ashuru 185,000 (kama vile Is. 10:16; 36:1-37:38; 2 Wafalme 18:13-19:37; 2 Nyak. 32:1-31).

G. Baadaye, Manase alilazimishwa kusalimu amri kwa Esarhaddon (681-669 K.K.) (kama vile 2 Nyak. 33:1-11).

H. Mwana wa Esarhaddon, Ashurbanipal (638-633 K.K.), alikuwa mfalme mwenye nguvu wa Ashuru. Baada ya kifo chake, wakati wa kipindi cha kuanguka kwa ghafla:
   1. Nabopolassar (625-605 K.K.) alianzisha Babeli Mpya iliyo huru.
   2. Psammetihus I (664-609 K.K.) alirejesha Misri kuwa huru.
   3. Yosia (640-609 K.K.) alirejesha Yuda katika uhuru.
   4. Cyaxaxes (625-585 K.K.) alianzisha Media huru.

I. Ninawi, mji wa ki-Ashuru ulianguka mnamo mwaka 612 K.K., kwa Nabopolassar na Cyaxaxes. Ashuru, mji mkuu wa zamani ulikuwa umekwisha anguka mnamo mwaka 614 K.K.

J. Ninawi ilichukua Ekari 1,850 na ilikuwa na maili 8 ya kuta zenye nguvu.

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI

A. Ufunguzi, 1:1

B. Zaburi ya ukari na neema ya YHWH, 1:2-8 (yenye mafumbo kwa sehemu).

C. uhalisia wa tabia ya Mungu, hukumu kwa Ninawi, ukombozi kwa Yuda, 1:9-2:2.

D. simulizi ya kijedwali ya kiushairi ya kuzungukwa na kuanguka kwa Ninawi, mji mkuu, 2:3-3:19.

VIII. KWELI KUU

A. Shabaha ya kitabu ni uharibifu wa Ninawi, mji mkuu wa Ufalme katili wa kiashuru. Ulifanywa mji mkuu na Senakeribu mnamo mwaka 700 K.K. Lilikuwa mashariki ukingoni mwa Mto Hedekeli na ulikuwa na ngome imara sana .
B. Mji uliharibiwa kabisa kikamilifu na Wababeli na wa-Medes mnamo mwaka 612 K.K., kama ilivyokuwa Ashuru hapo kabla mnamo mwaka 614 K.K. Walitumia mto ambao ulitiririka kuzunguka kuta. Walitengeneza njia mpya za maji ya mto kuingia katika mahifadhio na baadaye kuyaachilia yote kwa pamoja. Nguvu ya maji ilivunja chini sehemu kubwa ya ukuta, 2:6.
C. Mungu alitumia Waashuru katili kuhukumu watu wake (Is. 10:5) lakini sasa Waashuru walihukumiwa. Tunavuna tunachopanda, Gal. 6:7.

IX. MANENO NA/AU TUNGO NA WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHTASARI

A. Maneno n/au tungo
1. takatifu, 1:1 (NASB & NIV)
2. maono, 1:1 (NASB & NIV)
3. "Bwana si mwepesi wa hgasira," 1:3 (NASB & NIV)
4. "ngome," 1:7 (NIV, "kimbilio")
5. ngao, 2:5 (NIV, "ngao ya ulinzi")
6. "malango yam to yanafunguliwa na jumba la mfalme limeyeyushwa," 2:6 (NIV, "malango ya mto yanaachwa wazi na jumba la mfalme linaanguka")
7. "nitafunua marinda yako mbele ya uso wako," 3:5 (NASB & NIV)
8. "watoto wake wachanga walisetwa kwenye maahano ya njia kuu zote," 3:10 (NASB & NIV)


B. Watu
1. Beliali, 1:15 (NIV, "mbaya")
2. BWANA wa Majeshi, 2:13 (NIV, "Bwana mwenye nguvu")

X. MAENEO KI-RAMANI


1. Bashani, 1:4
2. Karmeli, 1:4
3. Lebanoni, 1:4
4. No-amoni (Thebesi), 3:8
5. Ninawi, 1:1

XI. MASWALI YA KI-MAUDHUI YA MWANAFUNZI

1. Nini makusudi makuu ya kitabu hiki?
2. Mtu anawezaje kuhusianisha 1:3 na 7?
3. Mtu anawezaje kuhusianisha Yona na Nahumu?
4. Kwanini Nahumu anachukuliwa kuwa mshairi mkubwa?
5. Ni kwa namna gani 2:6 inahusiana na historia ya kuanguka kwa Ninawi?
6. Kwanini mji wa Misri unatajwa katika 3:8-10?
7. Orodhesha sitiari shurutishi za 3:14-15.


MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE
KAS
MAGH
MASH
KUS

# PALESTINA




VIPIMO KATIKA MAILI

# UTANGULIZI WA HABAKUKI

I. JINA LA KITABU
   A. Hiki kinaitwa jina baada ya nabii huyu.
   B. Hili jina Habakuki linamaanisha "kupapasa au "kukumbatia."
   C. Katika tafsiri ya maandiko ya Agano la Kale, huyu anaitwa "Hambakoum" ambapo hili ni jina la ki-Ashuru lenye kumaanisha "mbogamboga."

II. URASIMISHAJI
   A. Kitabu hiki ni sehemu ya kipengele cha "manabii waliofuatia" (Ecclesiasticus 49:10).
   B. Hiki ni moja ya kipengele cha wale "Kumi na Wawili," kundi la manabii Wadogowadogo (Baba Bathra 14b)
      1. Kama vilivyo vitabu vya Yeremia, na Ezekieli, hivi vinashahabiana na gombo moja la chuo.
      2. Hiki kinawakilisha makabila kumi na mawili au uwakilishi wa namba za ushirika.
      3. Hiki kinaakisi mtazamo wa kitamaduni wa mtiririko wa vitabu.
      4. Mfululizo wa kipengele cha "Kumi na Wawili," au Manabii Wadogowadogo, umekuwa ukihusianishwa na wanazuoni wengi katika mpangilio wa mfululuzo wa matukio. Ni dhahiri kuwa Nahumu, Habakuki na Sefania ni kwa ajili ya ushirika.

III. AINA YA UWASILISHAJI – Si kawaida sana kuzungumza na Mungu kwa niaba ya watu. Sura ya kwanza ni karipio au yenye maana ya kuiwasilisha kweli kupitia mazungumzo husika.

IV. MWANDISHI
   A. Nabii huyu anazungumza na YHWH juu ya Yuda. Manabaii wote wanazungumza na watu kwa niaba ya Mungu.

   B. Nabii huyu anashabihiana moja kwa moja na kipindi cha Danieli, Yeremia, Ezekieli, Nahumu, na Sefania. Tunawahita watu hawa Manabii wa Karne ya Saba.
   C. Huenda huyu ni mwanamziki aliyehusiana na Kwaya ya Hekalu kwa sababu:
      1. 3:1 ina jina *Shigionoth*. Tanbihi ya toleo la NASB inaliita hili "muundo wa hisia za kiushairi za hali ya juu." Hili ni neno la kimuziki lenye maana isiyojulikana, ni pumziko au mwandamo.
      2. matumizi ya maneno mengine ya kimziki, *Selah* katika 3:3, 9, 13.
      3. matumizi ya kifungu kilicho katika 3:19, "ataniendesha katika mahali pangu palipoinuka."

V. TAREHE (Kumekuwa na nadharia kuu mbili)
   A. Utawala wa Manase (687-642 K.K.). Mara nyingi hii inahusianishwa na kipengele cha Habakuki kilicho katika Sheria na kushamiri kwa Wakaldayo, dora ya sasa ya Babeli (kama vile Habakuki 1:5).

   B. Utawala wa Yehoiakimu (609-598 K.K.). Hii ingewekwa katika kipindi cha Farao-Neco II aliyeusambaratisha mji na baadaye Nebukadneza kuchukua eneo lote baada ya kuyaondoa mabaki ya watu wa ki-Ashuru na Wamisri huko Karkemishi mnamo mwaka 605 K.K.
   C. Pseudo-Epiphanius, katika *Lives of the Prophets,* anasema kwamba huyu anatoka katika kabila la Simeoni. Huyu alijitenga na ushauri wa Nebukadneza II' mnamo mwaka 586 K.K. na kurudi baada ya kuanguka kwa mji na kufariki miaka miwili kabla ya kutoka uhamishoni. Hata hivyo, chanzo hiki ni cha baadaye na hakitegemewi.

VI. MAZINGIRA YA KIHISTORIA

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI
   A. Kitabu hiki kinajikita katika vipengele vikuu viwili:
      1. sura ya 1 na 2 – mazungumzo kati ya nabii na Mungu

2. sura ya 3 – shairi la kumsifu Mungu kwa kuitawala historia.

B. Mazungumzo kati ya Mungu na manabii wake, 1:2-2:20
   1. Manung'uniko ya Habakuki dhidi ya Mungu kukawia kuadhibu, 1:2-4
   2. Jibu la kwanza la Mungu, 1:5-11
   3. Tatizo la maadili ya Habakuki pamoja na jibu la Mungu, 1:12-2:1
   4. Mwaitikio wa pili wa Mungu, 2:2-5
      a. Mpango wa Mungu ni wa uhakika, andika, 2:20
         (1) baraka za imani, 2:4, 14, 20
         (2) hukumu ya uovu, 2:5, 6-20
      b. Yawapasa watu wa Mungu kuwa waaminifu wa agano, 2:4-5 (3:16-19)
      c. Mungu atawaangamiza wapagani na miungu iletayo machafuko, 2:6-20 (5 ole)
         (1) 2:6-8, kisasi cha machafuko
         (2) 2:9-11, kisasi cha machafuko
         (3) 32:12-14, kisasi cha machafuko
         (4) 2:15-17, kisasi cha machafuko
         (5) 2:18-20, ibada za sanamu

C. Zaburi ya Baraka za matendo ya uaminifu wa Mungu wa ukombozi uliopita na tumaini la siku zijazo, 3:1-19.
   1. Matendo ya Mungu yaliyopita ya ukombozi uliopita katika muundo wa juu wa kiushairi, kwa kutumia muundo wa stiari (3:1-15):
      a. kutoka
      b. uumbaji
      c. utekaji
   2. imani na uvumilivu wa manabii katika ukombozi wa Mungu japo hakuna ishara ionekanayo, (2:4; 3:16-19)

VIII. KWELI KUU

A. Haya ni maadili ya kiulimwengu. Dhambi itahukumiwa. Hata watu wa Mungu waliochaguliwa watawajibika kwa ajili ya matendo yao (Gal. 6:7).
B. Hata katika ulimwengu huu ulioanguka bado Mungu anaendelea kuyatawala matukio. Anatumia sababu za uovu, lakini pia atahukumu!
C. Inakubalika kumuuliza Mungu. Hata hivyo, mara nyingi ni uwepo wa Mungu si majibu ya kifikra yawezayo kutoshereza.
D. Kitabu hiki ni chanzo maarufu cha dhana ya thiolojia ya Paulo "ataishi kwa imani yake" (kama vile 2:4). Hatimaye uovu utasambaratika wenyewe. Watu wa Mungu lazima watembee katika imani katikati ya siku hizi za uovu! Imani lazima ihusianishwe na mambo ya sasa, 3:17-19.

IX. MANENO NA/AU VIFUNGU NA WATU WA KUWATAMBUA KIMUHTASARI

A. Maneno na/au Vifungu
   1. "hukumu yao na ukuu wao hutoka katika nafsi zao wenyewe," 1:7 (kama vile 1:11c) (NIV, "wamejiwekea sheria wao wenyewe na kujitangazia utukufu")
   2. "Ee Bwana, Mungu wangu, mtakatifu wangu," 1:12 (NASB na NIV)
   3. "Ee Jabali," 1:12 (NASB na NIV)
   4. "huwakamata katika wavu wake," mist. 15-17 (NIV, "hutoa dhabihu katika wavu wake")
   5. "lakini mwenye haki ataishi kwa imani yake," 2:4 (NASB na NIV)
   6. kuzimu 2:5 (NIV, "kaburi")
   7. ajitwikaye mzigo wa rehani, 2:6 (NIV, "ajitwikaye")
   8. "kikombe cha mkono wa kuume," 2:16 (NASB na NIV)
   9. Sala, 3:1 (NASB na NIV)

10. Selah, 3:3,9,13 (NASB na NIV)
11. masihi wako, 3:13 (NIV, "masihi wako")
12. "Yeye huifanya miguu yangu kuwa kama ya kulungu," 3:19 (NIV, "yeye hunifanya miguu yangu kama ya mbawala")


B. Watu – hakuna


X. MAENEO KI-RAMANI

1. Kaldayo, 1:6 (NIV, "Wababeli")
2. Temani, 3:3
3. Mlima Parani, 3:3
4. Midiani, 3:7

XI. MASWALI YA KI-MAUDHUI KWA MWANAFUNZI

1. Ni kwa namna gani kitabu hiki ni cha tofauti sana na vitabu vingine vya manabii wengine wadogowadogo?
2. Taja mazungumzo kati ya Mungu na nabii yaliyo katika sura 1-2.
3. Kwa nini inafikiriwa kwamba Habakuki alikuwa mwana-mziki?
4. Eleza sura ya 1:16-17.
5. Je! sura ya 2:4 inamaanisha nini katika muktadha wake? Ni kwa namna gani Paulo inaitumia hii katika Rum. 1:!7 na Gal. 3:11?


KAS
MAGH
MASH
KUS
MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE



PALESTINA
0 10 20 30 40
VIPIMO KATIKA MAILI

# UTANGULIZI WA SEFANIA

I. JINA LA KITABU
   A. Hiki kinaitwa jina kwa jina la nabii huyu.
   B. Jina lake lilimaanisha:
      1. "YHWH amejificha" au
      2. "YHWH hutazama"

II. URASIMISHAJI
   A. Kitabu hiki ni sehemu ya kipengele cha "manabii wa mwisho" (Ecclesiasticus 49:10).
   B. Ni sehemu ya kipengele cha "wale Kumi na Wawili," kundi la manabii wadogowadogo (Baba Bathra 14b):
      1. kama vilivyo., vitabu vya Yeremia. na Ezekieli, hivi vinaendana na gombo moja la chuo.
      2. hiki kinawakilisha makabila kumi na mawili au uwakilishi wa namba za ushirika.
      3. Hiki kinawakilisha mtazamo wa kitamaduni wa mtiririko wa vitabu.
   C. Mpangilio wa kipengele cha "wale Kumi na Wawili" au Manabii Wadogowadogo umekuwa ukihusianishwa na wanazuoni wengi kwa mtiririko maalumu. Ni dhahiri kwamba Nahumu, Habakuki na Sefania vinaunda umoja.

III. AINA YA UWASILISHAJI
   A. Huu ulikuwa unabii wa kisasa wa Kiebrania (ushairi) uliojikita katika suala la dhambi, hukumu na urejesho.
   B. 3:14-20 inaweza kuwa tenzi ya kale.

IV. UANDISHI
   A. Mara nyingi kitabu hiki kilikuwa na uzao usiyo sahihi: "...mwana wa Kushi, mwana wa Gedalia, mwana wa Amaria, mwana wa Hezekia," 1:1.
      1. Hili linamaanisha kwamba huyu alikuwa mwana wa uzao wa ufalme wa Yuda. Ikiwa Hezekia aliyeorodheshwa ni mfalme wa Yuda (715-687 K.K.) hii inaonekana kuwa sababu ya uzao mrefu.
      2. Huenda urefu huu ni kwa ajili ya kuuthibitisha Uyahudi wake kwa sababu ya jina la babaye lilikuwa *Kushi* (Mwe-Ethiopia).
   B. Wengi wanaamini kuwa huyu alikuwa umbu la Yosia na huenda alifundishwa na walimu walewale kama Mfalme wa ki- Mungu.
   C. Wengine watatu walio katiaka Agano la Kale wana jina hili hili: I Nya. 6:36-38; Yer. 21:1; II Fal. 25:18-21; 29:25; 37:3; 52:24-27; Zek. 6:10,14.

V. TAREHE
   A. Sefania anazungumza wakati wa uhai wa Mfalme Yosia (640-609 K.K.).
   B. Kwa sababu ya mivutano ya ndani ya Yuda iliyotajwa katika, 1:4-6, 8-9, 12; 3:1-3, inaonekana kwamba wapokeaji walikuwa Wa-yudea kambla ya ukarabati wa Yosia kufanyika (621 K.K.).

VI. MAZINGIRA YA KIHISTORIA
   A. Wengine wanaviona vitendea kazi vya ujio wa Mungu kama makutano ya wa-Scythia (NIV, mbinu ya Fransisco 626 K.K.) ambayo hapo awali yalishambuliwana Ashuru. Heroditus (I:103-106) inasema

kwamba Wa-scythia waliingia kupitia Palestina pamoja na Misri kabla ya kurudishwa na Farao Psammetichus I (663-609 K.K.) kwa kuwalipa.

B. Ingawa ujio wa Wa-scythia unawezekana, huenda ni Babeli iliyoivamia Yuda. Wanazuoni wengi wanawaona wavamizi kama walikuwa Wa-babeli.

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI (vilivyochukuliwa kutoka *Introduction to the Old Testament* na R.K. Harrison, uk. 939-940)

A. Siku ya Bwana, 1:1-2:3
1. nami nitayakatilia mbali mabaki ya Baali, 1:2-6.
2. siku ya Bwana i karibu, 1:7-13.
3. siku ile ya ghadhabu, 1:14-18.
4. mtafichwa katika siku ya hasira ya Bwana, 2:1-3.

B. Hukumu dhidi ya Mataifa ya Kigeni, 2:4-15
1. Filistia, 2:4-7
2. Moabu na Ammoni, 2:8-11
3. Misri, 2:12
4. Ashuru, 2:13-15

C. Ole na Baraka, 3:1-20
1. Ghadhabu kwa Yerusalemu, 3:1-7
2. Uhakika wa baraka kwa mabaki ya uaminifu, 3:8-20

VIII. KWELI KUU

A. Nabii huyu anaonya kuhusu kuwakaribia wale waliovamia Yuda. Sababu ya tendo hili la ghadhabu ilikuwa ni kuenea kwa ibada ya Sanamu ndani ya Yerusalemu iliyoanzishwa na Manase. Sefania anaitumia dhana ya "Siku ya Bwana." Mara nyingi manabii walitumia migogoro iliyokuwepo katika siku zile zao kuzisawiri nyakati zijazo, matukio ya siku za mwisho.
B. Kuna wito wa toba katika 2:3. Ni tumaini la Yuda pekee lililokuwa katika upendo (3:17) na uwepo wa ki-Masihi (3:15 na 17)!
C. Ni dhahiri kwamba Mungu aliitumia Ashuru kumwadhibu Israeli Ufalme huu wa nchi za Kiislamu (Irani) sasa inasimama kwa ajili ya kuhukumiwa lakini ndivyo ilivyo, vivyo hivyo, Yuda!

IX. MANENO NA/AU TUNGO NA WATU WA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

A. Maneno na /au Vifungu
1. "pamoja na makuhani," 1:4 (NASB na NIV)
2. "jeshi la mbinguni," 1:5 (NIV, "jeshi la kutisha")
3. "siku ya Bwana i karibu," 1:7 (NASB na NIV)
4. "wote warukao juu ya kizingiti," 1:9 (NIV, "wote waepao kutembea juu ya kizingiti")
5. "wafanya biashara," 1:11 (NIV, "jimbo la kibiashara")
6. "Na makundi ya wanyama watalala kati yake, wanyama wote wa mataifa", 2:14 (NASB na NIV)
7. "Kila mtu apitaye atazomea, Na kutikisa mkono wake," 2:15 (NIV, "wote waliopita kwa kejeli na kuikungu'uta miguu yao")
8. "mlima wangu mtakatifu," 3:11 (NIV, "kilima changu kitakatifu")

B. Watu


1. Kushi, 1:1
2. Milkomu, 1:5 (NIV, "molech")
3. Wakeherethite, 2:5 (NIV, "Mkerethite")


X. MAENEO KI-RAMANI

1. Gaza, 2:4
2. Ashkeloni, 2:4
3. Ashdodi, 2:4
4. Ekroni, 2:4
5. Sodoma na Gomora, 2:9
6. Ethiopia, 2:12 (NIV, “Wakushi”)

XI. MASWALI YA KI-MAUDHUI KWA MWANAFUNZI

1. Kwa nini Sefania ana mlolongo mrefu wa uzao kuliko manabii wote wa Agano la Kale?
2. Kwa nini unabii wa Sefania uhusuo hukumu ni wa kutisha kuliko gharika la Nuhu?
3. Taja na eleza dhana ya "Siku ya BWANA."
4. Kwa nini Yuda naye alikuwa mwenye dhambi na mwenye hatia kuliko Israeli?
5. Je, sura 3:9 ina jambo la kiulimwengu lenye kuhusiana na watu wa Mataifa? Kwa nini?
6. Ni kwa namna gani 3:17 inaonyesha moyo wa Mungu?


KAS
MAGH
MASH
KUS
MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE


PALESTINA
0 10 20 30 40
VIPIMO KATIKA MAILI

# UTANGULIZI WA HAGAI

I. JINA LA KITABU

A. Hiki kilipewa jina baada ya mhubiri wake.

B. Jina lake linamaanisha "Sikukuu." Yodi au "i" mwishoni inaweza kuwa ufupisho wa YHWH, ikiwa ni hivyo hii ni "sikukuu ya YHWH" (kama vile I Nyak. 6:30) au kiwakilishi "yangu" ambacho pia kingeweza kumrejelea YHWH.

II. URASIMISHAJI

A. Kitabu hiki ni sehemu ya kipengele cha "manabii wa mwisho" (Ecclesiasticus 49:10).

B. Ni sehemu ya kipengele cha "wale Kumi na Wawili," kundi la manabii wadogowadogo (Baba Bathra 14b):

1. kama vilivyo vitabu ya Isaya, Yeremia na Ezekieli, hivi vinaendana na gombo moja la chuo.
2. kinawakilisha makabila kumi na mawili au uwakilishi wa namba za ushirika.
3. hawa wanaakisi mtazamo wa kitamaduni wa vitabu vilivyo katika mtiririko.

C. Mtiririko wa kipengele cha "wale Kumi na Wawili" au Manabii wadogowadogo kimekuwa kikihusianishwa na wanazuoni wengi katika mfululizo wa mpangilio wa matukio. Ni dhahiri kwamba Hagai na Zekaria wanalinganishwa kihistoria.

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Huu ni mfululizo wa hotuba nne au tano (1:13).

B. Huu si wa kiushairi.

IV. UANDISHI

A. Hagai anatajwa katika Ezra 5:1; 6:14 na Zekaria 8:9 ambapo anahusianishwa na Zekaria. Huenda huyu alikuwa amekwisha kurejelea toka uhamishoni.

B. Huyu pia anatajwa katika I Esdras 6:1; 7:3; II Esdras 1:40 na Ecclesiasticus 49:11 hii ni nukuu toka Hagai 2:23.

C. Jerome anasema kwamba huyu alikuwa kuhani lakini hili ni tendo la kutokuelewana kutokea 2:10-19.

D. Ewald na Pusey wanatoa maoni kwamba 2:3 hii inamaanisha kwamba huyu aliliona Hekalu la Suleimani jambo ambalo lingemfanya awe na kati ya umri wa miaka 70 au 80.

E. Cyril wa Iskandria anataja maoni ya jumla katika siku zile zake ya kwamba huyu alikuwa malaika. Hili linatokana na kutokueleweka kwa neno la Kiebrania "mjumbe" katika 1:13.

F. Toleo la LXX lihusianisha Zaburi kadhaa na Hagai pamoja na Zekaria: 112, 126, 127, 137, 146-149.

G. Hotuba zote 4 za Hagai zinanukuliwa katika nafsi ya tatu ambayo inamaanisha:

1. mbinu ya kawaida ya kifasihi,
2. mwandishi au mhariri.

V. TAREHE

A. Hagai alikuwa nabii wa kipindi cha baada ya uhamisho sambamba na Zekaria, wa sasa.

B. Kitabu hiki kinapewa tarehe kuanzia siku ya kwanza ya mwezi wa sita (1:1) hadi siku ya ishirini na nne ya mwezi (2:10,20) ya mwaka wa pili wa Dario I Hystaspes (521-486 K.K.). Hivyo, tarehe hii ni mwaka 520 K.K. Hii ilikuwa miaka minne kabla ya kumalizika kwa Hekelu la pili mnamo mwaka 516 K.K., na kuutimiza unabii wa Yeremia kwa kuangalia miaka sabini ya uhamisho ambayo ilianza mnamo mwaka 586 K.K.

VI. MTIRIRIKO WA KIPINDI (makala hii imechukuliwa kutoka *The Minor Prophets* na Dkt. Theo Laetsch, ilichapishwa na Concordia, uk. 385.)

| Mwaka wa Utawala wa Dario | Mwaka K.K | Mwezi | Siku | Andiko | Maudhui |
|---|---|---|---|---|---|
| 2 | 520 | 6 | 1 | Hag.1-11 | Hagai nawahamasisha watu katika |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Sept/Oct. | | | shughuli |
| | | | 24 | Hag.1:12-15 | Watu wanaanza kujenga |
| | | 7<br>Oct/Nov. | 1 | Hag.2:1-9 | Utukufu wa mwisho wa Nyumba ya Mungu |
| | | 8<br>Nov/dec | ? | Zek.1-6 | Zakaria anaanza kutabiri |
| | | 9<br>Dec/Jan | 24 | Hag.2:10-19 | Mungu ataanza kubariki |
| | | | | Hag.2:20-23 | Ufalme wa Masihi unaanzishwa baada ya kushinda Nguvu za Ulimwengu |
| | | 11<br>Feb/March | 24 | Zek.1:7-6:8 | Maono ya Zakaria ya usiku |
| | | | | Zek.6:9-15 | Kupewa taji kwa Yoshua kwa kutambua Ukuhani wa Masihi |
| 4 | 518 | 9<br>Dec/Jan | 4 | Zek.7, 8 | Toba inahimizwa;Baraka zinahaidiwa |
| 6 | 516 | 12<br>Mar/April | 3 | Ezra 6:15 | Uwekaji Wakfu wa Hekalu |
| | | ? | | Zek.9-14 | Baada ya uwekwaji wakfu wa Hekalu |

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI – Sehemu hii imefupishwa kupitia hotuba ya nabii.
   A. Hotuba ya kwanza, 1:1-11, Kujengwa upya kwa Hekalu!
   B. Viongozi na watu wanaitikia, 1:12-15
   C. Hotuba ya Pili, 2:1-9, ukubwa wa Hekalu si tatizo!
   D. Hotuba ya Tatu, 2:10-19, Baraka za Mungu zitaachiliwa ikiwa watu watatii na kulijenga upya Hekalu
   E. Hotuba ya Nne, 2:20-23, Utawala wa Kiulimwengu wa Masihi ulionyeshwa ndani ya Zerubabeli.

VIII. KWELI KUU
   A. Kitabu hiki kinajikita katika kulijenga upya Hekalu la Pili ambalo lilikuwa limepingwa kwa miaka kadhaa hapo mwanzoni:
      1. kama vile Ezra 5:16 (mwaka wa 1- chini ya Sheshbaza)
      2. Ezra 3:8-13 (mwaka wa 2 – chini ya Zerubabeli)
   B. Ahadi za Mungu kuhusu baraka za kimwili za papo kwa papo na baraka za baadaye za ki- Masihi zinahusianishwa na kujengwa upya kwa Hekalu (urejesho wa Agano la Musa).
   C. Ukubwa wa Hekalu na fahari ya Hekalu havikuwa tatizo, bali kuwepo kwake. Uwepo wa Mungu ulioashiria kuwa kulikuwa na utukufu wa kweli!


IX. MANENO NA /AU VIFUNGU NA WATU
   A. Maneno na /au Vifungu
      1. "ninyi kukaa katika nyumba zenye mapambo ya mbao," 1:4 (NASB na NIV)
      2. "Zitafakarini njia zenu," 1:5,7 (NIV, "angalieni ...")
      3. "nami nitatikisa mataifa yote," 2:7 (NASB na NIV)
      4. "Utukufu wa mwisho wa nyumba hii utakuwa mkuu kuliko utukufu wake wa kwanza," 2:9 (NASB na NIV)
      5. "Zerubabeli... nami nitakufanya kuwa kama pete yenye muhuri," 2:23 (NASB na NIV)

   B. Watu
      1. Dario I, 1:1
      2. Zerubabeli, 1:1
      3. Yoshua, 1:1
      4. "Bwana wa Majeshi," 1:2 (NIV, "BWANA Mkuu")


X. MAENEO KI-RAMANI – HAKUNA!

XI. MASWALI YA KI-MAUDHUI KWA MWANAFUNZI

1. Nini dhima kuu ya kitabu hiki?
2. Kwa nini kurudi kwa Wayahudi baada ya uhamisho kulikuwa kwa nyakati ngumu katika Yuda?
3. Ni pengele gani vya sura 2 vilivyo vya ki-Masihi? Kwa nini?
4. Eleza 2:3.
5. Eleza 2:10-19.
6. Kwa nini mambo haya yaliyo makuu yanazungumziwa juu ya Zerubabeli wakati historia inanukuu mambo machache sana kuhusu kukamilika kwake? (2:20-23)


MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE
KAS
MAGH
MASH
KUS

# PALESTINA



# UTANGULIZI WA ZEKARIA

I. JINA LA KITABU

A. Hiki kinapewa jina la nabii huyu.

B. Jina lake lilimaanisha "YHWH hukumbuka," "alikumbukwa na YHWH," au "YHWH amekumbuka." Jina lake linadokeza kwamba YHWH bado alikuwa na Wayahudi na amelirejesha agano.

II. URASIMISHAJI

A. Kitabu hiki ni sehemu ya kipengele cha "manabii wa mwisho" (Ecclesiasticus 49:10).

B. Hii ni sehemu ya kipengele cha "Kumi na Wawili," kundi la manabii wadogo wadogo (Baba Bathra 14b):

1. kama ilivyo Isaya, Yeremia na Ezekieli, hawa wanaendana na gombo la chuo moja.
2. hawa wanawakilisha makabila kumi na mawili au uwakilishi wa namba za ushirika.
3. Hawa wanaukisi mtazamo wa kidesturi wa mtiririko wa vitabu.

C. Mpangilio wa vipengele vya "Kumi na Wawili" au Manabii Wakuu umekuwa ukihusianishwa na wanazuoni wengi ili kuweka mtiririko mzuri. Ni dhahiri kwamba vitabu vya Hagai na Zekaria vinaunda jozi ya kihistoria.

III. AINA YA UWASILISHAJI

A. Kitabu hiki ni mfano wa fasihi ya matukio ya siku za mwisho:

1. Sura 1-8 ni nathari za kibiblia.
2. Sura 9-14 kimsingi ni za kiushairi.

B. Aina hii ya uwasilishaji ilikuwa ya kipekee kwa Wayahudi. Mara nyingi hii illitumika katika nyakati za kukamilika kwa mvutano ili kueleza uhalisia kwamba Mungu anazidi kuitawala historia na angeleta ushahidi kwa watu wake.

C. Hii inabainishwa na:

1. hisia zenye nguvu za ukuu wa Mungu kiulimwengu,
2. mapambano kati ya mema na mabaya katika zama hizi,
3. matumizi ya sheria za maneno ya siri,
4. matumizi ya rangi,
5. matumizi ya namba,
6. matumizi ya wanyama, wakati mwingine wanyama/wanadamu,
7. Mungu huwasilisha ufunuo wake kwa njia ya ndoto au maono ambayo mara nyingi ni kupitia upatanisho wa kimalaika.
8. Kimsingi hii inajikita katika wakati ujao.

D. Baadhi ya mifano mingine ni:

1. Agano la Kale
   a. Danieli 7-12
   b. Ezekieli 37-48 (?)
2. Agano Jipya
   a. Mathayo 24, Marko 13, Luka 21, II The. 2
   b. Ufunuo
3. Isiyo ya kisheria
   a. I Enoko
   b. IV Ezra (Esdras)
   c. II Baruch

E. Jerome anakiita kitabu cha Zekaria kitabu cha maagizo zaidi katika Agano la Kale. Bado hiki kinaendelea kuzungumziwa kwa mapana ndani ya kitabu cha Agano Jipya:
   1. sura 1-8 katika kitabu cha Ufunuo.
   2. Sura ya 9-14 katika Injili.

F. Ni vigumu kuyafasiri maono haya lakini ikiwa tutayatunza mazingira ya kihistoria ndani ya akili zetu haya yatahusiana na tendo la kulijenga upya Hekalu la Yerusalemu baada ya uhamisho. Haya yanajikuta katika siku mpya ya msamaha na kuja kwa Masihi.

IV. MWANDISHI

A. Zekaria lilikuwa jina la kawaida la Kiebrania. Hili lilitamkika katika namna mbili: Zekaria au Zakaria. Kuna watu 27 katika Agano la Kale wanaotamkwa kwa herufi "e" na 2 ambao wanatamkwa kwa herufi "a."

B. Sura 1:1 inasema kwamba huyu ni kuhani (kama vile Ezra 5:1; 6:14; Neh. 12:4,16). Kwa nini Berechiah, ambaye anatajwa katika 1:1 na aliondolewa katika Ezra 5:1 na 6:14 haijulikani. Hili lingeweza kumfanya Zekaria kuwa nabii wa kipindi cha awali cha baada ya uhamisho kama Hagai na Malaki na huenda Obadia na Yoeli.

C. Wanazuoni wengi wa sasa wanaukataa umoja wa Zekaria. Hii ni kwa sababu sura 1-8 ni za tofauti sana na sura 9-14. Katika sura 1-8 nabii anaitwa jina na tarehe ya kihistoria inatolewa. Kwa uwazi mazingira ni ya kipindi cha baada ya uhamisho. Sehemu hii inazungumzwa kwa mapana na Yohana katika kitabu chake cha Ufunuo. Hata hivyo, sura 9-14 hazikupewa tarehe. Hapa hakuna nabii aliyetamkwa jina. Mazingira ya kihistoria ni ya matukio ya siku za mwisho. Sehemu hii inazungumziwa mara kwa mara katika Injili.

   Katika Mt. 27:9 Yesu inaipa sifa nukuu ya Yeremia ambayo inatoka katika Zekaria 11:12-13. Huu ndiyo mwanzo wa uelekeo wa kuupinga uandishi wa sura 9-14 hadi Zekaria. Hata hivyo, Magombo ya Bahari ya Chumvi yana kitabu cha Zekaria kama muungano. Kuna mambo kadhaa ya ndani yenye kuugusia muungano huu:
   1. matumizi ya namba "mbili" - 4:3; 5:9; 6:1; 11:7; 13:8,
   2. matumizi ya KAULI TAARIFA - 2:7,10; 3:2,8; 4:7; 9:9,13; 11:1-2; 13:7,
   3. matumizi ya kifungu "aliyepita kati yake, wala aliyerudi "ambacho ni cha kipekee kwa Zekaria - 7:14; 9:8,
   4. matumizi yaliyorudiwa rudiwa ya kifungu "asema Bwana" – kilichotumika mara 16,
   5. muundo wa neno *qal* wa kifungu "ikikaliwa" - 2:8; 7:7; 12:6; 14:10. (Hivi vinachukuliwa R.K. Harrison's *Introduction to the Old Testament*, uk.954.) Kwa mjadala zaidi uhusuo muungano wa kitabu hiki (kama vile E.J. Young's *Introduction to the Old Testament*, uk.280).

D. Uhalisia huu kwamba Zekaria unaundwa na kipengele cha kihistoria na kinachofuatia lazima uwe wa kushangaza. Tumeuona mwelekeo huu kabla ya:
   1. Isaya 1-39 na 40-66
   2. Ezekieli 1-29 na 30-48
   3. Danieli 1-6 na 7-12

E. Utangulizi mpya wa kitabu cha Agano la Kale wa Andrew Hill na John Walton uk. 421 unaifupisha migawanyo yote kwa mfululuzo wa uoanishi. Mbinu hii ya kifasihi iliyo thabiti inatoa ushahidi wa baadaye wa mwandishi mmoja.

V. TAREHE

A. Zekaria 1:1 inaeleza kwamba nabii alliianza huduma yake katika mwaka wa 2 na mwezi wa 8t wa utawala wa Dario I (522-486 K.K.). Wanazuoni wengi wanadai kwamba huyu ni Dario I Hystrapes

aliyeuchukua ufalme wa Uajemi baada ya Cambyses II (530-522), mwana wa Koreshi II, aliyefariki mnamo 522 K.K. Dario alikuwa jemedari wa Jeshi la Kiajemi.

B. Hili linaweza kutengeneza tarehe ya 519 au 520 K.K. (miezi 2 baada ya Hagai). Huyu alihubiri kwa miaka miwili (kama vile 1:1,7; 7:1).

VI. MAZINGIRA YA KIHISTORIA

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI (vilivyochukuliwa kutoka *Introduction to the Old Testament* na R.K. Harrison, uk. 950.

A. Nabii zenye Tarehe, sura 1-8
   1. Utangulizi na wito wa toba, 1:1-6.
   2. Maono manane yenye kuhusiana na ujenzi wa Hekalu la Yerusalemu, 1:7-6:15
      a. Watu wanne waliopanda farasi; ahadi ya urejesho wa ki-Ungu, 1:7-17
      b. Pembe nne zenye kutawanya na wafua chuma wanne, 1:18-21 (2:1-4 Ebr.)
      c. Ukuu wa Yerusalemu usiopimika, 2:1-13 (2:5-17 Ebr.)
      d. Kutakaswa kwa Yoshua, neno; kwake, 3:1-10
      e. Taa saba zilizo juu ya kinara cha taa cha dhahabu, 4:1-14
      f. Gombo la chuo kubwa lirukalo, 5:1-4
      g. Wanawake ndani ya efa wakipelekwa Babeli, 5:5-11
      h. magari ya vita manne waendao duniani, 6:1-8
   3. Kipengele cha kihistoria: Yoshua ishara ya Masihi, 6:9-15.
   4. Ulizo la Zekaria kuhusiana na tendo la kufunga, 7:1-8:23.

B. Nabii zisizo na Tarehe, 9-14
   1. Hukumu juu ya maadui wa taifa; kuja kwa mtawala wa amani, 9:1-17
   2. Kiongozi wa ki-Ungu kulikusanya kundi, 10:1-12
   3. Wachungaji wema na wapumbavu; kuteseka kwa kundi, 11:1-17
   4. Maono ya siku za mwisho, 12:1-13:6
   5. Hukumu ya ufalme wa ki-Ungu itakasayo, 13:7-14:21

VIII. KWELI KUU

A. Sababu kuu ya kitabu hiki ni kuwatumainisha Wayahudi waliorejea kwa ajili ya kulijenga upya Hekalu. Hili linaelezwa na Sheshbaza, Ezra 1:8; 5:16, lakini halikuendelezwa chini ya Zerubabeli. Hekalu lilikuwa limekataliwa kwa miaka kadhaa. Hagai anaeleza kwamba hii ni kwa sababu ya kutojali kwa watu ambapo Ezra anaeleza kwamba huu ulikuwa ujanja wa kisiasa wa majimbo yaliyokuwa yamezunguka, hasa Samaria.

B. Kitabu hiki ni cha ki-Masihi zaidi. Nabii zilizo nyingi zilizohusu maisha ya Yesu zilitoka katika sura. 9-14:
   1. mfalme ni mnyenyekevu amepanda punda, Naam, mwana-punda, 9:9,
   2. nikavitwaa vile vipande thelathini vya fedha, nikamtupia huyo mfinyanzi kama eneo la maziko, 11:13,
   3. mkazo juu ya uzao wa Daudi, 12:4-9,
   4. "nao watamtazama yeye ambaye walimchoma..." 12:10.

C. Upendo na utawala wa Mungu kiulimwengu unaonekana katika 2:11; 8:20-23; 14:9,16. Bali katika sura 9-14 uasi wa kiulimwengu wa watu wote unatiwa hofu, 12:3 na 14:2 (Zab. 2).

IX. MANENO NA/AU VIFUNGU NA WATU WA KUTAMBUA KIMUHTASARI

A. Maneno na /au Vifungu

1. Nirudieni, 1:3 (NASB na NIV)
2. "Naona wivu kwa ajili ya Yerusalemu, na kwa ajili ya Sayuni," 1:14 (NASB na NIV)
3. "na kamba itanyoshwa juu ya Yerusalemu," 1:16 (NASB na NIV)
4. pembe nne, 1:18-21 (NASB na NIV)
5. "nitakuwa ukuta wa moto kuuzunguka pande zote," 2:5 (NIV, "Mimi mwenyewe nitakuwa ukuta wa moto kuuzunguka pande zote")
6. "mboni ya jicho lake," 2:8 (NASB na NIV)
7. "Yoshua alikuwa amevaa nguo chafu sana," 3:3 (NASB na NIV)
8. gombo la chuo lirukalo, 5:1 (NASB na NIV)
9. vinyago, 10:2 (NIV, "sanamu za kuchonga")
10. vipande viwili : "Kibali na Umoja," 11:7, 14 (NASB na NIV)
11. "mimi nitafanya Yerusalemu kuwa kikombe.. jiwe la kuwalemea watu," 12:2-3 (NIV, "...jiwe lisilohamishika")
12. "maji yaliyo hai yatatoka katika Yerusalemu," 14:8 (NASB na NIV)

B. Watu wa Kutambua Kimuhtasari


1. Berekia, 1:1,7
2. malaika wa Bwana, 1:11; 3:1
3. Shetani, 3:1-2
4. Chipukizi, 3:8; 6:12
5. "hao wana wawili wa mafuta," 4:14
6. Hadadrimoni, 12:11 (NIV, "Hadadi Rimoni")

X. MAENEO KI-RAMANI


1. Sayuni, 1:14
2. Shinari, 5:11 (NIV, “Babeli”)
3. Betheli
4. Hamathi, 9:2
5. Bonde la Megido, 12:11
6. mlima wa Mizeituni, 14:4

XI. MASWALI YA KIMAUDHUI KWA MWANAFUNZI

1. Ni kwa namna gani kitabu cha Zekaria kilikuwa na uhusiano na kitabu cha Hagai?
2. Ni kwa namna gani maono ya 1:7-6:8 yalikuwa na uhusiano?
3. Orodhesha majina ya Masihi yanayopatikana katika kitabu hiki.
4. Watu gani ni miti miwili ya mizeituni ya sura ya nne 4?
5. Ni siku gani za kufunga zilizoorodheshwa katika sura 7-8?
6. Ziorodheshe nabii zilizo katika sura 9-14 ambazo zinahusiana na maisha ya Kristo.


KAS
MAGH
MASH
KUS
MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE

# PALESTINA



# UTANGULIZI WA MALAKI

I. JINA LA KITABU

A. Hiki kinapewa jina la nabii huyu.

B. Jina ake linamaanisha "Mjumbe wangu."

1. Hiki kinaweza kuwa cheo, "mjumbe wangu," 3:1.
2. Hili linaweza kuwa "Malaika wangu."
3. Hili linaweza kuwa jina sahihi.

II. URASIMISHAJI

A. Kitabu hiki ni sehemu ya kipengele cha "manabii wa mwisho" (Ecclesiasticus 49:10).

B. Hii ni sehemu ya kundi "Kumi na Mawili," ya manabii wadogowadogo (Baba Bathra 14b):

1. kama alivyo Isaya, Yeremia na Ezekieli, hawa wnaendana na gombo la chuo moja.
2. hiki kinayawakilisha makabila kumi na mawili au uwakilishi wa namba za ushirika.
3. Hiki kinauakisi mtazamo wa kidesturi wa mpangilio maalumu wa vitabu.

C. Mpangilio wa "Kumi na Mbili" au Manabii wadogo wadogo umehusianishwa na wanazuoni wengi katika mtiririko maalumu. Kwa namna iliyo wazi Malaki ndiye nabii mdogo wa mwisho.

III. AINA ZA UWASILISHAJI

A. Huu unatumika kutoa shutma ili kwa ajili ya kuiwasilisha kweli. Huu ni muundo wa maswali na majibu. Kweli hii iliwasilishwa na kisha mnung'unikaji aliyestahili aliuliza swali au kutoa pendekezo juu ya kile alichokizungumza mzungumzaji.

B. Malaki amekuwa akiitwa "Socrates wa Kiebrania"

C. Wote Paulo na Yakobo waliitumia njia hii kuiwasilisha kweli.

D. Muundo huu unaweza kuonekana katika, "Lakini ninyi mwasema,...", 1:2, 6, 7(mara mbili), 12, 13; 2:14, 17 (mara mbili); 3:7, 8, 13, 14.

E. Huu si ushairi wa Kiebrania.

IV. UANDISHI

A. Hili neno la Kiebrania "*malachi*" lililotumika katika 1:1 linamaanisha "malaika" au "mjumbe."

1. Wengi hulichukulia hili kama jina halisi.
2. Toleo la LXX linalichukulia hili kama jina (kama vile 3:1).
3. Origen alifikiri kuwa hili lilimrejelea malaika.

B. Kitabu cha Sheria za Kiyahudi (Mecillah 15a) kinasema kuwa Modekai aliandika kitabu.

C. Targum ya Kiaramu ya Jonathan inasema kuwa huyu alikuwa mdogo kwa Ezra. Fasiri hii ilikuwa na wafuasi kama : Jerome, Rashi na Calvin.

D. Josephus katika *Antiquities of the Jews*, 11:4-5 anayataja majina yote ya watu walikuwepo baada ya uhamisho isipokuwa Malaki.

E. Jina lake halijitokezi katika kiunganishi cho chote kwa nukuu zo zote za Agano Jipya zitokanazo na kitabu hiki.

F. II Esdras anawaorodhesha manabii wote waliofuatia baada ya uhamisho kama Hagai, Zekaria na Malaki.

G. Kwa kuwa hakuna kitabu kingine cha kinabii kisicho na jina, Lazima kitabu cha Malaki kiwe na jina halisi. Kumbuka, uandishi hauathiri uvuvio.

V. TAREHE

A. Kuna uhusiano mkubwa kati ya usuli wa kihistoria wa Nehemia na Malaki:

1. mvutano juu ya utoaji zaka, Mal. 3:8; Neh. 10:32-39,

2. masikini walikuwa wakinyanyaswa, Mal. 3:5; Neh. 5:1-5,
3. mwingiliano wa ndoa za kidini, Mal. 2:10,11; Neh. 13:1-3, 23-24 (Ezra 9:1-2).

B. Uchaguzi sahihi zaidi unaonekana kuwa kati ya 450-430 K.K., baada ya Nehemia kurudi kwa mfalme Artashasta I, Neh. 13:6.

VI. UHUSIANO WA KIHISTORIA KATI YA WAEBRANIA NA EDOMU, 1:2-5

A. Waliambiwa kuwaheshimu hawa kama jamaa zao:
1. Hesabu 20:14
2. Kumbukumbu la Torati 2:4-6

B. Walikabiliana nao mara nyingi:
1. Hesabu 20:14-21
2. Waamuzi 11:16 na kuendelea
3. I Samweli 14:47-48

C. Unabii dhidi yao:
1. Hesabu 24:18
2. Isaya 34:5 na kuendelea; 63:1 na kuendelea
3. Yeremia 49:7 na kuendelea
4. Maombolezo 4:21-22
5. Ezekieli 26:12 na kuendelea; 35:13 na kuendela; 36:2-6
6. Amosi 1:11-12

VII. VIPENGELE VYA KIFASIHI

A. Muhtasari wa kitabu cha Malaki unaufuatisha mwenendo au makaripio yake sita. Malaki anazungumza kwa niaba ya Mungu, watu waliitikia na Malaki anazungumza kwa niaba ya Mungu kwa mara nyingine.

B. Muhtasari
1. Upendo wa Mungu kwa Wayahudi waliorejea, 1:2-5
2. Shutuma za makuhani, 1:6-2:9
3. Shutuma za Mungu juu ya talaka na ndoa za kuchanganya dini, 2:10-16
4. Shutuma za Mungu juu ya mtazamo wao mbaya (Mungu wa haki yuko wapi?), 2:17-3:6
5. Shutuma za Mungu juu mkono wa Hekalu, 3:7-12
6. Shutuma za Mungu juu ya mtazamo wao mbaya (Kumtumikia Mungu ni upuuzi!), 3:13-4:3
7. Maonyo ya mwisho na ahadi, 4:4-6

VIII. KWELI KUU

A. Malaki anazithibitisha dhambi za kutojali na kupungukiwa imani kwa Wayahudi waliorudi.

B. Kitabu hiki kina semi kadhaa za kiulimwengu. Mungu atatumia Israeli kuufikia ulimwengu, 1:5, 11, 14; 3:12.

C. Watu wa Mungu wanaikaidi tabia yake:
1. 2:17 –Mungu hutenda katika haki.
2. 3:6 – Sifa ya Mungu ya kutokubadilika ndiyo sababu pekee inayoifanya Israeli iendelee kuwepo.
3. 3:14 – Ya kwamba kumtumikia Mungu hakuna faida.

D. Kitabu hiki ni kama tumaini la ki-Masihi, 3:1; 4:5.

IX. MANENO NA/AU VIFUNGU NA WATU WA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

A. Maneno na/au tungo

1. neno, 1:1 (NASB na NIV)
2. "Lakini ninyi mwasema..." 1:2 (NIV, "Lakini mwauliza...")
3. "mtoapo sadaka walio vilema na wagonjwa," 1:8 (NIV, "wanyama walio viwete au wagonjwa")
4. "Nanyi mmelidharau," 1:13 (NIV, "mnazinusa kwa dharau")
5. "nitaikemea mbegu kwa ajili yenu," 2:3 (NIV, "nitavikemea vizazi vyenu")
6. "amemwoa binti ya mungu mgeni," 2:11 (NASB na NIV)
7. "Bwana mnayemtafuta atalijilia hekalu lake ghafula," 3:1 (NASB na NIV)
8. "kitabu cha ukumbusho ," 3:16 (NIV, "gombo la chuo la ukumbusho")
9. "jua la haki litawazukia, lenye kuponya katika mbawa zake," 4:2 (NASB na NIV)

B. Watu


1. Esau, 1:2-3
2. Yakobo, 1:2
3. Lawi, 2:4
4. wachawi, 3:5
5. mgeni , 3:5
6. Eliya nabii, 4:5


X. MAENEO KI-RAMANI

1. Edomu, 1:4
2. Yuda, 2:11
3. Israeli, 2:11
4. Horebu, 4:4

XI. MASWALI YA KI-MAUDHUI KWA MWANAFUNZI

1. Je! kitabu cha Malaki kina muundo gani?
2. Kwa nini Esau anatajwa katika 1:2?
3. Ni kwa namna gani kuhani na watu wanaonyesha kutomheshimu YHWH?
4. Laana inatajwa katika eneo lipi katika 2:2; 3:9 inayotokana na Maandiko? Je! hii ilihusisha nini?
5. Kwa nini Mungu anasema kuwa anachukia kuachana? 2:16
6. Ni kwa namna gani ilimpasa Masihi kuja ghafla ndani ya Hekalu?
7. Kwa nini 3:6 ni ya muhimu sana?
8. Je! Mungu anaahidi utajiri utokanao na kutoa zaka?
9. Je! Eliya alikuja kabla ya Yesu?


MASHARIKI YA KARIBU
YA KALE
KAS
MAGH
MASH
KUS


PALESTINA
0 10 20 30 40
VIPIMO KATIKA MAILI